Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA SITA

**Kikao cha Ishirini na Saba – Tarehe 13 Julai, 2009**

*Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

**MHE. JOB Y. NDUGAI - MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA:**

Taarifa ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka 2008/2009 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

**MHE. GRACE S. KIWELU – (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI):**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

**NAIBU WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

Randama za Makadirio ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

**NAIBU WAZIRI WA WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):**

Taarifa ya Mwaka ya Benki Kuu ya Tanzania kwa mwaka 2007/2008 *(The Annual Report of the Bank of Tanzania for the Year 2007/2008).*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 195

### Ukarabati wa Chumba cha Kuhifadhia Maiti Hospitali ya Mkoa wa Singida

**MHE. MGANA I. MSINDAI (K.n.y. MHE. MOHAMMED G. DEWJI)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Hospitali ya Mkoa wa Singida ni kiungo na tegemezi kubwa kwa wananchi wa Singida na kwa kuwa ukarabati uliofanywa na Serikali katika Hospitali hiyo haukuhusisha upanuzi wa chumba cha kuhifadhia maiti ikiwa ni pamoja na kukiongezea ukubwa:-

Je, Serikali itafanya lini ukarabati wa chumba cha kuhifadhia maiti ikiwa ni pamoja na kukiongezea ukubwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Gulam Dewji, Mbunge wa Singida Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Hospitali ya Mkoa wa Singida imefanyiwa ukarabati mkubwa na Serikali katika mwaka wa fedha 2007/2008 ambao haukuhusisha upanuzi wa chumba cha kuhifadhia maiti. Ukarabati uliofanywa ulizingatia zaidi hali halisi ya uchakavu uliokuwepo wa sehemu ambazo zilikarabatiwa.

Aidha, kuanzia mwaka 2008/2009 fedha zilitengwa kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali mpya ya Mkoa shilingi bilioni (2) na mwaka 2009/2010 shilingi bilioni (2) nyingine ziliidhinishwa kuendeleza ujenzi ambacho ndicho kipaumbele kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo kuhusu hitaji la upanuzi wa chumba cha maiti Serikali imeshaliona hilo na Mkoa ulimwomba wakala wa Majengo Tanzania *(Tanzania Building Agency* kufanya makadirio ya gharama za ukarabati.

Aidha, makadirio yaliwalishwa (*BOQs*) ya kiasi cha shilingi 55,364,600/=. Mkoa unajipanga kuona uwezekano wa kuweka suala la upanuzi wa chumba cha kuhifadhia maiti katika Hospitali ya Mkoa kama kipaumbele katika mwaka wa fedha 2010/2011.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mji wa Singida umepanuka sana na watu wameongezeka kwa wingi na kwa kuwa barabara karibu zote zinazopita hapo Singida zimeshawekwa lami ni zingine zinaendelea kuwekwa lami kwa hiyo kuna ajali nyingi sana zinatokea. Na kwa kuwa chumba cha kuhifadhia maiti siyo jambo la kuchagua ni jambo la dharura na sasa hivi tunapitisha Bajeti Waziri anaweza kuwasaidia watu wa Singida na Mikoa inayozunguka Singida kujenga chumba cha kuhifadhia maiti kama ni jambo la dharura na ifanyike mwaka huu wa fedha? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nakubaliana naye kwamba Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, imetekelezwa sana katika Mkoa wa Singida na barabara ukienda pale sasa hivi utashangaa hutaamini kwamba uko Singida na kwamba hiyo sasa inasababisha pia na mambo ya ajali kujitokeza pale. Mimi nadhani nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge Mgana I. Msindai.

Labda nionyeshe kwa vipi sasa hiyo kazi anayoisema kwamba inaendelezwa. Nimesema hapa hospitali itakayojengwa katika Mkoa wa Singida itakuwa ni Hospitali ya Rufaa wala siyo Hospitali ya Mkoa na ndiyo maana tumepeleka bilioni 2 tukapeleka na bilioni nyingine mbili. Hiyo, moja kwamba tutahakikisha tunapanua uwezo mkubwa na kwa kiwango kikubwa na haya makubwa anayosema yamefanyika hapa mpango wake ni huo. Ningepata nafasi ningeweza nikaendeleza zaidi.

Lakini kuhusu eneo la Manispaa sasa linalozungumzwa hapa nilipokuja nakuja nicheki na Mkuu wa Mkoa wa Singida na nimecheki na watu wangu global fund walikuwa wamepeleka hela pale zikabaki, hizi hela zilizobaki milioni 55 wameziombea kibali na Katibu Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ameidhinisha kwamba watumie hela hizo kwa ajili ya kusaidia hiki chumba cha maiti.

Kwa hiyo, upanuzi anaouzungumza Mheshimiwa Mgana Msindia utachukuliwa. Hiyo, hospitali ambayo tunaijenga sasa hivi tutaibakisha pale Singida itabaki kama Hospitali ya Manispaa ya Singida na ni ya kisasa ambayo itakuwa na mambo ya kisasa.

Kwa hiyo, suala la kwamba ajali zitatokea na matatizo yatatokea pale, hiyo Serikali yenu imeshafanya kazi yake imemaliza hakuna tatizo. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tatizo lililo Mkoani Singida linafanana na lile lililo kwenye Hospitali Kuu ya Mkoa wa Kilimanjaro. Je, baada ya kutoa maombi kadhaa hapa Bungeni mwaka huu hospitali hiyo itafikiriwa katika kupanua chumba cha maiti?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shally Raymond Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Kilimanjaro kama ifuatavyo:-

Labda hapa ni-*declare interest* kwa sababu hii ni Hospitali ya Mkoa kwa hiyo mimi natoka Siha kule na sisi tunatumia hospitali hiyo hiyo wasije wakasema kwamba sikujali hilo. Lakini hapa mpaka niende nikajue mambo yenyewe vizuri, nikaangalie vizuri, tukacheki vizuri. Lakini la msingi ambalo tunalozungumza hapa Hospitali ya Mkoa kwa kweli bajeti yake inapitia kwenye Ofisi ya *RAS* Mkoa wa Kilimanjaro.

Ninamuomba Mheshimiwa Shally Raymond aje tuangalie vizuri na kama tunaona kwamba kwa kweli hili ni tatizo pale, mimi nakili kwamba ni tatizo kwa sababu tunafika pale kuna tatizo pamoja na kwamba kuna *KCMC* pale ili tuweze kusaidiana kwa pamoja tuweze hili tatizo ambalo Mheshimiwa Shally Raymond analizungumzia. (*Makofi*)

Na. 196

**Magari Madogo kwa Makatibu Tarafa**

**MHE. MTUTURA ABDALLAH MTUTURA (K.n.y. MHE. VITA R. KAWAWA** aliuliza:-

Kwa kuwa Makatibu Tarafa wamekuwa na maeneo makubwa ya kazi zao za utawala na usafiri wao wa pikipiki na kwa kuwa wengi wao hupatwa na maradhi ya kifua kikuu kutokana na upepo na baridi hivyo kuathiri afya zao na utendaji kazi wao:-

Je, Serikali inaweza kuweka katika mpango wa kupatiwa magari madogo au hata Bajaji ili kuwawezesha katika ufanisi wa kazi zao?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa Mbunge wa Namtumbo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Maafisa Tarafa ni watumishi wa Serikali kama walivyo watumishi wengine. Katika marekebisho ya sheria za Serikali za Mitaa Na. 7 na 8 za mamlaka za Miji na Wilaya za mwaka 1982 na mwongozo wa uwajibikaji, Maafisa Tarafa wanawajibika kwa Wakuu wa Wilaya na pia kwa sasa wanawajika kwa Mkugurenzi wa Halmashauri. Hivyo nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge Vita Kawawa kuwa majukumu yao ya kusimamia maendeleo katika Wilaya yameongezeka.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa kwa hivi sasa Maafisa Tarafa, wanatumia pikipiki kama vyombo vya usafiri katika ufuatiliaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo katika tarafa zao. Hata hivyo ofisi yangu haijapata malalamiko kuwa watumishi hao wanapata maradhi ya kifua kikuu kwa sababu ya kutumia pikipiki.

Hata hivyo Serikali inatambua kuwa ziko tarafa zenye mazingira magumu ya miundombinu kwa matumizi ya pikipiki kama chombo cha usafiri wakati wa ufuatiliaji wa shughuli zao.

Mheshimiwa Spika, naomba kueleza kuwa Serikali imeanza kuyatazama maeneo yenye mazingira magumu na Mikoa imeelekezwa kutambua tarafa zenye mazingira magumu ya miundombinu ya usafiri na kutenga katika bajeti za Mikoa fedha za kununua magari madogo aina ya Suzuki kwa awamu na si bajaji kwa sababu uwezo wa bajaji kupita katika miundombinu tuliyonayo hasa ya vijijini ni dhahiri kuwa hazitawezesha kufika maeneo korofi na hazifai katika maeneo yenye mapori makubwa na wanyama wakali.

**MHE. MTUTURA ABDALLAH MTUTURA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wilaya ya Namtumbo pamoja na Wilaya jirani ya Tunduru ina ukubwa wa eneo lisilopungua kilomita za mraba 18,000 na kuifanya Wilaya hiyo iwe na tarafa zilizo mtawanyiko ili kuweza kufika mtawanyiko mrefu kuweza kufikia Makao Makuu ya Wilaya.

Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nasi kuzifanya Wilaya hizi mbili ziwe za kwanza kupatiwa huduma hiyo ya usafiri wa magari ya Suzuki kabla ya Wilaya zingine?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kwa taarifa ya Bunge lako tukufu mimi nilipoanza kazi kwa mara ya kwanza nilifanya katika Wilaya Tunduru kwa miaka 5 kwa hiyo nakili kwamba anavyozungumza hapa zile Tarafa za Nakapanya na zile za Matemanga kwamba zimetawanyika sana, mimi nimefundisha kule kwa hiyo, nafahamu kwamba Mheshimiwa Mtutura anachozungumza ni kweli.

Ukiingia katika tarafa yoyote lazima urudi kwenye Main road huwezi kukatisha humo humo ukatokea kwenye tarafa nyingine. Kwa hiyo, kuna tatizo pale.

Lakini sasa turudi kwenye suala ambalo analizungumzia hapa anachosema ni kwamba zile Wilaya ziwe za kwanza Namtumbo na Wilaya ya Tunduru msimamo wa Serikali sisi tulishaagiza hapa tukawaambia Ma - *RAS* wetu kwamba wao waangalie sasa habari ya Bajaji tuachane nayo, Bajaji haifai vijijini lakini muangalie uwezekano wa kupata Suzuki.

Mheshimiwa Spika, lakini baadaye tukuja hapa na msimamo wa Serikali tukasema kilimo kwanza. Tuliposema kilimo kwanza sasa, kilimo kwanza ni maagizo ya Serikali hapa mimi nikisema hapa na Mzee mwenyewe kakaa hapa nyuma anasikiliza ninavyojibu kwa hiyo, hapa ni *powertillers*, matrekta na kadhalika. Habari ya kununua magari tukasimamisha na hii ikakumbwa humo humo. Sasa kama kutakuwa kuna maombi maalum ndipo tutaruhusu lakini kwa sasa hivi msimamo ni kilimo kwanza. Nashukuru kwa hilo. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kuna matatizo ya kibajeti kuhusu kununua magari kwa Makatibu Tarafa na kwa kuwa tarafa nyingine ni kubwa sana kwa mfano Tarafa ya Mbinga Mjini ina Kata 13 na njia mojawapo ambayo mimi naiona ni kugawa hizi tarafa unaweza kupata mbili au tatu. Je, Serikali inaweza kufikiria hiyo kama njia mbadala? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, sasa hapa limeingia zoezi lingine jipya kwa maana sasa ile nilikuwa naelewa mambo ya magari na nini. Lakini niseme tu kwamba hapa tunao utaratibu huu wa kuunda vijiji, kata, pamoja na tarafa. Sasa sisi tutaliangalia na hili zoezi limekuwa linaendelea na kwa kweli tumeshakabidhi kwa mamlaka inayohusika ili iweze kufanya uamuzi yaani mambo yameshapita pale kwa maana zoezi lenyewe tumeshalipita tayari. Sasa labda tukutane na Mheshimiwa Kayombo tuangalie vizuri.

Lakini kwa hapa kumwambia kwamba tuwezi kuunda mamlaka nyingine mpya hapa itakuwa ni vigumu kwa sababu ya zoezi lenyewe. Lakini natambua tatizo lake na kwa hiyo tunaweza tukali-*consider* kwa tukapendekeza mamlaka inayohusika.

**MHE. MANJU S. MSAMBYA:** Mheshimiwa Spika, naafiki kabisa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Lakini katika majibu yake kwa sababu amesema kilimo kwanza na sote tunatambua kwamba Makatibu Tarafa ndiyo miongoni mwa maafisa watakaosimamia mkakati wa kilimo kwanza isingekuwa vizuri na wenyewe likachukuliwa kama suala la dharura ili wapatiwe usafiri hii maana ni muhimu sana?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, niliwahi kukueleza hapa huko Kigoma ndiyo kabisa nimefanyakazi wakati nikiwa kada wa Chama cha Mapindizi nilikuwa nafanyakazi kule.

Kwa hiyo, naelewa hii *concern* ambayo anaileta hapa. Labda niseme moja tu msimamo wa Serikali kwa sasa hivi ni kwamba Makatibu Tarafa wetu ambao tunawaita Maafisa Tarafa, siyo Makatibu Tarafa, Makatibu ni kitu kingine. Hawa tumesema

kwamba wapewe pikipiki na hizi pikipiki tumeruhusu kabisa, pikipiki wamekuwa nazo sasa ni kweli kabisa kama anavyosema yeye hapa kwamba kuna mazingira magumu ambayo hata pikipiki ukitaka kuitumia na ukizingatia majukumu ambayo tumewapa, huyu Afisa Tarafa anayezungumzwa hapa sasa hivi anawajibika kwa Mkuu wa Wilaya kwa maana Serikali Kuu lakini anawajibika pia kwa mkurugenzi Mtendaji kwa maana ya Serikali za Mitaa kwa maana *D by D* ndicho anachozungumza hapa.

Kwa hiyo, majukumu yamepanuka sana na ni kweli kwamba Maafisa Tarafa wetu wanapata matatizo. Sasa kwa sasa hivi hapa ambacho naweza nikasema na namuomba ndugu yangu Manju Msambya asinitie majaribuni bali aniokoa na yule muovu anisaidie tu hapa kwa sasa hivi tunachozungumza ni habari ya pikipiki.

Sasa kama kuna maombi maalum kama kuna gari lolote la kununuliwa mpaka kibali kitoke kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu kikitamka kwamba unaruhusiwa kununua gari. Sasa hayo mamlaka sina nina mamlaka tu ya kujibu hivyo nilivyosema hapa, lakini linaweza likaja hapa. (*Makofi*)

Na. 197

**MHE. MWANAWETU SAID ZARAFI** aliuliza:-

Kwa kuwa, likizo ni haki ya kila mtumishi ambaye huipata kila mwaka isipokuwa kwa Askari ambao hupata likizo kila baada ya miaka mitatu:-

(a) Je, ni watumishi wa ngazi zipi hupata likizo kila mwaka na kila baada ya miaka mitatu?

(b) Je, ni nini hasa kusudio la likizo mara baada ya kipindi cha kufanya kazi mwaka mmoja au miaka mitatu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwanawetu Said Zarafi, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Awali ya yote ningependa kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge, kuwa pamoja na kwamba likizo ni haki ya kila mtumishi, kila haki ina utaratibu wake wa kutolewa au mhusika kuipata. Kwa mantiki hiyo, watumishi wote wenye ajira za kudumu wanastahili kupata likizo kwa utaratibu uliowekwa. Likizo inatakiwa kuchukuliwa kila mzunguko wa likizo.

Kwa mujibu wa Kifungu Na. 31 (1) cha Sheria ya Ajira na Mahusiano kazini (1) cha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya mwaka 2004, ikisomwa kwa pamoja na Kanuni 97 (2) ya Kanuni za Utumishiwa Umma za mwaka 2003, Kanuni H. 4 (b) ya

Kanuni za Kudumu za Utumishiwa Umma Toleo la Mwaka 1994 wapo watumishi wanaostahili likizo ya siku 28 katika mzunguko wao wa kila mwaka.

Hata hivyo, kwa mujibu wa Sheria ya Polisi Sura 322 ikisomwa kwa pamoja na Kanuni za Kudumu za Magereza (*Prisons Standing Orders*) toleo la 4 la mwaka 2003, Askari Polisi na Magereza wanao utaratibu wao wa kuchukua likizo kulingana na makundi ya vyeo vyao. Askari wenye ngazi za juu, kuanzia Mkaguzi Msaidizi na kuendelea kuchukua likizo ya siku 28 kila mwaka. Lakini kwa wale Askari wa ngazi zilizo chini ya Mkaguzi Msaidizi wao huchukua likizo zao kila baada ya miaka mitatu ikiwa ni jumla ya siku 84 kutokana na majukumu na matakwa ya kazi zao.

(b) Madhumuni ya likizo ni kumuwezesha mtumishi kupumzika na kupata anguvu mpya na ari ya kufanya kazi kwa ufanisi zaidi. Ni jambo la maana kwa kila mtumishi kupewa nafasi ya kupumzika kama masharti yake ya kazi inavyoelekeza.

Waajiri wanahimizwa kuandaa ratiba za likizo kwa kila mwka wa fedha. Watumishi wote wafahamishwe kuhusu ratiba hizi za likizo ili kuhakikisha kwamba wanafahamu muda wao wa kuchukua likizo na waajiri wahakikishe kwamba watumishi wanachukua likizo zao kwa muda uliopangwa bila visingizio vyovyote.

**MHE. MWANAWETU SAID ZARAFI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kutokana na maelezo aliyosema mtumishi ana haki ya kupumzika baada ya mwaka au miaka mitatu na kwa kuwa askari wetu wanafanyakazi kwa muda mrefu wa muda wa miaka mitatu na hii inawapelekea kuchoka sana na vile vile wanapokwenda likizo ya miezi mitatu wanakuwa matatizo ya kurudi nyumbani kwa sababu wanakosa fedha na kwa sababu malipo yao hayatekelezwi kama ipasavyo kwa mujibu wa likizo yao ya miaka mitatu.

Je, Serikali haioni kuwa ni wakati muafaka wa kubadili sheria hii ili kuwawezesha askari hawa waweze kwenda likizo ya mwezi mmoja kama wanavyokwenda watumishi wengine? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu suala kwamba kwa nini waende kila baada ya miaka mitatu ni matakwa ya sheria. Lakini pia kama nilivyosema kwamba wanakwenda likizo kwa mujibu wa vyeo vyao.

Wapo wale ambao wanakwenda kila mwaka na wapo wale ambao wanakwenda kila baada ya miaka mitatu. Sasa wale wanaokwenda kila mwaka ni kundi dogo sana ukilingasha na hawa ambao wanakwenda kila baada ya miaka mitatu.

Kama tunavyofahamu kundi askari ambao ni wa ngazi za chini ndiyo wale ambao wanatekeleza amri za kijeshi za mara kwa mara na pia ndiyo wale ambao wanashughulika zaidi katika operesheni ambazo ni za kijeshi kama zote ambazo tunazifahamu. Kwa hiyo, kutoa likizo kwa kundi kubwa kama hilo kutaathiri kwa kiasi kikubwa utendaji kazi wa Jeshi la Polisi.

Pia kuhusu suala la fedha napenda kumhakikishia Mbunge kwamba sasa hivi hasa kwa kuanzia na bajeti hii Serikali imehakikisha kwamba masuala ya likizo matibabu yanazingatiwa katika bajeti ya kila Wizara husika.

Na. 198

**Uchimbaji wa Mabwawa na Malambo katika Mbuga za Wanyama**

**MHE. JANETH B. KAHAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa maeneo ya Hifadhi za Wanyama kama vile Serengeti, Selous na kadhalika hukumbwa na ukame sana nyakati za kiangazi na kusababisha wanyama kusafiri na kutafuta maeneo yenye maji *(migration)* na huvutia sana watalii:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia wanyama ambao hawamo katika *migration zones* kupata maji kwa njia ya kuchimba malambo na mabwawa ya maji?

(b) Kama Serikali imeweza kuchimba malambo ya maji, je maeneo hayo yako katika mbuga zipi?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Janeth Bina Kahama, Mbunge Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, muda mrefu sasa Tanzania imekuwa ikitekeleza uhifadhi wa wanyamapori katika mazingira yao ya asili tofauti na nchi zingine duniani, kama kule

Ulaya, ambako wanyama huhifadhiwa katika maeneo yenye uzio, hata kwenyenyumba na kupatiwa huduma mbalimbali kama vile maji, chakula, matibabu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, uhifadhi katika Tanzania unafanyika kwa kutenga maeneo ya asili bila kubadilisha mifumo ya maisha ya wanyama walioko na kuwaacha waendelee kuishi katika maeneo yao ya asili. Kwa kuzingatia uhifadhi wa aina hiyo, Tanzania imekuwa maarufu na kuwa na kivutio kikubwa kwa watalii duniani kote.

Mheshimiwa Spika, yapo maeneo nchini yaliyokuwa na mabwawa kwa ajili ya matumizi mbalimbali kwa wananchi kisha yakawa yametolewa na wananchi hao kwa ajili ya Hifadhi za Wanyamapori.

Baadhi ya mabwawa haya ni Bwawa la Nyasirori na Bwawa la Kawanga yaliyoko katika Pori la Akiba la Grumeti na Bwawa la Dindira lililoko katika Hifadhi ya Mkomazi. Kwa sasa Serikali haichimbi mabwawa katika hifadhi kutokana na matakwa ya uhifadhi asilia na ukosefu wa fedha wakati mwingine.

Hata hivyo uwezekano wa kuchimba mabwawa katika maeneo machache unawezekana pale inapobainika kuwa hiyo ndiyo njia pekee ya kunusuru wanyama na iwapo uwezo wa kifedha unaruhusu kwa jambo hilo kufanyika.

**MHE. JANETH B. KAHAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu. Nilitaka kujua kwa sababu amesema kuwa kuna wanyama huko nje Ulaya ambao wanaangalia katika nyumba na sehemu nyingine wanapewa chakula na maji. Nilitaka kuelewa katika nchi yetu ya Tanzania kuna watu binafsi ambao wanafanya hivyo?

Kama hao watu binafsi wapo iwapo hawa wanyama wakali wanaoishi nao kama nilivyoona kwenye gazeti mwanamke mmoja ameishi na chui wengi na iwapo anafariki:-

(a) Je, hawa wanyama wakali ambao kwa kweli wanatisha na kuathiri nani anawaangalia baada ya hapo?

(b) Kwa kuwa tulikuwa na taasisi ya *TSPCA* nchini hapa Tanzania ya kuangalia wanyama *(The Society of the Prevention of Cruelty to Animals)* kwa muda mrefu sijasikia kabisa kuhusu chama/taasisi hii inaendelea. Nilitaka kujua taasisi hii ipo na kama ipo inajiuzaje na inaelezaje Taifa letu? Ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimshukuru na kumpongeza mama Mheshimiwa Kahama kwa kuwajali wanyama na kujua kwamba ni rasilimali muhimu kwa Taifa. Niseme kwa sheria tuliyokuwa nayo kabla ya mwaka huu 2009, ilikuwa haitoi nafasi kwa sekta binafsi kuhifadhi wanyama. Sheria tuliyoipitisha, Sheria namba 5 ya mwaka 2009 yenyewe imeweka bayana kwamba sasa tutaruhusu sekta binafsi kushiriki katika uhifadhi. Sheria inaruhusu watu binafsi kuanzisha ranches, kuanzisha zoos na namna nyingine yeyote ya kuifadhi wanyama.

Mheshimiwa Spika, Sasa sasa hivi tuko kwenye atua ya kutenfeneza kanuni. Kanuni zitakapokuwa zimekamilika ndiyo zitakazo elezea ni namna gani wanyama wanaoifadhiwa na watu binafsi wataweza kulindwa na hata pale wanapotokea kuleta madhara ni namna gani wanaowahifadhi kwenye maeneo yao watawajibika. Kwa hiyo hilo limezingatiwa kwenye Sheria tuliyopitisha.

Mheshimiwa Spika, Kuhusu chama ambacho ameulizia, hicho chama kipo ingawa hakijakuwa maharufu sana kutokana na wakati mwingine na ukosefu wa fedha.kwa sasa hivi eneo hili tunalitazama na nafikiri kwamba kwa mikakati ambayo tumeiweka wataweza kujulikana zaidi kuliko ilivyokuwa mwanzo.

**SPIKA:** Tunaendelea Waheshimiwa na swali linalofuata ambalo ni la Wizara hiyo hiyo, linaulizwa na Mheshimiwa Kidawa Saleh.

Na. 199

**Utaratibu wa Utunzaji wa Historia ya Nchi Yetu**

**MHE. KIDAWA H. SALEH** aliuliza:-

kwa kuwa nchi nyingi duniani huweka utaratibu wa kutunza historia ya nchi kwa kuhifadhi majengo ya kihistoria, Makumbusho, yenye kutengeneza filamu maalaum zinazoonesha harakati za viongozi wao wa miaka ya nyuma, waliopigania ukombozi na uhuru wa nchi zao, na kwa kuwa jambo hilo lanajenga uelewa wa historia ya nchi kwa vijana, kujenga uzalendo na pia ni chanzo cha mapato kupitia utalii.

(a) Je, ni njia ipi kubwa ya utumiaji wa historia inayotumika hapa tanzania?

(b) Je, ni kwa kiasi gani uzalendo wa vijana wa tanzania umekuzwa kwa kutumia utaratibu huu?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuyatunza majengo ya kale yalioko Kilwa Kisiwani ili watalii wengi watembelee Kisiwa hicho?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, kwanza kabla ya kijibu swali la Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh Mbunge Viti Maalum naomba kwanza kumshukuru na kumpongeza kwa ufuatiliaji wa utunzaji wa historia ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, Mbunge Viti Maalum, lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifutaavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, hapa Tanzania, utumiaji wa historia umegawanyika katika njia kuu tatu ambazo ni Kielimu, Kiuchumi na Kijamii au Kiutamaduni.

Mheshimiwa Spika, Kielimu, kumbukumbu za kihistoria hutumika katika kuelimisha Umma kwa njia ya maonyesho, machapisho na tafiti zinazofanywa katika Makumbusho zetu kwa kushirikisha Vyuo Vikuu.

Aidha minara ya kihistoria kama vile mnara wa Azimio la Arusha uliopo Mkoani Arusha hutumika kutoa elimu ya historia kwa wanachi kwa njia ya kuona na kujisomea maelezo yanayowekwa katika minara hiyo. Pia elimu hutolewa kupitia somo la uraia mashuleni, vipindi vya redio na Televisheni hususani kipindi cha ,” Zamadamu“ cha *TBC1* ambacho kimeandaliwa kwa kushirikiana na Wizara yangu.

Mheshimiwa Spika, kiuchumi maeneo ya kihistoria yana mchango mkubwa katika kukuza uchumi wa nchi yetu kwa kuipatia Serikali mapato kutokana na utalii wa kiutamaduni. Kwa mfano maeneo kama vile Bonde la Oldupai, Magofu ya Kilwa na Songo Mnara nayo ni maarufu na hutusaidia sana kuleta fedha.

Kijamii au kiutamaduni, maeneo ya kihistoria ni sehemu muhimu ya historia na utamaduni wa Tanzania. Hapa Tanzania yapo maeneo mengi ya kihistoria yanayotumiwa kama sehemu za kuabudia au matambiko.

Mfano, Magofu ya Kunduchi (Dar es Salaam) ambako ndugu zetu kina Maneno uwa wanakwenda kuabudu pamoja na Magofu ya Kaole.

(b) Mheshimiwa Spika, matumizi ya maeneo ya kihistoria nilioleza katika kipengele (a) umeongeza uzalendo kwa vijana wetu kuthamini nchi yao.

Mfano, vijana wengi wameitikia wito kutunza maeneo ya kihistoria na kuelimisha jamii kuhusu historia ya nchi yetu. Hivi sasa vipo vikundi mbalimbali vya vijana vinavyofanya kazi ya kujitolea ya kuwatembeza wageni na uhifadhi wa magofu kwenye maeneo ya kihistoria kama vile Bagamoyo na Kilwa.

(c) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu wa kushirikiana na Wadau imekuwa na mpango na mikakati ya kuhakikisha eneo la Kilwa Kisiwani na Songo Mnara linaendelea kuhifadhiwa na kuhifadhi historia yake ili liendelee kuvutia watalii.

Wizara kwa kushirikiana Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni *(UNESCO)* , na Wahisani kama vile Serikali ya Norway, Japani na Ufaransa ilianzisha mradi wa dharura wa uhifadhi wa eneo la Urithi wa utamaduni la Kilwa Kisiwani na Songo Mnara mwaka 2005. Kupitia mradi huo wa magofu mengi yameweza kuhifadhiwa na kukarabatiwa. Maeno yaliyokarabatiwa ni pamoja na msikiti wa Ijumaa na gofu la Ikulu ya Kilwa iliyopo Songo Mnara.

**MHE. KIDAWA H. SALEH:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina swala moja la nyongeza. Kwa kuwa baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Sheik Abedi Amani Karume na viongozi wangine wa Hasisi wa wakati huo wamefanya kazi kubwa na iliyo tukuka ya kutuletea ukombozi na uhuru wa nchi yetu.

Je, Serikali haioni kuwa ipo haja sasa yakutengeneza filamu ya kuweza kuwaelimisha vijana wetu juu ya harakati za viongozi wetu hawa na ikaonyeshwa katika *TV* zote za hapa nchini ili kuibua uzalendo na uwelewa wa vijana wetu juu ya harakati hizo?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo. Ni kweli kwamba wahasisi wa Taifa letu ni watu muhimu sana na waliyoyafanya yanahitaji kuifadhiwa na vijana wetu wa sasa kuelimishwa. Kwa muda mrefu, Wizara imekuwa ikiweka kumbukumbu za wahasisi hawa kwenye makumbusho ya Taifa na tumekuwa tukiitumia makumbusho ya Butiama kutoa elimu.

Mheshimiwa Spika, Ukifika kwenye maktabaa ile inaeleza mambo mengi yanayohusu Mwalimu, lakini pia hata sehemu mbalimbali alizowahi kuishi ikiwepo nyumba ile ya Magomeni. Hili wazo la kutoa pana zaidi kupitia filamu na machapisho mbalimbali, ni wazo muhimu na sisi tumalichukua na tutaiweka kwenye mipango yetu. Kwa sasa au tuseme kabla ya swali hili, mpango uliokuwepo ni wa kuimarisha kumbukumbu za wahasisis kupitia makumbisho tulizokuwa nazo.

**MHE. DR. SAMSON MPANDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa makumbusho yaliyopo Kilwa Kisiwani,yanatumia Bandari kongwe ya Kilwa Masoko. Je, Serikali ina mpango gani kushughulikia Banbari ile ambayo ni kongwe na inapeleka watalii wengi kwa sasa? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli magofu ya Kilwa kama nilivyosema ni eneo muhimu sana kihistoria na sisi kama Wizara tumekuwa tukihifadhi eneo hilo na kama nilivyoeleza pia tumekuwa tukishirikiana na wadau mbalimbali lakini pia kupitia mradi wa *MASEF* ambao sasa upo Wizara ya Mifugo na Uvuvi nao umekuwa ukitoa mchango mkubwa wa uhifadhi katika eneo hilo la kihistoria.

Sisi nafikiri kwa sasa cha muhimu ni kuzungumza na wenzetu wa Miundombinu ili tuweze kuangalia uwezekano wa kuliboresha eneo la bandari kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameomba. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutazungumza na wenzetu wa Miundombinu kwamba ili tuweze kufanya kazi hii kwa upana na ukamilifu zaidi pamoja na makumbusho yenyewe ambayo tumekuwa tukiangalia au kuangalia magofu yenyewe basi tutaona ni namna gani ya tuweze kuboresha bandari pia.

**MHE. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa katika baadhi ya maeneo ya historia inasemekana kwamba kuna vitu ambavyo vilizikwa ardhini na wakati mwingine wanatoka watu nchi za nje kama vile *University of Sussex* waliwahi kufika maeneo ya Mkumbuu Pemba na kuna Wajerumani maeneo ya Milima ya Same. Je, Serikali inatambua sehemu zote hizo za historia ambazo zilifichwa mali na wakoloni?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna maeneo mengi ambayo vitu vya kihistoria na vingine vinasadikika kuwa ni vyenye thamani kubwa zimefichwa na kwa asili ya neno kuficha maana yake ni vitu ambavyo vimewekwa bila ridhaa ya upande mwingine.

Sasa hivi Wizara imeanza mkakati wa kuzungumza na watu hawa waliokuwa wakoloni wetu ili tuweze kupata orodha kamili ya vitu vya aina hiyo lakini pia vitu vya kihistoria ambavyo vilichukuliwa na wakoloni wenyewe vikahifadhiwa nje ya nchi mpango huu wa mazungumzo ulishaanza tangu mwaka jana na tunaendelea kuzungumza nao wakoloni wa kijerumani na hata waingereza ili tuweze kuwa na *stock* kamili kwa sababu sheria za kimataifa za uhifadhi wa kihistoria vinataka nchi iliyokuwa koloni ishirikiane na nchi ambayo ilikuwa mkoloni ili kuweza kutunza historia.

Kwa hiyo, kwa kuwa hawa ni wanachama wa *UNESCO* tutashirikiana nao na mpango huo tumekwisha kuunza.

Na. 200

**Nauli Vijijini**

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE** aliuliza:-

Kwa kuwa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini *(SUMATRA)* inafanya kazi zake mijini zaidi kuliko Wilayani na Vijijini; na kwa kuwa, vyombo vya usafiri vijijini vimeachwa bila udhibiti wowote hali inayosababisha wamiliki wa vyombo hivyo kujipangia nauli kubwa jinsi wanavyopenda na hivyo kuwaumiza wananchi:-

(a) Je, Serikali ina maelezo gani juu ya hilo?

(b) Je, ni chombo gani chenye wajibu wa kudhibiti usafiri na nauli vijijini?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, *SUMATRA* ni Taasisi ya Serikali iliyoanzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 9 ya mwaka 2001, kwa lengo la kusimamia na kudhibiti huduma za usafiri wa nchi kavu na majini nchini kote. Mpaka sasa Mamlaka inafanya kazi Makao Makuu pamoja na Ofisi zake za Kanda tano ambazo ni: Kanda ya Kaskazini (Moshi), Kanda ya Kati (Dodoma), Kanda ya Ziwa (Mwanza). Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ( Mbeya) na Kanda ya Mashariki ( Dar es Salaam).

Aidha, Mamlaka ina wafanyakazi wake kwenye ofisi zake za Mikoa ya Tanga, Arusha, Mtwara, Rukwa, Kagera na Kigoma. Kwa Mikoa ambayo Mamlaka haina wafanyakazi wake, inatumia wafanyakazi wa Ofisi za Makatibu Tawala wa Mikoa hiyo kuratibu shughuli zake.

Hata hivyo, Maafisa wa SUMATRA katika Kanda na Mikoa wamejiwekea utaratibu wa kutembelea Wilaya ndani ya Mikoa ili kutatua kero za wananchi hadi Vijijini.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka pia imekuwa ikishiriki katika vikao vya Mikoa ikiwemo Kamati za Ushauri Mikoa *( RCC's)* na kutoa elimu kuhusu shughuli za Mamlaka. Ni matumaini ya Serikali kuwa Wajumbe wa Vikao hivyo kutoka Wilayani hufikisha ujumbe wa Mamlaka hiyo hadi vijijini ambako SUMATRA haijawa na wawakilishi.

Kwa muundo na utaratibu huo wa ufanyaji kazi wa SUMATRA ni dhahiri kwamba huduma za chombo hiki huwafikia wananchi huko vijijini. Mpango wa muda mrefu wa *SUMATRA* kutokana na muundo wake ni kuongeza ofisi zao kwenye mikoa mingine ambako hawajafikisha huduma zao.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe mwito ya kwamba wakati *SUMATRA* inaendelea kijipanga katika ukamilishaji wa muundo wake. Pale penye ukiukaji wa Kanuni ikiwemo kutofuata viwango vya nauli vilivyoridhiwa na SUMATRA ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu ya Naibu Waziri lakini hata hivyo nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Baada ya Serikali kuamua kutenga fedha za kutosha katika Mfuko wa Barabara, Barabara vijijini zimekuwa nzuri na hivyo yale matarajio ya maisha bora kwa kila mtanzania yanaelekea katika mazingira mazuri zaidi na hivyo uchumi kule kijijini unachangamka na watu wanapenda kufanya movement. Hapa Mheshimiwa Naibu Waziri anazungumzia kwamba Mamlaka hii ya SUMATRA imejikita hasa katika Mkoa na pia hata hicho kikao cha ushauri cha Mkoa RCC kinafanya zaidi katika *level* ya Mkoa. Je, Serikali haioni kwamba kuna kila sababu ya kuweka Mamlaka hii katika ngazi ya Wilaya na hata ikibidi katika Kata kwa ajili ya kusimamia suala hili la usafiri vijijini?

Mheshimiwa Spika, la pili ni kwamba kwa mfano tuchukulie suala la nauli kutoka Kinusi –Chogola –Kibakwe mpaka Mpwapwa ni umbali usiozidi km 100. wananchi wanatozwa shilingi 8,000/- hadi 10,000/-. Lakini pia safari zao zinafanyika wakati wa usiku wa manane bila kuwa na msimamizi yeyote na tunavyojaribu kwa sababu hatuna mamlaka ya kisheria inayo- *control* kule kijijini inakuwa ngumu mno. Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kwamba iko haja katika kipindi hiki ambacho SUMATRA inajitanua kufika vijijini ku-*delegate power* hizi kwa mamlaka za Serikali zilizopo mpaka gazi ya vijiji?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu napenda kujibu maswala mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa George Boniface Simbachanawene, Mbunge wa Kibaki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nikubaliane sana na Mheshimiwa Mbunge Simbachawene ya kwamba barabara ya huko vijijini zimeboreka na kwa hiyo ile azma yetu ya kupeleka maisha bora kwa kila Mtanzania inaelekea kwenye azma yenyewe. Baada ya hayo, niseme tu kwamba muundo wa SUMATRA kama nilivyokuwa nimesema, unajielekeza huko ambako anazungumzia Mheshimiwa Mbunge ya kwamba tuhakikishe kwamba mamlaka hii inahudumia hadi Wilayani mpaka kwenye Kata. Lakini kama nilivyokuwa nimesema kwamba sasa hivi muundo huu ndo bado unaendelea kujitanua, sasa hivi tuko kwenye kanda na baadhi ya Mikoa.

Mheshimiwa Spika, Lakini mpango hapo baadae kadri tunavyozidi kuendelea, huduma hii itafika hadi vijijini, lakini kwa sasa hivi kama nilivyokuwa nimesema tume-delegate shughuli hii kufanywa na ,akatibu tawala wa Mikoa ambao wanafanya kazi hii vizuri sana. Niombe tu kwamba tushirikiane na hawa watu ambao sasa hivi tumewapa mamlaka haya kusimamia kwa niaba ya SUMATRA kutoa taarifa za ukiukwaji wa namna yeyote kama nilivyokuwa nimesema.

Mheshimiwa Spika, Lakini la (b) linafananafanana na haya niliyokuwa nimeyaeleza, swala la kupandisha nauli bila utaratibu, safari za kuondoka usiku, hay yote kusema ukweli ni ukiukwaji wa Sheria na kama nilivyosema kwamba ikijitokeza namna hiyo basi tutoe taarifa SUMATRA iweze ikachukua hatua. Mimi mwenyewe ni shaidi kwamba katika baadhi ya maeneo yangu ya Jimbo huko, safari zingine zilikuwa zinaanza kuanzia usiku wa manane saa 8 au saa 7. lakini tulitoa taarifa kwa wahusika na walichukua hatua na sasa hivi swala hilo limepita. Kwa hiyo, nitoe tu wito kwa wenzangu wengine wote waendelee kutoa taarifa kwa chombo hiki kinaweza kikawasimamia.

**SPIKA:** Swali fupi sana la nyongeza na la mwisho kwa swali hili Mheshimiwa Godfrey Zambi.

**MHE. GODFREY ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Nchi yetu ni kubwa na maeneo mengi mabasi hayaendi. Ninamfano mmoja kule Mbozi kuna barabara kutoka Mloo kwenda Kamsamba ambako mabasi hayaendi na usafiri mkubwa unaotumika ni wa malori. Kumekuwa na tatizo malori haya yanapobeba abiria askari wanayakamata magari haya na kutoza faini na kupelekea abiria kuhangaika sana njiani. Sasa Serikali inatoa tamko gani kwa maeneo yale ambayo mabasi hayaendi na usafiri unaotegemewa na wananchi ni malori peke yake?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba tatizo la usafiri hapa nchini bado linatutatiza sana kwa sababu baadhi ya maeneo kama alivyosema mabasi hayafiki lakini baadhi ya maeneo hata hayo malori hayafiki. Kwa hiyo suala hili wakati linaendelea kutafutiwa ufumbuzi na kuboresha huduma za usafiri nchini kote tuombe tu kwamba kwa vile vyombo ambavyo vinatumika sasa hivi tutaendelea kushirikiana na vyombo vinavyohusika angalau kutoa ahueni ya namna fulani ambayo itawawezesha wananchi kuweza kusafiri badala ya kuhangaishwa huku na kule.

Na. 201

**Kuuganisha Mji wa Tabora na Barabara ya**
**Mtwara- Dar es Salaam- Mwanza**

**MHE. AZIZA SLEYUM ALLY (K.n.y. MHE. SIRAJU JUMA KABOYONGA** aliuliza:-

Kwa kuwa, ujenzi wa barabara ya Mtwara- Dar es Salaam – Mwanza unaendelea vizuri na karibu utakamilika:

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa uhakika wa kuunganisha mji wa Tabora katika barabara hiyo kupitia Nzega umbali wa kilometa 115?

(b) Je, ni lini hasa ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami utaanza?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mbunge wa Tabora Mjini lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Serikali imekwishaanza maadalizi ya kuijenga barabara ya Tabora- Nzega yenye urefu wa kilometa 116 kwa kiwango cha lami kwa lengo la kuunganisha Mji wa Tabora na Barabara Kuu itokayo Dar es Salaam kuelekea Mikoa ya Ziwa, ikiwemo Shinyanga,

Mwanza, Mara na Kagera. Kazi ya upembuzi yakinifu wa barabara hii ilikamilika mwaka 2008 kwa gharama ya *Euro* 370,600. Usanifu wa kina unaofanywa na kampuni ya COWIAS ya Denmark kwa gharama ya shilingi bilioni 1.2 unaendelea na unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba 2009.Serikali imetenga shilingi bilioni 5.6/- katika mwaka wa fedha 2009/2010 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

**MHE. AZIZA SLEYUM ALLY**: Kwa kuwa Serikali imetenga pesa ndogo ya kutengeneza barabara hii kwa kiwango cha lami. Je, Waziri anaweza kutuhakikisha pesa hizo zitakazomalizia barabara hii zitapatikana lini? Swali la pili, kwa kuwa wakandarasi wengi huchelewa kukamilisha utengenezaji wa barabara kwa wakati. Haoni sasa barabara hii kuna haja ya kuweka wakandarasi wawili na barabara hii ianze kujengwa kuanzia Tabora kwenda Nzega?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, hili la kwanza kwamba fedha ni ndogo nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge ya kwamba fedha hizi ni za kuanzia na kama nilivyosema katika jibu la msingi hapa kwamba utaratibu wa maandalizi ya kuijenga barabara hii ulishaanza kwa kufanya upembuzi yakinifu pamoja na ufanifu. Sasa hizi fedha shilingi bilioni 5.6 zilizotengwa kwa mwaka huu wa fedha kwa sababu hizi ni kwa ajili ya mwaka huu mmoja wa fedha utagharamiwa kwa kulipa kwanza fedha za awali kwa mkandarasi na ujenzi wa tabaka la kwanza la barabara kwa km 15 na ujenzi wa tuta la barabara km 30. Kwa hiyo ni katika kipindi hiki cha mwaka huu wa fedha. Lakini tutaendelea kutenga fedha kila mwaka na kazi itakuwa inaendelea. Lakini katika suala la kwamba barabara hii au makandarasi wanachelewesha kazi hii sisi tutakuwa makini sana kuhakikisha kwamba kila fedha itakapotengwa mkandarasi anasimamiwa kwa karibu kuhakikisha kwamba barabara hii inajengwa kwa mujibu wa utaratibu wa uliokubalika. Suala la kwamba barabara hii ianzie Tabora kwenda Nzega Serikali imelizingatia hilo barabara hii itaanza Tabora kuelekea Nzega.

Na. 202

**Kukamatwa kwa Rais wa Sudan**

**MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN** aliuliza:-

Kwa kuwa hivi karibuni Mahakama ya Kimataifa ya Makosa ya Jinai ilitoa amri ya kukamatwa Rais wa Sudan kwa shutuma mbalimbali:-

(a) Je, shutuma hizo ni zipi?

(b) Tangu amri hiyo itolewe, ni Marais wangapi wameshapata amri kama hiyo na utekelezaji wake umekuwaje?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, Mbunge wa Kikwajuni, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, amri ya kukamatwa Rais wa Sudan Mheshimiwa Omar Hassan Ahmad Al Bashir, ilitolewa na Mahakama ya Kimataifa ya Makosa ya Jina *(ICC)* tarehe 04 Machi, 2009. Rais Omar Al Bashir anashutumiwa kuidhinisha na kuchochea makosa ya jinai chini ya Kifungu cha 25 (3) (a) cha Sheria iliyoanzisha Mahakama hii (au Mkataba wa Roma), ambayo ni:-

(i) Kuamrisha kwa makusudi uvamizi dhidi ya Raia wa Seudan waliokataa kujihusisha moja kwa na vita nchini Sudan; na uporaji mali ambayo ni makosa ya kivita chini ya Vifungu vya Sheria ya Mahakama ya *ICC.*

(ii) Mauaji, uangamizaji, kuhamisha raia kwa nguvu, utesaji au ukatili na ubakaji ambayo ni makosa dhidi ya binadamu chini ya vifungu mbalimbali vya Sheria ya Mahakama ya ICC.

Mheshimiwa Spika, chini ya Kifungu cha 58(1) cha Mkataba wa Roma, Mahakama iliona ni lazima kumkamata Rais Al Bashir sasa ili kuhakikisha kwamba:-

(i) Anasimama mbele ya mkondo wa sheria;

(ii) Hatazuia au kuhatarisha upelelezi unaoendelea kuhusiana na makosa ambayo anatuhumiwa kutenda; na

(iii) Hataendelea kuidhinisha au kuchochea utendaji wa makosa hayo.

(b) Mheshimiwa Spika, tangu amri hiyo itolewe, hakuna amri nyingine yoyote kama hii iliyotolewa kwa Rais mwingine yeyote alioko madarakani Barani Afrika na duniani kote. Rais Al Bashir hajakamatwa au kujisalimisha kwenye Makahama ya ICC hadi sasa.

**MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN:** Mheshimiwa Spika, nchi ya Israel nayo inafanya madhambi kama hayo kwa wananchi wa Palestine na hasa akina mama na watoto ambao hawana hatia. Je, huyo kiongozi wa Israel ni lini naye atatolewa hati kama hiyo naye akumbane na Mahakama kama hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Israel inawatendea vibaya wananchi wa Palestine.

Lakini Israel si mwanachama wa *ICC* na kutokana na hali hiyo hailazimiki kushirikiana na *ICC* katika kumpeleka kiongozi yoyote wa Israel kwenye Mahakama ya ICC. Kwa sababu Israel ni mwanachama wa Umoja wa Mataifa chombo chenye Mamlaka ya kumpeleka kiongozi yoyote wa Israel ambaye anatuhumiwa na makosa kama hayo ni Baraza la Usalama baada ya kupokea maombi kutoka kwa *prosecutor* wa *ICC.*

Kwa hiyo, baada ya kuridhika *prosecutor* wa *ICC* itabidi apeleke makosa ya aina hiyo ndipo apeleke kwenye maombi hayo kwenye Baraza la Usalama ili mtuhumiwa aweze kukabidhiwa kwa ICC. Lakini niseme tu Marekani ni Mjumbe wa kudumu wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa. Sasa tuelewe kweli Israel atakwenda? (*Makofi*)

**MHE. JOHN S. MALECELA**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Bara la Afrika katika miaka michache iliyopita liliteseka sana kutokana na askari Mamluki wakati huo wakiitwa kwa lugha ya kigeni *mercenaries* ambao wakiua na kutesa watu na wengi wao bado wako hai na wanaishi katika nchi ambazo ni wanachama wa ICC. Je, Serikali haioni umuhimu wa hao *mercenaries* kupeleka majina yao kwenye Mahakama hizo ili nao wakahukumiwa kama hivi wanavyosema Al-Bashir apelekwe?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Mahakama hii inashughulikia watu wote wale wenye maovu kama yalivyo ndani ya Mkataba wa Rome. Hawa *mercenaries* nao wanapaswa kupelekwa mbele ya Mahakama hii kwa ajili ya kukabili mkondo wa Sheria. Lakini basi lazima *prosecutor* atoe maombi kwa nchi husika ili hawa waliofanya maovu dhidi ya binadamu waweze kukabidhiwa kwa ICC. Lakini mpaka sasa haionekani *prosecutor* wa ICC ametoa ombi lolote kwa nchi zinazohusika.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika nashukuru. Kwa kuwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri yanaonesha wazi jinsi ambavyo Serikali yetu inatambua uhalali wa mashtaka dhidi ya Rais wa Sudan. Je, Serikali itakuwa tayari kumkamata pale ambapo atakuja Tanzania?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli *ICC* au *Procetor* wa *ICC* ametoa *warrant* ya kumkamata Ahmad Al Bashir, Rais wa Sudan ili akabiliane na mashitaka kwa mujibu aliyoyafanya.

Lakini niseme hivi, ni kweli nchi wanachama za *ICC* za Kiafrika na nchi nyingine lazima zishirikiane na *ICC* katika kufanya upelelezi na kuwakamata watuhumiwa na kuwakabidhi kwa *ICC.* Lakini kutokana na hali ilivyo sasa Rais Al Bashir akija Tanzania hatutaweza kumkamata. *(Makofi)*

Kwa sababu katika Mkutanoa wa *AU* uliyofanyika Silty Libya kuanzia tarehe 2 na 3 mwezi huu, iliazimiwa kule kwamba sasa nchi za Kiafrika kwa sababu ya kutothaminiwa maoni yake na Umoja wa Mataifa na Jumuiya ya Ulaya kwamba tungeomba suala la kukamatwa kwa Al Bashir lisogezwe mbele kwa sababu tuna matatizo ya usalama na amani katika Darfur, tungojee tumalize kule kwanza. Si Umoja wa Mataifa, si Jumuiya ya Ulaya iliyojibu ombi hilo la *African Union.* Kwa hivyo hata akija Tanzania kutokana na Azimio hatutaweza kumkamata na kumkabidhi kwa *ICC. (Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge ingawa muda wa maswali umefikia kikomo, lakini mtakumbuka tulikuwa na Hati za kuwasilisha tano, zimechukua muda. Kwa hiyo maswali mawili yaliyosalia tutayamaliza, tukianzia na hili la Wizara ya Ushirikiano la Afrika Mashariki linaloulizwa na Mheshimiwa Ally Khamis Seif, Mbunge wa Mkoani.

Na. 203

**Tanzania Zanzibar na Jumuiya ya Afrika Mashariki**

**MHE. SALIM ABDALLAH KHALFAN (K.n.y. MHE. ALI KHAMIS SEIF)** aliuliza:-

Kwa kuwa jumuiya ya Afrika Mashariki ilipoanzishwa mwaka 1967 Tanzania Zanzibar ilikuwa mwanachama:-

Je, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ingepata hasara gani kama Zanzibar ingalikuwa mwanachama wa Jumuiya hiyo sasa?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** alijibu :-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Ali Khamis Seif Mbunge wa Mkoani, napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama tunavyojua Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zinaongozwa kwa mujibu wa Katiba na Sheria. Ibara ya 4, Ibara ndogo ya 3 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inatamka kwamba:

Kwa ajili ya utekelezaji bora wa shughuli za umma katika Jamhuri ya Muungano, na kwa ajili ya mgawanyo wa madaraka juu ya shughuli hizo baina ya vyombo vinavyotajwa katika iabara hii, kutakuwa na Mambo ya Muungano kama yalivyooredheshwa katika Nyongeza ya kwanza iliyoko mwishoni mwa Katiba hii, na pia kutakuwa na mambo yasiyo ya Muungano ambayo ni mambo mengine yote yasiyo

Mambo ya Muungano. Katika orodha hiyo iliyotajwa hapo juu masuala ya Mambo ya Nchi za Nje ni miongoni mwa masuala ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo kwa ruhusa na kwa niaba ya Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ali Khamis Seif kama ifuatavyo:-

Mwaka 1967 Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Jamhuri ya Kenya na Jamhuri ya Uganda zilitia saini Mkataba wa kuunda Jumuiya ya Afrika Mashariki ambapo Tanzania tuliingia katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kama Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (ambayo inajumuisha Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar).

Mheshimiwa Spika, ili kuzingatia kuwa maslahi ya pande zote mbili za Muungano yanazingatiwa kikamilifu Serikali zetu, yaani Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar huhusishwa kikamilifu katika shughuli zote za Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, ikiwa ni pamoja na katika mikutano ya kisekta, majadiliano mbalimbali katika Jumuiya na uandaaji wa sera, mikakati na programu mbalimbali za Jumuiya.

Mheshimiwa Spika, kwa kutofuata utaratibu wa sasa, hasara ambayo ingepatikana ni uvunjaji wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo tumeapa kuilinda. Vilevile hasara nyingine ambayo ingepatikana ni kudhoofisha umoja wetu.

Mheshimiwa Spika, Mataifa mengine makubwa Duniani yenye mfumo kama wa kwetu yanafuata utaratibu kama tunaofuata kushiriki katika masuala ya kimataifa ili kuimarisha umoja wao na kuwa na sauti na ushawishi mkubwa katika masuala ya kimataifa.

**MHE. SALIM ABDALLAH KHALFAN:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswala mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza, kama Zanzibar ingelikuwa mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Tanzania ingekuwa na Wabunge 18 katika Jumuiya hiyo.

Je, Tanzania haioni kwa kutokuiruhusu Zanzibar kuingia kwenye Jumuiya hiyo ya Afrika Mashariki imepunguza nguvu zake za maamuzi katika Jumuiya hiyo ya Afrika Mashariki? *(Makofi)*

Swali la pili, kwa kuwa Katiba ndiyo iliyoizuia Zanzibar kuingia kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki, na hivyo kupunguza nguvu za maamuzi kwenye Jumuiya hiyo.

Je, Serikali haioni sasa kwa umuhimu wa kuongeza nguvu Jumuiya hiyo ya Afrika Mashariki na kwa maslahi mengineyo kwa pande mbili za Jamhuri ya Muungano ya Tanzania. Ipo haja sasa ya kuleta marekebisho ya Katiba ili Zanzibar nayo iingie kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mhesihmiwa Spika, kama nilivyokwishakusema awali kwamba upo umuhimu mkubwa wa kuendelea kuheshimu na kulinda Katiba ambazo tumeapa kuziendeleza. Kama nilivyosema kwamba hata mataifa mengine makubwa yanafuata utaratibu wa kwetu, mfano kama Marekani, *United Kingdom*, *UAE* na wengine wanaufuata utaratibu huu kwa sababu ya kujenga nguvu zaidi. Tutakapoingia kama nchi mbili tutaongeza nyongeza ya malipo. Hivi sasa kulipia kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa mwaka ni zaidi ya dola milioni 5. Kwa maana tukiongeza Zanzibar pale unalipia hizo. *(Makofi)*

Kwa hiyo hayo unayoyafikiria unatuongezea gharama na mzigo zaidi. Jambo la msingi ni kupeleka hoja sahihi na kwa hakika kujitayarisha vizuri katika kutetea maslahi ya nchi yetu kwa manufaa ya pande mbili za Muungano wetu. *(Makofi)*

Na. 204

**Tatizo la Uvujaji wa Mitihani nchini**

**MHE. USSI AMME PANDU** aliuliza:-

Kwa kuwa mara nyingi kumetokea uvujaji wa mitihani na kusababisha baadhi ya mitihani kuahirishwa isifanyike na kusababisha usumbufu mkubwa kwa watahibniwa wa Taifa kwa ujumla:-

(a) Je, Serikali inasema nini kuhusiana na tatizo hili kubwa nchini?

(b) Je, kuendelea kutowachukulia hatua wale wanaovujisha mitihani siyo sawa na kuwalinda wahalifu hao?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ussi Amme Pandu, Mbunge wa Mtoni lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inasikitishwa saana na matukio ya uvujaji wa m itihani kwani ni jambo linalodhoofisha juhudi za Serikali za kutoa na kuboresha elimu nchini. Tatizo hilo linatokana na ukosefu wa maadili kwa baadhi ya watu wanaohusika na uendeshaji wa Mitihani katika hatua mbalimbali.

Serikali imekua ikichukua hatua za kuimarisha usalama wa mitihani na kupunguza mianya ya uvujaji wa matukio ya aina hiyo yanapojitokeza.

Aidha katika bajeti itakayowasilishwa hapa Bungeni, Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kunuua mitambo mipya ya kuchapa mitihani na mitambo ya *CCTV* ili kudhibiti nyendo zote zinazofanyika ndani ya Ofisi za Baraza la Mitihani.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikiwachukulia hatua wote wanaobainika kusababisha uvujaji wa mitihani. Kuhusu mtihani uliovuja wa *Basic Mathematics* wa Kidato cha Nne 2008, Serikali iliunda Kamati ya Uchunguzi kubaini chanzo cha uvujaji na kupendekeza namna ya kuziba mianya ya uvujaji wa mitihani.

Kutokana na matokeo ya uchunguzi, maofisa wanne wa Baraza la Mitihani la Tanzania waliobainika kufanya uzembe katika kusimamia taratibu za mitihani wameachishwa kazi na hatua zaidi zinaendelea kuchukuliwa kama ambavyo Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Elimu atakavyoeleza kwenye hotuba yake.

**MHE. USSI AMME PANDU**: Ahsante Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kumwuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tatizo la uvujaji wa mitihani ni la siku nyingi na limekuwa ni tatizo sugu. Sasa pamoja na hatua zinazochukuliwa na Serikali za kuwafukuza kazi wale ambao wamevujisha mitihani hiyo. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri haoni sasa adhabu hiyo ni ndogo na kama kuna uwezekano wakaongeza adhabu hiyo hata kufungwa jela? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, kwa kusema ukweli na kwa dhati, nimeeleza kwenye jibu la msingi kwamba hatua za awali baada ya uchunguzi imebainika kwamba waliohusika wameachishwa kazi baada ya hapo Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana kama hotuba yake atasema na ili kufuata Sheria ni lazima watu hawa watapaswa kupelekwa Mahakamani. Maana hatuwezi sisi kusema tunawafunga mwaka mmoja, au siku mbili kwa kigezo kipi maana bahati mbaya hatuna Mahakimu wala Wathamini wa kuweza kujua hasara iliyopatikana kwenye Serikali. Naomba tuvute subira. *(Makofi)*

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Ahsante Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wanaoshughulika na uchapaji wa mitihani wanaingia katika sehemu za uchapaji na simu za mikononi, je Serikali haioni kwamba simu za mikononi zinasaidia kuchangia kutuma maswali kwa njia ya ujumbe kwa kutumia simu hizo?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, si jambo la kawaida watahiniwa, na wanaochapisha mitihani kuingia na simu za mkononi. Naomba tu niseme bayana kwamba Mheshimiwa Spika, ni vizuri tukaandaa utaratibu pengine tukawachukua, Kamati yetu tukawaonyesha namna Baraza la Mitihani linavyoendesha shughuli zake. Tunajitahidi sana sana kuwa waangalifu na kuziba mianya. Lakini ikumbukwe jamani, binadamu aliyeumbwa na Mwenyezi Mungu akapewa kichwa kikafunikwa na moyo wake dhamira yake huwezi ukaijua. Kila kukicha teknolojia zinaongezeka, tumeagiza hapa kwamba katika bajeti ya

mwaka huu na ninawaomba mtupitishie bila mizengwe, bila vikwazo ili tuwapatie Baraza la Mitihani fedha ya kutosha waweze kuweka hivyo vitu ambavyo wenzetu wanatumia. Tutamaliza hii kero lakini sote kwa pamoja humu ndani, hebu tuhubiri uaminifu na uadilifu katika majukumu na uwajibikaji wetu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umepita na maswali yamekwisha. Matangazo, nitaanza na wageni. Leo tunao wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ambao ni Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Bi. Salome Sijaona, yule pale ahsante sana. Maafisa Waandamizi 14 ambao sikupewa majina wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Naomba wasimame tafadhali. Ahsante sana. *(Makofi)*

Karibuni sana kusikiliza mjadala wa Wizara yenu. Wageni wa familia wanaongozwa mke wake Mheshimiwa Waziri Chiligati ambaye ni Mwalimu Glena na watoto wawili pamoja na Shemeji na dada yake Waziri. Wale pale karibuni sana. Wapo pia wageni wa Mheshimiwa Waziri Chiligati ambao wanatoka Jimboni kwake, kule Manyoni. Manyoni Mashariki. Wageni hao ni Kamati ya Siasa ya Wilaya CCM wakiongozwa na Ndugu Hussein Masao, Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya ya Manyoni. Yule pale. Karibuni sana, wageni wetu kutoka Manyoni karibuni sana. *(Makofi)*

Pia wapo Waheshimiwa Madiwani wanne wakiongozwa na Mheshimiwa Mosses Matonya, Mwenyekiti wa Halmashauri. Wale pale. Karibuni sana Waheshimiwa Madiwani pamoja na Mwenyekiti. Yupo pia Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Manyoni, Ndugu Fotunata Malya. Naomba asimame, aah yeye yuko huku. Ahsante sana. Wapo Makada 12 wa Chama cha Mapinduzi kutoka Manyoni ambao nao sikutajiwa jina, wale Makada kutoka Manyoni, wale pale. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo pia Makada 16 kutoka CCM Makao Makuu hapa Dodoma. Wale pale, ahsante sana. Karibuni sana. Wageni wa Mheshimiwa Felix Mrema, wawili ni Bi. Rehema Karia, Katibu wa UWT Ngarenaro. Yule pale ahsante na Godwin Malisa na Jeremiah Sumari. Jeremiah Sumari tena, wawakilishi wa *National Housing Flates* za Kibla Levolosi na Ngarenaro. Hawa ni wawakilishi wa *National Housing.* Karibuni sana, karibuni sana, watetezi wa wapangaji. Wapo wageni wa Mheshimiwa Lucas Selelii, ambao ni Bi. Rose Selelii, mkewe Mheshimiwa Mbunge. Ahsante sana.

Hatujamwona! Aah yule pale, yule kule, mkono wangu wa kushoto. Waheshimiwa Wabunge wanaomba usimame tena. *(Kicheko/Makofi)*

Ahsante sana. Mnajua Shemeji huyu, Mheshimiwa Lucas Selelii ni mmoja wa Wabunge ambao tunawapenda sana humu Bungeni, ndiyo maana. Wapo pia Madiwani 11 kutoka Nzega na Katibu wa Madiwani. Wale Madiwani kutoka Nzega. Wale pale. Ahsante sana. *(Makofi)*

Hii Nzega Madiwani wote ni wanawake. Basi si mbaya, naona hawa badala ya *fifty, fifty* wao wamefanya mia kwa mia. Naelekezwa hapa kwamba ni wageni wa Wabunge wote wa Mkoa wa Tabora, karibuni sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Benson Mpesya ni Ndugu Mbuna ambaye ni Mkuu wa Chuo cha Wafanya Kazi, Mbeya. Ahsante sana. Mgeni wa Mheshimiwa Monica Mbega, Mbunge wa Iringa Mjini na Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro. Ni ndugu Thomas Ngawaiya, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi Mkoa wa Kilimanjaro. Karibu sana. *(Makofi)*

Kama mnavyofahamu Mheshimiwa Ngawaiya alipata kuwa Mbunge hapa, kuna fununu kwamba yupo katika harakati za kutaka kurudi. Sasa sijui anamtishia nani. Basi hayo mtaelewana huko huko Kilimanjaro. *(Makofi)*

Wapo akina mama 50, naona hawa wametoka hawa, kutoka KKKT Dayosisi ya Kaskazini Mashariki Lushoto. Niliona walikuwa pale ambapo vijana wameingia pale. Tunawakaribisha hata hivyo. Wako wanafunzi 17 kutoka Chuo cha Taaluma za Hosteli na Utalii, Dar es Salaam. Ndiyo hawa wameingia ahsante sana. *(Makofi)*

Sekta ya Utalii inawategemea sana, tunawaombeni mfanye vizuri katika masomo, mfanye bidii ili tuongeze wanataaluma katika masuala ya utalii. Karibuni sana pamoja na Wakufunzi. Wako wanafunzi 56 kutoka shule ya Msingi Kamtui Kidatu. Nadhani wamekosa nafasi watakuwa katika Ukumbi ule wa *Basement.*

Matangazo ya kazi. Mheshimiwa William Shelukindo, Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, anahitaji Wajumbe wote wa Kamati ya Nishati na Madini mkutane Ukumbi Na. 231 saa 8 mchana. Kwa hiyo, saa 8 mchana Ukumbi Na. 231 Wajumbe wa Kamati ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Haroub Masoud, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, anaomba Wajumbe wote wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii mkutane katika Ukumbi wa Pius Msekwa B, saa 7 mchana. Kwa hiyo, saa 7 mchana Ukumbi wa Pius Msekwa B, Kamati ya Maendeleo ya Jamii.

Waheshimiwa Wabunge matokeo ya michezo mbalimbali iliyochezwa *weekend* ni kwamba kama ilivyo ni nadra sana timu yetu kufungwa kwa bahati mbaya. Kutokana na nusu ya timu walishiriki katika dansi siku ya Ijumaa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Bendera siku nyingine tuangalie tusiwe na halfa ya dansi halafu siku ya pili kucheza mpira. Kwa hiyo, kutokana na udhaifu huo timu ya *TBL* iliifunga timu ya Bunge magoli matatu kwa moja. Lakini jambo la kufurahisha ni kwamba kwenye timu ya Netiboli tuliwafunga *TBL* 13 kwa 7 kwenye kuvuta ndiyo ndiyo ushindi mkubwa kabisa. Kama mnavyojua timu yetu ilikuwa na Mheshimiwa Marombwa, Mheshimiwa Selelii, Mheshimiwa Msindai, Mheshimiwa Mwinchoum Msomi na kadhalika. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi nilikuwapo pale uwanjani, ilikuwa siyo kuvuta, sijui uite kuvuta kamba maana yake walipoanza walivutwa moja kwa moja *TBL* waliporejea upande wa pili, pia wakavutwa moja kwa moja. Vivyo hivyo hivyo timu ya kuvuta kamba ya

wanawake nayo tulipata ushindi kamili, walivutwa mara mbili. Nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwijage ananikumbusha kwamba kuna wageni wa Chama cha CUF kutoka Bukoba ambao ni Amatusi Makubo, naomba asimame tafadhali. Domina Richard, Jeston Kamauza na Venanti Rwegasira. Karibuni sana, karibuni sana, mmetoka mbali sana Bukoba, karibuni sana. *(Makofi)*

Huo ndiyo mwisho wa matangazo. Sasa ninalo tamko la mwongozo. Nianze kuipunguza hii miongozo hii. Huu ni ufafanuzi wa Spika kuhusu madai ya kutumia lugha ya kuudhi Bungeni. *(Makofi)*

## UFAFANUZI WA SPIKA

**SPIKA:** Ufafanuzi wa Spika, kuhusu madai ya kutumia lugha ya kuudhi Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, mara kadhaa katika Mkutano huu na hata iliyopita Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakisimama na kuomba mwongozo wa Spika kwa kumtaka Mbunge anayechangia afute kauli yake kwa kuhisi kuwa kauli hiyo ni ya kuudhi na haistahili kuwa lugha ya kibunge. Kwa kuwa malalamiko haya yamekuwa yakijirudia rudia na kufikia hatua ya kupoteza maana kamili ya lugha ya kuudhi *(unparliamentary language)*, nimeamua nitoe ufafanuzi na mwongozo kuhusu suala hili.

Waheshimiwa Wabunge**,** ufafanuzi kuhusu lugha ya kuudhi, katika Mabunge mengi duniani Kanuni za mijadala zinazuia matumizi ya lugha za kuudhi, kwa maneno mengine, lugha isiyo ya Kibunge *(unparliamentary language.)* Katika Kanuni za Bunge letu, Kanuni ya 64 inaainisha mambo yasiyoruhusiwa Bungeni katika mijadala.

Miongoni mwa mambo yasiyoruhusiwa ni kutumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha mwingine - Kanuni ya 64(1)(g). Uamuzi kwamba maneno gani ni ya kuudhi na yapi siyo ya kuudhi yako ndani ya mamlaka ya Kiti, kwa kuzingatia hali halisi ya mjadala, hulka ya Mbunge mchangiaji na utamaduni wa Mabunge yenye mfumo kama wetu.

Haya yote matatu lazima yazingatiwe. Mathlani tumekuwa na Wabunge ambao wana hulka kama ya uchekeshaji. Sasa anapotamka hata kama neno linakuwa gumu kidogo Kiti hakiwezi kusema huyo ameudhi. Ni jambo la kawaida kwamba katika mazingira ya pekee pale ambapo mjadala unapopamba moto mzungumzaji anaweza akajikuta akitumia maneno makali. Waheshimiwa Wabunge pamoja na Waheshimiwa Mawaziri ni binadamu na wanaweza kuwa na hisia kali katika mambo wanayojadili.

Kwa hiyo, kutafsiri Kanuni hii inayozuia “maneno ya kuudhi” kwa wigo mfinyu kuna hatari ya kuminya ule uhuru wa majadiliano uliopo katika Ibara ya 100 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Isitoshe Bunge ni uwanja wa siasa za ushindani

ambapo katika kutetea maslahi ya kiuwakilishi, migongano ya mitazamo na hata ya lugha haiwezi kuepukwa. *(Makofi)*

Ukiwataka Waheshimiwa Wabunge wazungumze Bungeni mithili ya mashahidi Mahakamani, utakuwa umeiondoa ladha yote ya mijadala Bungeni. Ipo mifano kadhaa katika Mabunge mbalimbali duniani ambapo katika mazingira hayo niliyoyazungumzia, Wabunge wamenukuliwa wakitoa maneno makali ambayo kwa tafsiri finyu unaweza kuyaita ni ya maudhi au hata ya matusi. Mathalani, kutoka Bunge la New Zealand baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wa huko katika nyakati mbalimbali wamenukuliwa katika *Hansard* yao wakitamka yafuatayo bila kuchukuliwa hatua: -

· Mwaka 1949 Mbunge mmoja aliwaita Mawaziri kuwa ni kwa Kiingereza *"Hypnotized rabbits."* (yaani sungura walioduwazwa na wasio na maamuzi ya kujitegemea); ndiyo anawaita hivyo Mawaziri.

· Mwaka 1963 Waziri mmoja alimwita Mbunge wa kike kwamba, kwa Kiingereza ***"****a vicious woman"* (mwanamke katili).

· Mwaka huo huo, Mbunge mmoja alimwelezea Mbunge mwingine kuwa ni kama nanukuu *"a tired snail returning home from a funeral."* (Konokono aliyechoka akirejea kutoka kwenye mazishi); *(Kicheko/Makofi)*

· Mwaka 1966 Mbunge mmoja alikuwa anachangia hoja, baadhi ya Wabunge wenzie walimpigia kelele na kumzonga kuwa amalize na kukaa chini anapoteza wakati. Yeye akawajibu *"shut up yourself, you great ape"* (funga mdomo we mwenyewe, sokwe mkubwa). *(Makofi)*

Katika Bunge la *"House of Commons"* London , Uingereza mijadala inapopamba moto maneno makali hutumika, kwa mfano karne iliyopita Mbunge Benjamin Disraeli alimshambulia Waziri Mkuu Sir Robert Peel, kama ifuatavyo: -

Nanukuu, "*I find that for between thirty and forty years the right honourable gentleman has traded on the ideas and intelligence of others (loud cheering)* Ndiyo *Hansard.*

> *"His life has been a great appropriation clause (shouts of laughter and cheers). He is a burglar of others' intellect … There is no statesman who has committed political party larceny on so great a scale (Renewed laughter)." (W.F. Monypenny 1912, Vol. II, 353)." (Kicheko).*

Iko kwenye ukurasa *Volume II, 353* ya *Hansard* ya Uingereza. Tafsiri yake ile, huyu mtu anamsema Waziri Mkuu, anasema hivi:-

> *"Najua kwamba kwa miaka kati ya 30 na 40 Mheshimiwa ameishi kwa kutumia mawazo na akili za wenzake (shangilio la nguvu). Maisha yake yote yamekuwa ni ya ubinafsishaji wa maoni ya wenzie (vicheko na*

> *kushangiliwa). Hakuna mwanasiasa ambaye amekuwa hodari zaidi kuliko huyu katika uhalifu wa wizi mkubwa wa ajenda za kisiasa. (Vicheko tena).”*

Waheshimiwa Wabunge, kwa mifano hiyo, sio nia yangu kuwashawishi mtumie maneno kama hayo au maneno mengine makali na yanayoweza kuumiza wengine. Hata hivyo, kama nilivyowahi kuwaasa siku za nyuma, mwanasiasa hasa Kiongozi anatakiwa awe na ngozi ngumu inayohimili mikwaruzo ya maneno makali ya siasa bila kuchubuka kwa urahisi! Aidha, katika Mkutano huu maneno yaliyosemekana ya kuudhi humu Bungeni si makali zaidi kuliko hayo niliyonukuu na kwa hiyo hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa kwa wahusika wala hawakutakiwa kuyafuta.

Kwa mfano, kumsema Mbunge fulani kwamba kasema ovyo ovyo au hata Waziri fulani alaaniwe kwa kujipendelea, haifikii kiwango cha athari cha kutakiwa maneno hayo yafutwe. Kikubwa hapa, Kiti huangalia ikiwa ipo nia mbaya na ya dhati ya kudhalilisha. Je, anayoyaongea kwa nia ya dhati, anataka kumdhalilisha mwingine? *(Makofi).*

Jambo la pili ni kwamba, Wenyeviti wa Bunge *(Presiding Officers)* ni Wasaidizi wa Spika na Naibu Spika katika kuendesha Shughuli za Bunge. Wanapokalia Kiti cha Spika na kuendesha Vikao vya Bunge wanafanya hivyo kwa niaba ya Spika na kwa wakati huo wanakuwa wanatekeleza mamlaka ya Spika na wanastahili heshima ile ile anayopewa Spika na Naibu Spika. *(Makofi).*

Kwa mujibu wa Kanuni ya 67(2) Spika anaposimama wakati Mbunge anachangia, Mbunge huyo anatakiwa kuketi mahali pake na Bunge litabaki kimya ili Spika aweze kutoa maelekezo au taarifa anayokusudia kuitoa. Aidha, Spika anawajibika kutilia nguvu Kanuni za Bunge na anaweza kumtaka Mbunge yeyote anayekiuka utaratibu ajirekebishe. Kitendo cha Mbunge kuendelea kusimama na kubishana na Kiti ni kudharau na kudhalilisha Kiti pamoja na Bunge na kinatoa taswira mbaya kwa jamii. *(Makofi).*

Kanuni zetu zimeweka wazi kuwa Mbunge yeyote ambaye hataridhika na uamuzi wa Spika anaweza kuwasilisha sababu za kutoridhika kwake kwa Katibu wa Bunge ambaye ataitisha Kamati ya Kanuni, kupitia malalamiko yake. Utaratibu wa kushughulikia malalamiko hayo pia umefafanuliwa katika Kanuni ambapo wanapolalamikiwa Spika au Naibu Spika hawashiriki katika Kikao husika, wanabaki Wabunge tu, kuamua.

Kwa kuzingatia misingi hiyo miwili niliyoieleza, tarehe 24 Juni, 2009 Mheshimiwa Kabwe Zitto, hakuathiri Kanuni yoyote kwa kutamka kwamba Mheshimiwa Waziri fulani alijibu “ovyo ovyo”. Tatizo hapa ni kwamba Mheshimiwa Zitto aliendelea kuyakaidi Mamlaka ya Kiti kwa kauli. Kwa hilo, ninamwagiza amwombe radhi Mheshimiwa Mwenyekiti, Zubeir Ali Maulid, humu Bungeni. Amwombe radhi humu Bungeni na tukifanya hivyo, shauri hili litakuwa limefungwa. *(Makofi).*

Uamuzi huu wa Spika, umetolewa tarehe 13 Julai, 2009. Ahsanteni sana Waheshimiwa. Mutagawiwa nakala ili iwe ni mwongozo. Katibu kwa shughuli inayofuata. *(Makofi).*

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mwongozo wa Spika, Mheshimiwa Yahya Kassim Issa.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 68 (7).

Mheshimiwa Spika, tumesikia maelezo yako, lakini Tanzania tuna silika zetu na tuna taratibu zetu na ustaarabu wetu. Lakini kuna nchi kuna mambo ukifanya hata kwamba uko katika jamii, inakuwa ni jambo la kawaida. Bunge hili linaangaliwa sio Tanzania tu, lakini nchi nyingi kwa yale ambayo tunayafanya na Tanzania tuna sifa ya ustaarabu wa mambo yetu. Sasa hii kauli uliyoitoa, wewe ni Kiongozi, lakini hatuoni kwamba sasa tunavuka nje ya maadili yetu? *(Makofi).*

Mheshimiwa Spika, kwamba mtu anainuka na amevunja heshima, na Watanzania wote wanatuona na wanaelewa lugha ile aliyoitumia na wanaelewa kwamba lugha ile si ya kistaarabu na ni lugha potofu ndani ya Bunge. Na sisi ndio tunataka kuonesha mfano wakati tuko katika chombo hiki ambacho wananchi wote wanakiamini katika mwenendo wake. *(Makofi).*

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa nataka maelezo zaidi kwa kweli, kuhusu suala hili tuzidi kupata Mwongozo na tuzidi kulifikiria.

**SPIKA:** Inashangaza Mheshimiwa, huu ndio Mwongozo nimekwishautoa. Sasa huwezi kuniuliza Mwongozo mwingine. Mimi nimesema yote hayo kwamba tunatazama hulka ya Mbunge, hali ya mjadala ilivyo; kuna watu wanafanya masihara na watu wanacheka tu, ingawa mtu angesema maneno hayohayo yangekuwa hayakubaliki katika jamii.

Sasa hayo yote yanatamwa ndio tunafikia hapo. Mifano niliyoitoa ni kuwaonesheni ukomo wa tamaduni nyingine, lakini ni kweli kabisa sisi tuna tamaduni zetu na Kiti kitayazingatia hayo. Lakini baadhi yenu mnataka mtu akiwa Mbunge anachangia asioneshe hisia zake, asikasirike, sasa haiwezekani hiyo. Sisi tunaozungumza ni binadamu. (Makofi/Kicheko).

Nimetoa hapa kwamba, anayetazamia kwamba mazungumzo humu yawe kama ya mashahidi Mahakamani, basi hapa sio mahali pake. Anatakiwa atafute kazi nyingine tu maana siasa ina mikiki mikiki na huwezi kuvumilia, kama jambo kweli umelizungumza

mwaka wa kwanza, halikutekelezwa, mwaka wa pili, unakaribia kupigiwa kura, halafu uzungumze tu kama vile ni jambo la kawaida, samahani, hamna kitu namna hiyo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, huu ndio Mwongozo na mtagawiwa. *(Makofi/Kicheko).*

Katibu, kwa hatua inayofuata.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2009/2010
### Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa juhudi zake za kusimamia uchumi wa nchi yetu. Aidha, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa DR. Ali Mohammed Shein Makamu wa Rais na Waziri Mkuu Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, kwa juhudi zao za kusimamia amani, kuendeleza umoja wa kitaifa, kukuza uchumi na kupambana na ufisadi nchini.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Manyoni Mashariki kwa kunipa ushirikiano mkubwa katika shughuli mbalimbali tulizozianzisha na kuzitekeleza kwa mafanikio makubwa na kwa kunivumilia wanapokuwa hawanioni Jimboni wakati nikitekeleza majukumu ya Kitaifa.

Vilevile, napenda kumpongeza Mheshimiwa Lolensia Bukwimba kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Busanda, Mchungaji Levison Mwanjale, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini na Mheshimiwa Oscar Mukasa kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Biharamulo Magharibi. Ushindi walioupata umeonyesha imani kubwa waliyonayo wananchi kwao binafsi na kwa Chama cha Mapinduzi.

Aidha, nampongeza Mheshimiwa Charles Nyanguru Mwera kwa kuchaguliwa kuwa mbunge wa Jimbo la Tarime kupitia *CHADEMA.* Pia, napenda kutoa salamu za rambirambi kwa familia za Wabunge wenzetu na Watanzania wote waliopoteza maisha yao kwa ajali na sababu mbalimbali nchini, Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi, Amen. *(Makofi).*

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru kwa dhati Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mbunge wa Kongwa kwa ushirikiano na ushauri wao ambao umeiwezesha Wizara hii kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeendelea kutekeleza shughuli zake kwa kuzingatia Sera na Sheria za ardhi. Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2025, Malengo ya Milenia, *MDGs*, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini, *MKUKUTA*, na Ilani ya Uchaguzi ya *CCM* ya Mwaka 2005. Mambo ya msingi yaliyoainishwa katika miongozo hiyo yanalenga kuboresha maisha ya wananchi; kudumisha amani, utulivu na umoja; utawala bora; kujenga uchumi madhubuti na endelevu; kuboresha afya; mazingira na makazi endelevu.

Wizara yangu imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia miongozo hiyo ikiwemo kubadilisha ardhi kutoka hali ya mtaji mfu na kuwa mtaji hai ili iweze kuwasaidia wananchi waondokane na umaskini. Mabadiliko haya yatapatikana kwa kuongeza kasi ya kupima ardhi Mijini na Vijijini na kuwamilikisha wananchi.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya *CCM* ya Mwaka 2005. Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005 imetoa maelekezo mbalimbali kuhusu utekelezaji wa majukumu katika Sekta ya Ardhi, ili kuwezesha ardhi itumike kikamilifu kama nyenzo na mtaji kwa lengo la kujiletea maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Maeneo muhimu yanayohusika ni kama ifuatavyo:-

(i)Mheshimiwa Spika, Kifungu 42 (a). Kuhusu utekelezaji wa Mkakati wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania, *MKURABITA*, kwa lengo la kuwawezesha Watanzania kurasimisha ardhi na nyumba zao ili waweze kuzitumia kupata mikopo ya benki na mifuko mingine ya fedha inayokopesha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu urasimishaji wa ardhi na nyumba nchini, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri za miji, Wananchi na Wadau mbalimbali imetambua milki za nyumba kwenye maeneo yaliyojengwa kiholela katika Miji ya Mwanza nyumba 6,053, Dar es Salaam 264,360, Tanga 3,945, Moshi 1,019 na Dodoma 5,651. Idadi hii inafanya milki za nyumba zilizotambuliwa kuanzia Desemba 2005 hadi 2009 nchini kuwa 281,028.

Kati ya milki hizo, leseni za makazi 86,953 zimeandaliwa na kutolewa kwa wananchi kuanzia mwaka 2005 hadi Juni 2009. Leseni hizo zinaimarisha usalama wa milki, zinatumika kama dhamana, na zinarahisisha uhamisho wa milki. Aidha, wananchi kwa kutumia leseni za makazi wamepata mikopo kutoka taasisi mbalimbali za kifedha za *CRDB, NMB, DCB, Azania Bank Limited, Barclays Bank, PRIDE* na mfuko wa pembejeo hasa baada ya muda wa uhai wa leseni kuongezwa kutoka miaka miwili hadi mitano. Wizara inaendelea kuhamasisha wananchi waendelee kushirikiana na mamlaka zinazohusika katika kutambua milki hizo ili leseni nyingi zaidi ziweze kutolewa na wazitumie kupata mikopo kwa ajili ya kuanzisha miradi ya maendeleo.

kwa lengo la kurasimisha ardhi ya kijiji, Wizara yangu ikishirikiana na Halmashauri za Wilaya imeendeleza jitihada zake za kutoa hati za kumiliki ardhi kimila. Hati hizi zina hadhi sawa kisheria na hati zinazotolewa katika ardhi ya jumla *(granted right of occupancy)*. Hati hizi zinasajiliwa na kuhifadhiwa katika Masjala za wilaya na vijiji ambazo zimeendelea kukarabatiwa au kujengwa. Kati ya mwaka 2005 na Juni 2009 jumla ya masjala za wilaya 10 na 121 za vijiji zilikarabatiwa au kujengwa na jumla ya hati milki za kimila 19,073 zilitolewa.

Vile vile vyeti vya ardhi ya vijiji 1,487 vilitolewa (Jedwali Na.1). Hati za kimila pia zimeanza kutumiwa kama dhamana kwa wakulima kupata mikopo kutoka kwenye mabenki, mfuko wa pembejeo na taasisi zingine za kifedha.

(ii)Mheshimiwa Spika, Kifungu 42( b). Kuendeleza kwa nguvu mpya kazi inayofanywa na Halmashauri za Wilaya katika kutambua mipaka ya vijiji na kuvipatia vyeti vya kumiliki ardhi ili matumizi ya ardhi yawe endelevu nchini kote.

Mheshimiwa Spika, sambamba na kurasimisha ardhi mijini, kazi ya kupima mipaka ya vijiji inaendelea. Kati ya mwaka 2005 hadi Juni 2009 jumla ya Vijiji 4,390 vimepimwa idadi hii inafanya jumla ya vijiji vilivyopimwa nchini kuwa 9,500 na kubakiwa na vijiji ambavyo bado havijapimwa 1,500 nchini kote. Aidha, katika kipindi hicho Wizara yangu imetayarisha Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi ya Vijiji 582 katika Wilaya 30.

(iii)Mheshimiwa Spika, Kifungu 42 (c). Kuendelea kurahisisha taratibu za upatikanaji wa hatimiliki za ardhi.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imejiwekea mkakati wa muda mrefu wa kuboresha taratibu za upatikanaji wa hatimiliki za ardhi mijini na vijijini. Hatua hizo ni pamoja na kuanzisha Ofisi za Ardhi za Kanda tano (5) katika Miji ya Dar es Salaam, Mbeya, Mwanza, Moshi na Dodoma ambapo mchakato mzima wa kuandaa hati unaanza na kukamilika katika ngazi ya Kanda; kuondoa sharti la kupewa Barua ya Toleo (Letter of Offer) kabla ya kuandaliwa hatimiliki; kuboresha kumbukumbu za ardhi na kutumia mifumo ya kompyuta katika kutoa hatimiliki za ardhi. Hatua zote hizi zinalenga kuhakikisha kwamba hatimiliki ya ardhi inapatikana ndani ya siku 180. Vilevile, kati ya Desemba 2005 hadi Juni 2009, jumla ya hatimiliki za ardhi mijini 40,510 zilitolewa

(iv)Mheshimiwa Spika, Kifungu 42 (d). Kupima na kutayarisha ramani za msingi za nchi yetu kwa ajili ya kupanga mipango mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inaendelea na jukumu la kutayarisha ramani za msingi za nchi kwa lengo la kuwezesha kuandaa na kutekeleza mipango mbalimbali ya maendeleo ikiwemo Mipango Kabambe ya Miji, umwagiliaji, utalii, Matumizi Bora ya Ardhi, mazingira n.k. Tangu mwaka 2005 hadi Juni 2009 ramani za msingi za miji katika

mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Kagera, Mara, Kigoma, Mtwara, Lindi, Ruvuma, Mbeya na Iringa zilitayarishwa.

Mheshimiwa Spika, Kujenga uwezo wa kupata wataalamu na vitendea kazi kwa ajili ya kupima na kutayarisha ramani za maeneo ya maji, maziwa na bahari kupitia Tangazo la Serikali Na. 467 la Desemba 2000.

Mheshimiwa Spika, tangu kutolewa kwa tangazo la Serikali Na. 467 la Desemba 2000, Wizara yangu imeendelea kupata ramani za majini *(Hydrographic Charts)* na kupata taarifa zinazohusu usalama majini kwa njia ya ushirikiano na taasisi za kimataifa za haidrografia kama vile *International Hydrographic Organization (IHO)* na *United Kingdom Hydrographic Office (UKHO)*. Changamoto iliyopo ni gharama kubwa za kupata zana na utaalam wa upimaji majini.

(v)Mheshimiwa Spika, Kifungu 68 ( c). Kuendelea kuimarisha utafiti kuhusu vifaa vya ujenzi na kufikisha matokeo ya utafiti huo kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi katika kipindi cha Desemba 2005 mpaka Juni 2009 imeboresha maabara yake kwa kufunga baadhi ya vifaa vipya ili kuwezesha kupata matokeo bora ya utafiti. Wakala uliendeleza mbinu na teknolojia rahisi za utengenezaji wa vifaa vya ujenzi na kusambaza matokeo ya utafiti katika Wilaya 40, mashine za matofali ya udongo na saruji yanayofungamana 350, mashine za kutengenezea vigae vya kuezekea 80 na kalibu *(mould)* za vigae 800. Aidha, katika kipindi hicho mashine inayotumia dizeli kutengeneza matofali ya aina hiyo imekamilika na mashine kama hiyo inayotumia umeme inaboreshwa zaidi.

(vi) Mheshimiwa Spika, Kifungu 68 (d). Kuendelea kuelimisha na kuhamasisha wananchi kujenga nyumba bora kwa kutumia vifaa vya ujenzi vya gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, kati ya mwaka 2005 na Juni 2009 Wakala wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi umeendelea kutoa mafunzo kwa vitendo na kuhamasisha kuhusu ujenzi wa nyumba za gharama nafuu na kujenga nyumba za mfano katika Halmashauri za Wilaya 40. Hii imefanya wananchi wengi kuanza kutumia teknolojia hii ya ujenzi inayotumia matofali ya udongo na saruji yanayofungamana. Aidha, Wizara inashirikiana na Makampuni kutoka sekta binafsi kuwezeshwa kuingizwa nchini teknolojia mpya ya vifaa vya ujenzi wa nyumba vya bei nafuu. Kwa mfano, kampuni ya *INOVIDA* kutoka Ujerumani inajenga kiwanda Dar es Salaam cha vifaa vya ujenzi wa nyumba visivyotumia saruji, nondo wala mbao.

(vii)Mheshimiwa Spika, Kifungu 68(f). Kusimamia uanzishwaji wa taasisi za kutoa mikopo kwa ajili ya ujenzi na ununuzi wa nyumba nchini.

Mheshimiwa Spika, mchakato wa maandalizi ya rasimu ya Sera ya Maendeleo ya Nyumba ya Taifa umekamilika baada ya kufanyiwa rejea iliyozingatia mtikisiko wa uchumi duniani ambao kwa kiasi kikubwa ulisababishwa na utoaji wa mikopo kwa ajili ya ujenzi na ununuzi wa nyumba.

Aidha, nafurahi kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa Sheria ya Mikopo ya Nyumba na ile ya Kumilikisha Sehemu za Jengo zilizopitishwa na Bunge Oktoba, 2008, ziliridhiwa na Mheshimiwa Rais Desemba, 2008 kama Sheria Na. 16 na 17 na zimeanza kutumika rasmi Mei, 2009 baada ya kukamilisha Kanuni na Sheria ndogo zinazohusika. Hivi sasa, Wizara imeanza mchakato wa kuelimisha na kuhamasisha umma ili wananchi wazielewe Sheria hizi na pia waelewe namna ya kutumia fursa zilizomo katika Sheria hizo kuhusu kupata mikopo ya muda mrefu kwa ajili ya kujenga au kununua nyumba. Benki tatu zimeanza kutoa mikopo ya nyumba *(Azania Bank, Commercial Bank of Africa na Stanbic Bank),* Benki nyingine zinajiandaa kufungua dirisha la kutoa mikopo ya Nyumba.

(viii)Mheshimiwa Spika, Kifungu 68 (g). Shirika la Nyumba la Taifa kuendelea kujenga nyumba za makazi na za biashara kwa ajili ya kuuza na kupangisha na kuzifanyia matengenezo zilizo chini yake.

Mheshimiwa Spika, tangu mwaka 2005 hadi Juni, 2009, Shirika la Nyumba la Taifa lilikamilisha ujenzi wa nyumba za makazi 271 katika maeneo ya Dar es Salaam, Chato, Ruangwa na Chalinze kwa gharama ya shilingi bilioni 7.4. Vilevile Shirika linaendelea na ujenzi wa nyumba nyingine 124 katika miji ya Arusha, Dodoma na Dar es Salaam kwa gharama ya shilingi bilioni 10.3. Kwa upande wa majengo ya vitega uchumi Shirika lilikamilisha ujenzi wa majengo matatu kwa gharama ya shilingi bilioni 2.9 katika miji ya Iringa, Kigoma na Arusha. Majengo mengine mawili yanaendelea kujengwa kwa gharama ya shilingi bilioni 42 katika miji ya Dar es Salaam na Shinyanga. Kuhusu miradi ya ubia inayoshirikisha sekta binafsi, Shirika limekamilisha ujenzi wa majengo 25 kwa gharama ya shilingi bilioni 41 na ujenzi wa majengo mengine 48 unaendelea kwa gharama ya shilingi bilioni 90 katika miji ya Dar es Salaam, Morogoro, Mwanza na Arusha. Aidha, Shirika linaendelea kutenga kiasi cha asilimia 25 ya mapato yake yatokanayo na kodi za pango kila mwaka kwa ajili ya kuzifanyia matengenezo nyumba zake 16,021.

(ix)Mheshimiwa Spika, Kifungu 68 (h). Kuendeleza miradi ya kupima viwanja katika miji hasa kwenye Makao Makuu ya Mikoa.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuongeza idadi ya viwanja vilivyopimwa mijini, Wizara yangu imeendelea kutekeleza miradi ya upimaji wa viwanja mijini kwa kushirikiana na Halmashauri za Miji na Wilaya nchini. Kati ya mwaka 2005 na Juni 2009 wizara ilikopesha Halmashauri 37 jumla ya shilingi billioni 5.8 kwa lengo la kupima viwanja 34,500 na idadi ya viwanja vilivyopimwa katika kipindi hicho ni 19,480.

Pia, Wizara kwa kushirikiana na Manispaa za Jiji la Dar es salaam imefanikiwa kupima viwanja 1,483 katika miradi ya kuendeleza upya eneo la Kurasini na kituo kipya cha huduma *(Satellite Town)* cha Luguruni.

(x)Mheshimiwa Spika, Kifungu 108 (f). Kutekeleza Mpango wa Uboreshaji wa Mfumo wa Sheria hususan Ujenzi wa Majengo ya Mabaraza ya Ardhi na Nyumba katika Ngazi za Wilaya na kuajiri Mahakimu wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, kati ya mwaka 2005 na Juni 2009 jumla ya Mabaraza 16 ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya yaliundwa katika ngazi ya Wilaya nchini na Wenyeviti (Mahakimu) 29 waliajiriwa kuendesha Mabaraza hayo. Idadi hiyo inafanya jumla ya Mabaraza yaliyoundwa kufikia 39 na Wenyeviti walioajiriwa hadi sasa kufikia 52. Mashauri 38,023 yalipokelewa, kati ya hayo mashauri 22,247 yalisikilizwa na kuamuliwa. Pia, ukarabati wa ofisi za Mabaraza ya Maswa, Kondoa, Korogwe, na Ukerewe umekamilika na ukarabati wa Mabaraza ya Geita na Iramba unaendelea. Vilevile, elimu ya Sheria ya Mahakama za Ardhi ilitolewa katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Arusha, Manyara, Dodoma, Singida, Shinyanga, Mbeya na Ruvuma.

Mheshimiwa Spika, Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2008/2009 na Malengo ya Mwaka 2009/2010. Ukusanyaji wa Mapato:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imekuwa ikitekeleza mikakati mbalimbali kwa lengo la kuboresha ukusanyaji wa mapato. Mikakati hiyo ni pamoja na kuboresha kumbukumbu za ardhi za wamiliki wa viwanja na mashamba na kuhamasisha ukusanyaji wa kodi kwa njia ya matangazo ya televisheni, redio, magazeti na kutuma hati za ukumbusho na madai kwa wamiliki.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2008/09, Wizara ilikuwa na lengo la kukusanya jumla ya Shilingi 18,209,520,000 kutokana na vyanzo mbalimbali. Hadi kufikia Juni 2009, Wizara imekusanya jumla ya Shilingi 13,403,597,103 ambazo ni sawa na asilimia 74 ya lengo. Kati ya makusanyo hayo, Shilingi 12,398,197,010 ambazo ni sawa na asilimia 92.4 ya makusanyo ni kodi ya pango la ardhi itokanayo na viwanja na mashamba. Pamoja na juhudi kubwa zinazofanywa na Wizara katika ukusanyaji wa kodi bado kuna changamato kubwa itokanayo na baadhi ya wamiliki wa ardhi kutokuwa na utamaduni wa kulipa kodi kwa hiari.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2009/10 Wizara yangu ina lengo la kukusanya kiasi cha Shilingi 15,550,006,000. Maduhuli haya yatakusanywa kwa kutumia mikakati ifuatayo:- Kuelimisha wananchi kwa njia ya matangazo, televisheni, redio na magazeti; kuongeza wigo wa walipa kodi ya ardhi kwa kukamilisha upimaji katika maeneo mbalimbali; kutoza viwango stahiki vya kodi ya ardhi kwa kuhuisha matumizi ya ardhi; kufuatilia kwa karibu vituo vya makusanyo ili kudhibiti mapato kwa mujibu wa sheria za fedha; kujenga uwezo na kuboresha vituo vya makusanyo kwa kuvipatia vifaa mbalimbali zikiwemo kompyuta na programu za kukadiria kodi na kuboresha hazina ya kumbukumbu za ardhi. Natoa wito kwa Halmashauri kutoa

kipaumbele katika suala la ukusanyaji wa kodi ya pango la ardhi kwani hayo ni mapato ya Serikali. Pia, natoa wito kwa wamiliki wa ardhi kuwa na utamaduni wa kulipa kodi ya pango la ardhi ili kuboresha ardhi kwa hiari na kwa wakati.

Aidha, kwa kuwa asilimia 20 ya makusanyo hurejeshwa kwenye Halmashauri za Miji na Wilaya husika, napenda kuzikumbusha Halmashauri kwamba fedha hizo zitumike kuendeleza sekta ya ardhi kama kununua vitendea kazi, kupima viwanja au kuweka miundombinu za kijamii na sio vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, Matumizi. Katika mwaka wa fedha 2008/09, Wizara yangu iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 27,286,790,000. Kati ya fedha hizo Shilingi 4,090,215,000 zilitengwa kwa ajili ya mishahara, Shilingi 13,807,707,000 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na Shilingi 9,388,868,000 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi Juni 2009 jumla ya fedha zilizotumika ni 24,871,902,382.65. Kwa mwaka wa fedha 2009/10 Wizara inalenga kutumia jumla ya Shilingi 33,483,299,000 katika utekelezaji wa majukumu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Maendeleo ya Ardhi. Ardhi ni rasilimali muhimu na yenye mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi wa nchi hii. Kwa kuzingatia umuhimu huu, Wizara yangu inaendelea kutoa huduma za maendeleo ya ardhi zenye misingi na lengo la kuimarisha uhakika na usalama wa miliki. Huduma hizo ni pamoja na kutoa hatimiliki za ardhi, kutwaa ardhi kwa manufaa ya umma, kufanya ukaguzi na uhakiki wa miliki kwa madhumuni ya kutatua migogoro kiutawala. Wizara pia inashughulikia uhamasishaji wa uanzishaji wa Masjala za Ardhi za Wilaya na Vijiji kwa lengo la kusajili na kuhifadhi hatimiliki za kimila pamoja na kutoa elimu ya sheria za ardhi kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Utoaji Milki. Mojawapo ya majukumu ya Wizara yangu ni kutoa hati za kumiliki ardhi kwa wamiliki wa ardhi kwa madhumuni ya kuhakikisha usalama wa milki. Pia, hati hizo zinawapatia wananchi fursa ya kuzitumia kujipatia mitaji ya kujiendeleza. Katika mwaka wa fedha 2008/09 Wizara ililenga kutayarisha hati 14,000, hata hivyo lengo hili lilivukwa ambapo jumla ya hati 14,436 zilitayarishwa na kusainiwa (Jedwali Na.2). Kasi ya utayarishaji wa hatimiliki imeongezeka kutokana na kufunguliwa na kuanza kufanya kazi ofisi za ardhi za kanda katika Miji ya Moshi, Mwanza, Dodoma, Mbeya na Dar es salaam ambazo zinasimamiwa na Makamishna wa Ardhi Wasaidizi. Kwa mwaka wa fedha 2009/10 Wizara yangu itaendelea kuziimarisha ofisi hizo, na pia kufungua Ofisi ya Kanda ya Kusini katika Mji wa Mtwara.

Vilevile kupitia Ofisi za Ardhi za Kanda, Wizara itatayarisha na kusaini hati 20,000. Ninatoa wito kwa wananchi, viongozi na watendaji wa Mikoa, Wilaya na Halmashauri kutoa ushirikiano na kuhakikisha kuwa huduma zinazohusu masuala ya ardhi katika kanda zinapatikana kama ilivyo kusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Ukaguzi na Uhakiki Milki. Katika kipindi cha mwaka 2008/09 Wizara yangu iliendelea kutatua migogoro ya ardhi kiutawala kwa nia ya kuhakikisha usalama wa milki na kuboresha kumbukumbu za umiliki wa ardhi. Migogoro hiyo inatokana na baadhi ya wananchi kughushi nyaraka za umilikishaji, ugawaji wa kiwanja kwa zaidi ya mtu mmoja na wamiliki wa asili ambao hawakulipwa fidia.

Mheshimiwa Spika, Migogoro mingi ya aina hii imejitokeza katika maeneo ya Mbezi, Jangwani Beach, Tegeta, Ununio na Boko mjini Dar es Salaam na hivyo kulazimika kuwa na mkakati maalum wa kushughulikia matatizo hayo. Katika mwaka 2008/09 Wizara ilitoa nyaraka mpya za umiliki kwa viwanja 4,098 kati ya 4,500 vilivyokusudiwa. Hii inafanya jumla ya viwanja vilivyopewa nyaraka mpya tangu kuanza kwa mkakati mwaka 2004/05 kuwa 6,013. Kwa mwaka 2009/10 Wizara itaendelea kuhakiki milki za viwanja 4,500 kati ya viwanja 8,518 vilivyobaki katika maeneo hayo.

Napenda kusisitiza umuhimu wa wamiliki wote katika maeneo hayo kuwasilisha nyaraka zao za umiliki wa ardhi Wizarani ili wapewe nyaraka mpya.

Mheshimiwa Spika, Utwaaji na Ubatilishaji Milki za Ardhi. Kwa kuzingatia Sera ya Taifa ya Ardhi na Sheria za Ardhi mwananchi anayemilikishwa ardhi anawajibu wa kuiendeleza na kulipa kodi ya pango la ardhi. Mmilikaji anayeshindwa kutekeleza masharti hayo miliki yake hubatilishwa kwa mujibu wa sheria. Aidha, upo utaratibu wa kisheria ambapo ardhi inapohitajika kwa manufaa ya umma hutwaliwa. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2008/09 Wizara ilishughulikia utwaaji wa ardhi na ubatilisho wa milki 391.

Mheshimiwa Spika, kisheria mmiliki wa ardhi anayo haki ya kuuza, kugawa, au kuweka rehani ardhi anayomiliki. Kabla ya kutumia haki zake hizo, ni lazima apate kibali cha Kamishna wa Ardhi au Afisa Ardhi Mteule katika Halmashauri husika. Katika mwaka wa fedha 2008/09 Wizara yangu ilitoa vibali vya uhamisho wa milki 372 na rehani 44 kati ya lengo la kutoa vibali vya kuweka rehani na uhamisho kwa miliki 1,000. Kwa mwaka wa fedha 2009/10 Wizara yangu imeweka lengo la kushughulikia na kutoa vibali 400.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Sheria ya Ardhi ya Vijiji. Wizara yangu imeendelea na jukumu la utekelezaji wa Sheria ya Ardhi ya Vijiji, Na. 5 ya mwaka 1999. Sheria hii ndiyo inayoweka utaratibu wa utoaji wa hati miliki za ardhi vijijini kwa ajili ya kuhakikisha usalama wa milki za ardhi na kutoa fursa kwa wananchi kutumia hati hizo kujipatia mikopo kutoka vyombo vya fedha.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa Fedha wa 2008/09 Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri za wilaya na wadau mbalimbali iliwezesha ukarabati wa masjala 3 za wilaya na 3 za vijiji. Vilevile, Vyeti vya Ardhi ya Vijiji 714 na Hati za Hakimiliki za Kimila 5,803 zimetolewa. Kwa Mwaka wa Fedha 2009/10, Wizara yangu itatoa Hati za Hakimiliki za kimila 100,000 katika vijiji 92 katika wilaya 15 nchini.

Mheshimiwa Spika, Elimu kwa Umma. Katika mwaka 2008/09 Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Miji na Wilaya na wadau mbalimbali imeendelea kutoa elimu ya Sera, Sheria za Ardhi na Matumizi Bora ya Ardhi katika Wilaya 20 nchini. Vilevile, elimu hiyo ilitolewa kwa kutumia vyombo vya habari. Kwa mwaka 2009/10 Wizara itachapisha nakala za vitabu vya Sheria ya Ardhi ya Kijiji na kanuni zake 10,000 na mwongozo wa kutolea elimu ya Sheria ya Ardhi ya Kijiji nakala 10,000 kwa lengo la kuzipatia Halmashauri ili wazitumie kutoa elimu na kuhakikisha wananchi wanapata uelewa mzuri wa sheria za ardhi.

Mheshimiwa Spika, Usajili wa Hati na Nyaraka za Kisheria. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2008/09 Wizara yangu ilikuwa na lengo la kusajili Hati za kumiliki ardhi pamoja na Nyaraka za kisheria 32,000. Lengo hilo limevukwa kwa kusajili Hati Miliki na nyaraka za kisheria 37,033. Kati ya hizo Hati Miliki 14,436 pamoja na nyaraka 14,922 zimesajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Hati Sura Na. 334. Aidha, nyaraka 7,151 zimesajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Nyaraka Sura na. 117 (Jedwali Na.3). Pia, rehani ya mali zinazohamishika 524 zimesajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Rehani ya Mali zinazohamishika Sura na. 210.

Kwa mwaka wa fedha 2009/10 Wizara yangu ina lengo la kusajili Hatimiliki na Nyaraka za Kisheria 42,000, kati ya hizo 16,000 ni Hatimiliki na 26,000 ni nyaraka za kisheria. Aidha, Sheria ya Usajili wa Hati Sura ya 334 itafanyiwa marekebisho ili kuboresha kazi ya usajili wa hati na nyaraka.

Mheshimiwa Spika, Uthamini wa Mali. Wizara imeendelea na majukumu ya kuthamini nyumba na mali nyinginezo kwa madhumuni ya kulipa fidia, kutoza kodi ya ardhi, mauzo *(transfer)*, mizania *(balance sheet)*, kuomba mikopo, mirathi na bima. Katika mwaka wa fedha 2008/09 Wizara iliweka lengo la kuthamini na kuidhinisha taarifa za uthamini wa nyumba na mali nyinginezo 5,000. Hadi Juni 2009 jumla ya nyumba na mali nyinginezo 8,896 zilithaminiwa na kuidhinishwa. Kwa mwaka wa fedha 2009/10 itaendelea kuthamini na kuidhinisha taarifa za uthamini wa nyumba na mali nyinginezo 10,000. Pia, kutokana na haja ya kushirikisha wadau wengi zaidi katika kazi za uthamini rasimu ya Sheria za Kusimamia Kazi za Uthamini na Wakala wa Milki ilianza kurejewa katika mwaka 2008/09. Kwa mwaka 2009/10 muswada wa sheria hiyo unategemewa kufikishwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Kuanzishwa kwa Hazina ya ardhi *(Land Bank)*. Katika kutekeleza kauli mbiu ya kitaifa ya "Kilimo Kwanza" Wizara yangu imepewa jukumu la kuratibu uanzishwaji wa Hazina ya Ardhi (*Land Bank)* kwa ajili ya kutenga ardhi kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi katika kilimo cha mashamba makubwa na ya kati. Sifa muhimu ya kipande cha ardhi kuingizwa katika HAZINA ni kwamba kisiwe na Haki

ya mtu mwingine, kiwe kimepimwa na kutayarishiwa Hatimiliki, pia kiwe na Miundombinu ya msingi kama vile barabara au reli.

Katika mwaka wa fedha uliopita (2008/09) Wizara yangu kwa kushirikiana na Shirika la *Investment Climate Facility (ICF)* ilikagua na kutambua maeneo yanayofaa kwa mashamba katika Wilaya za Handeni, Bagamoyo na Mkuranga na maeneo kwa ajili ya viwanda na Hoteli katika Jiji la Dar es salaam. Baada ya kubaini vipande vya ardhi kwa ajili ya kuingizwa kwenye HAZINA ya ardhi, imedhihirika kwamba ardhi hiyo inahitaji fedha nyingi kwa ajili ya kulipa fidia, kupima, kujenga miundombinu na kutayarisha Hati Miliki ambazo zitakabidhiwa kwa Kituo cha Uwekezaji. Wizara inashirikiana na *Investment Climate Facility (ICF)* kupata fedha kwa ajili ya mradi huu. Hatua hii itaondoa usumbufu mkubwa wanaoupata wawekezaji katika kilimo cha mashamba makubwa. Aidha, ardhi itakayotengwa kwa ajili hii haitahusisha mashamba ya wanavijiji wala haitoathiri mahitaji ya baadaye ya wanakijiji husika.

Mheshimiwa Spika, Kumbukumbu za Ardhi na Mawasiliano. Toka Wizara yangu ilipoanza kutumia mifumo ya kompyuta mwaka 2004/05, huduma nyingi za ardhi hivi sasa zinatekelezwa kwa kutumia mifumo ya kompyuta. Mpango wa muda mrefu wa mafunzo ya kompyuta kwa watumishi wa Wizara na ofisi za ardhi katika Halmashauri unatekelezwa kwa awamu. Vilevile, imebuniwa mifumo inayotumia teknolojia ya kisasa na imeanza kutumika kuboresha kumbukumbu na huduma za ardhi kwa wananchi. Baadhi ya mifumo hiyo ni pamoja na mfumo wa kumbukumbu za ardhi *(Management of Land Information Systems)*, mfumo wa kuhifadhi kumbukumbu za upimaji *(Surveys Registration System)* na mfumo wa kukadiria kodi za ardhi *(Land Rent Management System*). Hadi sasa mbali ya Makao Makuu, jumla ya ofisi za ardhi za Halmashauri 23 na Ofisi za Usajili wa Hati nne (4) zinatumia kompyuta kuboresha na kuhifadhi kumbukumbu za ardhi katika ofisi zao.

Katika mwaka 2008/09, Wizara ilifanikiwa kutoa taaluma ya matumizi ya kompyuta katika Ofisi saba (7) za Ardhi za Halmashauri za Babati, Bukoba, Kigoma/Ujiji, Lindi, Singida, Songea na Sumbawanga na kuziunganisha Ofisi za Ardhi za Manispaa za Ilala, Kinondoni, na Temeke kwenye mtandao wa Wizara. Hadi kufikia Juni 2009, taarifa za viwanja 48,000 kati ya viwanja 88,000 zimetambuliwa na kuhifadhiwa kwenye kompyuta katika vituo hivyo.

Mheshimiwa spika, kwa mwaka wa fedha 2009/10, Wizara yangu itaziwezesha Ofisi za Ardhi za Halmashauri za Wilaya saba (7) kupata mafunzo ya kutumia kompyuta, kuimarisha kumbukumbu za ardhi na kuboresha huduma na kupanua wigo wa makusanyo ya maduhuli ya Serikali. Natoa wito kwa Halmashauri zote nchini kuhakikisha kuwa na kumbukumbu sahihi za ardhi ili kupunguza migogoro na kuwa na miliki salama za ardhi katika maeneo yao kwa lengo la kuboresha huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Mabaraza ya ardhi na Nyumba ya Wilaya. Katika mwaka wa fedha 2008/09, Wizara yangu imeunda Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya sita (6) katika Wilaya za Ukerewe, Maswa, Iramba, Kondoa, Korogwe na Mkuranga kwa lengo

la kusogeza huduma ya utatuzi wa migogoro ya ardhi karibu na wananchi. Idadi hii inafanya jumla ya mabaraza ya ardhi na nyumba yaliyoundwa nchi nzima kufikia 39. Kwa mwaka wa fedha 2009/10, wizara yangu inakusudia kuboresha na kuimarisha Mabaraza hayo kwa kuyapatia watumishi wa kutosha na vitendea kazi ili migogoro iweze kupatiwa ufumbuzi kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, kuongezeka kwa uelewa wa wananchi juu ya thamani ya ardhi na wakati huo huo Mabaraza ya ardhi katika ngazi ya vijiji na kata kutofanya kazi kwa ufanisi, kumesababisha ongezeko kubwa la mashauri katika Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya. Hadi Juni, 2009 jumla ya mashauri 18,957 yalisajiliwa na kati yake, mashauri 7,123 yameamuliwa na 11,834 yanaendelea kushughulikiwa. Pamoja na kuongezeka kwa kasi ya utatuzi wa migogoro, bado kuna ongezeko kubwa la mashauri yanayofunguliwa katika mabaraza hayo hivyo kusababisha mlundikano wa mashauri katika mabaraza mengi nchini. Natoa wito kwa Halmashauri zote nchini kuimarisha Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji na Kata ili yafanye kazi kwa ufanisi kwa nia ya kupunguza mashauri katika ngazi ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imeendelea kutoa elimu chini ya Sheria Namba 2 ya mwaka 2002 *(The Land Disputes Courts Act, 2002).* Elimu hii inawajengea uwezo wajumbe wa Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji na Kata ili waweze kutoa haki kwa wananchi katika migogoro wanayoshughulikia. Aidha, nakala za mwongozo wa Sheria Na. 2 ya mwaka 2002 zilizokwisha sambazwa katika Halmashauri mbalimbali nchini zinaendelea kuwaelimisha wananchi juu ya mfumo mpya wa utatuzi wa migogoro ya ardhi na nyumba.

Mheshimiwa Spika, Huduma za Upimaji na Ramani. Wizara yangu inaendelea na utekelezaji wa jukumu la kusimamia upimaji ardhi na utayarishaji wa ramani za msingi nchini. Upimaji ardhi huwezesha kupata vipimo, ukubwa na mipaka ya vipande vya ardhi, taarifa na takwimu ambazo ni msingi wa usimamizi wa ardhi katika sekta zote.

Mheshimiwa Spika, Utayarishaji wa Ramani. Utayarishaji wa ramani za msingi una hatua kuu tatu; maandalizi yanayohusu upigaji picha za anga au za *satellite;* Upimaji picha *(ground photo control)* na Uhakiki ardhini ambao ni ukusanyaji wa taarifa na takwimu zinazostahili kuonyeshwa kwenye ramani na hatua ya mwisho ni kurasimu ramani. Katika mwaka 2008/09 Wizara yangu ilikamilisha hatua ya upimaji picha na uhakiki ardhini kwa ajili ya utayarishaji wa ramani za Kitalu cha Kiomboi na miji 10 kanda ya kusini. Pia, maandalizi ya utayarishaji wa ramani za msingi katika vitalu vya Kagera, Musoma na Mbeya yalianza. Maandalizi ya utayarishaji wa ramani za Jiji la Dar es salaam na za miji 15 kanda ya kaskazini mashariki yaliendelea. Kwa mwaka wa fedha 2009/10 Wizara yangu itafanya uhakiki ardhini kwa ajili ya utayarishaji wa ramani katika vitalu vya Kagera, Musoma, Mbeya, miji 10 kanda ya magharibi na Jiji la Dar es salaam. Pia, Wizara yangu itaanza maadalizi ya kutayarisha ramani ya Wilaya ya Nzega katika uwiano wa 1:350,000.

Mheshimiwa Spika, msingi wa kupima na kutayarisha ramani ni kuwa na mfumo na mtandao wa alama za msingi za upimaji nchi nzima. Mtandao wa aina hii huongeza kasi, ufanisi na kupunguza gharama za upimaji. Wizara yangu imeanza kujenga mtandao wa nchi nzima ambao ukikamilika utakuwa na alama za msingi 600 zitakazokuwa na wastani wa umbali wa kilomita 30 kati ya alama moja hadi nyingine kwa maeneo ya vijijini na kilomita 10 kwa maeneo ya mjini. Katika mwaka wa fedha 2008/09 jumla ya alama 87 (*Zero Order* and *First Order Reference Points*) ambazo ni muhimili wa mtandao huo zimesimikwa na zimepimwa katika awamu ya kwanza. Kwa mwaka 2009/10 alama nyingine 300 zitasimikwa na kupimwa (Ramani Na. 1). Katika mwaka wa fedha 2008/09 Wizara imeanza kuandaa Sera ya Taifa ya Upimaji Ardhi na Ramani kwa lengo la kuratibu na kutoa miongozo ya kusimamia shughuli za upimaji ardhi nchini ili kuongeza ushiriki wa sekta binafsi na taasisi mbalimbali za ndani na nje ya nchi katika upimaji wa ardhi. Sera hiyo itakamilika mwaka 2009/10.

Mheshimiwa Spika, Mipaka ya Ndani ya Nchi. Migogoro ya mipaka ndani ya nchi bado ni tatizo katika baadhi ya Wilaya. Mwaka jana nilitoa wito kwa Wakuu wa Wilaya wafanye mikutano ya ujirani mwema ili kufahamu na kutambua mipaka ya wilaya zao. Katika mwaka wa fedha 2008/09 Wizara yangu imeshirikiana na *TAMISEMI* na Halmashauri za Wilaya kutatua migogoro ya mipaka ya kiutawala kati ya Wilaya za Kilindi na Kiteto, Manyoni na Sikonge na Hifadhi za Taifa za Serengeti, Kasulu na Muyowosi. Kwa mwaka wa fedha 2009/10 Wizara yangu itaendelea kushirikiana na *TAMISEMI* kutafsiri mipaka kwa lengo la kutatua migogoro ya mipaka kati ya Wilaya za Bariadi na Magu pamoja na Hifadhi ya Mikumi na Vijiji vinavyoizunguka. Napenda kusisitiza kuwa wenye jukumu la kutatua migogoro ya mipaka ni wale wanaopakana, chini ya usimamizi wa *TAMISEMI*. Wizara yangu husaidia kutoa tafsiri ya mipaka iliyopo katika Matangazo ya Serikali *(GNs)*.

Mheshimiwa Spika, Mipaka ya Kimataifa. Kazi za kushughulikia mipaka ya Kimataifa sharti ifanywe kwa ushirikiano wa pamoja na nchi zinazopakana. Katika mwaka wa fedha 2008/09 wataalam wa Wizara yangu kwa kushirikiana na wa Msumbiji walikamilisha uelimishaji na uhamasishaji wa wananchi wanaoishi mpakani kutambua na kulinda alama za mpaka. Mwaka 2009/10 mpaka huo utahakikiwa na kuongezewa alama.

Mheshimiwa Spika, mpaka kati ya Tanzania na Malawi una sehemu mbili: Mto Songwe na Ziwa Nyasa. Kwa upande wa mto Songwe Benki ya Maendeleo ya Afrika imeonyesha nia ya kufadhili Programu ya Uendelezaji wa Bonde la Mto Songwe inayoendana na kudhibiti mkondo wa mto usihamehame. Makubaliano ya pamoja kuhusu utekelezaji wa Programu hii yalisainiwa mwezi Januari 2009. Kwa upande wa mpaka ndani ya Ziwa Nyasa, mwaka 2008/09 kamati imeundwa kukusanya nyaraka mbalimbali za kihistoria, kisheria na kidiplomasia kuhusu mipaka ya maziwa kwa lengo la kujenga hoja ili kuweka msingi wa majadiliano na Malawi.

Mheshimiwa Spika, Upimaji wa Mipaka ya Vijiji. Upimaji wa Mipaka ya Vijiji nchini huwezesha kutolewa kwa Vyeti vya Ardhi ya Vijiji, kupanga matumizi bora ya ardhi na hatimaye kutolewa kwa Hati za Hakimilki za Kimila. Katika mwaka 2008/09 Wizara yangu iliahidi kupima mipaka ya Vijiji 500 katika mikoa mbalimbali nchini. Hadi

Juni, 2009 jumla ya vijiji 478 vimepimwa katika mikoa ya Mtwara na Ruvuma, hii ikiwa ni asilimia 96 ya lengo na kufanya idadi ya Vijiji vilivyopimwa nchini hadi sasa kufikia 9,500. Kwa mwaka wa fedha 2009/10, Wizara yangu itaendelea na upimaji wa mipaka ya vijiji 1,500 vilivyobaki katika Mikoa ya Arusha, Dodoma, Kagera, Kigoma, Kilimanjaro, Manyara, Mara, Mbeya, Morogoro, Mwanza, Pwani, Ruvuma, Shinyanga, Singida na Tabora.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Kuendeleza Viwanja. Mfuko wa kuendeleza viwanja *(PDRF)* ulianzishwa kwa madhumuni ya kukabiliana na ukosefu wa viwanja mijini kwa kuzikopesha fedha Halmashauri na kuzitaka kurejesha mikopo kwa wakati ili kuwezesha Halmashauri zingine nazo kupata mikopo. Katika mwaka 2008/09 Halmashauri za Miji na Wilaya 13 zimeidhinishiwa kukopeshwa jumla ya Tsh. 710,000,000. Pamoja na jitihada za Wizara yangu kuzikopesha Halmashauri, kasi ya kurejesha mikopo hairidhishi. Hadi kufikia Juni 2009 Halmashauri 46 zilikuwa zimekopeshwa jumla ya Shilingi 766,336,935. Aidha, kupitia mikopo hiyo, Halmashauri husika zimeweza kupima na kugawa kwa wananchi jumla ya viwanja 3,709. Katika kipindi hicho Halmashauri 28 tu zimerejesha jumla ya Shilingi 380,625,919. Nahimiza Halmashauri ambazo hazijarejesha mikopo hiyo kurejesha ili Halmashauri nyingine ziweze kunufaika na fursa hiyo.

Mheshimiwa Spika, Upimaji wa Ardhi Ndani ya Maji. Madhumuni ya upimaji wa ardhi ndani ya maji ni kutayarisha ramani za kuonyesha umbile la ardhi iliyo chini ya maji hususan milima, mabonde, miinuko na kina cha maji. Ramani hizo ni nyenzo muhimu za kuongozea vyombo vya majini na matumizi mengine. Ujenzi wa uwezo wa kufanya upimaji majini uko katika sura mbili; kupima na kutayarisha ramani katika malango ya bandari na nje. Katika mwaka 2008/09 Wizara yangu imepeleka wataalam sita kupata mafunzo ya muda mfupi kuhusu upimaji majini. Pia, leseni tatu za programu maalum ya kufanyia mahesabu na uchoraji wa ramani za nchi kavu na majini zilinunuliwa. Kwa uwezo uliopo, Wizara yangu inatarajia kuanza kupima na kutayarisha ramani katika milango ya bandari zetu. Kwa maeneo ya nje ya bandari, tutaimarisha ushirikiano na nchi tunazopakana nazo pamoja na mashirika ya kimataifa ya Haidrografia ili kufanya kazi hiyo kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, Kuongeza Ukanda wa Kiuchumi Baharini. Katika mwaka wa fedha 2008/09 nililiarifu Bunge lako kuwa Tanzania ingeanza mchakato wa kuwasilisha Umoja wa Mataifa maombi ya kuongeza Ukanda wa Kiuchumi Baharini (*extended continental shelf*) kwa mujibu wa Sheria ya kimataifa kuhusu Bahari *(The United Nation Convention of the Law of the Sea).* Hadi kufikia Juni 2009 Wizara yangu kwa kupitia kamati zinazoshughulikia suala hili ilifanya tafiti baharini na ilifanya mikutano na nchi za Kenya na Shelisheli ya kukubaliana misingi ya kugawana eneo ambalo linawaniwa na nchi zote. Nafurahi kuliarifu Bunge lako kuwa Tanzania imewasilisha Umoja wa Mataifa Andiko lake la awali tarehe 7.5.2009. Tarehe ya mwisho ya kuwasilisha andiko Umoja wa Mataifa ilikuwa ni 13.5.2009. Kwa kuwasilisha andiko hilo, Tanzania imepewa fursa ya kukamilisha na kuwasilisha andiko kamili katika kipindi cha miaka miwili ijayo.

Mheshimiwa Spika, Upimaji Milki. Katika mwaka wa fedha 2008/09 Wizara yangu imeweza kuratibu na kuidhinisha upimaji wa viwanja 38,710 na mashamba 623 kati ya lengo la viwanja 20,000 na mashamba 800 Aidha, Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi na sehemu ya hifadhi ya Taifa ya Ruaha zilipimwa. Kwa mwaka wa fedha 2009/10 Wizara itaratibu na kuidhinisha upimaji milki wa viwanja 35,000 na mashamba 1,000 katika Halmashauri mbalimbali nchini. Aidha, Wizara itaendelea kuimarisha na kuboresha utunzaji wa kumbukumbu za upimaji ardhi na kuzibadili kuwa za kielektroniki.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009 Wizara yangu imekamilisha zoezi la kupeleka kumbukumbu za upimaji katika Kanda 5 za Sekta ya Ardhi zilizoanzishwa. Kwa mwaka wa fedha 2009/2010, Wizara itakasimu mamlaka ya kusimamia upimaji milki katika Mikoa yenye Wapima Ardhi Wakuu. Kwa mikoa isiyokuwa na Wapima Ardhi Wakuu, Wizara kwa kushirikiana na *TAMISEMI* inafanya utaratibu wa kupata Wataalam wenye sifa za kukasimiwa mamlaka hayo. Lengo ni kukasimu kazi hizi katika Mikoa yote ili kuboresha utendaji kazi na kusogeza huduma za upimaji ardhi karibu na wananchi.

Mheshimiwa Spika, Maendeleo ya Miji na Vijiji. Majukumu ya Wizara yangu katika kupanga na kusimamia uendelezaji wa miji na vijiji hapa nchini yanazingatia Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 na ile ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000 pamoja na Sheria zinazohusika na uendelezaji wa miji. Sheria hizo ni pamoja na Sheria ya Mipangomiji ya mwaka 2007 na Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, Uandaaji Mipango ya Uendelezaji Miji. Katika upangaji wa miji, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri huandaa mipango ya jumla *(General Planning Schemes)* ya aina mbili ya kuongoza uendelezaji wake.

Mipango hiyo ni ile ya muda mrefu *(Master Plans)* ambayo inatoa mwongozo wa uendelezaji kwa miaka ishirini na mipango ya matumizi ya ardhi ya muda mfupi *(Interim Land Use Plans)* ambayo huchukua miaka kumi.

Katika Mwaka wa fedha 2008/2009, mipango ya matumizi ya ardhi ya muda mfupi ya miji ya Kyela, Maswa, Kasulu na Kibondo ilikamilishwa. Pia, mipango ya muda mrefu ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji na mji wa Chuo Kikuu cha Dodoma *(Dodoma University Satellite Town)* ilikamilishwa. Kwa mwaka wa fedha 2009/2010, Wizara yangu itaandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya muda mfupi kwa miji ya Rujewa, Isaka, Kahama, Manyoni na Kilolo na ya muda mrefu ya Jiji la Tanga na mji wa Bagamoyo. Sambamba na hayo, kazi ya uhuishaji wa mpango kabambe *(Masterplan Review)* wa Jiji la Dar es Salaam litafanyika. Napenda kuhimiza Halmashauri ambazo hazina mipango hiyo, zifanye jitihada ya kutenga fedha kwa ajili hiyo. Aidha, kwa ile

miji ambayo tayari ina mipango hiyo ianze kuitekeleza ikiwa ni pamoja na kuandaa mipango ya kina *(Detailed Layouts)* ili kuweza kupata viwanja vya kupima na kuviendeleza.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri zinazohusika huandaa mipango ya uendelezaji upya maeneo mbalimbali ya miji *(Redevelopment schemes)*. Lengo la mipango hii ni kuboresha mazingira, mandhari ya miji, huduma za kiuchumi, kijamii na kutumia kikalimilifu ardhi kulingana na thamani. Uboreshaji huo utasaidia kuvutia uwekezaji na kuchangia ukuaji wa uchumi wa Taifa. Katika mwaka wa fedha 2008/2009, Wizara yangu ilikamilisha mipango ya uendelezaji upya maeneo ya *Oysterbay*, Masaki na Magomeni Jijini Dar es Salaam. Kwa mwaka wa fedha 2009/2010 Wizara yangu itakamilisha mpango wa uendelezaji upya eneo la kati la Manispaa ya Temeke na kuandaa mpango wa eneo la kati la Manispaa ya Songea. Ili mipango hiyo iweze kuleta manufaa yanayotarajiwa, natoa wito kwa mamlaka za miji kusimamia kikamilifu masharti ya uendelezaji yaliyoainishwa kwenye mipango hiyo.

Mheshimiwa Spika, uandaaji mipango ya uendelezaji vijiji, Wizara yangu imeendelea kuratibu kazi za uandaaji mipango ya matumizi bora ya ardhi ya vijiji mbalimbali. Lengo ni kuhakikisha kuwa mipango iliyoandaliwa na Serikali za vijiji inapitia utaratibu sahihi na inakidhi viwango vya kitaalamu, pia. Mipango hiyo inazingatia mkakati wa Taifa wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini na sheria ya uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ya mwaka 2007.

Katika mwaka wa fedha 2008/2009 Wizara yangu ilianza kuandaa mwongozo wa kuandaa mipango ya kina ya makazi vijijini. Kwa mwaka wa fedha 2009/2010, Wizara yangu itakamilisha mwongozo wa kuandaa mipango ya kina ya makazi au maeneo ya kati ya vijiji (vijiji miji). Pia, mipango ya kina ya vijiji 20 katika Wilaya za Bagamoyo, Babati na Bariadi itaandaliwa. Vijiji vitakavyoandaliwa mipango ya kina ni vile vinavyokua kwa kasi na ambavyo vimekwishaandaliwa, Mipango ya Matumizi ya kina na ambavyo vimekwishaandaliwa mipango ya matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mipango ya uendelezaji miji, kutokana na msongamano mkubwa wa mizigo uliopo katika bandari ya Dar es Salaam, Wizara yangu tangu mwaka 2006 imekuwa ikitelekeza mradi wa kuendeleza upya eneo la Kurasini ili liweze kutumika kikamilifu kwa shughuli zinazohusiana na huduma za Bandari ambacho ni kitega uchumi muhimu sana kwa Taifa letu. Eneo hilo ambalo lilivamiwa na kuwa makazi yasiyopangwa lilitengwa rasmi katika *Master Plan* ya Dar es Salaam mwaka 1979 na katika Mpango wa Kuendeleza upya eneo la Kurasini wa mwaka 2002 kwa ajili ya upanuzi wa Bandari.

Katika kutekeleza kazi hii, Wizara imeendelea kulipa fidia kwa wakazi wa eneo hili na kuwahamishia kwenye maeneo mbadala ili kuweza kupata maeneo huru na kupima viwanja vikubwa na kuvimilikisha kwa njia ya zabuni kwa wawekezaji kwa ajili ya shughuli za kibandari. Hadi Juni, 2009 jumla ya mali 1,173 zimehakikiwa katika eneo hili na kulipwa fidia inayofikia jumla ya Shilingi bilioni 29.4. Ulipaji fidia huu umewezesha upatikanaji wa viwanja 18 vilivyopimwa vyenye ukubwa wa ekari 62.6.

Kwa mwaka wa fedha 2009/2010 na kumaliza kabisa tatizo la ukosefu wa maeneo kwa shughuli za kibandari katika bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, uhamasishaji, ujenzi holela katika miji yetu bado ni tatizo kubwa. Sera na sheria zinaelekeza kurasimisha maeneo haya kwa kushirikiana na Halmashauri za Miji na Wilaya ili wananchi waweze kupata huduma za misingi na kuongeza usalama wa miliki. Katika mwaka wa fedha 2008/2009, Wizara ilishirikiana na Manispaa ya Kinondoni kuandaa mipango ya kina kwa ajili ya kuongoza uendelezaji wa maeneo ya Kimara na Mbezi katika jiji la Dar es Salaam. Pia, kwa kushirikiana na Halmashauri ya Jiji la Mwanza imetambua milki za nyumba 6,053 katika maeneo mbalimbali yaliyojengwa kiholela. Vilevile, kwa kupitia mpango huu, jumla ya viwanja 400 vilipimwa katika jiji la Mwanza. Kwa mwaka wa fedha 2009/2010, Wizara itaendelea na kazi ya urasimishaji wa ardhi na nyumba katika majiji ya Mwanza na Dar es Salaam. Aidha, kwa kushirikiana na Halmashauri za miji na Wilaya itaandaa programu ya Taifa ya kurasimisha makazi. Programu hii itakuwa dira ya kuboresha makazi na kukabili tatizo la ujenzi holela nchini. Natoa wito kwa Halmashauri za miji na Wilaya kutoa ushirikiano katika maandalizi ya programu inayokusudiwa ya kurasimisha makazi nchini.

Mheshimiwa Spika, mipango ya uendelezaji vituo vya huduma na miji mipya, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri za jiji la Dar es Salaam inaendelea na jitihada za kupunguza msongamano wa watu na magari katikati ya jiji kwa kuanzisha vituo vya huduma za jamii *(satellite towns)* katika maeneo ya pembezoni mwa jiji la Dar es Salaam pamoja na uanzishaji wa mji mpya wa Kigamboni (Kigamboni *New City).* Mpango wa jiji la Dar es Salaam wa mwaka 1979 ulipendekeza uanzishwaji vituo hivyo kwa kuzingatia barabara kuu zitokazo nje ya Dar es Salaam. Vituo hivyo ni Pugu Kajiungeni barabara ya Pugu, Kongowe barabara ya Kilwa, Kimbiji na Mji Mwema barabara ya Kigamboni na Bunju barabara ya Bagamoyo.

Katika mwaka 2008/2009 Wizara iliendelea na utekelezaji wa kuanzisha kituo katika eneo la Luguruni lenye ukubwa wa ekari 178 ambapo wakazi 259 wenye maeneo hayo wamelipwa fidia na kuwezesha kupatikana kwa viwanja 325 vya matumizi mbalimbali. Viwanja hivyo vimekwishaanza kuuzwa kwa njia ya zabuni kwa waendelezaji mbalimbali. Aidha, eneo la Kwembe kati ambalo lina ukubwa wa ekari 458 limepimwa na kupatikana viwanja 1,200. Viwanja hivyo vitatumika kuwahamishia wananchi ambao walihamishwa kutoka kwenye eneo la Kituo cha Huduma cha Luguruni, pamoja na wale wa eneo la Kwembe Kati ambao maeneo yao yametumika kwa ajili ya miundombinu na huduma mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Jiji la Dar es Salaam na Manispaa ya Temeke inaandaa mji mpya wa Kigamboni katika eneo lenye ukubwa wa hekta 5,533. Mji huo mpya utazihusisha Kata za Mjimwema, Kigamboni, Vijibweni na Kibada. Kazi zilizofanyika ni pamoja na uhamasishaji katika ngazi zote kuanzia Mkoa hadi Serikali za Mitaa, utambuaji wa wakazi na miliki zao unaendelea *(Social economic survey)* na mtaalamu mwelekezi wa kusanifu Mji mpya wa Kigamboni ameteuliwa. Lengo ni kuboresha eneo la Kigamboni kwa kuwekewa miundombinu ya kisasa, huduma

za kijamii za kisasa, huduma za kiuchumi (utalii), na kadhalika. Katika mpango huu, wakazi wa Kigamboni hawatahamishwa kupelekwa nje ya Kigamboni bali watapangwa upya ndani ya eneo hilo ili wawe wa kwanza kunufaika na maboresho yatakayofanyika. *(Makofi)*

Kwa mwaka 2009/10, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Jiji la Dar es Salaam, itaendelea na kazi ya uendelezaji wa Kituo cha Luguruni, uandaaji mpango wa uendelezaji mji mpya Kigamboni na itaanza kazi ya uendelezaji wa Kituo cha Huduma za Jamii katika eneo la Kongowe.

Mheshimiwa Spika, jukumu la usimamizi na udhibiti wa uendelezaji wa miji ni la Serikali za Mitaa. Mfumo uliopo katika usimamizi wa miji ni hafifu na hivyo ujenzi holela unaendelea bila kujali viwango na matumizi stahili ya eneo. Hii imefanya sehemu kubwa ya miji yetu iendelezwe bila mpangilio hivyo kutokuwa mahali nadhifu na salama pa kuishi. Wizara inashirikiana na TAMISEMI kuona uwezekano wa kuweka mfumo utakaosaidia katika usimamizi na udhibiti wa uendelezaji wa miji yetu kama inavyotarajiwa kwa sasa na wakati ujao. Kwa mwaka 2009/2010 Wizara itakamilisha kanuni za Sheria ya Mipangomiji na kuendelea kuelimisha umma kuhusu Sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, mpango ya matumizi bora ya ardhi ni nyenzo muhimu sana katika uendelezaji wa ardhi na rasilimali zake kwa ufanisi, kuondoa migogoro baina ya watumiaji ardhi na uimarishaji miliki za ardhi hususan za kimila. Vilevile, kupitia mipango hiyo na kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na.5 ya Mwaka 1999, inawezesha upatikanaji wa maeneo ya ardhi kwa ajili ya wawekezaji, kuhifadhi mazingira na kuongeza ustawi wa maendeleo ya kiuchumi na jamii ya watumiaji ardhi ambao wengi wao ni wananchi wa kawaida wanaoishi vijijini.

Katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu kupitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, ilikamilisha Programu za Utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Matumizi Bora ya Ardhi *(The National Land use Plan).* Programu hizo zipo 12 nazo ni Programu ya Kuimarisha TUME, Kilimo, Mifugo, Uvuvi, Misitu, Wanyamapori, Madini, Nishati, Miundombinu, Rasilimali Maji, Utalii na Uwanda/Uoto asili. Madhumuni ya Programu hizo ni kuonyesha nafasi ya Wizara ya Ardhi katika kuchangia maendeleo ya Sekta hizo kwa kupatikana ardhi kwa matumizi mbalimbali. TUME imesambaza programu hizo kwa Wizara mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji wa pamoja. Kwa mwaka wa fedha 2009/2010, TUME itaanza kutekeleza programu mbili za kipaumbele kwa kushirikisha watumiaji wakuu wa ardhi ambao ni Kilimo na Mifugo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2008/2009 Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi iliendelea kushirikiana na Halmashauri za Wilaya, Wizara ya Maliasili na Utalii, Mifugo na Uvuvi, taasisi ya MKURABITA, Asasi zisizo za kiserikali na wadau mbalimbali kuwezesha uandaaji na utekelezaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi katika ngazi za Wilaya na Vijiji. Katika kipindi hicho, Tume imekamilisha Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi ya Wilaya nane za Mtwara, Pangani, Lindi, Mkuranga, Muheza, Mkinga, Namtumbo na Bagamoyo na Wilaya nyingine 11 na Vijiji 108. Katika vijiji hivyo, maeneo ya huduma za jamii pamoja na hifadhi za vyanzo

vya maji, misitu, ufugaji, wanyamapori, maeneo ya kilimo cha umwagiliaji na mashamba makubwa yametengwa kwa kushirikisha wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010 TUME inakusudia kutayarisha na kutekeleza mipango ya matumizi bora ya ardhi kwa ushirikishwaji katika vijiji 100 vya mfano katika Mikoa ya Kagera, Arusha, Manyara, Morogoro, Rukwa, Mara, Dodoma, Mtwara, Singida na Mwanza na kuwezesha kutayarisha mipango ya matumizi bora ya ardhi ya Wilaya mbili za Bariadi na Babati. Pia, Tume itatoa mafunzo kwa watendaji ngazi ya Wilaya juu ya sheria za ardhi na mbinu shirikishi za utayarishaji wa mipango ya matumizi ya ardhi.

Vilevile, Tume itakamilisha uandaaji wa Kanuni za Sheria Na.6 ya Mwaka 2007, uandaaji mipango ya matumizi bora ya ardhi ya mabonde ya Ziwa Tanganyika na Victoria kwa ajili ya kuhifadhi mazingira na kuelekeza uwekezaji. Tume itafanya tafiti mbalimbali kuhusu masuala ya ardhi hasa katika maeneo yenye migogoro ya ardhi hususan katika Wilaya ya Kilosa uhamiaji mijini kutoka vijijini, ushirikishwaji wa wananchi katika kuendeleza ardhi mijini na viwango vya matumizi ya ardhi mijini na vijijini. Napenda kutoa wito kwa Wizara mbalimbali kutenga bajeti ya utekelezaji wa programu zilizoainishwa katika Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi. Pia, Halmashauri za Wilaya zote nchini zitenge fedha kwa ajili ya kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya Wilaya na Vijiji.

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya nyumba, pamoja na kuwa hali ya uendelezaji wa nyumba nchini bado sio nzuri, Wizara yangu inatambua mchango mkubwa ambao Sekta ya Nyumba inaweza kutoa ajira na kukuza uchumi. Kuongezeka kwa uwekezaji katika sekta ya nyumba nchini kutachangia katika kuongezeka kwa nafasi za ajira, kuinua mapato ya watu, kuboresha mazingira ya kuishi na hivyo wananchi kuweza kujiendeleza kiuchumi na kijamii. Pamoja na juhudi za Serikali za kuanzisha Idara ya Nyumba na kuanza kuweka mazingira stahili ya uendelezaji wa nyumba nchini, bado kuna haja ya sekta ya nyumba kupewa kipaumbele katika mipango ya Taifa ya kukuza uchumi na kuondoa umasikini.

Kwa mwaka 2009/2010 Wizara yangu itaendelea na jukumu la kuweka mazingira mazuri yatakayowezesha wadau mbalimbali kushiriki katika kuboresha hali ya nyumba nchini, hii ikiwa ni pamoja na kuendelea kuwahamasisha wadau wa sekta ya nyumba nchini waweze kuweka miundombinu na kujenga nyumba za kutosha na za bei nafuu kwa ajili ya kuuza na kupangisha.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009 Wizara yangu imeifanyia marejeo rasimu ya Sera ya Maendeleo ya Nyumba kwa kuzingatia hali ya mtikisiko wa uchumi duniani uliosababishwa kwa kiasi kikubwa na utaratibu usiokuwa makini wa utoaji mikopo ya nyumba. Kwa mwaka 2009/2010 sera hii itakamilishwa na hivyo kutoa mwongozo wa uendelezaji nyumba hapa nchini. Aidha, Wizara yangu itatoa elimu kwa umma kuhusu maudhui ya Sera hii na kufanya utafiti kuhusu hali ya nyumba kwa lengo la kuandaa miongozo na nyaraka mbalimbali kuhusiana na uendelezaji wa sekta ya

nyumba nchini. Vilevile taarifa hizo zitakuwa msingi wa kuandaa programu ya Taifa ya uendelezaji wa nyumba kwa lengo la kuboresha hali ya nyumba.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009 Bunge lako lilipitisha Sheria ya Umiliki wa Sehemu za Majengo Na.16 ya mwaka 2008 na Sheria ya Mikopo ya Nyumba Na.17 ya mwaka 2008. Sheria zote mbili tayari zimeanza kutumika rasmi Mei, 2009 baada ya Wizara yangu kukamilisha matayarisho ya Kanuni na Sheria ndogo zinazohusika. Sheria hizi zitawezesha uwekezaji mkubwa katika sekta ya nyumba na hivyo kuchangia uendelezaji wa miji endelevu. Kwa mwaka 2009/2010 Wizara yangu itatoa elimu kwa umma kuhusu Sheria hizo. Natoa wito kwa wananchi wote kutumia fursa zinazotolewa na Sheria hizo ili wajiendeleze kiuchumi na kijamii na wapate nyumba bora. Vilevile natoa wito kwa mabenki yaanze kutoa mikopo ya nyumba kwa kutumia hizo sheria mbili.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba tayari baadhi ya mabenki kama *Azania Bank Limited, Commercial Bank of Africa Ltd* na *Stanbic Bank Limited* yameendelea kutoa mikopo ya nyumba, bado kuna changamoto kubwa inayowakabili wakopaji ambayo ni riba kubwa inayotozwa na mabenki hayo ambayo sio chini ya asilimia 17 kwa mwaka. Changamoto nyingine ni pamoja na kipato kidogo wanachopata wananchi walio wengi na kipato kisichokuwa cha uhakika kinachotokana na shughuli ambazo siyo rasmi, wamiliki wengi wa ardhi kutokuwa na hati miliki au leseni za makazi ambazo zinahitajika kuwekwa rehani (dhamana) kwa mikopo ya mabenki, ukosefu wa chombo cha fedha cha kukopesha mabenki kwa muda mrefu *(liquidity facility)* ukizingatia kwamba mikopo ya nyumba huwa ya miaka 15 hadi 25 au zaidi.

Kwa mwaka 2009/2010 Wizara yangu itashirikiana na Wizara ya Fedha na Uchumi na Benki Kuu ya Tanzania kuwezesha kuanzishwa kwa chombo *(Mortgage Liquidity Facility)* kitakachotoa mtaji kwa mabenki ili yaweze kutoa mikopo ya muda mrefu. Aidha, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau wengine itaweka utaratibu wa kuanzisha upya na kuimarisha vyama vya ushirika wa Nyumba *(Housing Cooperatives)* na vyombo vya ujenzi wa nyumba ambavyo vitamwezesha mwananchi wa kipato cha chini kufaidika na mikopo ya nyumba. Vilevile Wizara itashirikiana na Taasisi nyingine kuhamasisha wananchi kujiunga na vyama vya kuweka na kukopa *(Saccos)* na kuanzisha shughuli mbalimbali za kiuchumi ili kuinua mapato yao na sehemu ya mapato hayo itumike katika kuboresha nyumba zao.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Mikopo ya Nyumba kwa Watumishi wa Serikali, unaendelea kutoa mikopo kwa ajili ya ujenzi, ukarabati na ununuzi wa nyumba kwa lengo la kuwawezesha watumishi hao kupata makazi bora. Tangu mfuko uanzishwe mwaka 1992, jumla ya maombi 2,422 yanayohitaji zaidi ya Shilingi bilioni 40 hadi Juni, 2009 yamepokelewa. Kati ya maombi hayo watumishi 1,169 walikopeshwa ikiwa ni asilimia 48.9 ya waombaji wote. Jumla ya fedha zilizokopeshwa tangu mfuko uanzishwe hadi mwezi Juni, 2009 ni Shilingi bilioni 5.4. Jumla ya marejesho ya mkopo yalikuwa Shilingi bilioni 1.1.

Katika mwaka wa fedha 2009/2010, Wizara yangu itaendelea kuboresha ukusanyaji wa marejesho ili mfuko uweze kuhudumia watumishi wengi zaidi. Aidha, kwa kuzingatia mazingira mapya yanayotokana na Sheria ya Mikopo ya Nyumba, Wizara yangu itaangalia upya muundo wa Mfuko ili kuona uwezekano wa mfuko huu kutumika kama dhamana kwenye mabenki kwa ajili ya kutoa mikopo ya nyumba kwa Watumishi wa Serikali. Serikali itashauriana na mabenki ili yaweze kutumia dhamana hiyo kuwakopesha watumishi wengi zaidi na kwa viwango vikubwa zaidi kuliko hali ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi *(NHBRA)*, jukumu la Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi *(National Housing and Building Research Agency - NHBRA)* ni kufanya tafiti, kuelimisha, kukuza, kushauri, kuhamasisha na kusambaza matokeo ya utafiti na utaalam wa ujenzi wa nyumba bora na za gharama nafuu. Lengo la Wakala ni kuinua na kuboresha viwango vya nyumba kwa kutumia vifaa vilivyotafitiwa na vipatikanavyo hapa hapa nchini jambo ambalo litaongeza ubora wa maisha ya wananchi mijini na vijijini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2008/2009 maabara ya wakala imeboreshwa ili kuwezesha kupata matokeo bora ya utafiti. Wakala ulifanya tafiti za kuendeleza mbinu na teknolojia rahisi za uzalishaji wa vifaa vya ujenzi na kusambaza mashine 40 za kufyatulia matofali yanayofungamana *(interlocking brick making machines);* mashine 20 za kutengenezea vigae vya kuezekea pamoja na kalibu *(moulds)* zake kwa wananchi. Uhamasishaji na mafunzo kwa vitendo ulihusisha vijana kutoka Wilaya ya Bukoba Vijijini, Mikoa ya Shinyanga, Dodoma, Morogoro na Dar es Salaam. Pamoja na kazi hizo, wakala ilifanya kazi za ushauri kwa wateja mbalimbali kutoka mikoa ya Mbeya na Singida na kwa Jeshi la Polisi, Magereza na Taasisi ya Uhasibu *(TIA)* Jijini Dar es Salaam. Wakala uliendelea kutangaza shughuli zake kwa kushiriki katika maonyesho mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa na kujitangaza katika vyombo mbalimbali vya Habari.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2009/10 Wakala utaendesha semina za uhamasishaji na mafunzo kwa vitendo *(practical training)* katika Mikoa ya Shinyanga na Kagera na kujitangaza katika vyombo mbalimbali vya habari na kushiriki maonyesho ya Kitaifa na Kimataifa. Wakala pia utaendelea kutoa huduma za ushauri kwa kutumia vifaa na teknolojia vilivyotafitiwa na Wakala na kupatikana hapa hapa nchini. Napenda kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge kuzishauri na kuzihamasisha Halmashauri za Wilaya katika Majimbo yenu zitumie huduma za Wakala kwa kazi za ujenzi wa majengo mbalimbali hasa nyumba za walimu wa shule za Msingi na Sekondari na Zahanati ili kunufaika na huduma za Wakala na pia kusambaza teknolojia.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC)* katika mwaka 2008/2009 Shirika la Nyumba la Taifa liliendelea kutekeleza majukumu yake ya kujenga Nyumba za makazi na biashara, kufanya shughuli za ukandarasi na kusimamia miliki za nyumba zake. Kuhusu ujenzi wa nyumba za makazi na biashara, Shirika lilikamilisha ujenzi wa nyumba 16 za makazi eneo la Chato pamoja na maduka na ofisi 66 eneo la Kibla –

Arusha kwa jumla ya gharama ya Shilingi bilioni 2.2. Miradi iliyoendelea kutekelezwa ni pamoja na nyumba za makazi 34 eneo la Mbweni JKT – Dar es Salaam; nyumba 48 eneo la Kibla – Arusha, nyumba 40 eneo la Medeli – Dodoma, nyumba mbili Mtaa wa Chwaku Dar es Salaam, jengo la biashara la ghorofa tano katika Mtaa wa Balewa – Shinyanga. Miradi hii ikikamilika itagharimu kiasi cha Shilingi bilioni 11.2. Mradi mwingine wa biashara ni ule wa *NHC House* unaojengwa Jijini Dar es Salaam chini ya mpango wa *"Build – Operate –Ttransfer" (BOT)* utakaogharimu Shilingi bilioni 41.3.

Kwa mwaka wa fedha 2009/2010, pamoja na kuendelea na utekelezaji wa miradi ya ujenzi iliyotajwa hapo juu, Shirika litaanza ujenzi wa miradi mipya. Miradi hii itajumuisha ujenzi wa nyumba za makazi 172 eneo la Kibada – Dar es Salaam, Babati 16, Mvomero 16 na majengo 12 ya biashara katika miji ya Dar es Salaam, Kigoma, Lindi, Moshi, Morogoro, Mtwara, Songea, Sumbawanga, Singida na Tabora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Shirika liliendelea kutekeleza miradi ya ubia kwa kushirikisha sekta binafsi. Miradi nane iliyogharimu Shilingi bilioni 22 imekamilika na mingine 44 ya Shilingi bilioni 91 inaendelea. Kwa mwaka wa fedha 2009/2010 Shirika linategemea kuanza miradi 10 ya majengo ya biashara yatakayojengwa kwa njia ya ubia Jijini Dar es Salaam. Shirika pia litaendelea na ujenzi wa kandarasi wa bweni la wanafunzi la Chuo Kikuu cha Mzumbe utakaogharimu Shilingi milioni 976.4.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009 Shirika liliendelea na ukusanyaji wa kodi za pango na kuzifanyia matengenezo nyumba zake 16,021. Shirika lilikusanya kodi za pango kiasi cha Shilingi bilioni 30.7. Kiasi hiki ni sawa na asilimia 88 ya mapato ya Shirika. Shirika pia lilifanyia matengenezo makubwa majengo 719 na nyumba 2,889 kwa gharama ya Shilingi bilioni 6.9.

Kuanzia Agosti, 2009, Shirika litaongeza kodi za pango kwa kuzingatia mkakati uliopangwa mwaka 2005/2006 wa kuongeza viwango vya kodi kwa awamu ili kufikia asilimia 85 ya viwango vya soko ifikapo mwaka 2011. Ongezeko hili litapandisha kodi kutoka asilimia 40 ya bei ya soko hadi kufikia asilimia 55 ya viwango vya soko. Madhumuni ya kuongeza kodi, ni kuongeza mtaji ili Shirika liweze kujenga nyumba zaidi na kuzifanyia matengenezo nyumba zake. Napenda kutoa wito kwa wapangaji kulipa kodi hizi mpya kwa kuwa ongezeko lake bado ni dogo sana likilinganishwa na kodi inayotozwa kwenye sekta binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya Sheria ya Mikopo ya Nyumba kuanza kufanya kazi pamoja na ile ya kumilikisha Sehemu ya Majengo, mwelekeo wa shirika hili utabadilika kabisa kutoka kwenye mwelekeo wa kupangisha nyumba na kukusanya kodi *(Land Lord)* na kuwa na mwelekeo sasa wa kufanya biashara ya kujenga nyumba na kuuza nyumba kwa wananchi *(Estate Developer).* Kwa msingi huu, Shirika la Nyumba la Taifa litauza baadhi ya Nyumba zake. Narudia, baadhi sio zote kwa wapangaji wake. Baadhi ya Nyumba zilizopo katika maeneo muhimu kiuchumi (*prime areas)* zitajengwa upya ili zihudumie watu wengi zaidi na kuingiza mapato makubwa zaidi. Pia, baadhi ya nyumba kwa sasa zitabaki bila kuuzwa ili zitumike kama dhamana ya kupatia mikopo katika mabenki.

Mheshimiwa Spika, huduma za utawala na rasilimali vatu, Wizara yangu imeendelea kutoa huduma za utawala na usimamizi wa rasilimali kwa madhumuni ya kuboresha utendaji kazi na kuongeza ufanisi. Katika mwaka wa fedha 2008/2009 Wizara imeendelea kuimarisha utawala bora kwa watumishi kuzingatia maadili mema ya utendaji, kuondokana na vitendo vya rushwa, kujali wateja na kutoa huduma kwa wakati. Vilevile Wizara yangu iliendeleza mapambano dhidi ya UKIMWI kwa kuhamasisha watumishi kujikinga na kupima afya zao.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2008/2009 Wizara yangu iliandaa mpango wa rasilimali watu ili kubaini mahitaji halisi ya watumishi, sifa na ujuzi wa watumishi waliopo na ujuzi zaidi utakaohitajika kutekeleza majukumu ya Wizara kwa ufanisi zaidi. Jumla ya watumishi wapya 110 waliajiriwa, watumishi 140 walipandishwa vyeo na watumishi 110 walipelekwa mafunzoni. Katika mwaka wa fedha 2009/2010 Wizara inatarajia kuajiri watumishi wapya 112 na kuwapatia mafunzo watumishi 150.

Mheshimiwa Spika, ili kushughulikia tatizo la uhaba wa watumishi wa Sekta ya Ardhi katika Halmashauri zote nchini, Wizara yangu imetoa mwongozo wa idadi stahiki ya watumishi wa Sekta ya Ardhi, sifa na vitendea kazi muhimu kwa Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, inayosimamia Halmashauri nchini. Utekelezaji wa mwongozo huo utafanyika kwa ushirikiano kati ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na HAZINA. Kwa mwaka 2009/2010, Halmashauri zote zinategemewa kuomba ikama ya kuajiri watumishi wanaohitajika ili kukidhi mahitaji makubwa yaliyopo. Aidha, Wizara yangu imetoa ombi na ushauri kwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwamba ione uwezekano wa kuruhusu wataalam wa ardhi waajiriwe moja kwa moja kutoka vyuoni na kupangiwa vituo vya kazi kwenye Halmashauri mbalimbali ili kukabiliana na tatizo sugu la upungufu wa wataalam hawa katika Halmashauri zote nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuweka mazingira bora ya kazi, Wizara yangu inaendelea na ukarabati wa jengo la Wizara. Ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, Wizara imeendelea kununua vitendea kazi kama vile vyombo vya usafiri, kompyuta, samani na vifaa vingine vya kitaalamu.

Mheshimiwa Spika, Usimamizi wa Rasilimali, katika mwaka 2008/2009 Wizara imeendelea kusimamia vyema rasilimali zake kwa kutumia mfumo wa kielektroniki uitwao *Facility Management Tool*. Mfumo huu umewezesha kuhifadhi na kutunza kumbukumbu za rasilimaliwatu *(Human Resource Management)*, kumbukumbu za masjala *(Records Management)*, vitendea kazi kama magari *(Vehicles Management)*, kompyuta, samani *(Asset Management)*, kumbukumbu za wateja wanaofika Wizarani *(Visitors Management)*. Kuwepo kwa mfumo huu wa usimamizi wa rasilimali kunawezesha kufanya maamuzi sahihi ya matumizi ya rasilimali zilizopo.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha huduma na uhusiano baina ya Wizara na wateja, Wizara yangu imeendelea kutoa mafunzo kwa watumishi waliopo na wapya juu ya huduma bora kwa mteja *(Customer Care Awareness)* na kutumia Mkataba wa Huduma kwa Mteja *(Client Service Charter)*. Katika jitihada za kuboresha mapokezi ya

wateja wetu Wizara imebuni mfumo wa kompyuta *(visitors management tool)* wa kuweka kumbukumbu za wageni wanaofika Wizarani kupata huduma. Kati ya mwezi Januari na Juni, 2009, jumla ya wateja 243,080 walifika Wizarani sawa na wastani wa wateja 740 kwa siku. Aidha, Wizara yangu imeendelea kupokea na kuyashughulikia malalamiko ya wateja kwa njia mbalimbali ikiwepo njia mpya ya kielektroniki iitwayo *Complaints Management Tool.* Katika mwaka 2008/2009 jumla ya malalamiko 3,975 yalipokelewa na 2,857 yameshughulikiwa na kupatiwa ufumbuzi, hii ni sawa na asilimia 71.8 ya malalamiko yaliyopokelewa.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza malengo ya Milenia ya kuhakikisha afya bora kwa watumishi, Wizara imeendelea na mkakati wake wa kuwaleta watoa ushauri nasaha na kupima UKIMWI kwa hiari kila baada ya miezi mitatu, huduma ya dawa na lishe imeendelea kutolewa kwa watumishi wanaoishi na virusi vya UKIMWI kila mwezi. Kwa mwaka wa fedha 2009/2010, Wizara yangu itaendeleza kasi ya mapambano dhidi ya maambukizi ya virusi vya UKIMWI.

Mbali na kupambana na maambukizi ya UKIMWI, Wizara yangu imeanzisha utaratibu wa kupima afya za watumishi kwa magonjwa kama kisukari, moyo na shinikizo la damu ili kudumisha afya za watumishi ambayo ni nguvu kazi muhimu ya Wizara. Wizara vilevile imeanzisha utaratibu wa kukagua mazingira ya kazi ya wafanyakazi ili kuchukua hatua za kuwakinga na madhara yanayoweza kuathiri afya zao.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa habari sahihi na kwa wakati ni muhimu sana katika kudumisha Utawala Bora na Uwajibikaji. Katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu imeendelea kuboresha mawasiliano kwa umma kwa njia ya redio na televisheni pamoja na kushiriki katika maonyesho mbalimbali ya kitaifa kama vile wiki ya Utumishi wa Umma na Nane Nane. Lengo ni kuwaelimisha wananchi juu ya huduma mbalimbali zinazotolewa na Wizara. Kwa mwaka wa fedha 2009/2010, Wizara yangu itaendelea kuboresha mawasiliano kwa kutoa elimu kwa umma kwa njia mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeendelea kuvisimamia Vyuo vya Ardhi vya Tabora na Morogoro ambavyo vinatoa mafunzo ya upimaji ardhi na urasimu ramani katika ngazi ya Diploma, umiliki ardhi na uthamini pamoja na uchapaji ramani katika ngazi ya cheti. Jumla ya wahitimu 104 wanategemewa kuhitimu katika mwaka wa fedha 2008/2009 katika vyuo vyote viwili. Kwa mwaka wa fedha 2009/2010, Vyuo vitaendelea kutoa mafunzo kwa wanafunzi 200 katika fani zinazosimamiwa na vyuo hivyo na kuboresha mitaala hiyo ili kuendana na mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia. Aidha, katika mwaka wa fedha 2009/2010 Wizara itaanza mpango wa kukipanua Chuo cha Ardhi Tabora ili kuongeza idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa kwa kozi zinazotolewa katika chuo hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ardhi ya Tanzania ina ukubwa wa Kilomita za mraba 942,600, kati yake kilomita za mraba 888,200 ni eneo la nchi kavu. Ardhi hii ndiyo

rasilimali ya msingi inayowezesha kutumika kuleta maendeleo kupitia sekta zote. Hata hivyo ili ardhi iweze kutumika kuleta maendeleo ni lazima kila kipande kitambuliwe, kipimwe, kimilikishwe na kipangiwe matumizi. Changamoto inayotukabili ni kuwa mpaka sasa ardhi iliyopimwa na kumilikishwa inakadiriwa kuwa asilimia moja tu ya ardhi yote. Matokeo ya hali hii ni kutumia ardhi hiyo bila mipango stahiki, kutokutumia ardhi iliyopo kikamilifu na kuongezeka kwa migogoro baina ya watumiaji mbalimbali. Ili kukabiliana na changamoto hiyo Wizara kwa kutumia mkopo wa Benki ya Dunia imeanza kuweka Mfumo wa Alama za Msingi wa upimaji ardhi na utayarishaji wa ramani *(Geodetic Reference Frame)* ambao utawezesha kuharakisha upimaji ardhi kwa gharama nafuu na utayarishaji wa ramani. Pamoja na mkopo wa Benki ya Dunia, Serikali Kuu na Serikali za Mitaa haina budi kuwekeza katika upimaji wa ardhi, utayarishaji ramani upangaji wa matumizi ya ardhi na umilikishaji ardhi kwa wananchi Mijini na Vijijini.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kwamba sehemu kubwa ya nchi yetu haijapimwa, wananchi wengi hawana hatimiliki, leseni za makazi, wala hatimiliki za kimila. Hivyo, hawanufaiki na mikopo kwa kukosa dhamana. Changamoto iliyopo kwa Serikali na Wizara yangu ni kuandaa nyaraka hizo na kuzitoa kwa wananchi pale ambapo ardhi hiyo imeshapimwa. Kwa sasa wanachi wanashindwa kutumia rasilimali ardhi kujiletea maendeleo yao ya kiuchumi na kijamii jambo ambalo linachelewesha vita vya kujiondoa katika umasikini.

Mheshimiwa Spika, maendeleo endelevu ya ardhi hayawezi kupatikana bila ya kuwa na mipango ya matumizi bora ya ardhi. Ardhi iliyopangiwa matumizi inaweza kutumika kikamilifu kwa malengo yaliyowekwa. Changamoto iliyopo ni kwamba vijiji na Wilaya nyingi hazina mipango hiyo. Ili kukabiliana na changamoto hizo Wizara kupitia TUME ya Matumizi ya Ardhi ikishirikiana na wadau mbalimbali imeanzisha programu zinazowezesha kupanga mipango ya matumizi ya ardhi kwa vijiji na Wilaya. Hata hivyo, kasi ya utekelezaji wa mipango hiyo ni ndogo kutokana na ukosefu wa fedha za kutosha. Changamoto iliyopo ni kwa Halmashauri na Wizara mbalimbali kutenga fedha kila mwaka kutekeleza programu mbalimbali chini ya Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilianzisha mfumo wa utatuzi wa migogoro ya ardhi na nyumba unaoanzia ngazi ya Kijiji hadi Taifa. Changamoto iliyopo ni kuwa mfumo huu bado haufanyi kazi kwa ufanisi. Mabaraza ya Ardhi ya vijiji na Kata hayajaimarishwa ipasavyo kuweza kufanya kazi kwa ufanisi. Katika ngazi ya Wilaya Mabaraza ya Ardhi na Nyumba yanaundwa kwa awamu kutokana na uwezo mdogo wa Serikali. Kwa sababu hiyo, mabaraza hayo yanakabiliwa na mlundikano wa mashauri yanayofunguliwa ama moja kwa moja au kwa njia ya rufaa. Pamoja na changamoto hiyo, Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI inaendelea kutoa mafunzo kwa viongozi wa Mabaraza ya Vijiji na Kata. Kwa upande wa mabaraza ya Wilaya, kupitia mkopo wa Benki ya Dunia, Wizara imewezesha baadhi ya Mabaraza ya Wilaya kupunguza mlundikano wa mashauri.

Mheshimiwa Spika, Serikali inahitaji akiba ya ardhi kwa ajili ya shughuli mbalimbali zikiwa ni pamoja na uwekezaji, huduma za kijamii, ofisi za Mabalozi na kutekeleza miradi maalum. Changamoto inayotukabili ni kutokuwepo kwa ardhi kwa ajili ya matumizi hayo. Hii ni kutokana na uwezo mdogo wa Serikali kulipa fidia na kupima. Ili kukabiliana na changamoto hii, Wizara inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanzisha Hazina ya Ardhi *(Land Bank).*

Mheshimiwa Spika, gharama za fidia kwa wananchi zinalipwa kwa kuzingatia mahali ardhi ilipo, maendelezo na gharama nyinginezo kulingana na uthamini uliofanyika kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999. Changamoto iliyopo ni wananchi kulalamikia viwango vya malipo ya fidia. Kutokana na changamoto hiyo, Wizara chini ya Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali inaandaa utaratibu wa kuhuisha viwango vya fidia ili kuendana na mabadiliko ya bei za soko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika miji yetu kuna kasi kubwa ya ongezeko la idadi ya watu mijini ikilinganishwa na uwezo wa kukidhi mahitaji husika ya ardhi na miundombinu. Ongezeko hilo linakadiriwa kuwa la wastani wa asilimia 6.0 kwa mwaka, kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2002. Hivi sasa inakadiriwa kuwa zaidi ya Watanzania 10,375,000 wanaishi mijini ambao ni sawa na asilimia 25 ya idadi ya watu wote nchini (ambao ni takribani milioni 41.5). Changamoto iliyopo ni kuwepo kwa ongezeko la ujenzi holela mijini ambapo asilimia zaidi ya sabini ya wakazi mijini wanaishi katika maeneo hayo na Vijiji vinavyokua haraka na kuchukua sura ya kimji. Ili kukabiliana na hali hiyo, Serikali imefanya jitihada mbalimbali za kurasimisha makazi yasiyopangwa na kutoa leseni za makazi na kuandaa hati za kumiliki ardhi. Vilevile, Serikali inaboresha miundombinu ya msingi katika maeneo hayo. Katika maeneo mengine ya Miji, Serikali inaendelea kuandaa mipango ya muda mrefu na ya kina ili kupunguza kasi hiyo. Pamoja na juhudi zote hizo changamoto za kuendeleza miji iliyopangwa ni kubwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi zinazofanywa na Wizara yangu ikishirikiana na Halmashauri kuhusu kumilikisha ardhi kwa wananchi mijini, bado ipo changamoto ya kumilikisha ardhi iliyokwishapimwa na kuwepo na utunzaji hafifu wa kumbukumbu za ardhi. Juhudi zinazochukuliwa ni pamoja na kufupisha mlolongo mrefu wa umilikishaji kwa kuondoa barua ya toleo na kusogeza huduma za sekta ya ardhi kwenye ngazi za Kanda. Juhudi nyingine ni kulinda usalama wa hatimiliki kutokana na wimbi la matapeli wanaoghushi nyaraka ambapo hati mpya zinaandaliwa kwa kutumia teknolojia ya kompyuta na kuimarisha mfumo wa kumbukumbu *(database).*

Mheshimiwa Spika, licha ya kuanzishwa kwa Idara ya nyumba katika Wizara yangu, bado sekta ya nyumba inakabiliwa na changamoto ya kutokuwepo kwa mfumo wa kiutawala kuhusu uendelezaji wa nyumba katika ngazi za Halmashauri za Miji na Wilaya. Uendelezaji wa nyumba umeendelea kubaki kuwa ni jukumu la mtu mmoja mmoja bila uratibu, miongozo na udhibiti kutoka Serikalini. Pia, pamoja na kuwa na Sheria ya Mikopo ya Nyumba, wananchi walio wengi hasa wa kipato cha chini hawatafaidika na mikopo hiyo kutokana na masharti ya kuwa na mali isiyohamishika (nyumba) na kipato kisichokuwa cha uhakika cha kila mwezi cha kuwezesha kulipia mkopo. Hivyo, Serikali itaendelea kuandaa mfumo utakaowawezesha wananchi kuishi

kwenye nyumba bora ikiwa ni pamoja na kuanzisha ushirika wa ujenzi wa nyumba na vikundi vingine vya ujenzi wa nyumba vilivyo karibu na wananchi.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Nyumba la Taifa, Shirika la Nyumba la Taifa lina uwezo wa rasilimali ya majengo yenye thamani kubwa. Hata hivyo, shirika halijaweza kutoa mchango unaotarajiwa kwenye sekta ya makazi na uchumi wa Taifa. Changamoto iliyopo ni kulibadilisha Shirika kutoka katika hali yake ya sasa ya mpangishaji wa nyumba na kulifanya litumie majengo yake katika mfumo wa biashara ya kujenga na kuuza nyumba ili kukuza mtaji wake na hivyo kupata uwezo wa kuwekeza zaidi katika maendeleo ya makazi nchini.

Mheshimiwa Spika, wakala umekuwa ukifanya juhudi kubwa za kutafiti na kusambaza matokeo ya tafiti zinazofanywa kwa wananchi. Changamoto iliyopo ni kuwa baada ya kukamilisha utafiti hakuna mfumo wa kupokea matokeo ya tafiti hizi na kuzipeleka kwenye viwanda vya uzalishaji au wajasiriamali ili teknolojia hii iwafikie wananchi. Kwa mfano, kwa sasa mahitaji ya mashine za kutengeneza matofali yanayofungamana ni makubwa kuliko uwezo wa wakala lakini hakuna kiwanda kilichotayari kupokea teknolojia hiyo ya kuzalisha mashine za kuweza kukidhi mahitaji ya soko.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi napenda kuwashukuru kwa dhati wale wote walioshirikiana nasi katika kipindi cha mwaka 2008/2009 katika kutimiza malengo yetu. Shukurani zetu pia ziwaendee washiriki wetu wa maendeleo *(Development Partners)* wanaoshirikiana nasi katika kutekeleza programu na mipango yetu ya Sekta ya Ardhi. Wahisani, taasisi za kimataifa, nchi na mashirika hayo ni pamoja na Benki ya Dunia, Shirika la Maendeleo la Ujerumani *(GTZ)*, Kamisheni ya Umoja wa Ulaya *(EU)*, Denmark, Uingereza, Sweden na Uholanzi kupitia Mradi wa "*Business Environment Strengthening for Tanzania*" *(BEST)* na Mkakati wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania (MKURABITA), *UN – Habitat* na *Investment Climate Facility (ICF).* Vilevile, natoa shukrani za pekee kwa Serikali ya Norway kwa kuisaidia Wizara kutekeleza mradi wa kuongeza eneo la ziada katika mpaka wetu ndani ya Bahari ya Hindi nje ya Ukanda wa Kiuchumi Baharini *(Extended Continental Shelf). (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwashukuru wananchi na wadau mbalimbali hasa sekta binafsi kwa ushirikiano wao katika kutekeleza malengo ya sekta ya ardhi. Shukurani za pekee ziwaendee Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa michango yao kupitia njia mbalimbali zikiwa ni pamoja na kuuliza maswali ambayo imechangia katika kuimarisha huduma zitolewazo na Wizara. Naomba mwendelee na moyo huo ili tuweze kuendeleza sekta hii ambayo ni muhimili wa shughuli za maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, shukurani zangu hazitakuwa kamili bila ya kuwashukuru viongozi wenzangu katika Wizara nikianzia na Katibu Mkuu Bibi Salome Sijaona. Aidha, nawashukuru Wakuu wa Idara, viongozi wa Taasisi zilizo chini ya Wizara, watumishi na wataalamu wote wa Wizara kwa kujituma katika kusimamia utekelezaji wa

majukumu ya Wizara. Naomba waendelee na juhudi hizo katika kipindi kijacho ili tuweze kutekeleza malengo tuliyojiwekea kwenye sekta yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kufuatia mwelekeo wa Serikali wa kuelekeza nguvu zake katika kuimarisha kilimo, kupitia kauli mbiu ya “Kilimo kwanza” , Wizara yangu ina jukumu kubwa la kuhakikisha kuwa ardhi inamilikishwa kwa wakulima wadogo, kwa kutoa hatimiliki za kimila kwa mashamba yao, pia kutenga maeneo *(Land Bank)* kwa ajili ya mashamba makubwa na viwanda vya mazao yatokanayo na kilimo. Aidha, matumizi mengine makubwa ya ardhi yakiwemo ya uendelezaji wa nyumba *(Real Estate Development),* mahoteli, viwanda na kadhalika yanatengewa maeneo. Haya yote yatatekelezwa iwapo HAZINA ya ardhi itaanzishwa na kuimarishwa.

Vilevile, baada ya kukamilika kwa Mpango wa Taifa wa Matumizi Bora ya Ardhi, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri na wadau wengine ina jukumu la kuhakikisha kuwa maeneo yenye migongano na migogoro sugu ya matumizi ya ardhi yanapatiwa ufumbuzi. Kufuatia hili, Wizara yangu itaendelea kushirikiana na Halmashauri kuhakiki, kupima, kupanga matumizi ya ardhi, kusajili na kutoa hati katika maeneo hayo ili kuwezesha kuwepo kwa usalama wa milki na hivyo kuondoa migogoro kati ya watumiaji mbalimbali wa ardhi.

Natoa rai kwa Mamlaka na Taasisi mbalimbali kutoa ushirikiano unaotakiwa kuhakikisha kuwa ardhi inaziwezesha sekta zote kwa lengo la kuwaondolea wananchi umaskini.

Mheshimiwa Spika, maombi ya fedha kwa mwaka 2009/2010, ili Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi iweze kutekeleza majukumu na malengo yake ya mwaka 2009/2010, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishe Makadirio ya Mapato na Matumizi kama ifuatavyo:-

Mapato ya Serikali Sh. 15,550,006,000/=. Matumizi ya Kawaida; Matumizi ya Mishahara Sh. 5,962,158,000/= Matumizi Mengineyo *OC* Sh. 15,507,598,000/=. Jumla Sh. 21,469,756,000/=. Matumizi ya Maendeleo Sh. 12,013,543,000/=. Jumla ya Matumizi ya Mishahara, Matumizi Mengineyo na Matumizi ya Maendeleo ni Sh. 33,483,299,000/=.

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru tena wewe na pia Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara kwa anuani ya *www.ardhi.go.tz.*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAWASILIANO SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa hotuba nzuri kabisa. Sasa namwita Mheshimiwa Mwenyekiti au Mwakilishi

wake kwa ajili kutupatia maoni ya Kamati, ni Mheshimiwa Lucas Selelii kwa niaba ya Mwenyekiti.

**MHE. LUCAS L. SELELII - (K.n.y. MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 99(7) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kuhusu, utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009 na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti na Wanakamati wenzangu, napenda kumpongeza Mheshimiwa *Capt*. John Z. Chiligati, kwa kazi nzuri anayoiendeleza katika kuingoza Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, pamoja na Ndugu Salome Sijaona kwa kuendelea kuwa Katibu Mkuu wa Wizara hiyo. Mwenyezi Mungu awatangulie na kuwalinda katika utekelezaji wao wa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa kwa kushinda katika uchaguzi jimboni Biharamulo, hongera sana na Kamati yangu kwa ujumla inakutakia kila la kheri katika kuwakilisha wananchi wako wa Biharamulo na watanzania wote kwa ujumla katika Bunge letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ina idara saba na vitengo tisa, Idara hizo ni Maendeleo ya Huduma ya Ardhi, Upimaji wa Ramani, Maendeleo ya Nyumba, Sera na Mipango, Utawala na Utumishi, Mifumo ya Habari na Mawasiliano na Idara ya Upangaji wa miji na Vijiji. Aidha, Wizara inazo Taasisi na Mashirika yanayofanya shughuli zake chini ya uangalizi wa jumla wa Wizara ambayo ni Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Wakala wa Taifa wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi *(NHBRA),* Chuo cha Ardhi Tabora na Chuo cha Ardhi Morogoro.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ilikutana na watendaji wakuu wa Wizara hii wakiongozwa na Mheshimiwa Waziri katika Ofisi za Bunge Mjini Dodoma. Katika kikao hicho, Kamati ilipitia utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa Mwaka 2008/2009, pia ilipitia makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2009/2010. Aidha majadiliano yalifanyika kwa kuzingatia yafuatayo:-

- Dira ya Wizara ambayo ni kuwa mlezi/msimamizi wa uhakika wa hakimiliki ya ardhi, nyumba bora na zenye hadhi na makazi endelevu kwa ajili ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi;
- Dhima ya Wizara;
- Uongozi na Muundo wa Wizara;
- Majukumu ya Idara na Vitengo mbalimbali Wizarani;
- Maelezo ya Taasisi zilizo chini ya Wizara;
- Utekelezaji wa maagizo mbalimbali ya Kamati ya Bunge katika mwaka wa fedha 2008/2009; na

- Kazi zilizopangwa kufanyika katika mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, katika kujadili bajeti ya Wizara hii, Kamati ilipata maelezo ya kina toka kwa Mheshimiwa Waziri, alieleza kwamba maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Mwaka 2009/2010 chini ya Mpango wa Muda wa Kati wa Bajeti *(MTEF)* yamezingatia maelekezo mbalimbali ya Serikali, bei katika soko na vipaumbele ambavyo Wizara imejiwekea.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kwa Wizara kwa mwaka wa fedha 2008/2009. Katika mwaka wa fedha 2008/2009 Wizara hii iliidhinishiwa kiasi cha Sh. 9,388, 868,000/= kwa ajili ya miradi ya maendeleo hadi kufikia Mei, 2009, Wizara imepokea jumla ya Sh. 6, 504, 539,497 sawa na asilimia 69.3 tu ya fedha za miradi.

Mheshimiwa Spika, jumla ya Sh. 12,629,747,356/= ambazo ni maduhuli ya Serikali zimekusanywa kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato. Kiasi kilichokusanywa ni sawa na asilimia 69.4 ya lengo la mwaka. Kati ya makusanyo hayo, Sh. 11, 472, 980,777/= ambazo ni sawa na asilimia 90.8 ni mapato yanayotokana na kodi ya pango la ardhi.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa fedha uliopita Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ilitoa maoni, ushauri na maagizo katika maeneo mbalimbali kuhusiana na sekta ya ardhi, Shirika la Nyumba la Taifa*(NHC)* na taasisi mbalimbali zilizo chini ya Wizara. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara kwa kiasi kikubwa imefanyia kazi maeneo husika na hatua za utekelezaji zimeonekana. Hata hivyo, katika maeneo mbalimbali, mfano mipango miji, pango za nyumba, mipaka na migogoro ya ardhi ambayo Kamati imeona juhudi zaidi zinahitajika.

Mafanikio na changamoto katika utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2008/2009, Mafanikio, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imeweza kutekeleza maoni na ushauri wa Kamati yako tukufu ya Bunge kama ifuatavyo:-

i) Jumla ya taarifa za wamiliki 60,160 kutoka katika miji saba ya Babati, Bukoba, Ujiji, Lindi, Singida, Songea na Sumbawanga zilitambuliwa na kuingizwa kwenye kompyuta, sawa na asilimia 68 ya lengo la kutambua wamiliki 88,400;

ii) Kupima mipaka ya vijiji 478 sawa na asilimia 95.6 ya lengo la kupima vijiji 500 kwa mwaka. Upimaji wa mipaka ya vijiji ulifanyika katika wilaya za Tandahimba (vijiji 126), Newala (vijiji 123), Masasi (vijiji 107), Nanyumbu (vijiji 72) na Tunduru (vijiji 50);

iii) Jumla ya hati miliki 13, 476 zilisajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Hati. Hii ni sawa na asilimia 112.3 ya lengo la kusajili hati miliki 12,000 lililowekwa kwa mwaka;

iv) Jumla ya mashauri 9,228 yalifunguliwa katika Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya yaliyo 39 nchini kote. Kati ya mashauri hayo, mashauri 6873 yalitolewa maamuzi (kuamuliwa) na mashauri 11,279 yanaendelea kushughulikiwa. Kesi zilizoamuliwa ziliongezeka kwa asilimia 136.8 ikilinganishwa na lengo la kuamua kesi 5000 lililowekwa kwa mwaka;

v) Wizara imezikopesha Halmashauri za Miji na Wilaya, fedha kwa ajili ya kupima viwanja kupitia mfuko wa Mradi wa kupima viwanja Dar es Salaam na kupitia mfuko wa Mzunguko wa kupima viwanja Mijini. Mpaka kufikia sasa jumla ya fedha iliyotolewa ni kiasi cha Sh. 3.9 bilioni na viwanja vilivyopimwa kutokana na mifuko hii ni 21,600.

vi) Jumla ya vyeti vya Ardhi ya kijiji 2,173 na hati miliki za kimila 17,471 ziliandaliwa na kutolewa kwa wananchi.

vii) Jumla ya Mabaraza 39 yameundwa ili kusimamia mashauri/malalamiko ya ardhi kwa kuzingatia haki na sheria za ardhi zilizopo ili kupunguza migongano na migogoro ya ardhi.

viii) Elimu kwa umma imekuwa ikitolewa kwa wananchi kwa kupitia vyombo vya habari kama redio, televisheni, magazeti na mahojiano ya moja kwa moja na watendaji wakuu wa Wizara kwa mfano katika kipindi cha TUAMBIE. Hii ni katika kuwasaidia wananchi kupata uelewa wa haki zao za ardhi.

ix) Kuanza kwa ujenzi wa jumla ya nyumba 40 katika eneo la Medeli - Dodoma. Ujenzi huu unakusudia kukidhi mahitaji ya nyumba Mkoani Dodoma ambapo kuna ongezeko la watu kutokana na Vyuo vilivyopo na kuongezeka kwa Ofisi za Serikali na Mashirika.

x) Wizara imeendelea kutoa elimu ya namna ya kujikinga na ugonjwa wa UKIMWI kwa watumishi wake ili kuepuka maambukizi.

xi) Jumla ya watumishi saba walichukuliwa hatua za kinidhamu kutokana na kukiuka maadili ya kazi zao.

xii) Jumla ya watumishi 110 walihudhuria mafunzo ndani na nje ya nchi na pia watumishi 284 walioajiriwa mwaka jana walipatiwa mafunzo ya huduma kwa wateja. Mafunzo haya yalilenga kuongeza ufanisi wa kazi na taaluma zao.

Mheshimiwa Spika, changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa Bajeti ya 2008/2009, pamoja na jitihada zilizofanywa na Wizara katika utekelezaji wa Bajeti ya 2008/2009, Wizara iliendelea kukabiliwa na changamoto zifuatazo:-

i) Ukosefu wa wataalam wa kutosha katika sekta ya Ardhi hususan kwenye Halmashauri za Miji na Wilaya.

ii) Sekta ya Ardhi kuendelea kutopewa kipaumbele katika mgawanyo wa rasilimali.

iii) Ukosefu wa takwimu za milki za viwanja hali inayosababisha utoaji wa viwanja pandikizi *(double allocation)* pamoja na ukwamishaji wa upatikanaji wa mapato ya kutosha.

iv) Ukosefu wa mfumo rasmi unaowezesha wananchi kujenga nyumba kwa kutumia mikopo ya muda mrefu.

v) Wananchi kutokujua na kutotumia vifaa vya ujenzi wa nyumba bora na za gharama nafuu vilivyotafitiwa na Wakala (*NHBRA*).

vi) Uhaba wa nyumba kwa ajili ya makazi na biashara katika miji mikubwa na inayokua kwa kasi nchini.

vii) Kuongezeka kwa migogoro ya ardhi mahali ambapo inatekelezwa miradi ya kupima viwanja na upangaji wa miji.

viii) Wananchi wengi hawajaelewa matakwa ya Sera, Sheria za Adrhi na Mipango Miji Uhaba wa viwanja vilivyopimwa na vyenye huduma.

ix) Uhaba wa Rasilimali fedha na watu katika kusimamia na kudhibiti maendeleo ya miji na vijiji.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu imeridhika na namna Wizara inavyojitahidi kutatua baadhi ya matatizo yanayoikabili Wizara pamoja na Taasisi zake zilizo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo na ushauri wa Kamati kwa mwaka wa fedha 2008/2009, Sekta ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ni Sekta ambayo inahusu hali halisi ya kila siku ya maisha ya binadamu. Ni vyema Sekta hii ikaangaliwa kwa umakini kutokana na ukweli kwamba binadamu anategemea sana ardhi katika kupata riziki yake pamoja na malazi. Kwa kuzingatia hayo Kamati ina ushauri na mapendekezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, suala la ujenzi wa nyumba bora limepata mwamko mkubwa miongoni mwa wananchi wa Tanzania. Kamati inaishauri Serikali kuharakisha ukamilishaji wa Sera ya Taifa ya Nyumba ili wananchi wapate mwongozo bora wa ujenzi wa nyumba.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa kuboresha maisha bora kwa kila Mtanzania ni jambo linalotakiwa kupewa kipaumbele. Katika kuboresha maisha hayo ya Mtanzania ni

vema kila mwananchi akafaidika na mpango wa kujenga nyumba na kukodisha ama kuuza unaotekelezwa na Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC).* Kamati inashauri Serikali kuhakikisha inatenga maeneo ya wazi maalum kwa ajili ya michezo ya watoto *(Play grounds)* na shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC)* ndio Shirika la kwanza la umma kuanzishwa mara tu baada ya uhuru wa Tanganyika, kwa msingi kwamba binadamu ana mahitaji ya lazima kwa ajili ya uhai ambayo ni malazi (nyumba), chakula na mavazi. Kwa kuzingatia umuhimu wa Shirika hili Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha watumishi wote wa Shirika na Wizara wanatimiza wajibu wao kwa mujibu wa Sheria za Kazi, aidha, wale watakaobainika kuwa wabadhirifu wachukuliwe hatua haraka.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali iorodheshe idadi ya nyumba zote zilizokuwa chini ya Msajili wa Majumba na idadi ya wapangaji wote wa nyumba hizo, aidha, ripoti ya namna wanavyolipa pango za nyumba hizo iwasilishwe mbele ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni pametokea migogoro ya ardhi na mipaka baina ya Shirika la Hifadhi za Taifa na wananchi wanaozunguka maeneo ya hifadhi ya Ruaha kwa upande wa Wilaya ya Mbarali. Kamati inashaiuri Wizara kushirikiana na *TANAPA* katika kutafuta ufumbuzi wa tatizo hili. Aidha, watendaji wa Wizara ya Ardhi wanaohusika na uwekaji wa mipaka katika maeneo mbalimbali wahakikishe wanatekeleza wajibu wao kwa usahihi ili kupunguza migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, migogoro mingi ya ardhi nchini inasababishwa na baadhi ya watendaji katika ngazi mbalimbali za usimamizi wa ardhi kutokufuata sheria za ardhi, ingawa sheria mpya zipo na ni nzuri kutumika kwa mazingira ya sasa. Kutokana na kutokufuata sheria za sasa, vitendo vya utekelezaji wa sera mbalimbali za ardhi vimekuwa haviendi sambamba na sera hizo na sheria, matokeo yake kumekuwa na migogoro ya ardhi na mianya ya rushwa hasa katika masuala ya upangishaji na ujenzi wa nyumba na umilikishaji wa ardhi. Baadhi ya mambo yanayokiuka sheria ni ujenzi wa uzio na hoteli kwenye fukwe za bahari na kuzuia watu kuingia baharini wakati sheria ya ardhi inasema fukwe zinatakiwa kuwa huru kwa kila mwananchi kwenda kupumzika. Kamati inashauri Serikali kuchukua hatua za kisheria kwa wadau wote wanaokiuka Sheria mbalimbali za Ardhi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inasisitiza Wizara iendelee kuongeza juhudi kutoa elimu kwa umma hasa katika upande wa Sera na Sheria zinazohusu utumiaji, uhifadhi na utoaji wa ardhi ili wananchi waelewe zaidi haki zao za umilikaji wa ardhi.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Mwaka 2007 inaipa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi uwezo wa kuratibu utayarishaji na utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi na kuhamasisha umma kushiriki kwenye utekelezaji huu. Kamati inasisitiza kwamba Tume iharakishe kutekeleza Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi katika ngazi zote na hasa maeneo ya migodi ili kukabiliana na uharibifu mkubwa wa mazingira unaotokea katika maeneo mbalimbali hasa ya migodi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Wizara kupitia wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi (*NHBRA*) kuanzisha kanda maalum kwenye maeneo mbalimbali ya Tanzania ambazo zitakuwa zinarahisisha wananchi kujua matokeo ya utafiti wa mbinu mbalimbali za kuinua hali ya makazi ya wananchi kwa kutumia vifaa vya ujenzi vya gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, Wizara iendelee kusimamia na kuwahimiza watumishi wake kujilinda na ugonjwa wa UKIMWI ili kuepuka maambukizi mapya na upungufu wa nguvu kazi.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefurahishwa na mkakati wa mpango wa kuendeleza maeneo ya pembezoni mwa Jiji la Dar es Salaam (Luguruni Kata ya Kibamba) ambao Serikali imeuandaa kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ikishirikiana na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na Manispaa zake. Mpango huu ni changamoto kubwa ya kuhakikisha miji mipya iliyopangwa vizuri inajengwa.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Wilaya zetu hapa nchini bado zina uhaba mkubwa wa Mabaraza ya Ardhi ya Kata hivyo kusababisha malalamiko na kesi nyingi zinazohusu masuala ya ardhi kuchukua muda mrefu kusuluhishwa. Kamati inapendekeza kuwepo na kipaumbele katika kuanzisha mabaraza haya ya kata ya ardhi, ili kupunguza migogoro mingi ambayo kwa sasa inatatuliwa kimila zaidi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kutopunguza vyuo vya ardhi vilivyopo hapa nchini badala yake Serikali kwa kipindi kijacho cha fedha itenge bajeti ya kutosha kuhakikisha vyuo hivyo vinatoa elimu ya kutosha ili kuongeza idadi ya wataalam wa ardhi hapa nchini, ambao wamekuwa adimu hasa kwenye halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, maombi ya fedha kwa mwaka 2009/2010. Makadirio ya Mwaka wa fedha 2009/2010 ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi yameandaliwa kwa kuzingatia matakwa ya mwongozo wa utayarishaji wa bajeti kitaifa na maeneo ya kipaumbele yanayolenga katika kutekeleza sera na mikakati ya Wizara. Baada ya uchambuzi wa kina, Kamati inakubaliana na Makadirio ya Bajeti ya Wizara, Fungu 48, jumla ya Sh. 33,483,299,000/= kati ya hizo, Sh. 12,013,543,000/= ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo, Sh. 15,507,598,000/= ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na Sh. 5,962,158,000 ni kwa ajili ya matumizi ya mishahara.

Mheshimiwa Spika, Hivyo Kamati inaliomba Bunge lako tukufu lijadili na kupitisha fedha zinazoombwa.

Mheshimiwa Spika, aidha napenda kuwatambua Wajumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ambao ndio waliochambua bajeti hii nao ni Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mheshimiwa Hassan R. Khatib, Mheshimiwa Fuya G. Kimbita, Mheshimiwa . James Daudi Lembeli, Mheshimiwa William V. Lukuvi, Mheshimiwa Zakia Hamdani Meghji, Mheshimiwa Mariam Salum Mfaki, Mheshimiwa Dkt. Charles O. Mlingwa, Mheshimiwa Raynald Alfons Mrope, Mheshimiwa Prof. Raphael B. Mwalyosi,

Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo, Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, Mheshimiwa Hadija Saleh Ngozi, Mheshimiwa Juma Suleiman N'hunga, Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Lucas Lumambo Selelii, Mheshimiwa Jacob Dalali Shibiliti, Mheshimiwa Dkt. Guido G. Sigonda, Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud, Mheshimiwa Anastazia J. Wambura, Mheshimiwa Aziza S.Ally, Mheshimiwa Lucy T. Mayenga na Mheshimiwa Michael Lekule Laizer.

Mheshimiwa Spika, Hitimisho. Kwa niaba ya Wanakamati wenzangu, napenda kumshukuru Mheshimiwa Kapteni Mstaafu John Z. Chiligati - Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Katibu Mkuu wake Ndugu Salome Sijaona, Wakurugenzi wa Idara na Watumishi wote wa Wizara hii na Taasisi ama Mashirika yaliyo chini ya Wizara hii, kwa ushirikiano mkubwa walioipatia Kamati katika kipindi chote ambacho tumefanya nao kazi. Kamati inawashukuru sana na kuwatakia mafanikio makubwa zaidi katika kazi za Ujenzi wa Nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwashukuru Wajumbe wenzangu kwa ushauri na busara zao zilizoniwezesha kama Mwenyekiti wa Kamati kuiongoza Kamati hii. michango yao kwa wakati wote ilitolewa kwa uwazi na uadilifu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kumshukuru kwa dhati Katibu wa Bunge Dr. Thomas Kashililah na Makatibu wake wasaidizi wa Kamati hii Ndugu Michael Kadebe, Grace Bidya na Yona Kirumbi kwa kazi nzuri walioifanya ya kuratibu shughuli zote za Kamati, pia nawashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuihudumia Kamati ipasavyo katika hatua zote za maandalizi ya taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, na kwa niaba ya Kamati naunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Lucas L. Selelii kwa kuwasilisha mawazo au maoni ya Kamati na sasa namuita Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa masuala ya ardhi. Mheshimiwa John M. Cheyo!

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI - WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi hii kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2009/2010 kwa mujibu wa kanuni za Bunge kifungu cha 99(7) toleo la 2007.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote kwa nafasi ya kipekee kabisa naendelea kukishukuru Chama cha *United Democratic Party* (UDP) na wananchi wa Jimbo la Bariadi Mashariki kwa kunipa nguvu kwa kuniunga mkono ninapotetea hoja za matatizo yao, ardhi na michango lukuki, fidia ya mashamba na kadhalika. Nawashukuru Madiwani wote wa Bariadi wanavyonisaidia kuwatumikia wananchi wa Bariadi kwa wakati wote

nikiwa Bungeni, wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri Mheshimiwa Mathusela Matondo Diwani wa Dutwa (UDP).

Aidha, namshukuru Mke wangu mpenzi Elizaberth, watoto wetu wote na familia kwa kuwa msingi imara kwa kazi yangu ya Kibunge. Namshukuru kwa dhati Katibu wangu wa Jimbo - Mheshimiwa Diwani Njile Kingi Idebe kwa kunisaidia kuwatumikia wananchi wa Jimbo la Bariadi mashariki bila kuchoka.

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia nafasi hii kwa niaba ya wakulima wa Pamba jimboni na ni na hakika kwa niaba ya wakulima wote wa Pamba kumshukuru Rais na Waziri Mkuu na Serikali yote kwa kusikia kilio chetu cha bei ya Pamba na kukubali kutoa ruzuku na sasa bei ni Sh. 430/= kwa kilo moja badala ya Sh. 360/= kwa kilo ambayo ilikuwa hasara kubwa kwa wakulima. Naomba wakulima wasikie hiyo bei mpya na wasikubali kupunjwa, Serikali yao na watendaji wa Serikali wawasaidie wakulima waliouza mapema kwa bei ya Sh. 360/= kwa kilo, walipwe mapunjo ya Sh. 80/= kwa kilo kwa sababu hii ni fedha ya Serikali na walengwa na haki yao waipate. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu naona unanisikiliza hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani zangu za dhati kwa Wabunge wote wa Kambi ya Upinzani chini ya uongozi wa Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na Mhe. Dr. Willibrod Slaa kwa ushirikiano mzuri wanaonipa ndani na nje ya Bunge. Pia napenda nachukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri Capt. John Chiligati kwa hotuba yake aliyoitoa leo asubuhi, akisaidiwa na wafanyakazi wote wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu - Mrs. Salome T. Sijaona na sasa naomba Bunge lako Tukufu lisikilize maoni ya Kambi ya Upinzani juu ya Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa imani waliyonipa kwa kunichagua kuwa mwakilishi katika Bunge la Afrika. Nasema Ahsante sana. Sitaangusha Taifa langu hata siku moja.

Mheshimiwa Spika, kabla hatujaeleza changomoto zinazohusu ardhi ya Tanzania na matumizi yake, ni vyema tukajikumbusha takwimu zinazoelezea ardhi tuliyonayo. Tanzania ina eneo la ardhi lipatalo 886,200 kilomita za mraba. Kufuatana na taarifa ya hali ya mazingira ya mwaka 2008, inaonyesha asilimia 75% haitumiki au ni ngumu kuitumia kutokana na hali yake ya uasili (Mito, maziwa, milima, miamba na kadhalika), kikubwa cha kuangalia ni ekari karibu milioni kumi tu katika milioni 95 ndiyo inatumika kwa kulima. Aidha, Ardhi yote ya Tanzania Bara inaweza kugawanywa katika makundi yafuatayo:-

(1) Misitu 2,697,000.5ha. 2.8%;
(2) Misitu ya nyika (woodland) 37,629,000.3ha 39.7%;
(3) Bush land (nyika) 17,390,000ha 18.3%;
(4) Grassland 19,472,000.ha 20.5%;
(5) Ardhi inayolimwa 10,065,000ha 10.6%;
(6) Ardhi ya wazi (Open Land) 131,000ha 0.1%;

(7) Eneo la maji (Water features) 7,392,000ha 7.8%; na
(8) Ardhi nyingine 67,000ha. 0.1%.

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya ardhi yanaelekezwa zaidi katika maeneo yafuatayo:-

- Kilimo kwa ajili ya mashamba madogo na makubwa ya kibiashara;
- Matumizi kwa ajili miji inayokua;
- Ardhi kwa ajili malisho ya mifugo; na
- Shughuli nyingine za uchumi kama vile madini na utalii.

Aidha, kwa upande wa utawala wa ardhi, inaweza kuigawanywa katika makundi yafuatayo:-

- Ardhi ya hifadhi ambayo ni kwa ajili ya wanyamapori, mapori na mbuga za Taifa;
- Adhi za vijiji, ambazo ni ardhi yote iliyo chini ya Mamlaka ya vijiji kwa mujibu wa sheria Na.5 ya mwaka 1999; na
- Ardhi ya jumla ambayo iko chini ya Sheria ya Na.4 ya mwaka 1999.

Mheshimiwa Spika, kati ya hekta milioni 44 zinazofaa kulimwa, utafiti wa mwaka 2006, ulionyesha kwamba ardhi inayolimwa ni hekta milioni 10 tu na wakulima hawa wana ardhi ya chini ya hekta mbili kwa kila kaya na hii itatofauti kati ya Mkoa na Mkoa. Aidha, kutokana na tafiti hizo, inaonyesha kwamba wakulima wengi hapa Tanzania hawana ardhi ya kutosha, hivyo basi, dhana na kauli mbiu ya Serikali ya Kilimo kwanza, ni dhahiri kuwa haitekelezeki bila kuangalia sheria zetu za ardhi na jinsi tunavyoweza kupanga matumizi ya rasilimali ardhi tuliyopewa na mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ardhi haitoshi kutokana na mgawanyo tuliouonyesha hapo juu na matumizi ya ardhi kwa ajili ya kilimo ni asilimia 10.6 tu ya ardhi yote, Kambi ya Upinzani inapendekeza yafuatayo:-

- Utafiti ufanyike ili kubaini jinsi ya kutumia hekta milioni 34 zaidi ya hekta milioni 10.1 zinazotumika kwa sasa, kwani

- utafiti unaonyesha ukikusanya ardhi yote inayoweza kutumika kwa kilimo ni zaidi ya hekta milioni 44.

Kwa kuwa ardhi inayoongelewa katika Sheria Na. 5 na ile inayoongelewa katika Sheria Na. 4 kwa uhalisia ni ile ile na hakuna utenganisho ulio wazi. Hali hili ni chanzo kikuu cha migogoro. Aidha, ardhi hugawiwa na mamlaka mengi. Kwa mfano, *TIC* inaweza kummilikisha mgeni ardhi ya uwekezaji bila kuzingatia kama ardhi hiyo ni ya wanakijiji na kwa hiyo, Serikali inaweza kutwaa ardhi kwa shughuli za uchumi na kuwauzia wawekezaji bila ya kujali maeneo hayo kuwa yanatumiwa na wanakijiji. Mifano mingine ni upanuzi wa Hifadhi *(Expansion of National parks, Ruaha, Loliondo hunting block)*, upanuzi wa bandari Kurasini. Hivyo basi, ni lazima tuifanyie marejeo sera ya ardhi na tuangalie upya sheria zote mbili za ardhi kwa nia ya kuziunganisha na kuwa sheria moja ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, kukithiri kwa Migogoro ya Ardhi nchini. Kambi inatumia nafasi hii kuchangia katika vyanzo vya migogoro ya ardhi nchini. Takwimu za Wizara ya Ardhi zinathibitisha kuna migogoro ya ardhi. Mwaka 2008/2009 mashauri 9,228 yalifunguliwa na Wizara inategemea mashauri 5000 kufunguliwa kila mwaka na mashauri 11,279 yanaendelea kushugulikiwa katika mabaraza mengi nchini na kuna migogoro mingi ambayo hayamo katika mkondo rasmi. Ukweli ni kwamba kuna migogoro mingi ya ardhi. Aidha, hivi karibuni migogoro ya ardhi kati ya makundi mbalimbali ya watumiaji imeongezeka nchini. Migogoro baina ya wakulima na wafugaji, wanavijiji na wawekezaji na wanavijiji na Serikali zao za vijiji ama Serikali Kuu, imeripotiwa katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, migogoro hii imefikia hatua ya uvunjifu wa amani, upotevu wa maisha na mali na kuongezeka kwa chuki miongoni mwa raia. Kwa siku za karibuni, Wilaya za Tarime, Kilosa, Kiteto, Kilindi zimelipuka kwa mapigano kati ya wakulima na wafugaji na kuna tarifa za fukuto la migogoro kama hiyo karibu katika maeneo yote yenye wafugaji nchini zikiwemo Wilaya za Mbarali, Kilombero, Mahenge, Rukwa na baadhi ya Wilaya za Mkoa wa Manyara hususan Hanang. Katika Wilaya ya Kilosa wafugaji wengi walipoteza ng'ombe zao na fedha zao kwa operesheni iliyofanywa na Serikali kwa kutumia nguvu ya Jeshi la Polisi kwa kiwango cha kuvunja haki za binadamu na kuchafua jina la Tanzania kimataifa.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Kilosa takribani watu wanane walipoteza maisha na wengine 800 kukimbilia vijiji vya jirani kujihifadhi wakati mapigano yalipoibuka kati ya wakulima na wafugaji mwezi Novemba mwaka jana. Wilayani Kilindi, taarifa za vyombo vya habari zilikariri kuwa watu watano wameshapoteza maisha na wengine takribani 500 wamepoteza makazi yao baada ya nyumba zao kuchomwa moto katika mapigano ya wakulima na wafugaji mwezi Novemba mwaka jana. Vile vile katika Wilaya ya Kiteto, migogoro imefikia hatua ya kutoa roho za watu na uharibifu wa mali. Ipo pia migogoro isiyokwisha kati ya makundi ya koo mbalimbali za Kikurya Wilayani Tarime yote hiyo ikihusisha ardhi.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa tafiti mbalimbali ambazo zimefanywa zinaonyesha kuwa, migogoro mingi kijiini ambayo inishia kwa watu kuuwana, kiini chake ni ardhi ambayo inakuwa adimu kwa mahitaji ya watumiaji mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, ukiachia migogoro ya asili kama vile baina ya wakulima na wafugaji, au kijiji na kijiji kuhusu mipaka na kadhalika siku za hivi karibuni kumeibuka wimbi la migogoro inayohusiana na uwekezaji katika maeneo ya vijiji kwa ajili ya kilimo cha mashamba makubwa, uchimbaji madini na vito na shughuli mbalimbali zinazohusiana na utalii. Uchukuaji wa maeneo mengi umekuwa ukifanywa bila wananchi kuwa na uelewa wa kutosha wa nini kinafanyika hadi pale mradi husika unapoanza ndipo wananchi hugutuka na wakifuatilia ndipo hugundua kuwa wamepoteza ardhi yao.

Mheshimiwa Spika, mara chache hutokea wakalipwa fidia stahili lakini sehemu nyingi ardhi imekuwa ikitololewa bure na wananchi kwa ahadi kuwa watapata fursa za ajira kwenye mashamba au viwanda au migodi ikianza kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri ni wananchi wa maeneo ya migodi ya madini kama Kahama, Buzwagi, Nzega, Tarime na sehemu nyingine za uwekezaji wa nishati uoto kama Rufiji, Kisarawe na Kilwa wakati wa uanzishaji wa mashamba kwa ajili ya nishati uoto. Tafiti zinaonyesha kuwa zaidi ya hekta 641,000 zimegawiwa kwa wawekezaji hadi sasa kwa ajili ya kilimo cha nishati uoto nchini, nyingi zikiwa Wilaya za Pwani kama vile Bagamoyo (zaidi ya 200,000), Kilwa (zaidi ya 200,000), Rufiji (zaidi ya 50,000), Kisarawe (zaidi ya 10,000) na nyingine nyingi kwa Wilaya nyinginezo.

Mheshimiwa Spika, migogoro hutokea pale ambapo wananchi wanagoma kuondoka hadi wapewe fidia au haki zao nyinginezo mfano Buyuni, Chanika, Ilala, (vs Mradi wa viwanja elfu 20) na Wazo Vs Kiwanda cha Twiga Cement/Jeshi, Kipawa upanuzi wa kiwanja cha *International Airport Dar es Salaam.*

Mheshimiwa Spika, ufugaji umekuwa ukilaumiwa sana kwa kuchangia migogoro ya ardhi lakini katika hali halisi, sekta ya ufugaji ni mojawapo ya sekta majeruhi wa mfumo mbovu wa usimamizi wa rasilimali ardhi. Hii ni kutokana na ukweli kuwa wafugaji wamekuwa wakielekezewa lawama nyingi bila kuwekewa huduma zinazowawezesha kutulia na kuacha kuzurura na mifugo yao kutafuta malisho na mahitaji mengine.

Mheshimiwa Spika, takwimu za Wizara ya Uvuvi na Maendeleo ya Mifugo zinaonyesha kwamba kati ya hekta milioni 88.62 za raslimali ardhi hekta milioni 60 ni uwanda ufaao kwa malisho ya mifugo yenye uwezo wa kubeba jumla ya ng’ombe milioni 20. Kwasasa takwimu zinaonyesha kwamba tuna jumla ya ng’ombe 18,398,327 *(National sample Census of Agriculture 2002/03- National report).*

Mheshimiwa Spika, kwa takwinu hizo, yapo maeneo ambayo yakigawiwa kwa wafugaji bila kuingiliwa na watumiaji wengine, migogoro mingi ya ardhi inaweza kuepukwa. Lakini tofauti na hilo, maeneo mengi yanatengwa kuwa hifadhi za wanyamapori (takribani asilimia 30 ya ardhi yote ya Tanzania) na kwa shughuli nyingine za kiutalii mifugo inasahaulika. Hivi punde Serikali imetangaza kwamba imetenga hekta million 1.3 rejea hotuba ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, lakini utaratibu wa kumilikisha wafugaji haukuelezwa. Aidha, hata wafugaji waliohamishiwa kusini, Rufiji na kwingine hawajamilikishwa maeneo hayo na kwa hiyo, hawana kinga ya kisheria na wanaweza kuondolewa wakati wowote. Hali hii inaongeza migogoro na siyo haki. Kambi ya upinzani inamwomba Waziri mwenye dhamana ya ardhi hatima ya wafugaji nchini.

Mheshimiwa Spika, mapungufu katika mfumo wa kumiliki ya ardhi, yapo baadhi ya mapungufu katika mfumo wenyewe wa umilikaji wa ardhi ambayo yanatokana na mgawanyo usio sawia wa mamlaka juu ya ardhi na utoaji wa haki kwa watumiaji. Kwa sehemu kubwa, mfumo unalimbikiza mamlaka kwenye dola na watendaji wake na hivyo kuwafanya wananchi wa kawaida kukosa uhakika wa milki *(securtiy of tenure)* katika

ardhi wanayoitumia na kuitegemea kimaisha. Hili linasababisha mgongano wa maslahi baina ya watumiaji na mmiliki ambaye kwa maana hii ni dola.

Mheshimiwa Spika, kupanuka kwa miji huwafanya baadhi ya waathirika wa upanukaji wa miji kutafuta maeneo mbadala kwa ajili ya shughuli za kilimo na ufugaji, lakini katika kufanya hivyo hujikuta wakiingilia pia haki za watumiaji wengine wanaowakuta katika ardhi wanayohamia. Kwa mfano Jiji kama Dar es Salaam limekuwa likipanuka na kumeza maeneo ya pembezoni ambayo kimsingi humilikiwa kimila na wakazi wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, hata pale fidia inapolipwa huwa haiendani na viwango halisi vya soko la maeneo husika. Mfano mzuri ni migogoro iliyoibuka wakati wa viwanja 20,000 kuanzia mwaka 2003 hadi leo ipo kwa baadhi ya maeneo kama Buyuni, Bunju, Tuangoma, kibada na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, licha ya kutungwa kwa sheria za utatuzi wa migogoro na kuundwa vyombo vya kutafuta suluhu ya migogoro hiyo, bado kumekuwa na ucheleweshaji mkubwa wa kesi za ardhi na hivyo kuendeleza ama kuwaweka wahusika katika hali ya kutokufahamu nani hasa ana haki ya matumizi katika eneo linalogombaniwa.

Mheshimiwa Spika, hali hii huendelea kuchochea migogoro na pia kukwamisha shughuli za maendeleo maana inakuwa vigumu kufanyia kazi eneo lenye kesi Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, Mipango ya Serikali isiyozingatia maandalizi kabla ya utekelezaji, kwa mfano maandalizi duni ni operesheni za kuwahamisha wafugaji kutoka eneo moja mpaka jingine mara nyingi zimekuwa hazizingatii mahitaji halisi ya jamii hizo wala kufanyika kwa maandalizi ya kutosha na hivyo kusababisha wafugaji kuingia kwa wingi katika baadhi ya maeneo ambayo hayakulengwa kuwa ya wafugaji wanaohama. Hii imechangia katika kuleta migogoro ya maeneo ya malisho kati ya wafugaji na wafugaji na pia wafugaji na wakulima kama ilivyotokea kwa baadhi ya maeneo ya Kilwa, Rufiji, Kisarawe, Kilosa, Rukwa, Kilombero na Mahenge.

Mheshimiwa Spika, kukosekana kwa mipango bora ya matumizi ya ardhi imekuwa ni chanzo kikubwa na kichocheo cha ongezeko kubwa la mifugo katika eneo dogo. Lakini pia kwa wakulima kutumia nafasi hiyo kuingilia maeneo ya wafugaji na hivyo kuchochea migogoro ama kuwalazimu wafugaji kuhama kutoka katika maeneo yao ya asili na kuelekea katika maeneo mengine ya nchi.

Mheshimiwa Spika, tatizo la elimu ya kutosha pengine ndilo tatizo sugu kwa wananchi na hata baadhi ya watendaji nane ambapo wengi wao hawajui haki zao za ardhi na namna wanavyoweza kuzipata. Hii inasababisha wananchi wasishiriki katika maamuzi mbalimbali yanayohusu raslimali zao hasa ardhi na matokeo yake husababisha

kutokuelewana miongoni mwao pale ambapo ardhi imegawiwa kwa watumiaji wengine bila wao kuwa na taarifa za kutosha kushiriki kikamilifu kwenye maamuzi.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi imetokea watendaji wa Idara ya ardhi katika Halmashauri kugawa maeneo zaidi ya mara moja, kuuza maeneo ya wazi na hata kujiingiza katika vitendo vya rushwa. Hali hii pia huchochea migogoro. Sanjari na tatizo hili, wapo wanasiasa ambao kimsingi hawana mamlaka juu ya ardhi lakini wamekuwa wakijihusisha na ama usimamizi wa ardhi au usuluhishi wa migogoro ya ardhi. Hali hii pia huchangia migogoro hasa pale wanapoingiza maslahi yao ya kisiasa na kuingilia shughuli za utendaji.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hayo yote na ili kuepusha madhara mbalimbali yaliyokwishaainishwa hapo awali, ni vyema Serikali na wadau wengine mbalimbali wakazingatia masuala muhimu yafuatayo ili kuepusha na kutokomeza migogoro ya ardhi inayoendelea ambayo imezidi kuleta madhara makubwa kwa wananchi hususani wanavijiji wasio na hatia:-

Moja, wanasiasa waache kuchochea migogoro kwa maslahi yao ya kisiasa. Yapo maeneo ambayo wanasiasa hutoa ahadi za kumaliza matatizo ya ardhi kwa makundi mbalimbali karibu na uchaguzi kisha huacha kuyashughulikia matatizo hayo hadi karibia na uchaguzi mwingine. Wabunge wa Wilaya za Hanang na Kilindi wamelalamikia sana tatizo hili katika migogoro ya ardhi inayoendelea majimboni mwao hivi sasa.

Mbili, Watendaji wafuate taratibu za kisheria na haki kwa mujibu wa miongozo iliyomo katika sera na sheria za ardhi za 1999 yaani sheria ya ardhi Na. 4 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5. Watendaji na wanasiasa wasiohusika na masuala ya ardhi waache kuingilia na kutenda majukumu yasiyowahusu, Mfano, Wakuu wa Wilaya, Mikoa na kadhalika.

Tatu, Mianya iliyo katika Sheria za Ardhi inatumika kuwanufaisha wenye kipato kikubwa huku wanyonge wakiporwa haki zao kwa mgongo wa sheria hiyo hiyo. Mfano, Sheria Na. 4 inatamka kuwa ardhi ya kijiji isiyotumika wala kukaliwa itahesabika kuwa ni ardhi ya jumla. Kwa tafsiri hii, ardhi hiyo inaweza kuhamishiwa katika kundi la ardhi ya jumla toka ardhi ya kijiji na kugawiwa kwa kufuata taratibu za Sheria Na. 4 wakati kimsingi ardhi hiyo inapaswa kuwa chini ya usimamizi wa Serikali za Vijiji chini ya Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5. Tunatoa wito kwa Serikali kufanyia kazi mapungufu haya ambayo sio mara ya kwanza kupigiwa kelele kuwa yanasababisha uporaji wa ardhi ya vijiji. Ardhi ya jumla iandikishwe na ijulikane wazi, uamuzi wa kuwa na hazina ya ardhi ni mwelekeo mzuri na ninamshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kusema hilo leo. *(Makofi)*

Nne, uwekezaji katika ardhi za vijiji usiozingatia maslahi ya wananchi usitishwe mara moja hadi pale taratibu zinazotoa tija kwa makundi yote husika zitakapobainishwa na kueleweka kwa makundi hayo hususan kwa wanavijiji wanaotumia na kumiliki ardhi hiyo kwa kujikimu. Bila hivyo, migogoro kati ya wawekezaji wenye nguvu kiuchumi na

ambao maslahi yao yanalindwa dhidi ya wananchi ni lazima itatokea mfano mradi wa *North Mara Mining*.

Tano, Mfumo wa utatuzi wa migogoro hauendani na mahitaji halisi ya wananchi katika maeneo yao. Hii ni kutokana na ukweli kuwa mabaraza ya ardhi ya vijiji na yale ya Kata mengine hayajaundwa na kwa yale yaliyokwishaundwa hayajawezeshwa kufanya kazi kwa kukosa mafunzo, vitendea kazi na huduma kwa ujumla. Hali hii imesababisha watendaji na wanasiasa wasiohusika na utatuzi wa migogoro kama vile Wakuu wa Wilaya, Madiwani na Wabunge kupata kisingizio cha kuingilia kati kila migogoro inapojitokeza wakati mwingine kwa maslahi ya kisiasa. Serikali itenge bajeti maalum kuwezesha uundaji na uendeshaji wa mabaraza na Mahakama za Ardhi ili kuwaondolea wananchi shida ya kutafuta haki kwa umbali mrefu.

Sita, kumekuwa na matumizi ya nguvu kupita kiasi wakati wa utatuzi wa migogoro ya ardhi. Rai ya Kambi ya Upinzani kwa Serikali ni kuwa ielekeze jitihada katika kujenga mfumo wa utatuzi wa migogoro unaokidhi mahitaji ya wananchi badala ya kutumia nguvu za Polisi au Jeshi la Polisi kwa kutumika kikosi cha kutuliza ghasia au kitengo cha operesheni maalum limekuwa likitumiwa dhidi ya raia kama ilivyokuwa kwa Wilaya ya Mbarali wakati wa operesheni Ihefu, Tarime wakati wa mapigano ya kikabila na Kilosa wakati wa mapigano ya wakulima na wafugaji mwishoni mwa mwaka jana. Rai ya Kambi kwa Serikali ni kuwa ielekeze jitihada katika kujenga mfumo wa utatuzi migogoro unaokidhi mahitaji ya wananchi badala ya kutumia nguvu za Polisi au Jeshi kwani sio rahisi kuhakikisha uwepo wa Polisi wakati wote katika eneo la mapigano.

Saba, masuala kama vile huduma za majosho, madawa, chanjo, uhakika wa malisho na uhakika wa soko la mifugo hayawezi kuachwa mikononi mwa mfugaji mmoja mmoja. Vinginevyo, wafugaji wataendelea kuhamahama siku zote kufuata malisho na hizo huduma nyingine na hii itaendelea kuwa chanzo cha migogoro. Kwa upande wa wafugaji, mabadiliko ni suala la mchakato ambao huchukua muda mrefu, hivyo ni vyema Serikali ikajiepusha na fikra kwamba itageuza utamaduni wa wafugaji kwa awamu moja ya utawala. Jambo hili linahitaji maandalizi ya kina kutengeneza miundombinu itakayowezesha kuongeza tija ya mfumo wa ufugaji kwa manufaa ya wafugaji na kwa pato la Taifa pia. Soko la mifugo lipo ndani na inje ya nchi

Nane, viwanda vya nyama ndio duni na hivi vikiongezeka matumizi yataongezeka na hakuna haja sera ya kupunguza mifugo. Kambi inawashangaa wanaohamasisha kilimo kwanza na huku wameshindwa kabisa kutawala (*manage*) NEEMA ya mazao mengi ya mifugo.

Kuna umuhimu kwa Serikali kuliangalia upya suala la mgawanyo wa raslimali hasa ardhi kati ya wanajamii, makundi ya wazalishaji wadogo wadogo wakulima wadogo na wakubwa, wafugaji, wachimbaji madini, wawindaji na waokotaji na hata wavuvi. Endapo hakuna mlingano na haki katika hili, suala la migogoro ya ardhi litaendelea kuisumbua nchi bila suluhu.

Tisa, aidha, sera za uwekezaji mkubwa katika ardhi ni muhimu sasa ziangaliwe upya na maslahi ya wazalishaji wadogo yapewe kipaumbele hasa katika kipindi hiki ambacho vijana wengi wamekosa shughuli muhimu za kuwawezesha kujikimu. Kwa ardhi yetu hii kubwa na nzuri, vijana wengi wanaweza kujishughulisha na badala ya kukaa bila kazi lakini ardhi nayo ikibaki mikononi mwa wachache ugumu wa maisha kwa vijana utaendelea kuwepo tu.

Kumi, Serikali ina ardhi takribani hekta milioni mbili ambazo ziko mikononi mwa Serikali na mashirika yake kama vile JKT, Magereza, *NAFCO,NARCO* na Wizara ya Kilimo na hazitumiki kikamilifu. Kwa msukumo wa kilimo kwanza Serikali ifikilie namna ya kutumia ardhi hii kwa tija badala ya kuhodhi.

Mheshimiwa Spika, ardhi yote ya Tanzani ipo chini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa niaba ya wananchi na hivyo kuifanya ni mali ya umma. Kwa madhumuni ya kuhakikisha kunakuwepo usalama na mgawanyo wa ardhi, Tanzania imetunga sheria tatu zinazohusu ardhi. Sheria hizo ni Sheria Na.4 ya Ardhi ya mwaka 1999, Sheria Na.5 ya Ardhi ya Vijiji ya mwaka 1999 na Sheria Na.2 ya mwaka 2002 ya kusuluisha migogoro ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, Mtanzania anaweza kuomba na kupewa hatimiliki ya ardhi ya kati ya miaka 33 na 99. Rais pekee ndiye mwenye mamlaka ya kufuta umiliki wa kipande cha ardhi, pale tu kama ardhi hiyo inatakiwa kwa matumizi ya umma. Aidha, muathirika wa uamuzi huo wa Rais ana haki ya kufidiwa kwa muda bila ucheleweshaji wa aina yoyote.

Mheshimiwa Spika, Sheria zimetoa utaratibu wa mgawanyo wa ardhi ya Tanzania katika makundi manne, kama ifuatavyo:-

- Umiliki kwa Sekta ya umma, *(state leasehold)* chini ya utaratibu huu, mamlaka ya umma inaweza kukodisha ardhi kwa watu binafsi au kwa jamii *(communities)* kwa kipindi cha muda maalum, kama vile miaka 33,66;

- Hati miliki binafsi *(private right of occupancy)*, hii inahusu ardhi inayomilikiwa na watu mmoja mmoja kwa masharti ya kuiendeleza kwa kilimo, mifugo au kwa ajili ya kuwa sehemu ya kutolea huduma;
- Umiliki wa kimila, chini ya utaratibu huu, umiliki huwa ni wa kurithishana miongoni mwa jamii husika;

- Umiliki wa pamoja au miliki ya kijiji, hapa ardhi inamilikiwa na kijiji chini ya sheria, ardhi inatakiwa kuwa *"surveyed"* na kuwekewa mipaka kisha kupewa cheti cha umiliki. Hapa kijiji kina haki ya kutumia ardhi hiyo kwa matakwa yake.

Mheshimiwa Spika, katika taarifa ya utekelezaji wa Wizara kwa mwaka 2008/2009. Wizara ilipima viwanja 18 na kati ya hivyo 14 viliuzwa. Kambi ya Upinzani inataka kufahamu, kwani kama tulivyoeleza hapo hakuna utaratibu wa kuuza viwanja katika sheria bali kuna kumilikisha viwanja.

Mheshimiwa Spika, aidha, ukiangalia vitabu vya mapato ya Serikali *(volumeIrevenue estimate),* mapato mengi yanatokana na kodi ya ardhi, kwa mfano mapato ya kodi ya ardhi yalikuwa Shilingi bilioni 12 kwa mwaka 2007/2008 na mwaka 2008/2009 makisio yalikuwa Shilingi bilioni 17.4 na mwaka 2009/2010 makisio ni Shilingi bilioni 14.5.

Mheshimiwa Spika, hakuna fedha inayoonyeshwa kuwa imetokana na uuzaji wa viwanja. Kambi ya Upinzani inamtaka Waziri aliambie Bunge lako Tukufu misingi ya kisheria ya Serikali kuuza ardhi kwa tenda na mapato hayo yanaonyeshwa vipi kwenye vitabu vya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa miji hauepukiki lakini lazima ufanyike kwa mpango ili uweze kuchukua nafasi yake katika uchumi kwa tija, ukuwaji wa miji hufuatana na ongezeko la watu katika sehemu ndogo na shughuli kama vile viwanda na sehemu za kufanyia biashara kama vile maduka na ofisi.Aidha watu wanaohamia mijini hugeuza mitindo yao ya maisha na mahitaji yao.Tanzania kama nchi nyingine za kiafrika na Asia zimeshuhudia ongezeko kubwa la watu katika miji. Mwaka 2000 idadi ya watu Tanzania ilikadiriwa kuwa milioni 33.53 na watu milioni 11.02 asilimia 32 walikuwa wanaishi mijini. Inatarajiwa ifikapo mwaka 2030, Tanzania itakuwa na idadi ya watu milioni 63.1 na milioni 35, asilimia 55 watakuwa wanaishi mijini. Hii ni zaidi nusu ya watu wote nchini na kwa hiyo, hii itakuwa ni changamoto kubwa sana kwa Serikali. Hali hii inaletelezwa na uhamiaji unaokisiwa kuwa asilimia 6.5 kila mwaka kwa watu kutoka vijijini kuja mjini kutafuta kazi na maisha mazuri zaidi. Kasi ya uhamiaji itazidi jinsi ardhi ya kijiji inavyopungua na bei ya mazao kushuka.

Mheshimiwa Spika, kasi ya ukuaji wa makazi ya mji umeambatana na makazi yasiyopimwa na zaidi ya asilima 60 ya wakazi hawana huduma kama vile maji,umeme,mazingira mazuri ya taka na ni changamoto kwa Serikali na vyombo vyake. Aidha, Kambi ya Upinzani inatambua kama tulivyosema katika hotuba zetu miaka iliyopita kwamba kurekebisha miji ni kazi ngumu na ghali kwa Serikali na wananchi wanaoishi katika maeneo husika na ni vizuri Serikali ikatangulia mapema kupima makazi kabla ya watu hawajavamia na kujenga holela.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mradi wa kupanga upya matumizi ya kurasani na jambo hili tulilitolea taarifa mwaka uliopita. Malalamiko ya wananchi wa Keko Matangini, yanahusu nyumba zimewekewa alama X kama tulivyotaarifu Bunge lako, lakini mpaka hivi sasa Serikali iko kimya na wananchi hawajalipwa fidia yao kama kutakuwa na kuondolewa pale. Jambo hili ni hasara kubwa kwa wananchi kwani hawawezi kuendeleza mahali pao na wapangaji wao wanahama kwa kuelewa kuwa nyumba hizo zinaweza kubomolewa wakati wowote ule kwa nguvu kama inavyotokea mara kwa mara. Aidha, wenzao wa Keko Akida na Keko Machungwa wamepewa vyeti vya makazi ambavyo vinatambulisha uhalali wa nyumba zao kuwepo katika maeneo yasiyopimwa. Jambo hili linaongeza wasiwasi kwa wakazi wa Keko Matangini juu ya hatima ya nyumba zao.

Mheshimiwa Spika, mtindo wa Wizara hii kutangaza eneo fulani ni la mradi, sio geni na kila litokeapo halitekelezwi kwa muda unaotakiwa kama vile mradi wa Kipawa, mradi wa Kibamba Luguruni na sasa mradi wa wakazi wa Kigamboni haijulikani utakamilika lini. Jambo hili ni kinyume cha dhana ya sheria za ardhi zinazotaka wale wanaoguswa na miradi ya Serikali lazima wapewe fidia bila usumbufu na ucheleweshaji wa aina yoyote.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inamtaka Waziri alieleze Bunge lako, wakazi wote waliomo kwenye mkumbo huu wa miradi mbalimbali ya Serikali, kama tulivyotaja hapo juu ni lini watapatiwa haki zao stahili?

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutambua kazi nzito ya kupima upya makazi, Kambi ya Upinzani miaka miwili iliyopita tuliiomba Serikali kutangulia kupima maeneo kuliko kusubiri wananchi waingie katika maeneo mbalimbali halafu waondolewe kama wavamiaji. Kwa hili tunataka kutambua kazi inayofanyika katika jiji la Mwanza kwa kupima na kumilikisha wananchi maeneo ya Buswelu, Ilemela, Luchelele na sehemu nyingine kabla ya wananchi hawajavamia na kujenga kiholela. Jambo hili ni zuri na Kambi ya Upinzani inahimiza kuwa huu uwe ndio mtindo wa kuendeleza makazi yetu, tukizingatia ukweli tulioeleza awali kwamba watu takribani watu milioni 35 watakuwa wamehamia katika miji mbalimbali nchini, takribani nusu ya Watanzania wote mwaka 2030.

Mheshimiwa Spika, mwisho, Kambi ya Upinzai imesikiliza matatizo mengi sana ya Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC)*, ni shirika kubwa na la muda mrefu ambalo lilianzishwa kwa madhumuni hasa ya kuhakikisha Watanzania wanapata makazi bora. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuliangalia kwa makini shirika hili kwani kuna malalamiko makubwa ya wananchi juu ya utendaji kazi wake.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa John Momose Cheyo kwa kuwasilisha maoni hayo ya Kambi ya Upinzani. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, orodha yangu ina wachangiaji 13. Wawili ni ambao hawajachangia, kwa hiyo, wao ni dhahiri watapata nafasi. Wapo waliochangia mara moja katika hoja zilizopita, kwa vyovyote vile sidhani kama zaidi ya kumi watapata nafasi. Kwa hiyo, nitaanza na Mheshimiwa Ponsiano Nyami, atafuatiwa na Mheshimiwa George Lubeleje na ajiandae Mheshimiwa Ephraim Madeje. Mheshimiwa Ponsiano.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwa mtu wa kwanza kuchangia. Naipongeza Wizara kwa kuandaa hotuba yao vizuri, nitaipongeza zaidi kama hotuba hiyo itaambatana na utendaji madhubuti wa kazi walizozipanga. Pili, naomba niwapongeze Mheshimiwa Lolensia Bukwimba na Mheshimiwa Oscar Mukasa kwa kuchaguliwa kwao na kuingia hapa Bungeni. Karibuni sana.

Mheshimiwa Spika, nianze na kuchangia kuhusiana na Shirika la Nyumba la Taifa. Ni Shirika ambalo ni zuri na ni miongoni mwa Mashirika ya kwanza kabisa kuundwa mara tu, tulipopata uhuru na hasa uhuru wa Tanganyika wakati ule na madhumuni makubwa ilikuwa ni kumwezesha mwananchi wa kawaida kabisa na hata Mtumishi wa kawaida, aweze kupata makazi yenye gharama nafuu katika maeneo ya mijini, maana uwezo wa mwananchi wa kawaida na mtumishi wa kawaida kujenga nyumba, haukuwepo wakati huo. Kadri tulivyozidi kuendelea, Shirika hili limekuwa halitendi haki kwa watumishi na hata kwa wananchi wa kawaida na sababu kubwa ni uroho tu na ubinafsi. *(Makofi)*

Shirika hili ukijaribu kulichunguza sana na bahati nzuri mimi nimejaribu kulichunguza, pengine sio kwa ukubwa kiasi hicho, lakini ninalifahamu. Utakuta kuna ubadhirifu mkubwa sana, kuna wizi mbaya sana, rushwa ni ya hali ya juu, watu wanadhulumiwa, wanaomba kupata nyumba, mtu wa kawaida ni hovyo hovyo hupewi nyumba. Wanapeana kwa kupendeleana, wanapeana wengine kwa undugu, urafiki na kubwa zaidi ni rushwa. Kama ninasema uongo, naiomba Serikali iunde Tume ikachunguze maneno yangu nayoyasema na mimi nitawasaidieni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ukiingia kwenye ujenzi wa nyumba zinazojengwa, hizo zinazotolewa taarifa hapa na Mheshimiwa Waziri, zinajengwa kwa ubia. Ukiingia hapo ndani ndipo kuna ufisadi mkubwa! Serikali haipati lolote bali hao wabia ndio wanapata zaidi kuliko Serikali. Hata ule mpango unaosema kwamba angalau miaka kama 14, tufanye miaka 15 baada ya nyumba hizo kuwa zimejengwa, ziwe ni mali ya Shirika lenyewe, hilo halitekelezwi, bali huchukua miaka mingi tena zaidi ya miaka 20 ambapo wanaofaidi ni wale wabia kuliko Serikali. Hatuwezi tukafika.

Mheshimiwa Spika,. wabia wale wanapofaidi maana yake ni kwamba, wanashirikiana na baadhi ya watumishi waliomo humo na mimi sielewi Bodi ya Wakurugenzi iliyopo inafanya shughuli gani hasa. Lakini mbaya zaidi ni kwamba, kama pia Mheshimiwa Waziri, alivyosema hapa, ni kubomoa nyumba katika baadhi ya maeneo na kujenga nyumba mpya. Sawa!

Mheshimiwa Spika, unapobomoa katika eneo hilo maana yake ni kwamba, unatoa usumbufu kwa wale waliokuwepo katika eneo hilo. Tuna eneo kubwa Tanzania na hasa katika miji yetu, kwanini msiende kujenga maeneo yanayopimwa mapya badala ya kuendelea kumoboa majengo? Mkijenga maeneo mapya, basi mkitaka kubomoa katika eneo mlilokusudia kulibomoa, wale muwaondoe hapo muwapeleke katika maeneo mapya mliyojenga.

Lakini pia ni lazima mtazame mfumo wa majitaka, mahali pale mnapobomoa na kujenga: Je, iliandaliwa hivyo? Pameandaliwa? Matokeo yake mnavyojenga holela kwa kutozingatia utafiti huo, mvua zinapokuja katika miji yetu, miji inafurika kutokana na ujenzi holela ambao ninyi mnadhani ni ujenzi salama, kumbe ulikuwa ni ujenzi holela. Kwa hiyo, naomba hilo lirekebishwe. Lakini, mimi nadhani Mheshimiwa Waziri, hebu unda Tume ya watu waaminifu, wachunguze ubadhirifu uliopo katika Shirika la Nyumba. Hali ni mbaya sana na rushwa ni mbaya sana.

Mheshimiwa Spika, nije kwenye upande wa migogoro ya ardhi. Migogoro ya ardhi kama ilivyosemwa hapa, huko mie ninayemhurumia sana ni mwananchi. Wananchi na hasa wananchi wa vijijini wanadhalilishwa sana. *(Makofi)*

Pamoja na kuwepo utaratibu wa kwamba kutakuwa na Mabaraza ya vijiji, Mabaraza ya Kata, na baadaye Wilaya na kuendelea, pale yanapokuwa yapo, kwanza moja, wananchi wenyewe hawajaelewa vizuri sheria inayotaka kuunda mabaraza haya. Elimu haijatolewa vya kutosha na kwa namna hiyo, Mabaraza haya yanapokuwepo yamekuwa ni kichocheo kikubwa cha kuwanyanyasa wananchi wa kawaida na rushwa imeingia huko na wao wenyewe wanaoendesha hawajui utaratibu wa kuendesha mabaraza hayo. Kwa hiyo, imekuwa ni vurugu tupu. Lakini bado hadi leo hii katika migogoro hii kinachonisikitisha na hata kwenye wilaya yangu ipo, ni jinsi Mahakama za Mwanzo zinavyoingilia kutoa hukumu katika migogoro hii ya ardhi, au mashamba na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Sheria inawakataza, lakini wao wanaigeuza ile sheria kumpa haki wanayemtaka wao kwa kuweka kipengele kile cha Sheria inayosema kwamba, "Kuingia kwa nguvu katika eneo *(trace passingP"* wanaitumia kimakosa. Kwenye Mahakama zangu za Mwanzo, imefanyika na hasa Mahakama ya Namanyere. Siwezi kutaja Hakimu ni nani, lakini yupo Hakimu ambaye analindwa na wakubwa wake na wanaponisikia waniulize, analindwa kwa sababu gani? Barua zangu wanazo, ushahidi wetu wanao, lakini wanalindana. Rushwa zile zile!

Mheshimiwa Spika, kwanini tuzidi kumyanyasa mwananchi? Kwanini tumtungie sheria ambazo zinamkandamiza yeye mwenyewe? Tunashindwa kumwelimisha na tunashindwa hata kumsimamia. Kwanini tukae tunasema maneno kila siku maneno, maneno mazuri, kumbe tunampaka mafuta kwa kutumia mgongo wa chupa, lakini matatizo anayo? Kwanini? Umefika wakati wa kumjali mwananchi na sio kujijali sisi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, kuna migogoro ya mipaka ya nchi. Mipaka inasogezwa kwetu, wanaohusika hawalishughulikii sana na ukitaka kuiona hiyo, hata ndani ya nchi hakuna ule umuhimu unaowekwa na viongozi wetu wa ngazi ya Wilaya au Mikoa kutazama hasa mipaka yetu, ni ipi? Haipo. Pamoja na maagizo mbalimbali yaliyotolewa na Mawaziri wenyewe na Serikali kwa ujumla, lakini bado hili nalo halitekelezwi.

Waheshimiwa Wabunge, tuliopo humu, hivi ni kweli na sisi tunaelewa fika mipaka ya maeneo yetu na hasa ile ya Wilaya au Mkoa? Hili ni muhimu, hiyo ndiyo itakayoondoa migogoro ya kugombana kwetu.

Mheshimiwa Spika, katika dakika zangu za mwisho za kuchangia, niongelee jambo la mwisho la upimaji wa viwanja. Huku ndiko kuna rushwa kali na mbaya. Kupandanisha viwanja, kumezidi na kwa pale Sumbawanga, wale wenzetu wanaogawa viwanja pale Mkoani ni mabingwa wa kufanya hayo. Mimi mwenyewe nimekwishapandanishiwa mara mbili. Mimi huyo! Juzi nilipokwenda kuhoji kwamba

mbona kiwanja changu naona amejenga mtu mmoja mwenye asili fulani, wakasema Mheshimiwa ukitaka kulifuatilia hilo tutafungwa wengi, tutakupatia kiwanja kingine mahali fulani, hebu chagua kule tutakupatia kingine. Ni mara ya pili wanapandanisha viwanja vyangu. Sasa wananchi wengine wa kawaida je? Wale wengine inabidi watoe rushwa kubwa. Viwanda na makazi halikadhalika, tunakwenda wapi?

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri hebu atazame watu wake wa ardhi. Kule Bagamoyo sasa hivi wanataka kupima kiwanja kikubwa kabisa cha ndege cha Kimataifa, pamoja na eneo la biashara kubwa. Sasa hivi tayari kuna mgogoro wa wananchi kudhulumiwa viwanja na maafisa ardhi. Kesi ziko kwake lakini zinakaa miaka nenda rudi. Sio huko tu, nadhani Tanzania nzima kila unapokwenda ni migogoro. Kwanini usichunguze kwanza watumishi wako ndani humo na wengi uwafyeke? *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla hivi mnaridhika na mipango ya miji yetu ilivyo? Mbona ni holela mno inavyojengwa? Hivi ninyi hamtembei mkaona katika miji ya wenzenu wa Afrika tu? Acheni wale wa Ulaya na kadhalika tulikokwenda huko, hawa wa Afrika wanavyopanga miji yao, hamwoni kwamba miji yetu ni hovy, na tunaosababisha iwe hovyo ni sisi wenyewe viongozi? Hamlioni hilo? Mji unapangwa lakini hao hao kwenye Wizara, kama matumizi ya ardhi yamepangwa labda ni kwa ajili ya soko au bustani ya kupumzikia au eneo la kupumulia mji, hao hao ndio wanakwenda kugawa kwa rushwa na mnawajua na ninyi mnawaachia. Kwanini? Lakini kama kiwanja hujakipima na unasema tutapima hili eneo mtu asijenge, mtu anakwenda kujenga Afisa ardhi yupo, kwanini asizuiwe mapema?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi. Kwanza kabisa, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ardhi ndiyo msingi wa maendeleo kwa sababu bila ardhi huwezi kulima, bila ardhi huwezi kujenga nyumba, lakini ardhi ikitumika vibaya inakuwa na migogoro, inakuwa na madhara makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, mimi nianze na hili la migogoro kati ya wakulima na wafugaji. Hili limekuwa ni tatizo kubwa sana hapa nchini, lakini uwezo wa kulitatua tatizo hili tunao. Vijijini kuna Serikali chini ya Sheria Na. 7 na Na. 8 iliyoanzisha Serikali za Mitaa kwamba, kijiji kina Serikali kamili.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka wakati wa ‘Oparesheni Vijiji’, vijiji vilishauriwa vipange au vitenge maeneo kwa ajili ya wakulima na wafugaji. Lakini kuna baadhi ya vijiji hawakufanya hivyo, kwa hiyo, matokeo yake ni kwamba, hawa wafugaji sasa wanaishi pamoja katika vijiji na kuwa na kero kubwa na ndio maana kunakuwa na mapigano kati ya wafugaji na wakulima.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Wizara iweke mikakati na zoezi hili limeshaanza. Wafugaji watengewe maeneo yao kwa sababu mifugo hatuwezi kuikataa. Mifugo ni raslimali ambayo inaiongezea pato nchi yetu, hatuwezi kukataa kabisa kwamba sasa mifugo tuiondoe kabisa, hapana ila watengewe maeneo ambayo wataweza kuchungia mifugo yao ili kupunguza hii migogoro. Hii migogoro ni mikubwa sana, ukichukua mfano Wilaya ya Kilosa na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni suala la upimaji wa mipaka ya vijiji. Naipongeza sana Serikali, imefanya kazi nzuri, vijiji vingi vimepimwa, lakini naomba zoezi hili liendelee kwa sababu unapima kijiji, kinapata cheti na baadaye wananchi wanapata hatimiliki na zile hati zinawasaidia sana kupata mikopo katika vyombo vya kifedha kama mabenki. Kwa hiyo, zoezi hili liendelee.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, katika hotuba yake nimeona kwamba, katika mwaka wa 2009/2010 watapima vijiji kama 1500 katika Mikoa ambayo ameitaja. Kwa hiyo, waendelee na upimaji wa vijiji ili wananchi waweze kupata hati, kwa sababu ukiishapata hati au kijiji kikishakuwa na cheti, wanajua eneo lao na wanajua mipaka yao, kwa hiyo, inakuwa ni vigumu sana mtu kuja kuvamia eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, ni suala zima la ujenzi katika miji yetu. Tatizo kubwa la ujenzi holela katika miji ni kwa sababu miji yetu mingi sana imejengwa bila kufuata *master plan.*

Mheshimiwa Spika, *master plan* ni muhimu sana kwa sababu ndiyo inayokuelekeza maduka yawe wapi, majengo ya starehe yawe wapi, lakini hivi sasa unakuta kunajengwa, hapa nyumba ya kuishi, hapa kuna baa, hapa kuna mashine ya kusaga, ni tatizo kubwa sana na ujenzi holela, *squarters* ndiyo zimesababisha kero ya kubomoabomoa nyumba au maeneo mbalimbali katika miji yetu.

Mheshimiwa Spika, mimi ninajiuliza, haya maeneo Serikali inayafahamu, mtu anaanza kuchimba msingi, anaweka ukuta, anapaua nyumba na kupiga bati, lakini Serikali haimzuii. Akishakamilisha jengo, kesho ubomoe, ni hasara kubwa na kero kwa wananchi. Kwa hiyo, naishauri Serikali, Mheshimiwa Waziri na Wizara yako kwamba, maeneo yale kwa mfano sasa hivi tuna Wilaya mpya au miji ambayo haina *master plan,* basi irekebishwe, wajenge kwa kufuata *Master plan.* Hii itawafanya wananchi wakae katika mitaa ambayo hata usafi unaweza kuzingatiwa.

Mheshimiwa Spika, suala hili la ujenzi holela, kwa mfano mji wetu wa Mpwapwa, ulikuwa hauna *master plan* lakini, nashukuru Chuo cha Ardhi walitusaidia, walipima na kupata *Master plan,* sasa tunaurekebisha ili uweze kujengwa kama ulivyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, suala la mikopo kwa ajili ya kujenga nyumba. Tulipitisha sheria hapa Bungeni kwamba, sasa wananchi wapate mikopo kwa ajili ya kujenga nyumba au kununua nyumba, sasa utaratibu bado haujaanza wa kuwakopesha. Nashukuru

Mheshimiwa Waziri amelielezea hilo, lakini ni vizuri sasa wakati umefika Mheshimiwa Waziri, utaratibu ukamilike basi wananchi waweze kupata mikopo kwa ajili ya kujenga au kununua nyumba.

Mheshimiwa Spika, zamani tulikuwa na benki ya nyumba, ambayo sasa haipo lakini Serikali imefanya jambo zuri sana kutunga sheria ili wananchi wetu waweze kukopa na kununua nyumba. Tunahitaji wananchi wetu waboreshe mazingira yao, wajenge nyumba.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ujenzi wa nyumba, bado tuna tatizo kubwa la kupanda kwa bei ya bidhaa au vifaa vya ujenzi. Hilo nalo ni tatizo kubwa sana. Sasa hivi mfuko wa sementi ni zaidi ya Sh. 15,000/= bati zimepanda. Mimi nadhani huu mfuko wa kuwakopesha wananchi, ili waweze kujenga nyumba au kununua nyumba utasaidia sana. Lakini kubwa zaidi ni kuhakikisha kwamba, pamoja na kwamba, Serikali haina Tume ya Kudhibiti bei, lakini ipo haja kwa kweli, suala hili la upandaji wa vifaa vya ujenzi liangaliwe.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri. Naendelea kumpongeza yeye na Wizara yake, najua wanafanya kazi katika mazingira magumu, kama bajeti yao ingekuwa inatosha, basi vijiji vyote vingekuwa vimeshapimwa na wananchi wamepata hati, hata hizi *master plan* wangekuwa wameshawasaidia wananchi. Kwa hiyo, tunaomba bajeti ijayo ya mwaka 2010/2011, basi Wizara hii iongezewe bajeti ili waweze kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Ahsante sana.

**MHE. EPHRAIM N. MADEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie katika mjadala wa bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Chiligati, Katibu wake Mkuu na Watendaji wake wakuu, kwa bajeti nzuri ambayo imetuelezea kwa ufanisi mkubwa jinsi gani wametekeleza mpango wao wa kazi katika mwaka uliopita na pia wametupatia mwelekeo kwamba, yale waliyoyapanga kuyatekeleza mwaka huu yatakuwa ni mazuri.

Mheshimiwa Spika, ningependa katika mchango wangu nijikite katika matatizo ambayo yamekuwa yakiwapata wananchi wa Manisapaa ya Dodoma katika masuala ya ardhi hususani kwenye masuala ya fidia.

Mheshimiwa Spika, matatizo hayo kwa kiasi kikubwa yalianza kujitokeza baada ya Mamlaka ya Usitawishaji wa Makao Makuu *(CDA)*, kuundwa karibu miaka 30 au 40 iliyopita.

Mheshimiwa Spika, hapa naomba nisieleweke vibaya. Wananchi wa Manispaa ya Dodoma waliupokea uamuzi au azma ya Serikali kuhamia Dodoma, kwa mikono miwili

wakati ule ulipotangazwa na hata sasa hivi sisi watu wa Dodoma, tutarukaruka ile siku ikifika wakati Serikali itakapohamia Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mchango wangu kwa kweli unatetea haki za wale wananchi ambao walikuwepo katika ardhi ya Dodoma kabla *CDA* haijaundwa na ambao baadhi yao walijenga makazi yao hapa.

Mheshimiwa Spika, Sheria Na.4 ya mwaka 1999, kwa kweli ni Sheria ambayo iko wazi na imeeleza vizuri sana, haki za mwananchi katika ardhi yake. Katika sheria hiyo, misingi muhimu inayotawala sera ya ardhi katika nchi hii, imeainishwa na Waziri wa Ardhi, amepewa majukumu katika kutekeleza sera hiyo.

Mheshimiwa Spika, kama utaniruhusu, ningependa kunukuu vipengele mbalimbali hasa vile ambavyo viko katika sehemu ya pili ya Sheria hiyo, kifungu cha 3(b) na hapa ninanukuu kwamba, Sheria ya Ardhi inamtuma Waziri wa Ardhi kufanya yafuatayo: "*To ensure that, existing rights in recognised long standing occupation or use of land, are clarified and secured by law.*" Mwisho wa kunukuu. Tafsiri yake kwa kiswahili tunaweza kusema kwamba, "Kuhakikisha ya kwamba, haki za mwananchi zilizopo juu ya ardhi aliyonayo kutokana na hatimiliki au kutokana na matumizi yanayotambulika na jamii juu ya ardhi hiyo anayoikalia kwa muda mrefu au haki inayotokana na Sheria za kimila zinafafanuliwa na kutekelezwa na Sheria"

Mheshimiwa Spika, kama ukiniruhusu tena niende kwenye kipengele cha 3(g), kinasema; "*To pay full, fair and prompt compensation to any person whose rights of occupancy or recognized long standing occupation, or customary use of land is revoked or otherwise interfered with to their detriment by the state under this Act or is acquired under the land acquisition Act."* Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, tafsiri kwa Kiswahili kama ukiniruhusu ni kama ifuatavyo: "Kulipa fidia kamili na ya haki mara moja kwa mtu yeyote ambaye haki zake juu ya ardhi kama zilivyofafanuliwa kwenye sheria hii ambayo, kwa sababu moja au nyingine imetwaliwa ama na Serikali au kutokana na sheria yoyote ile"

Mheshimiwa Spika, kwenye sehemu ya tano ya sheria hii umetolewa ufafanuzi kuhusu wananchi au tuseme mwananchi na familia yake ambaye amejenga makazi kwenye sehemu ya ardhi, makazi ambayo yamedumu zaidi ya miaka mitatu na haki hiyo ni kwamba atatambulika kama vile ana hati rasmi katika ile ardhi. Pia anakuwa na haki ya kufidiwa endapo ardhi hiyo itatwaliwa kutokana na mahitaji ya Serikali kwa ajili ya matumizi ya umma. Naomba tena ninukuu ili kuonyesha haki hiyo chini ya hicho kipengele. Hiki ni kipengele cha 23.6. Kinasema: "*Where a person or family has occupied land in the same location for not less than three years, he or they shall be entitled to compensation under the land acquisition act where that land is to be acquired for public purpose or where that person or family is to be removed from the land as if the person or family had a right of occupancy in the land"*

Mheshimiwa Spika, katika Manispaa yetu kuna makundi mawili ambayo kwa kweli yameathiriwa vibaya sana kutokana na kutokutekelezwa kwa Sheria ya Ardhi na Mamlaka ambayo inahusika. Kama tunavyojua Mamlaka ya Ustawishaji wa Makao Makuu ilipewa hatimiliki ya ardhi yote ya Manispaa. Kwa hiyo, tungetegemea kwamba wao wangekuwa msitari wa mbele kuhakikisha kwamba haki za wananchi ambao wana ardhi au wana makazi katika eneo hili zinalindwa lakini kinyume chake hilo limekuwa halifanyiki. Makundi hayo ni wale ambao kabla ya kuundwa kwa *CDA* walikuwa na mashamba na makazi. Baadhi ya makazi yao kwa kweli yalikuwa ni duni kama unavyojua, lakini yalikuwa ni makazi yao. Kundi la pili ni wale ambao ama wamehamia kwenye maeneo ambayo yako katikati ya mji au pembezoni mwake, lakini wameshakaa katika hayo maeneo kwa zaidi ya miaka mitatu chini ya sheria. Hawa watu wanapata haki kama vile ambavyo nimeeleza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wananchi wa Dodoma kwa kweli wamekuwa wakilalamika sana kuhusu haya matatizo. Kuna mafaili na mafaili ya malalamiko ambayo yamekuwa yakipelekwa *CDA*, lakini kwa bahati mbaya mchezo wa danadana umekuwa ukichezwa hasa kati ya *CDA* na Ofisi ya Waziri Mkuu. Sasa wananchi wa Dodoma wanasema, wamechoka na wangependa kwa kweli Waziri ambaye ana dhamana ya ardhi aingilie kati. Tukiangalia mantiki kwamba *CDA* ni kweli wamepewa hatimiliki lakini hiyo hatimiliki inafanana na hatimiliki ya mtu yeyote mwingine katika nchi hii na ni Waziri wa Ardhi ndiye anawajibika kuhakikisha kwamba masharti ndani ya hiyo hatimiliki yanatimizwa. Baadhi ya masharti hayo ni kuhakikisha kwamba wale waliokuwa wanaikalia hiyo ardhi wanapewa haki zao.

Mheshimiwa Spika, kuna msemo wa Kiingereza unaosema: "*enough is enough.*" Sasa wananchi wa Dodoma wanasema imetosha. Ningechomekea kwa Kigogo ningesema: "*Chakatala.*" Ombi la wananchi wa Dodoma wanaomba watendewe haki chini ya sheria ambayo imeundwa au tuseme imetungwa na Bunge lako Tukufu kwa nia njema kabisa kwamba wananchi wa Dodoma wasiwe wageni katika ardhi yao na pale ambapo ardhi inatakiwa kwa ajili ya matumizi ya umma basi wapate haki yao kwa maana fidia ambayo ni ya haki na inayotolewa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, pili, tungeomba zoezi la bomoabomoa katika yale maeneo ambapo watu wameshakuwa na makazi zaidi ya miaka mitatu na wanalindwa na sheria likomeshwe hadi hapo ambapo Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu watatimiza masharti kama yalivyotamkwa katika sheria.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, sina mengi zaidi labda niongeze moja tu kwamba ili haya mambo yashughulikiwe kikamilifu mbele ya safari tungeshauri kwamba Waziri wa Ardhi aunde Tume ambayo itaangalia kwa undani zaidi matatizo ambayo yamekuwa yakiwasibu wananchi hawa ambao nimekuwa nikiwazungumzia tangu huo muda ambao nimeuzungumzia hadi hivi sasa ili suluhu ipatikane. Kama wanastahili kulipwa fidia yao walipwe, kama hawastahili waeleweshwe ili mambo yajulikane. Mambo haya yakifanyika kwa kweli nitajisikia huru sana kuunga mkono hoja. Ahsante.

**SPIKA:** Pole sana Mheshimiwa Madeje, Waziri amesikia. Nadhani mchangiaji wa mwisho kwa mchana huu ni Mheshimiwa Mariam Mfaki.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru na mimi kupata nafasi hii ili niweze kuchangia kuhusu hotuba ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha leo hii kwa usalama na amani tuko ndani ya Bunge lako Tukufu. Mimi sina mengi sana ya kuchangia ila nina mawili, matatu. La kwanza, nimpongeze tena Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wao wa Wizara. Kwa ujumla wanajitahidi kufanya kazi zao vizuri na kusimamia vizuri kwa sababu imewezesha kupitisha sheria mpya kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kupata mikopo katika Mabenki ya kujengea nyumba zao.

Mheshimiwa Spika, la pili, naomba nizungumzie juu ya suala la upimaji wa vijiji. Upimaji wa vijiji ni muhimu sana kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri kwamba unawezesha wananchi wakishapata hatimiliki zao wanaweza wakaenda wakakopa Benki wakajenga nyumba zao. Kwa kuwa suala hili ni kubwa na ni kazi kubwa na nchi yetu ni kubwa, vijiji ni vingi ni ngumu sana kuvipima kwa muda mfupi kila mwananchi akapata hati yake. Namshukuru tu Mheshimiwa Waziri ameeleza juu ya tatizo la upungufu wa watumishi. Ni kweli Wizara hii ina tatizo la upungufu wa watumishi, matokeo yake ndio kuchelewa kupima mipaka ya vijiji na kupima viwanja katika maeneo husika. Suala la kupima mipaka ya vijiji ndiyo kazi ambayo Wizara inaifanya. Lakini bado kazi kubwa ambayo ni kuwapimia wananchi ndani ya vijiji kila mmoja aweze kupata eneo lake na amilikishwe eneo lake ili liweze kumsaidia katika maisha yake.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi ardhi ni uchumi, ardhi ni maendeleo, ardhi ni muhimu kwa kila mwananchi. Kama itawezekana kila mwananchi akapata hatimiliki yake katika eneo lake ya aina yoyote kama ni ya kimila au ya kisheria na aina nyingine yoyote ya hatimiliki kwa kweli wananchi wetu watafaidika nayo. Mimi hofu yangu ni juu ya wananchi wetu vijijini inawezekana sheria hizi zikawasaidia sana wananchi waliopo mjini lakini walioko vijijini kidogo itakuwa ngumu. Sasa tusipoweka utaratibu mzuri wa kuwawezesha wananchi vijijini wakapimiwa maeneo yao wakapata hati kwa kweli mikopo ya nyumba wataisikia tu wala hawatafaidika kabisa. Lingine ambalo nilikuwa naliona katika Wizara hii hasa katika suala la upimaji ni suala zima la fedha. Wanahitaji kupewa fedha za kutosha kama inavyoonyesha katika bajeti yao kwamba mwaka huu fedha walizotengewa ni shilingi bilioni 14 tu. Zikiongezwa angalau zitaongeza juhudi na kuongeza kazi ifanyike kwa haraka ili wananchi waweze kufaidika na hizi hatimiliki.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la watumishi. Kama alivyosema Mheshimiwa Waziri kwamba watumishi ni wachache, lakini ningeomba pengine ichukuliwe kwamba kuna wastaafu watumishi wa Wizara ya Ardhi ambao bado wana nguvu zao hawa wakitafutwa au tangazo tu likitoka naamini watapatikana wakapewa mkataba labda wa miaka miwili au mitatu wakati tunasubiri watumishi wengine waelimishwe ingeweza ikasaidia sana kuharakisha suala la upimaji. Kwa hiyo, ningeomba Wizara iwakumbuke hao ambao nao bado ni hazina yetu ya wataalam.

Mheshimiwa Spika, lingine ningeomba nizungumzie suala la Shirika la Nyumba *(National Housing)*. Ni kweli mamlaka hii kwamba imeanza kazi ya kujenga na kuuza hapo baadaye ndio mpango wao. Lakini vile vile nilikuwa naomba, basi katika kujenga na kuuza pengine waangalie sana suala la bei. Bei za nyumba zisije zikawafanya wananchi wengine wakashindwa kuzinunua. Wajenge nyumba ambazo wananchi wengi waweze kuzinunua na vile vile wawasiliane na mabenki hayo ambayo yatakuwa yanakopesha. Muda wa kukopesha uongezwe, isiwe miaka 10 au 15 basi ifike hata miaka 20, 25, au 30 kwa sababu ukiangalia watumishi wengi ni wa mishahara ya kima chini. Sasa bila ya kuwapunguzia na kuwapa muda mrefu wa kulipa kwa kweli inawezekana kabisa wakashindwa kununua hizo kwa maana ya kwamba mtumishi anaweza akafanya kazi akastaafu bila ya kuwa na nyumba. Lakini ukiwauzia nyumba hizi za *National Housing* kwa kiwango cha muda mrefu na bei ndogo nina uhakika watumishi wengi wataishukuru Serikali na matokeo yake atakapostaafu hatakuwa tena anahangaika mitaani, atakuwa tayari ana nyumba yake, ataishi na watoto wake na kwa kweli maisha yake yatakuwa mazuri. Kwa hiyo, hilo lilikuwa ni ombi langu.

Mheshimiwa Spika, ombi la pili ni juu ya Mamlaka yetu ya *CDA*. Mamlaka ya Ustawishi Makao Makuu wanajitahidi sana kupima viwanja na nyinyi ni mashahidi nina uhakika Waheshimiwa Wabunge wote mmepata viwanja na mpaka vingine vimebaki havijakwisha.

**WABUNGE FULANI:** Hatuna bwana!!!!

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Spika, suala la viwanja, kinachotatiza tu pale ninachoomba nizungumzie ni juu ya ukubwa wa viwanja ama bei ya viwanja. Kuna aina mbili ya viwanja, kuna makazi na kuna viwanja vya biashara. Mimi sitaki kuzungumzia suala la viwanja vya biashara kwa sababu ile ni kila mmoja atajipima uwezo wake. Lakini kuna viwanja vya makazi bei ya chini kwa mara ya mwisho ambayo nimeiona sio chini ya Shilingi laki tano. Najua hilo kwa sababu tukiacha hivi vya mwisho mwisho lakini kipindi cha nyuma kidogo kwa kweli vya bei ya mwisho vilikuwa sio chini ya Shilingi laki tano. Sasa tungeomba basi katika vile viwango vya bei wananchi wa Dodoma sasa hivi wanajitahidi sana kujenga nyumba watashindwa kujenga nyumba kwa sababu ya ughali wa viwanja vya makazi.

Mheshimiwa Spika, tunaomba sana Wizara kwa sababu *CDA* iko chini ya Wizara yake basi wakae pamoja waone kwamba: Je, mwananchi wa kawaida kwa nyumba ya kawaida kabisa ya kuishi kiwanja hiki kinunuliwe bei gani? Niwaombe sana waangalie na washushe bei ili ikiwezekana kila mwananchi aweze kupata kiwanja. Kwa sababu sasa hivi Dodoma imekua, tunaishukuru Serikali kwa sababu imeinua hadhi ya Mji wa Dodoma, kwa hiyo, kila mwananchi anataka ajenge Dodoma. Kwa hiyo, naomba sana bei ya viwanja iangaliwe vizuri na iangaliwe upya.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie juu ya suala la Vyuo Vikuu. Nimeona vipo Vyuo Vikuu viwili sasa hivi. Kuna Chuo Kikuu cha Dodoma na kuna chuo kingine cha pili kinajengwa pale ambacho nadhani kiko chini ya *RC*. Nilichokuwa naomba, kwa sababu vyuo ni sehemu ambayo wananchi wanaweza kujifunza ama kwa kuona ama kwa

kusikia au kwa namna nyingine yoyote ile, hata kwa kuongea na wasomi ambao wanakuja, labda kuwatembelea majumbani na kadhalika. Nilichokuwa naomba, basi vyuo hivi visilundikwe mahali pamoja vitawanywe katika mji wa Dodoma kwa sababu bado tunayo maeneo makubwa hakuna sababu ya kuvilundika. Vyuo Vikuu ni elimu, ni watu wanataka kujifunza, ni somo kwa wananchi wetu. Kwa hiyo, nilikuwa naomba hilo visilundikwe mahali pamoja, vitawanywe vizunguke mji wa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa, nilikuwa naomba ramani yetu ya Wilaya ya Bahi tunachelewa kujenga Bahi au wananchi wanachelewa kujenga vizuri ni kwa sababu ramani haijakamilika. Niiombe Wizara kwa kushirikiana na *CDA* ramani hii itoke ili wananchi wapate maeneo yao waweze kuanza kujenga.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sina la nyongeza, naomba niunge mkono hoja hii na nashukuru kwa kunisikiliza, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mfaki. Waheshimiwa Wabunge, dakika zilizosalia hazituwezeshi kumpa mchangiaji anayefuata haki ya kuchangia kwa dakika 15. Kwa hiyo, tutaishia hapo kwa mchana huu. Sasa jioni kuanzia saa 11.00 hadi 12.30 tutakuwa na wachangiaji sita nitawataja Mheshimiwa Castor Ligallama atatangulia, atafuatiwa na Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, halafu Mheshimiwa Felix Mrema, Mheshimiwa Herbert Mntangi, sasa nimempandisha Mheshimiwa Halima Mdee kwa sababu wote toka asubuhi wamekuwa ni CCM basi kwa mamlaka yangu inabidi nichanganye. Kwa hiyo, Mheshimiwa Halima Mdee na mwisho tutamalizia na Mheshimiwa Clemence Lyamba. Lakini Mheshimiwa Dr. Zainab Gama ni vizuri awepo kwa sababu hatuwezi kujua kati ya hawa kama wasipotokea, basi naye anaweza kupata nafasi.

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo. Kumekuwa na malipo kadhaa yamekwama pale katika Ofisi ya Uhasibu Bunge lakini leo Katibu Mkuu wa Fedha amewasilisha fedha za Bunge na kwa hiyo kuanzia kesho kutwa asubuhi mambo yote yatakuwa sawa sawa. Mambo muhimu haya huwezi kuendelea bila ya matumaini yoyote. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya tangazo hilo nasitisha Shughuli za Bunge hadi hapo saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.50 Mchana Bunge lilifungwa hadi Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11:00 Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kama nilivyotangaza wakati nasitisha shughuli za Bunge mchana, bado orodha ya wachangiaji inaendelea lakini nitajitahidi ili mtoa hoja aweze kutoa majumuisho kwenye saa 12.15, kwa hiyo, sasa kwa mpangilio huo, wale niliowatamka, tutaanzia na Mheshimiwa Castor Ligallama atafuatiwa na Mheshimiwa Beatrice Shellukindo wakati huo Mheshimiwa Felix Mrema ajiandae.

**MHE CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Awali ya yote napenda kumpongeza Waziri, Katibu Mkuu kwa hotuba nzuri, inaeleweka. Mimi mchango wangu utajikita kwenye sehemu ya migogoro ya ardhi. Mwaka jana tarehe 7 Agosti, Bunge lako Tukufu lilipokaa kama Kamati ya Matumizi nilimwuliza Waziri kuhusu mgogoro ambao umedumu takribani miaka 14 na leo hii ni mwaka wa 15. Mgogoro huu katika Wilaya yangu, kati ya Kata ya Mchombe na Kata ya Chita, kwenye mpaka ambao jirani kuna Jeshi la kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, katika majibu ya Waziri na kwa ruhusa yako, naomba niyasome. Waziri katika majibu yake alisema: "*Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli Mheshimiwa Castor Ligallama katika mchango wake alitueleza hili tatizo la mgogoro wa mpaka kati ya JKT Chita na kijiji cha Ikule. Niseme tu kwamba tumepokea hoja yake na katika maelezo yake alisema kuwa Tume zilishapelekwa pale na TAMISEMI vili vile wamepeleka Tume na Ofisi ya Rais imeshapeleka Tume. Kwa hiyo mahali pa kuanzia tunapo, tutaangalia hizi Tume zimesemaje? Je, zenye mipaka zimesemaje na ramani zimekaaje? Nadhani atuachie tulifanyie kazi kwa nia ya kulimaliza ili mwakani tukikutana hapa tuzungumze mengine tusizungumze hili tena.*" Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, tunalizungumzia hili tena, halijakwisha. Tunalizungumzia hili tena kwa sababu nimepokea barua mbili. Moja kutoka TAMISEMI ambayo nimeipokea mwezi uliopita tarehe 13 na hii nimeipokea leo kutoka kwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, inahusu suala hili. Hizi barua zote nikianza na ile ya TAMISEMI, kwa kusema kweli bila kuficha, inaongeza tatizo. Sidhani kwamba ninavyomfahamu dada yangu Mheshimiwa Celina kwa mbali, ame-*sign* lakini sidhani kama aliandika yeye. Kwa sababu eneo lile analifahamu, sidhani kama angeweza kuandika barua hii.

Mheshimiwa Spika, kwa hali hiyo, inaongeza tatizo kuliko kupunguza. Ina maswali mengi kuliko majibu barua hii. Barua hii ya pili, toka kwa Waziri nayo vile vile ina-*refer* kwa kazi aliyofanya mtu mwingine sio Wizara yake. Kwa hiyo, tatizo linabaki pale pale kwa kuchukua taarifa. Kwa ujumla naweza kusema majibu ya barua hii ambayo niliwaandikia wanayafanyia kazi mezani kwa kutumia mafaili kuliko kwenda kwenye *site* na kuona mgogoro wenyewe ukoje.

Mheshimiwa Spika, mgogoro ule sio mkubwa sana ukiuangalia na kama laiti wananchi wangesikilizwa, sijui ni kitu gani viongozi wengi wa Serikali, wamekwenda, lakini hawakufanya mkutano na wananchi. Sasa kama, hata katika mashauri ya kawaida si unasikiliza pande mbili? Huyu anasemaje, huyu anasemaje. Sasa haya maamuzi ya kusoma kwenye mafaili na kuja kuleta *conclusion* ya suala zito lililodumu miaka 15 kwa barua ya *page* mbili kwa kweli imenisikitisha sana mimi kama mwakilishi wa wale watu.

Vijiji vile, labda nieleze kwa kifupi. Mambo mengine tunakubaliana yaliandikwa, ni kweli Jeshi lilipofika liliomba ardhi kijiji cha Chita mwaka 1977, sina ubishi na hilo. Lakini kijiji kile kiliwapa mahali, kwamba ninyi wenzetu mtakaa Kati ya..., sisi mipaka yetu mikubwa ni Mito. Mtakaa kati ya Mto huu na Mto huu na wakakaa haikuwa na matatizo. Mpaka 1994 ndio tatizo likaanza. Mheshimiwa Waziri hapa anasema tatizo

limeanza mwaka 2002, hapana. Tatizo limeanza mwaka 1994. Baada ya Jeshi kutokufuata mipaka ile ya mito upande mmoja wa kijiji mama, kile kijiji walichowapa wakajisogeza kilomita tano mpaka Kitongoji cha makutano, kutoka mto *land* mpaka kitongoji cha makutano.

Mheshimiwa Spika, upande huu mwingine ni Kata nyingine ambayo hawakuomba, wamevuka mto ule, mto ambao ni mpaka wa Kata kwa Kata, wakaenda Kata nyingine ambayo hawakuwahi kuomba, wakaichukua yote. Wakaichukua na vitongoji vyake, mpaka shamba lao likawa sasa linakutana na shamba la *Kilombero Plantation Limited* ambayo zamani lilikuwa *TACCO*. Wakachora na ramani sasa mwaka 2002. Mheshimiwa Waziri ananiambia mgogogro umeanza mwaka 2002 wakati kijiji cha Ikule, kilipokuwa kijiji kamili. Kijiji cha Ikule kiko Kata nyingine, kijiji cha Ikule hata kama kingekuwa kijiji mama kisingekuwa hata kijiji kamili Ikule, ingebaki kijiji mama, mpaka na Kata ya Chita unabaki mto ule ule Mkaja.

Mheshimiwa Spika, wale hawahusiki kabisa na suala hili. Sasa ramani hii, imekuwenda kufukia kile kijiji kilichoandikishwa mwaka 1999. Mwaka 2002 inachorwa ramani, inafukia kijiji cha mwaka 1999, sasa kama wanataka kufukia kile kijiji, toa *revocation notice*, futa kijiji halafu weka shamba. Kijiji kipo, kinatambulika na hati imetolewa na Serikali, leo unakifukia halafu unakwenda mbele na vitongoji vingine unafukia vyote vinakuwa shamba. Wale watu 5600 mtawapeleka wapi? Lakini yote ni shauri ya kutokwenda kwenye *site*. Laiti kama Serikali kwa mwaka mzima tangu tuongee tarehe 7 Agosti, 2008 ingelifika kule haya matatizo yasingetokea.

Mheshimiwa Spika, Lakini tunafanya kazi kwenye mafaili! Wananchi wale wamekata tamaa wakilima kwenye ardhi hii ambayo ilikuwa yao, ambayo Jeshi limetwaa, wananyang'anywa vitendea kazi vyao, majembe, wanatozwa kwa kila eka Sh. 10,000/=. Fikiria shamba lako umelilima miaka na miaka, halafu mtu anakuja anachukua na anakutoza Sh. 10,000/= kwa kila ekari! Majembe yako! Majembe unajua kwa mwanakijiji ni kitu, ni *asset* kubwa. Kupata jembe la Sh. 7,000/= ni kazi. Wanachukua wanakwenda nayo. Vitendo vingine, adhabu adhabu za kijeshi hizi, kupita kambini pale ni shida. Tuna kambi kama *Lugalo Baracks*, mbona watu wanapita! Kambi ipo huku na huku. Pale ni hivyo hivyo, lakini ukipita pale inabidi manyanyaso, ufanye nini, sasa hawa wanakijiji wanaona dah! Balaa gani hii? Na Serikali ipo! Kwa hiyo, tatizo hili limekuzwa na kutokwenda kuangalia hawa wanakijiji hasa wanachosema ni kitu gani.

Mheshimiwa Spika, Sasa baada ya wanakijiji kukata tamaa kabisa, wakaona waende wapi? Mimi Mbunge wao nimesema mwaka jana, wakaona wakimbilie kwa mwenye Serikali, Chama Cha Mapinduzi. Wakaenda kwenye Chama, chama Kata yao, kwenye Kata, Chama Wilaya na Chama Mkoa. Nazishukuru. Napenda kuchukua nafasi hii kushukuru Kamati za siasa za Kata ya Mchombe, Wilaya ya Kilombero ikiongozwa na Mwenyekiti Abdallah Kambangwa na Kamati ya siasa ya Mkoa ikiongozwa na Eng. Petru Kingu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hawa angalau wamekwenda na bila kumsahau Kamisa Mkuu wa Mkoa Lt. Col. Mstaafu Issa Machibya. Amekuja ameliona hili na akalichukua kama

ajenda likapelekwa kwenye Chama. Hao ndio wamekwenda kuwasikiliza wananchi. Wamekwenda kuwasikiliza wananchi na nafikiri kwa mwenendo tunaokwenda, suala litakwisha. Ilikuwa sijui kama nini! Ndugu zangu wengine wako humu ndani, wamekwenda kule, lakini wanaishia Jeshini, wanakwenda wanaishia Jeshini, wanakwenda wanaishia Jeshini. Mheshimiwa mmoja nilimpigia simu akiwa Morogoro, tafadhali ukishaingia Jeshini nenda kawasikilize na wananchi. Ndiyo bwana, kaishia Jeshini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nashukuru sana, tumechukua mkondo wenye Serikali wamewasikiliza wananchi wao na hatimaye nafikiri watakuja kwenu Serikali tena wakishamaliza mchakato, maana huu ni mchakato. Wako ndani ya mchakato na ni kitu rahisi. Watatafuta waliokuwa waanzilishi wa Kambi ile, bahati nzuri Mwenyezi Mungu amewaweka wapo, watatafutwa viongozi hawa wa katikati na karibu wote wapo. Hata kule kwenye vijiji tulipokwenda wote wapo, mwanzilishi kabisa, mtendaji wa kwanza wa kijiji kile kilichogawa ardhi yupo na mitasari ipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kata nyingine haihusiki, imekwenda kuingizwa kule. Kwa hiyo, mimi nilipendekeza kwa Waziri kwamba ramani ile ya mwaka 2002 ifutwe. Kwani ramani ni msahafu? Ifutwe! Ikifutwa ile mipaka itarudi kawaida. Nilifanya ushauri huo baada ya kuongea na Kamishna msaidizi wa kanda ya Mashariki katika Wizara pale. Akaangalia nikamweleza tatizo akaona kweli ramani ina matatizo tukakubaliana kwamba mkaandike barua tufute hii ramani. Kwa hiyo, nina imani kwamba barua yangu Waziri ameipata, lakini sijapata jibu juu ya pendekezo la kufuta ramani ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini yote yakiisha chama kikishafanya kazi yake, tutarudi Serikalini na mapendekezo ya chama yanawekwa wazi na tutaona nani mwenye haki. Lakini mimi nasema kabla kabisa hata maamuzi ya mwisho hayajafanyika, wananchi wana haki na wamenyanyaswa kweli. Wananchi wale wana haki. Kwa sababu hata mimi, kweli nikazanie kitu kwani mimi sina akili? Eeh! Jamani. Mbunge mzima na elimu yangu ya Chuo Kikuu na *experience* ya kufanya kazi kwenye Serikali miaka 10 na nina miaka 22 kwenye mashirika ya umma, hili naling’ang’ania kwani mimi siwezi kutafakari vitu jamani? Mimi nasema wananchi watashinda katika hili, watashinda! Ripoti iliyoandikwa kwa Rais ilimpotosha. Ilimpotosha Rais! Nadiriki kusema Rais alipotoshwa katika hilo na tuwe wazi, sisi ni binaadamu. Unaweza kukosea baadaye ukamwambia Rais kwamba samahani, uamuzi ule ulikuwa wa makosa. Ukweli ni huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tusipofanya hivi tutasemaje katika mikutano tujisahihishe? Si kuna kukosea? Kwa hiyo, mimi naomba kwa hilo niishie hapo nikiamini kwamba Wizara itafanya wajibu wake, sijui tena niseme mwakani tutakutana tena, mwakani liishe au litakwisha hapa katikati. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Castor Ligallama na pole sana na tatizo hilo. Tunaendelea. Namwita sasa Mheshimiwa Beatrice Shellukindo – Mbunge wa Kilindi, atafuatiwa na Mheshimiwa Felix Mrema wa Arusha Mjini na Mheshimiwa Herbert Mtangi – Mbunge wa Muheza ajiandae.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuweza kuchangia. Nilikuwa jimboni lakini niliposikia Wizara ya Ardhi ilibidi nije kwa kasi sana kwa sababu kuna mambo ambayo nadhani ni muhimu sana kuyasema na wananchi wa Kilindi na wananchi kwa ujumla wakayasikia.

Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri anayoifanya na ngumu na kubwa, lakini vile vile nampongeza Katibu Mkuu na Ofisi yake yote kwa kazi ambayo wanaifanya. Kwa kiwango kikubwa naweza kusema wanafanya kazi nzuri, mabadiliko tunayaona. Lakini ambapo pana mabadiliko pia pana mapungufu ambayo lazima niyasemee. Haya yote niseme kwamba nimekuja maalum kumshukuru sana kupitia kwako Mheshimiwa Spika, kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na wafuatao ambao nitawataja kwa kutusaidia sisi wananchi wa Kilindi.

Mheshimiwa Spika, tulikuwa na migogoro mikubwa sana ya mipaka, Vijiji vinne vikahamishiwa katika Mkoa wa Manyara ghafla tu jambo ambalo lilichanganya wananchi, kwa sababu tangu enzi za mkoloni wako pale na mipaka inafahamika. Tatizo hili kwa kweli lilisababisha kero kubwa sana na kwa kiwango kikubwa lilileta matatizo hata shughuli za maendeleo kusimama. Lakini namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kama kawaida kwa busara zake, aliagiza mamlaka husika ziweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, kazi imefanyika na imekamilika tunachosubiri ni yale tu mambo ya kiutaratibu kukamilika. Niseme hapa kwamba namshukuru sana Waziri wa Ardhi - Mheshimiwa Chiligati, namshukuru sana Mheshimiwa Celina Kombani - Waziri wa TAMISEMI nikisema hivyo na Mamlaka zao. Lakini kipekee pia nimependa sana kumshukuru Katibu Mkuu kwa sababu bila misukumo yake kwa Mawaziri hawa, Makatibu Wakuu wote wawili, nimshukuru sana Kamishna Msangi, kwangu mimi amekuwa msaada mkubwa; kuna mengine niliyokuwa nakwenda nayo pale nimepamba moto kama nini, nikifika pale ananituliza na kunieleza taratibu, kwa kweli namshukuru.

Mheshimiwa Spika, vile vile nimshukuru sana Mkurugenzi nadhani huyu wa ramani, Bwana Masele, naye kwa kweli kwa kiasi kikubwa alinisaidia na kunipa ufafanuzi jambo ambalo lilipelekea mimi sasa kushirikiana na wenzangu tukaweza kulifikisha kwa Mkoa wa Manyara, Bwana Shekifu Mkuu wa Mkoa wa Tanga wakati ule Abdulazizi - Mkuu wa Wilaya ya Kiteto Bwana Enjewele na wataalam wake wote, Kamati yake ya ulinzi na usalama, Mheshimiwa Sarah Dumba wa Kilindi na wataalam na Kamati ya Ulinzi na usalama. Kazi ilichukua muda mrefu takribani miezi mitano lakini nasema tunawashukuru wote, tunachosubiri sasa hivi ni kukamilisha tu kwa tamko, imekubalika mipaka ya mazoea itaendelea ila pale ambapo palikuwa na mgogoro kidogo pale pamefanywa hifadhi na pale ndipo tutakapotumia *GPS*.

Kwa kweli napongeza pale ambapo viongozi wetu wa Serikali yetu wanakuwa wanaangalia na kuona ili kutatua hili ni lazima tufanye jambo ambalo litaweza kuondoa kero. Nawashukuru sana kwa niaba ya wananchi wa Kilindi.

**SPIKA:** Kwa taarifa yako tu, Mheshimiwa Mzee nimemwona ameingia sasa hivi. Ahsante sana. Endelea Mheshimiwa.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, nilishakwambia wazee wako majumbani na vijijini wanaota moto, hapa ni Waheshimiwa Wabunge. Ninaomba niendelee. *(Kicheko)*

Nilikuwa nimefurahi sana, nimefarijika katika ukurasa wa 56 pale kuhusu ajira ya maafisa ardhi. Kwa kweli maafisa ardhi wengi tulionao wengine si kwamba tu hatuna, wako wachache wenye ubora unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, nimefurahi katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 56 ameweza kuona kwamba ni muhimu sasa watajaribu kuajiri wao moja kwa moja kutoka vyuoni kama Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI. Maana hapa wao ndio walikuwa wanaajiriwa kupitia TAMISEMI na wengi kwa kweli uzoefu wao na uwezo wao ulikuwa kidogo si wa kukidhi. Kwa hiyo, hiyo nimeipongeza na naamini Mheshimiwa Waziri atatekeleza kama alivyosema katika *speech* yake.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kabisa niseme kuna lugha inayoendelea kwamba Kilindi kuna ardhi. Jamani naomba nitamke kama mwanakilindi. Mimi sio mamlaka lakini nasema kwa niaba ya wanakilindi, Kilindi hakuna hiyo ardhi mnayofikiria. Maana kila mahali unapokwenda unasikia watu wahamishiwe Kilindi. Sisi wenyewe sasa hivi tumefika mahali tunatafuta pa kwenda. Kwa hiyo, naomba niweke wazi Tanzania nzima wasikie na zile barua ambazo zinafululizana, hatuna ardhi ya kugawa kwa sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli pia, hapa mimi nilikuwa nasema tuongeze nguvu kwenye hati miliki hasa hizi za kimila. Kwa mfano, Wilaya ya Kilindi mpaka sasa hivi hakuna hatimiliki ya kimila hata moja iliyotolewa. Tunazo hatimiliki kwa ajili ya vijiji vitano tu. Walikuja wataalamu maeneo ya Gitu, kwa Mwande na Kibirashi. Wakahamasisha pale wananchi wakaelewa, wanangojea kwa hamu sana lakini kusema za ukweli hawajarudi, naamini labda ni kutokana na bajeti. Naamini bajeti ya safari hii wataweza kufikiriwa na hili angalau sasa tuanze kutoa hati miliki.

Mheshimiwa Spika, nimeona orodha pale ya hati miliki karibu 19,000 na kitu, Kilindi hakuna hamna hata moja na wananchi wanahitaji sana kupata kumilikishwa ili waweze kupata mikopo na mengine kama ambavyo inavyofahamika muda haunitoshi kuelezea, lakini vile vile pamoja na kuisifu Wizara, bado hati zinachukua muda mrefu sana. Hapa *CDA* kwenyewe tumepewa viwanja lakini zile hati ni mlolongo. Zinachukua muda mrefu sana!

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri hili aliangalie na aone kwamba anaweza kupata suluhu. Lakini vile vile naomba niseme kama angalizo. Sasa hivi, kwa sababu sisi Tanzania ardhi haitolewi sera yetu, unakuta sasa katika uwekezaji, wanatumia Watanzania hawa hawa, kwa hiyo, inakwenda kwa wageni, mpaka tuje tushtuke tutoe hati miliki baada ya kufanya *Land Use Plan*, tutakuta kwa kweli tumechelewa.

Mheshimiwa Spika, naomba nije kwenye hili ambalo nataka kulisemea lakini naomba tu nieleweke kama taratibu haziruhusu basi, lakini nilikuwa nataka kuiomba sana Serikali kwamba kuna watu binafsi wana watu wao wanapangisha. Watanzania wengi tunafahamu kipato chao, hawana uwezo wa kujenga nyumba wote, sasa nilikuwa naomba Serikali iangalie namna ya kuwasaidia hawa watu. Mtu anapata mshahara kwa mwezi labda kipato cha shilingi laki mbili, kodi ya nyumba unaambiwa anatakiwa alipe ya mwaka mzima. Sasa nilikuwa naomba, Serikali ikae chini iangalie, kwa sababu kweli hizi nyumba za watu binafsi, wana haki ya kupanga wanavyotaka, lakini tuone tunawasaidiaje hawa watu ili ni tatizo linatokea mara nyingi kweli! Angalau wachukue kodi kwa kila mwezi au hata miezi mitatu. Lakini kwa kweli kwa mwaka mzima, athari ni kubwa sana kwa watu wetu.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naangalia Wizara kama inaweza ikafanya mazungumzo fulani au namna fulani ikabuni kwa hekima zake. *National Housing*, sijui kama imebadilika, lakini nakumbuka sera ya *National Housing* zilijengwa maalum kwa ajili ya watu wa kipato cha kawaida na cha chini, lakini mambo sasa hivi yamebadilika. Nakumbuka tulikuwa kwenye mkutano fulani nikiwa pamoja na Mheshimiwa Lucy Mhenga na Mheshimiwa Lucy Owenya walikuwa wakali sana juu ya suala hili.

Mheshimiwa Spika, ni kwa sababu sera imebadilika, hatuelewi. Imekuwa sasa ya watu wakubwa. Ukija kwenye kuuza zile nyumba, zinauzwa Shilingi milioni 80 na kuendelea. Kwa hiyo, yule mtu aliyekuwepo ndani analazimika kuondoka, hana huwezo. Lakini sio hivyo tu, kodi zimekuwa za juu sana. Mimi nyumba ninayoishi kwa mara ya tatu kwa mwaka huu mmoja imepandishwa kodi, juzi nimeambiwa imekuwa Sh. 358,000/=.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi afadhali, lakini wale watu wa chini wanaongezewa. Lengo la kuuza nyumba za Serikali ilikuwa kwa ajili ya kuwasaidia wale watumishi wa Serikali ambao wanaondoka wasiweze kuathirika. Wakapewa majumba na viwanja vikubwa vikubwa, hao watumishi ambao hawakubahatika kupata nyumba ya Serikali wako kwenye nyumba za kupanga, kwanini basi nao wasiuziwe? Au kama hawauziwi, basi wengine wameshafiwa labda waume zao wameshafariki wamebaki wajane na watoto. Wengine watoto wameshakuwa wakubwa wameondoka, wako pale wanaadhirika kabisa hawajui waende wapi.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba sana, Mheshimiwa Waziri hili aliangalie na watu wake wa *National Housing* hizi kodi hizi, tunawalenga wakina nani? Wakae kwenye hizo nyumba. Kama ni wale waliokuwa wanalengwa, basi turudi kwenye ile ile taratibu. Tusije tukaleta hoja binafsi. Lakini vile vile niseme, *National Housing* kwa utafiti kidogo niliofanya, kwa mwezi wanapata zaidi kwenye kodi zaidi ya milioni 800. Sasa kama hizo hela, zinafanya nini? Mimi nilifikiria umefika wakati *National Housing* sasa wawe ni watu wa kujenga, wanauza, wanajenga wanauza, kuliko hii ya kusema kwamba mnamuuzia fulani halafu baadaye zinabaki.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri amesema kuna baadhi ya nyumba zitauzwa, nyingine zitabadilishwa sijui kuwa majengo ya watu wengi. Ni zipi?

Mtachaguaje? Zipi ziwe zipi? Mimi kwa kweli nilikuwa naomba sana *National Housing* waende kwenye mfumo huo, wajenge wauze, wajenge wauze lakini hizi nyumba zibaki. Walikuja watu hapa nadhani na wewe ulikwenda kwenye uwanja wa maonyesho pale kwetu, walikuwa wanafanya *Cheap Housing*. Wanajenga nyumba kwa bei nafuu; Shilingi milioni 17 wanajenga nyumba ya vyumba vitatu na kasebule na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, hivi hawa wakipewa hela za kodi za mwezi mmoja, watagejenga nyumba ngapi za watumishi au za wananchi wa kawaida? Shilingi milioni 17 anajenga nyumba ya vyumba vitatu, sasa hii kodi ya mwezi mmoja tu akipewa na *National Housing* wanaweza wakafika wapi? Kwa kweli mimi nadhani hapa pana jambo lazima tuliangalie ili tufanye jambo sahihi ili kila mtu afurahie manufaa na matunda ya nchi hii yetu ya Tanzania ambayo wote kwa kweli kwa kiasi fulani tunachangia.

Mheshimiwa Spika, nakaribia kumaliza. Kuna tatizo ambalo naomba niliseme, unakuta kwa mfano labda mtu kwa sababu moja au nyingine eneo lake anaamua sasa kumwuzia mtu au kummilikisha mtu. Anakwenda ardhi, wana *check* mpaka pale kwenye mashine, pale wanafanya *search*, inaonekana kabisa Beatrice Matumbo Shellukindo ndiyo mwenye hiki kiwanja. *Process* zinaanza vizuri, ikifika mwisho kuja kwenye kutengeneza hati sasa, unaambiwa ilikosewa jina sio la kwake, kiwanja hakikuwa chake.

Mheshimiwa Spika, hili tatizo liko sana na mara nyingi nasikia watu wanaomba tuwasaidie na sisi wengine pia yametukuta. Mimi nilikuwa naomba sana hapa Mheshimiwa Waziri kama pengine hawezi kulitolea majibu kwa leo lakini nilikuwa namwomba sana hili suala aliangalie na wazidi kuimarisha katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, lakini mwisho kabisa, nikiwa nakuja hapa Bungeni nimepata simu. Mtanzania tu ametafuta namba yangu kajua kama nachangia, anasema sisi tuliojenga kwa pensheni zetu ndogo ndogo, tukafungiwa umeme, maji tumekaa miaka yote, leo tunaambiwa tubomoe twende wapi? Hili limezungumzwa na watu wengi. Lakini naomba Mheshimiwa Waziri sasa atoe tamko lake, pengine sio leo, lakini atueleze kwa hawa watu ambao walijenga wakafungiwa umeme, maji, simu, wamekaa wakilipa hata kodi wakati mwingine wanalipa kodi za eneo, leo hii anabomolewa anaambiwa aondoke. Hawa watu mnawafanyaje? Ni watu wa aina gani? Kwa sababu aliyekuwa anaongea ananieleza kuna fulani yule bwana alikuwa bosi wetu, yeye kwake hajabomolewa, sisi inapindishwa pindishwa tunaambiwa tuondoke.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niseme, binafsi niliona niseme hayo machache naunga mkono hoja, lakini naomba sana kwa haya mapungufu machache niliyosema, basi wayafanyie kazi, lakini naomba nikija Wizarani msinifukuze kwa sababu nimesema mapungufu. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, namwita Mheshimiwa Felix Mrema atafuatiwa na Mheshimiwa Herbert Mtangi wakati huo Mheshimiwa Halima Mdee ajiandae.

**MHE. FELIX C. MREMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja hii ya Waziri wa Ardhi, nitumie pia nafasi hii kumponngeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa asubuhi hii ya leo, niwapongeze pia Katibu Mkuu na viongozi wengine wote katika Wizara yake kwa kazi nzuri walioifanya na wanayoifanya kumsaidia Waziri katika kuandaa hotuba hii ya bajeti aliyotutolea asubuhi ya leo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri kaeleza vizuri sana umuhimu wa Wizara yake, katika uchumi wetu. Ardhi ikisimamiwa vizuri, ujenzi wa nyumba, maendeleo ya makazi yakiwa na msukumo mzuri na usimamizi mzuri utafanya kazi kubwa sana kuchangia ukuaji wa uchumi wetu. Haya mawili narudia, yakisimamiwa vizuri, haya yafuatayo yanawezekana.

Kwanza, ajira ya zaidi ya milioni moja kila mwaka, inawezekana kupatikana kutokana na sekta hii tu ya Wizara ya ardhi na maendeleo ya makazi. Kukua kwa uchumi kufikia zile asilimia nane mpaka tisa, kunawezekana kama Wizara hii ikifanya kazi yake vizuri. Kukinga uchumi wetu kutokana na athari zinazotokana na misukosuko nje ya nchi, inawezekana kama Wizara hii ikifanya kazi yake. Sasa ifanyeje kazi yake ili ichangie yale ambayo tunataka wachangie. Mimi nitajikita tu katika lile suala la nyumba na maendeleo ya makazi. Hii ndiyo ndoto ya kila binadamu duniani anataka awe na nyumba ya kuishi katika wakati wa maisha yake na sisi Watanzania sio tofauti.

Mheshimiwa Spika, sasa hali yetu ikoje hapa Tanzania? Kwa sababu ya mfumo wetu ambao haukuwa mzuri huko nyuma tuna *deficit* ya zaidi ya nyumba milioni mbili ambazo zilikuwa zinatakiwa kuwa zimejengwa lakini hazijajengwa. Wanasema pia kwamba kila mwaka hapa Tazania panahitajika nyumba 200,000 ku-*satisfy demand* ambayo inatokea kila mwaka, 120,000 zikiwa mijini na 80,000 zikiwa vijijini lakini baya zaidi wanasema kwamba ziko nyumba karibu 50,000 ambazo hazijakamilika zilizozamisha karibu shilingi trilioni 1.5 ambazo hivi sasa zimekuwa mtaji mfu *(dead capital)*.

Mheshimiwa Spika, sasa uchumi wenye kiwango kikubwa namna hii ya mtaji mfu *(dead capital),* ni uchumi wa kusikitisha sana. Waziri hapa inabidi ukose usingizi maana iko kwenye hali ambayo ni ngumu sana. Hao wananchi wamejitahidi sana katika mazingira magumu kujaribu kujenga makazi yao ya kuishi, lakini wakafika mahali wakashindwa na hamna mtu wa kuwasaidia. Sasa hebu fikiria, mtu anafanya kazi maisha yake yote, anastaafu, hajaweza kukamilisha nyumba yake ya kuishi, anatumia pesa zake zote za pensheni kujaribu kukamilisha, anashindwa kuikamilisha mpaka anakufa hajakamilisha nyumba yake ya kuishi. Lazima tukose usingizi, tukiona hali ya namna hiyo, maelfu ya watu wa namna hiyo wanahangaika kuwa na makazi ya kuishi na mfumo wa kuwasaidia haupo ili wakamilishe ndoto yao hiyo.

Mheshimiwa Spika, sasa kigezo kinachotakiwa, ni Wizara iwe na mikakati ya kuhesabu kila mwaka ni nyumba ngapi zinazojengwa na wananchi, kila mwaka, tumewezesha wananchi wangapi kujenga kila mwaka! Tukiwa na mipango madhubuti ya kuwawezesha wananchi kuweza kujenga nyumba hizo, ndio tutaweza kuwa na vigezo

vinavyoeleweka vya kupima tunawasaidia namna gani wananchi wetu kuwa na makazi bora ya wao kuishi. Vinginevyo tutakuja kusutwa, kwamba uongozi wetu tumeshindwa kutimiza wajibu wetu wa kusimamia sekta hii.

Mheshimiwa Spika, nieleze tu, tumefaulu sasa hivi kupitisha hizi Sheria mbili za *Mortgage Finace na Unit Titles Act* lakini bado tuna kazi ya kuzisukuma tasisi za kibenki ziweze sasa kutimiza wajibu wao wa kutoa hiyo mikopo ambayo inatakiwa. Ametuambia Waziri kwamba wanakamilisha taratibu, naomba wazikamilishe haraka ili sasa tuwe na njia ya kuziwajibisha hizi *Financial Institutions* kila mwaka ili waweze ku-*play their part*.

Mheshimiwa Spika, niseme bila msukumo wa makusudi wa Serikali, hii sekta haitaweza kutimiza wajibu wake. Marekani kwa makusudi kabisa wana kitu kinachoitwa *Fanie Mae* (*Federal National Mortgage Association),* iliyoanzishwa baada ya *Depression* kwa makusudi kabisa kujaribu kuwasaidia wale wenye kipato cha chini kuweza kupata nyumba za kuishi. Pamoja na matatizo ya ulafi yaliyotokea hivi juzi, bado Serikali haikuziachia hizi zife, imefanya kila jitihada kuhakikisha kwamba zinanusuriwa na zinaendelea kutimiza wajibu wao wa kuwasaidia hasa hawa wa kima cha chini kuweza kupata makazi ya kuishi na sisi hapa Tanzania tunatakiwa tufanya hivyo hivyo.

Mheshimiwa Spika, wanasema *National Housing Corporation, corporate mission* yao ilikuwa ni kuwasaidia wale wa kima cha chini na cha kati kuweza kupata makazi ya kuishi. Hiyo ndiyo ilikuwa mission yake toka mwanzo lakini, hivi karibuni wanaanza kusema sasa hivi wanaanza kushindana na sekta huria kwa ajili ya kutoa makazi sio kwa wale wa kima cha chini tena, kwa hao wengine ambao wanaweza kuhudumiwa na sekta hii huria. Nasema hapa tunafanya makosa makubwa kabisa, tuirudishe *National Housing* irejee kwenye kazi yake ile ya msingi ya kujenga makazi kwa ajili ya hawa wa kima cha chini na kati na wafanye kazi hiyo siyo ya kuwapangishia, mimi nawashukuru kwamba wanataka kujiondoa kwenye kuwapangishia, waendelee kujenga na kuwauzia maana kazi ya kupangisha *National Housing Corporation* haitaweza kufanya.

Mheshimiwa Spika, mmekiri wenyewe kwamba ukarabati ni kazi kubwa sana, kwa Shirika kukarabati yale majengo yote na hamtaweza kusimamia kwa nchi nzima, majengo yote ya *National Housing Corporation* kutokea Dar es salaam, pale mtakuwa mnajenga tu mwanya wa mizengwe na matatizo mengi. Tusiwafikishe watu huko, *lets cut our losses*, turahisishe kazi, jengeni kwa ajili ya kima cha chini na muwauzie.

Mheshimiwa Spika, ninao watu wangu wa Levorosi, wa Kibla, wa Ngarenaro, wako wengine wamekuja pale kusikiliza, Mheshimiwa Spika, leo asubuhi umewatambulisha, nakushukuru sana, wanalalamika juu ya hiyo kodi iliyotolewa na Shirika. Sasa nasema, tatizo litaendelea kuwepo, kila mwaka tutakuja hapa kulalamika kwamba kodi mliyopandisha ni kubwa. Sasa tutoke huko, wauzieni hawa watu hasa kwa sababu wengi walikuwa ni wale wa kima cha chini, lakini kubwa zaidi wengi ni wastaafu. Kuna Mzee Kamtwela, amefariki, kuna Mzee Msofe ambaye yuko pale mstaafu, wote ndio wa namna hiyo na wamekaa pale toka majengo hayo yalivyoanza mwaka wa 1975. Pango lile ukijumlisha walilokuwa wanalipa toka wakati huo mpaka leo, wangeliweza

kununua hayo maeneo ambayo wanayakodisha, wangeweza kabisa kuyanunua. Lile pango tu ukijumlisha lote, limerudisha gharama zote za *National Housing Corporation*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nasema, kama kuna utaratibu wa kuwauzia, wa kwanza kabisa kuuziwa ni hawa wa kima cha chini, toka mwanzo walikuwa kwenye hayo majengo na msijali kwamba eti ziko kwenye *prime area*, hata nao wanataka kufurahia *prime areas* na wao pia watakuwa katika nafasi nzuri zaidi ya kuwatafuta wawekezaji wakiwa huko ndani ya hizo *prime areas*. Tusiwaonee, tuwape nafasi ya wao nao kushiriki kikamilifu katika uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, narudia kusema, tatizo la makazi na nyumba siyo hizi 16,000 ambazo ziko chini ya *National Housing Corporation*, tatizo ni 200,000 kila mwaka ujenzi na hizo milioni mbili *deficit*, ndio tuweke akili zetu na nguvu zetu kuangalia tunawezaje kupunguza hili tatizo kubwa la makazi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kuna suala hili la *VAT*, wameniambia toka Arusha kwamba eti baada ya hotuba ya Waziri wa Fedha, sasa *VAT* kwenye kila pango, kwenye kila *invoice* ya kodi, wanatoza pia 18% ya *VAT*, mimi sikuielewa hotuba ya Waziri wa Fedha namna hiyo. Naomba Mheshimiwa Waziri, mkawasiliane na Waziri wa Fedha, je, ndivyo tulivyopitisha bajeti ya Waziri wa Fedha ili waweze ku-*add an additional* 18% kwa kodi ile ambayo sisi wenyewe tunalalamika kwamba ni kubwa mno na huko zamani usisahau walikuwa wanalipa 10% *Withholding Tax* na ilikuja baada ya kupunguza ile ya 15% ambayo ilikuwa inaonekana kwamba hailipiki. Sasa unatoka kwenye hiyo 10%, unaongeza nyingine 18%, unakwenda kwa huyu huyu wa kima cha chini ndiye anayebeba mzigo wote huo, hapana, mtihani mkubwa kabisa huu. Tafadhali sana muongee na Waziri wa Fedha, mkaliangalie suala hili kabla bajeti hii haijaisha kwamba je, kweli ndivyo tulivyofanya sisi wakati tukipitisha ile bajeti?

Mheshimiwa Spika, hapa pia niseme kwamba pengine ingeekuwa vizuri kama tungelipitisha ile *Finance Bill* baada ya hizi hotuba zote za bajeti, maana sasa hivi inaoenekana waliwahi pale, wakatuwekea vitu ambavyo pengine hatukuelewa vizuri tunafanya nini, sasa unakuja kukuta kwamba alah, kumbe ndivyo tulivyofanya vile! Wanalalamika kule wanasema ndiyo sisi Wabunge, ndio tumeongeza hiyo 18%, aha, aha, lazima twende *on record* tuseme siyo sisi, labda mfumo tu hapa umepita wakatulalia bila sisi kuelewa tumelaliwa namna gani?  Sasa, Waheshimiwa Wabunge, naomba tuamke kwenye hili.

Mheshimiwa Spika, namuomba Mheshimiwa Waziri, tafadhali sana, mkaliangalie tena suala hili la *VAT* maana hatima yake ni kuifanya Tanzania iwe ni most *expensive place, renting property* yake ya kuishi, ukiongeza hiyo 18% pamoja na 10% ya *Withholding Tax* na nafikiri sivyo tulivyokuwa tunapendelea. Mheshimiwa Waziri, nendeni tena mkaliangalie hilo na mtupatie majibu muafaka.

Mheshimiwa Spika, halafu mimi hili suala la kusema kwamba eti bajeti finyu, bajeti finyu, linanikera sana. Wenzetu Uganda wanaweza kupata pesa makusudi kabisa za

kusaidia *National Housing Corporation* ya kwao pamoja na Kenya wanasaidia *National Housing Corporation*, pesa za kusaidia kujenga makazi ya hawa wa kima cha chini na kima cha kati. Sisi hapa tunashindwaje? Kama wakati wote tunategemea pesa za *TRA*, lazima tutashindwa, bajeti itakuwa finyu. Lakini tuna *sources* nyingi tu katika nchi yetu za kuweza kutafuta hela kwa ajili ya kufanya mambo haya muhimu katika uchumi wetu. Tufanye kazi, tuwe wabunifu, tutafute hizo *sources* zingine ambazo ziko nchini kama jinsi Kenya wanavyotafuta, kama jinsi Uganda wanavyotafuta ili tupunguze hii kero ya makazi kwa hawa watu wetu wa kima cha chini hapa Tanzania ambao kweli sasa hivi inaonekana wameelemewa mno. Halafu inaonekana kwamba hata hatushituki kwamba kuna matatizo makubwa ya makazi katika nchi yetu. Namwomba Mheshimiwa Waziri akose usingizi kwa tatizo hili kubwa la makazi kwa ajili ya hawa watu wetu wa kima cha chini na kati katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, upimaji wa viwanja, inakuja pale pale, tunaambiwa bajeti finyu, bajeti finyu. Tusitegemee bajeti ya nchi yetu kwa ajili ya kazi hiyo kubwa ya upimaji wa viwanja. Tuwe wabunifu, tuwe wabunifu na naomba umsukume, najua wewe Waziri ni mpole sana, lakini kwenye hili upunguze upole, umfokee mwenzako wa Fedha, wafoke wenzako *BoT*, waambie bwana watafute mbinu za kupata fedha za kutosheleza ili kazi hii ya upimaji iende kwa haraka kama jinsi tunavyotaka katika nchi yetu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**SPIKA:** Kengele ya pili!

**MHE. FELIX C. MREMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii ambayo kwangu mimi naiona ni moja kati ya Wizara muhimu sana. Lakini vile vile nichukue fursa hii, kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji wote, kwa kazi nzuri ambayo wameendelea kuifanya.

Mheshimiwa Spika, yapo mabadiliko ambayo tunayaona, Wizara ya Ardhi ilikuwa imekaa vibaya sana. Sasa hivi kwa kiasi fulani malalamiko yanaanza kuonekana kama yanafanyiwa kazi na *inshallah* pengine yatapungua sana. Pamoja na kwamba hana Naibu Waziri, lakini anajitahidi yeye mwenyewe kuyafanya yote kwa bidii na kwa uwezo wake wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia matatizo makubwa hasa ya mashamba katika Wilaya ya Muheza na kwa sababu hiyo upungufu wa ardhi kwa wananchi wa Muheza. Nitalazimika hapa kuyataja mashamba ambayo kwa kweli yapo, tuna mashamba yasiyopungua 18 ya Mkonge. Sasa kama una mashamba zaidi ya 18 ya Mkonge yaliyochukua sehemu ya ardhi ya eneo lenu zaidi ya hekta 35,000, ninyi wenyeji wenyewe mmebakia na kiasi gani cha ardhi? Hapo ndipo matatizo yananza!

Mheshimiwa Spika, lipo Shamba la Mkonge Bwembwela, *Lewa Estate*, *Kibaranga Estate*, Azimio na Kilapula, Kumbulu, Fungo, Zeneti, Songa, Muheza Mkumbi, Kitisa, Furaha, Kigombe, Mlingoti na Shamba la Mpira la Kihuhwi. Ardhi yote imechukuliwa, nini matokeo yake? Madhara makubwa ni kama yafuatayo:-

Kwanza, wananchi walikuwa wanaishi katika maeneo hayo, ardhi ilipokuwa inahitajiwa na Wakoloni waliokuja kuweleza kupanda Mkonge, wananchi wakahamishwa kutoka katika maeneo waliyokuwa nayo, ardhi yao waliyokuwa wakiimiliki, wakasogezwa nyuma, wengi wa wananchi hao wakalazimika kupanda milima na leo wanaishi huko huko milimani, ardhi imechukuliwa. Lakini madhara mengine makubwa ni kwamba miundombinu ilipojengwa, ikaelekezwa kwenye mashamba hayo, reli ipo, barabara kweli ya lami ipo, lakini imepita katika mashamba hayo na sisi wote ni mashahidi tukipita na magari katika maeneo yale, barabara hizo kuu tunazoziona kando ya barabara hizo kuu ndio yameshamiri mashamba ya Mkonge, wananchi wanaishi wapi?

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyataja mashamba hayo, sasa naomba nizungumzie mashamba machache tu kwa sababu ya muda. Tuanze na hili shamba la *Bwembwela Estate*. Shamba hili lina ukubwa wa hekta 5,730, shamba moja tu na hili ndiyo shamba lenye utata mkubwa kwa sababu, shamba hili alijitokeza mwekezaji anayeitwa *TANFARMS*. Lakini *TANFARMS* hili ni jina tu la kibiashara, mwenyewe *TANFARMS*, ni Chavda. Akachukua fedha za Serikali kwa mamilioni, mimi siwezi kuzitaja hapa, anasema anaendeleza shamba, kapewa fedha na Serikali, Chavda akaingia mitini, akaondoka na fedha zote na shamba hakuliendeleza. Leo, kilichotokea ni nini? *CRDB* ndiye alikuwa mdhamini wa Chavda kwa hiyo akachukua shamba lile. *CRDB* amefanya nini? *CRDB* ameamua kuuza shamba lile kwa mwekezaji mwingine. Lakini angalia vichekesho, ninayo nakala hapa ya *Sale Agreement* iliyoingia yule Chavda ndiye alikuwa anaitwa *TANFARMS*, huu ni mkataba wa kuuza shamba lile, ni mkataba kati ya *TANFARM* na huyo mnunuzi. *TANFARM* ni Chavda ambaye alitutoroka, leo anakujaje kuingia mkataba wa kuuza shamba! Kumbe alikuwepo, kwa nini hatukumkamata wakati tunasema tunamtafuta na tunasema mpaka *INTERPOL* tumekwenda kule wameshindwa kumpata? Leo yeye *TANFARM* ndiye anaingia mkataba wa kuuza Shamba la Bwembwela! Ati ame-*appoint managers*, maana wamemwandika *TANFARM* hapa, *Receivers Managers* sijui watatu, *TANFARM* ndiyo wameuza! Mkataba huu sio batili! Watalaam wa Sheria hebu tuangalie, huu mkataba batili, *TANFARM* tunamtafuta, leo anaingia anauza shamba, halafu kamuuzia mtu anaitwa *AMC Limited,* jamaa wa Arusha.

Mheshimiwa Spika, lakini angalia ndani ya mkataba huu vichekesho vyake, Watanzania kweli dhaifu kweli kwenye mikataba. Hapa ndani shamba hekta 5,730 limeuzwa kwa Dola 30,000! Dola 30,000, ni shamba heka zote hizo pamoja na mali zilizoko kule na nyumba zaidi ya 50, Dola 30,000! Lakini, kibaya zaidi kwenye mkataba huu, zimeandikwa Dola 30,000, zinalipwa kwa *installment* kwa mikupuo miwili. Hii mikupuo miwili, mkupuo wa kwanza 15,000, wa pili 15,000 lakini ndani ya mkataba huu wameandika kwa tarakimu 15,000, lakini kwenye mabano kwa neno la Kiingereza wakaandika *twenty thousand shillings*, sasa ndio tafsiri ya Dola 15,000? Cha kushangaza na watu wazima wamesaini mkataba huo, hawakuliona hilo?

Mheshimiwa Spika, leo kuna ndugu zangu wa *World Vision* wako eneo lile la Bwembwela, Mkonge haulimwi katika maeneo yenye mabonde, wako pale Bwembwela wanataka kusaidia wananchi pale katika mpango wa umwagiliaji. Leo *World Vision* ambao kwa kweli nawapongeza sana, kazi nzuri wamefanya Muheza, wamesaidia ujenzi wa madarasa katika shule za Kwa Kibuyu, eneo hilo hilo la Tarafa ya Bwembwela, wamesaidia ujenzi wa shule za msingi katika Tarafa hiyo hiyo ya Bwembwela, shule nyingine ya Mihanga lakini wana eneo wanataka kuweka mpango wa umwagiliaji lipo ndani ya hilo eneo. Wanashindwa kuwawezesha wananchi kupata eneo la umwagiliaji kwa sababu ya utata wa umiliki wa shamba hilo, shamba ambalo tangu limenunuliwa mpaka sasa hivi wala haliendelezwi.

Mheshimiwa Spika, nitakwenda kwenye shamba lingine. Hawa wananchi walihamishwa Muheza kwenye maeneo tambarare, wamehamia mijini, sasa mpango wa hifadhi ya mazingira umekuja. Nilizungumzia hapa mpango wa *World Bank* na namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwa sababu alinisikiliza na ametupa ushauri tunautekeleza. Wananchi wale wamefukuzwa huku, wamepanda milimani, sasa mazingira inakuja, wanaambiwa wahame kule, waende wapi? Lazima warudi katika ardhi yao ya asili, sasa zile hekta 921 tumendelea kuzifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri, kwamba *notice* ya kuwapa wale waliokuwa wanamiliki shamba la Kibaranga ambalo tunataka wananchi wale wa Amani wapate maeneo ya hifadhi ya mashamba, karibu muda ule wa siku 90 utakwisha, nadhani mwisho wa mwezi huu au katikati ya mwezi wa nane, tutakuja rasmi kuendelea kusumkuma lile ombi letu tulilofikisha kwako la kutaka Hati za Mashamba haya niliyoyataja ambayo kwa kweli hayaendelezwi, zifutwe halafu tukae upya. Mashamba miaka 35 hayaendelezwi, watu wangahangaika! Idadi ya watu Tanzania imeongezeka na hata Muheza idadi ya watu imeongezeka. Tutafanya nini na tutakaa wapi? Tufute Hati hizi, tukae, kama mwendelezaji yupo makini, mwenye uhakika, mwenye uwezo wa kutaka kweli kuendeleza, basi huyo katika hekta 5,700 tunaweza tukawa radhi kumpa zaidi ya asilimia 50 na asilimia 50 wakapewa wananchi wanaohangaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mashamba hayo pamoja na kwamba Hati nyingine hazijulikani zilipo, hata kulipiwa hazilipiwi, sasa wewe hujalipia shamba *rent* kwa zaidi ya miaka 20, bado ni la kwako kisheria? Siyo kweli, siyo la kwako!

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nalipongeza pia Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, kwa maamuzi makini waliyofanya ya kuomba kufututiwa Hati kwa mashamba yaliyokuwa mengi. Yapo baadhi ya mashamba yanaendelezwa, kwa mfano, Shamba la Muheza Estate, mmiliki wake ni Agro Tanga, anajitahidi, anaendeleza shamba, tunaona. Lakini vile vile yeye, hata mimi nimezungumza nao, uwezo wa kulima shamba lote kwa sasa hawana. Kwa hiyo, wameruhusu wananchi wanalima katika baadhi ya maeneo, nawashukuru sana na ninaamini kabisa yale makubaliano tuliyofikiana nao ya kuwaruhusu hawa watu kulima kwa msimu, yataendelea na watu hawatabugudhiwa.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie pia mashamba mengine. Kuna Shamba hilo la Azimio na Kilapula. Shamba hilo tulipata wahisani tukalipima, watu wakapewa *offer* lakini unampaje mtu *offer* katika shamba ambalo Hati iko katika jina la mtu mwingine? Hivi hata ukipewa *offer* hiyo, utaweza kweli kuliendeleza shamba hilo? Kwa hiyo, tunataka hizi Hati kweli zifutwe ili wale wanaopewa *offer* waweze kuendeleza, kwa sababu hakuna mantiki yoyote ya kuweza kuendeleza shamba ambalo Hati yake haiko katika jina lako, iko katika jina la mtu mwingine. Hilo shamba la Azimio na Kilapula.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna mambo ambayo yanafanyika ya ajabu ambayo sisi watu wa Muheza yanatushangaza. Nimewahi kuzungumza hata hapa Bungeni kwamba tusaidiwe katika upimaji wa mashamba. Jibu ambalo nilipewa ni kwamba tayari kuna mtu amepewa hiyo *contract* ya kufanya kazi hiyo. Lakini ukienda Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, hawamjui mtu huyo. Kwa hiyo, yupo mtu anafanya kazi sijui analipwa na nani, wenye ardhi wenyewe hawajui na ninazo ramani ambazo tayari amekwishachora yule, lakini Halmashauri ya Wilaya ya Muheza haina ramani hizo, haina kabisa.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumze kidogo kuhusu nyumba hizi za *National Haousing*. Ukipita Dar es Salaam, ukatizama maghorofa yale ambayo unayafahamu kwamba ni ya *National Housing*, juu ya maghorofa hayo kuna vibanda vimejengwa vingi tu, kuna nyumba ambazo wala hazikuwepo katika *structure* za msingi. Nani amejenga *structure* zile zilizoko juu ya majengo yale? Nani ananufaika na kodi zinazolipwa katika *structures* hizo ambazo kwa kweli kwenye *base* ya nyumba za awali hazikuwepo? Inawezekana yapo mambo ambayo yanafanyika na viongozi wanayajua, lakini wanayafumbia macho. Baadhi ya *structure* zilizoko kule ni vibanda vya ovyo kweli kweli na vinatia aibu kuviona viko juu ya nyumba katika Majiji yetu na nina uhakika siyo Dar es Salaam peke yake, inawezekana hata katika nyumba za *National Housing* katika Miji mingine; Tanga, Moshi, Arusha, Mwanza na kadhalika hali kama hiyo ipo na inaendelea kufanyika.

Mheshimiwa Spika, mimi ninamtegemea sana Mheshimiwa Waziri hasa katika mapendekezo yetu ya kufuta Hati ya Mashamba hayo. Lazima tukubaliane, jamani jamani mmechukua ardhi kubwa kupita kiasi kwa Wilaya yetu ya Muheza ambayo pia tulikuwa pamoja na Wilaya ya Mkinga na ukienda Wilaya ya Mkinga, haya ninayoyasema ya Muheza utayakuta hivyo hivyo. Hali ni hivyo hivyo katika Wilaya ya Korogwe, kote tuna matatizo yanayofanana. Kwa hiyo, kwa kweli lazima tuhakikishe tunawasaidia wananchi wetu. Haiwezekani wananchi wakaendelea kuhangaika wakati ardhi ipo na haiendelezwi.

Mheshimiwa Spika, kama mashamba ya mkonge yangekuwa yanaendelezwa, pengine tusingekuwa na kitu cha kuzungumza, lakini hayaendezwi. Hati zile zifutwe, tukae upya, tugawane ardhi kwa mahitaji ya wananchi na mahitaji ya wawekezaji. Shamba la Mkonge la Kumbulu, yule mwekezaji yeye mwenyewe anakiri kwamba hizi hekta ni nyingi kwangu, siziwezi na yuko tayari kuzitoa, lakini atatoaje bila utaratibu huo wa kufuta Hati, halafu akapimiwe eneo ambalo kwa kweli anamudu kulifanyia kazi!

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja kwa sababu nina uhakika Hati za Mashamba yale zitafutwa, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa kuweza kunipa fursa hii ya kuchangia kwa vigezo ambavyo ulivitoa asubuhi, ninakushukuru sana.

Vile vile, nimpe pole Mheshimiwa Mbunge aliyetoka kuzungumza kwa yote ambayo yamemsibu kwenye Jimbo lake. Ninaamini Mheshimiwa Waziri atasikiliza na yeyote anayehusika atatekeleza wajibu wake ipasavyo ili wananchi wetu waweze kupata ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka jana wakati nikichangia bajeti ya Ardhi, nilizungumzia suala zima la mgogoro wa ardhi wa viwanja namba 695 na 696 vilivyopo Wilaya ya Kinondoni Jimbo la Kawe na kwa bahati nzuri na kwa nia njema kabisa, Mheshimiwa Waziri aliunda Tume yake ambayo kwa bahati mbaya ilimletea taarifa ambayo ni potofu. Halikadhalika, nashukuru kwa wale vigogo ambao niliwataja kipindi kile wakaja wakalalamika kwako, wakapeleka tarifa kwenye Kamati ya Maadili, ninaamini Kamati yako ililiangalia hili suala kwa mapana na haki itatendeka na naamini ukweli utadhihili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze moja kwa moja na suala zima la migogoro ya ardhi kama ambavyo Waheshimiwa wengine wamekuwa wakizungumza, Mheshimiwa aliyepita alivyozungumza, linapokuja suala zima la uwekezaji, wananchi wa Tanzania wanageuka wakimbizi katika nchi yao na kinachotokea ni kwamba Maafisa wanaohusika wanafanya kuangalia maslahi ya wawekezaji zaidi badala ya kuangalia maslahi ya wakazi wa eneo husika. Nalizungumza hili kwa sababu kuna mifano mingi imetokea au ambayo inaendelea kutokea katika kijiji cha Boko kilichokuwa Chasimba katika Wilaya Kinondoni.

Mheshimiwa Spika, kijiji hiki cha Boko kiliandikishwa kama kijiji kwa mujibu wa Sheria ya Kuandikishwa Vijiji ya mwaka 1976, kilipewa Hati ya Kijiji cha Ujamaa. Kijiji hiki kimekuwa na mgogoro kwa muda mrefu sana na Kampuni ya *Twiga Cement* na kwa takwimu na rejea ambazo zipo, kijiji hiki wakati kinaazishwa mwaka 1976 kilikuwa katika eneo halali na hali kadhalika Kiwanda hiki cha Twiga ambacho kipindi kile kilikuwa kinaitwa Kiwanda cha Saruji kilipata hati yake mwaka 1966 lakini kwa eneo ambalo ni tofauti na eneo ambalo kijiji hiki kilipo.

Mheshimiwa Spika, katika miaka ya 1990, kama ilivyo biashara, kiwanda cha Twiga ambacho kilikuwa kiwanda cha Saruji kikataka kujipanua. Sasa hapo ndipo mgogoro ulipoanza matokeo yake ni kwamba wanakijiji ambao walikuwa namba moja, namba nne na namba saba wakajikuta wanafukuzwa kwa nguvu ya Polisi na Dola katika maeneo yao ambayo ni yao kihalali.

Mheshimiwa Spika, nimezungumza hili kwa malengo ya dhati kabisa ya kumtaka Mheshimiwa Waziri wakati anajumuisha hoja zake atueleze kwa makini kabisa ni lini basi hiki kijiji kilifutiwa usajili? Kumekuwa na maelezo kwamba hawa wananchi wamepewa fidia, haya ni maelezo ambayo katika maeneo mengi ya migogoro yamekuwa yakitolewa wakati sio kweli kama ambavyo tunasikia wananchi wa Kipawa wanavyolalamika sasa hivi kwa kulipwa fidia ya uhamisho wa mwaka 1997.

Mheshimiwa Spika, japokuwa kuna maneno wanasema kwamba wamepewa fidia lakini wananchi wenyewe wanasema hawajapewa fidia. Uzuri ni kwamba wananchi hawa hawana tatizo na kuhama kama lengo ni kupanua uwekezaji lakini tatizo lao ni kwamba wanahamishwa kinguvu na kibaya kabisa unakuta aliyekuwa Waziri wa masuala mazima ya Mipango anafanya kuwasiliana na mwekezaji kwa lengo zima la kutaka kuwaondoa hawa wananchi pasipo taratibu kufuatwa.

Mheshimiwa Spika, mimi naamini Mheshimiwa Waziri kwa umakini wako, utalifuatilia suala hili kwa karibu na ikibidi uende mwenyewe kwa sababu uzoefu unaonyesha kuna upotoshaji mkubwa sana kwa Maofisa wa chini ambao unawatuma kufanya shughuli hizo.

Mheshimiwa Spika, niendelee na suala zima la migogoro ya ardhi haswa linapokuja suala zima la ufugaji. Tumekuwa tukishuhudia siku za hivi karibuni, Wilaya ya Kiteto, Kilindi, Kilosa, jinsi ambavyo wafugaji wetu wamekuwa wanafukuzwa kama mbwa katika ardhi yao ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nimepitia takwimu au taarifa ambayo inapatikana kwenye Wizara ya Uvuvi na Maendeleo ya Mifugo, taarifa hiyo inaeleza kwamba katika hekta milioni 88 za rasilimali ya ardhi nchini, hekta milioni 60 ni uwanda unaofaa kwa ajili ya mifugo na kwa mujibu wa huo utafiti katika hizo hekta milioni 60 ambao ni uwanda unaofaa kwa ajili ya mifugo unaweza kumudu mifugo milioni 20. Takwimu zetu za mifugo ambayo tunayo kwa mujibu wa taarifa za Wizara husika, tunaoa mifugo wasiozidi milioni 19. Sasa tafsri hii ya takwimu za Wizara inaonyesha wazi kwamba kumbe kwa ardhi ya Tanzania tuna uwezo kabisa wa kuweza kuhimili idadi ya mifugo tulio nayo, kwa hiyo, kinachotakiwa ni mipangilio kujua kipi kikae wapi na saa ngapi. Nashauri Mawaziri badala ya kuchukua hatua za harakaharaka za kuwafukuza Watanzania wenzetu wafugaji, watekeleze wajibu wao kikamilifu na kuweza kupembua kujua ni eneo gani linafaa na eneo gani halifai kuliko kuchukua hatua za harakaharaka.

Mheshimiwa Spika, miaka kadhaa iliyopita kulitokea machafuko kadhaa katika bonde la Ihefu kutokana na mgogoro wa ardhi. Ni masikitiko yangu kwamba *report* hii imegeuka siri lakini tarifa ambazo zipo zinaonyesha kwamba kutokana na ule utendaji wa

wale viongozi wa chini, wakiongozwa aliyekuwa Mkuu wa Wilaya, Mama Hawa Ngulume, walikuwa wanakusanya fedha kutoka kwa wafugaji, wanawatoza kama *penalt* ya kuwa na mifugo, gharama ambayo ilifikia karibia bilioni tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini mpaka sasa hivi hatujaambiwa hizo bilioni tano walizozichukua, zimepelekwa wapi na walichukua kwa misingi gani. Tunaambiwa Hawa Ngulume, aliyekuwa Mkuu wa Wilaya, peke yake, aliweza kukusanya karibia shilingi bilioni moja sasa badala ya mtu kama huyu kuwajibishwa, tunaambiwa kuwa mtu huyu amepumzishwa, sasa hivi amenyimwa Ukuu wa Wilaya na inasemekana anataka kurudi Singida kwa Mama Chilolo kuwania Ubunge.

Mheshimiwa Spika, nadhani kuna umuhimu wa kuanza kuwachulia hatua watu wote waliohusika na uovu huo na pia Serikali kuleta taarifa ya Bonde la Ihefu. Kodi za Watanzania zilitumiwa kwa hiyo, kama Bunge, kama Watanzania wana haki ya kujua nini kilichojiri mle ndani na siyo *report* tunafanya siri kwa sababu tuna *interest* zetu binafsi labda na watu ambao wamehusika katika ule mchakato mzima.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala zima la Shirika la Nyumba la Taifa. Watu wengi wamezungumza hapa asubuhi na kwa uchungu sana na kweli inasikitisha hasa ukizingatia madhumuni makubwa ya kuanzishwa kwa Shirika hili. Madhumuni makubwa yalikuwa ni kuweza kuwasaidia Watanzania wengi ambao wana uwezo mdogo wa kifedha na hawawezi kumudu gharama za kuweza kujijengea makazi yao huku nje kwa ushindani wa kisoko.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha na sijui ni lini Sera ya Shirika la nyumba imebadilika sasa hivi. Kama alivyozungumzia mchangiaji aliyepita, wanaangalia bei ya soko. Sasa unapoangalia bei ya soko kwa kusema nyumba katika bei ya soko labda ni shilingi 300,000 ama shilingi 350,000 ama shilingi 500,000 hivyo unawatoza Watanzania ambao wanaishi katika nyumba za shirika gharama hizo hizo, inakuwa imeua dhana nzima ya ujenzi wa yale majengo.

Mheshimiwa Spika, mimi nahisi huu mkakati umefanywa kwa makusudi. Kwa sababu kama alivyozungumza Mheshimiwa Mrema mwaka jana tumepitisha Sheria mbili, *Morgage Finance* na Sheria ya Vipande (umiliki wa vipande) sasa kutokana na Sheria hiyo ya umiliki wa vipande kuwepo na kutokana na Sera nzima ya Shirika letu la kuuza nyumba, inaonekana kabisa huu ni mkakati wa dhahiri wakijua wakiongeza kodi wanauhakika hawa Watanzania maskini hawatakuwa na uwezo wa kulipa hizo kodi, wataziacha nyumba na wakiziacha nyumba wanakuja wale matajiri, vigogo wenye uwezo wakulipa kodi na wao watakaa kule na matokeo yake hawa vigogo ndio watakaouziwa nyumba hizo.

Mheshimiwa Spika, nadhani hili siyo sahihi na Mheshimiwa Waziri anawajibu kabisa wa kuhakikisha kwamba Sera ambayo ilikuwepo kwa ajili ya Shirika letu la Nyumba inaendelea ili kuepusha dhana na misemo ambayo sasa hivi imekuwepo kwamba kuna ufisadi mkubwa sana katika Shirika la Nyumba. Siwezi kusema moja kwa moja kwa sababu sina uthibitisho lakini ukweli ni kwamba Waziri anatakiwa aangalie

kwa makini  na mimi niungane kabisa na mzungumzaji aliyepita kwamba kuna haja Waziri kama Waziri aunde Tume. Ushauri wangu ni kwamba asiunde Tume ambayo itamdanganya kama ile iliyomdanganya katika viwanja vya Kawe 695 na 696, aunde Tume itakavyokuwa makini ambayo itampa majibu sahihi

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninashukuru na ninaamini kwamba Mheshimiwa Waziri atatoa majibu yaliyo muafaka.

**MH. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kutimiza moja ambalo nilikuwa nimeombwa na Mheshimiwa Rais hapo majuzi tulipokutana Gairo, alinitumia kama tarishi mahsusi, mwakilishi, kuwa niwasilishe salamu kwa wapiga kura wa Jimbo la Mikumi, nachukua fursa hii kuwapa salamu za Mheshimiwa Rais wananchi wa Jimbo la Mikumi na Wilaya ya Kilosa.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kilosa tulitembelewa na viongozi wengi katika kipindi tangu uchaguzi mpaka hivi sasa. Napenda kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Makamu wa Rais Dr. Ali Mohamed Shein, kwa jinsi alivyokuja kutuhani kwenye mafuriko mwaka 2006.  Alikuja Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, Waziri kiongozi katika kuzindua Sekondari ya Kidodi. Alikuja Katibu wa CCM Taifa, Mheshimiwa Makamba kuja kuhamasisha wananchi kujenga Imani kwa Chama chetu. Mwisho Mheshimiwa Rais mwenyewe alivyozuru Jimbo la Mikumi na Wilaya ya Kilosa mwezi Novemba mwaka jana ambapo alituachia changamoto nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru kwa ahadi zote alizozitoa za fedha milioni mbili kwa kidochi Sekondari, shilingi milioni mbili, kituo cha Afya kwa kijiji cha Ruaha, gari la wagonjwa katika hospitali ya kituo cha Afya cha Tundu, usanifu wa dharura wa maji katika mji mdogo wa Mikumi, maji ya bomba kijiji cha Ulaya Kibaoni, pamoja na gari la wagonjwa na hamasa kubwa aliyotupa kulishughulikia tatizo sugu ambalo linandelea hivi sasa la wakulima na wafugaji. Alitupa moyo, tufuate moyo wa kutekeleza hayo.

Mheshimiwa Spika, baada ya saalam hizo, napenda kuingia moja kwa moja katika hoja za hotuba hii kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa Mheshimiwa Waziri wa Ardhi ameninyakulia hoja moja nilitaka kuipigania sana hapa. Lakini ni kwa sababu baada ya kusikia kilio cha wananchi ambacho niliwakilisha kuhusu umuhimu wa kupima upya mipaka ya Hifadhi ya Mikumi na vijiji vinavyopakana nayo, nimeona kwenye bajeti fedha zimetengwa maalumu kwa ajili ya kufanya kazi hiyo. Napenda sana kuipongeza Wizara hiyo kwa kuwa sikivu.

Mheshimiwa Spika, napenda nitoe hoja nyingine ambayo inawahusu wananchi walioitikia wito wa Serikali kuhama katika maeneo ya milimani ili kupisha matumizi bora ya ardhi na kuhifadhi mazingira kwenye milima ya Vidunda, wakazi zaidi ya 200 wanakaribia 300 waliitikia wito kwa hamasa iliyotolewa na Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa pamoja na Shirika la *WWF*, wananchi walikubali kuhama, walitathiminiwa mali zao na makazi na waahidiwa kupewa maeneo mbadala.

Mheshimiwa Spika, walipewa hekari 600 katika kijiji cha Mkangawalo Wilaya ya Kilombero lakini kwa bahati mbaya sana kipindi walipopewa eneo hilo kilikuwa kimekaribia sana wakati wa masika, pamoja na kwamba misaada ilifanyika ya kupatiwa mbegu na wakapanda mpunga lakini eneo lile lilikuwa si sahihi kwa sababu kila mwaka hukabiliwa na mafuriko makubwa. Hata hicho kilichopandwa kwa msaada huo, kilizolewa na maji na hata kuhatarisha maisha kwa baadhi ya waliohamishiwa katika eneo lile. Walilazimika kurudi na kuanza kutafuta mahali pengine pa kujihifadhi mpaka hivi leo, waliahidiwa eneo lingine la mbadala lakini mpaka sasa hawajapata. Tathmini iliyofanywa kusudi wapewe fidia kwa *form* zilizotoka Wizarani hazijaleta matunda yoyote kwa sababu hawajapata fidia. Kwa hali hiyo, wana njaa, hawana pa kulima na wanasubiri. Wizara inatamka nini kuhusu kuwaokoa wananchi hawa ambao kwa nia njema walihama kupisha matumizi bora ya ardhi na uhifadhi wa mazingira na mpaka leo wanatangatanga wakidai fidia ofisi hadi ofisi bila mafanikio. Naomba Mheshimiwa Waziri wakati anajumuisha atupatie kauli inayoweza kuwapa moyo wananchi hawa wanaohangaika.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu mashamba kubwa. Mkoa wa Morogoro umeteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa ghala la chakula lakini yapo mashamba makubwa mengi tu ambayo Halmashauri ilishapeleka maombi ya kufutiwa hati kwa vile yametelekezwa lakini majibu mpaka sasa hayajatoka.

Mheshimiwa Spika, katika ziara ya hivi karibuni ya Mheshimiwa Rais, wananchi wa kijiji cha Mhenda waliomba shamba lililokuwa la Mamlaka ya Pamba zamani na ambalo limetelekezwa, wagawiwe ili washiriki kikamilifu katika mpango mzima wa FAMUGATA. Mheshimiwa Rais alilichukua hilo, akielekeza Halmashauri Mkoa na Wizara ya Ardhi waangalie namna ya kulishughulikia halafu naye ataangalia kilichopendekezwa ili kuona ufumbuzi uwe nini lakini majibu hayajapatikana mpaka sasa. Namwomba Mheshimiwa Waziri afuatilie suala hili na kuona wamefikia wapi katika maombi hayo.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika, mwezi wa tano, wananchi wa kijiji cha Changarawe Kata ya Masanzi, wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu alipofanya ziara maeneo hayo pamoja na ya wafugaji walimuomba kwamba shamba la Miombo *Estate*, limilikishwe kwa wananchi kwa sababu limetelekezwa muda mrefu na hata anayesemekana analishughulikia au kulisimamia shamba hilo halitumii inavyostahili, wameng’oa miundombinu yote na wamewafanya wananchi waliokuwa wanafanya kazi miaka mingi wakodishe kulima kwa kama Nyarubanja vile shilingi 5000 kwa kila heka kwa mwaka. Mheshimiwa Waziri Mkuu alilipokea ombi hilo alipofika eneo lile na aliahidi kulifanyia kazi baada ya kuwa amewasiliana na Wizara. Nilikuwa napenda kupata majibu kuhusiana na suala hili na uamuzi au mapendekezo ambayo yametolewa.

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala linalohusu ardhi hii inayogombewa baina wakulima na wafugaji. Suala hili katika Wilaya ya Kilosa limekuwa nia la kisiasa kabisa. Sisi ambao hatuna sauti za kusema kwa jazba kama Waheshimiwa Ndugu zangu na rafiki yangu Ole Sendeka ambaye tunataniana mara chache chache, tunaonekana hatuwatetei

vya kutosha wakulima katika maeneo yetu lakini kumbe ni ustaarabu na hekima ya kuchagua maneno ya kujenga hoja katika kupata ufumbuzi wa tatizo hili ili tusije tukapanda kwenye meza hapa kwa jazba tukaanza kutupiana viatu huku na huku jambo ambalo linaweza likahatarisha na kuwagawa wananchi kule waliko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo naiomba Serikali na hasa kupitia Waziri wa Ardhi, ripoti ambayo inasemekana imekamilika ije haraka kwa majadilano na ningeshauri kabisa tusiwaache wakulima wadogo wadogo kushirikishwa katika mikutano hiyo kwa sasbabu wao ndio wanaojua mwiba unachoma wapi. Pia tusiwaache wafugaji wadogo wadogo katika mazingira yale kushiriki katika vikao hivi vinavyoonekana ni vya watu wakubwa kwa sasabu nao ndio wanaojua wapi mwiba unapowachoma. Bila sisi kusikia moja kwa moja kwa wanaohusika kule chini, tunaweza kufanya maamuzi tukifikiri ni sahihi kumbe si sahihi na yatatupeleka mahali pabaya. Naomba sana ripoti hiyo ije haraka.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Kilosa siyo siri juzi tulikuwa na Halmshauri ya CCM Mkoa, kiujumla tulipata *impression* kwamba upendwa wa Chama chetu na viongozi wake katika maeneo yale umeshuka chini kwa sababu ya tatizo hili kutokupata ufumbuzi mpaka hivi sasa. Tunahatarisha imani na ushindi wa Chama chetu katika maeneo haya. Ni lazima tupate ufumbuzi wa haraka juu ya jambo hili kusudi twende kifua mbele katika kuhakikisha kwamba suala hili linapata ufumbuzi wa kudumu ili tuweze kuendelea na mambo mengine inavyostahili. Nilikuwa naelezea kupungua kwa umaarufu wa Chama chetu.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu tunapozungumzia matatizo ya ardhi kwa wakulima na wafugaji tutambue kwamba wakulima kwa asili yao ya kulea mmea ni watu wataratibu na wapole, mmea huwezi kuulea kwa purukushani kama wanavyofanya wenzetu wafugaji kwa kupiga fimbo mifugo yao inapokwenda pembeni kula huku na huku, ndio maana ni wastaarabu na wastahimilivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa wanapochokozwa, wakulima wamelea au wamehudumia mimea yao kwa zaidi ya miezi sita, ikiwa ni tegemeo lao la chakula na shibe kwa mwaka mzima, ng’ombe anafika anakula chakula kile, inamuuma vibaya mno. Kwa hiyo, ndio maana kunakuwa na hasira kubwa sana miongoni mwa wakulima kiasi kwamba kwa kweli wana haki wakati mwingine kuchukua sheria mkononi kwa maana tu ya hasira na jazba ya kuona kwamba amewekwa katika hali ya njaa kwa mwaka mzima wakati amehudumia mimea yake. Ndio maana nasema tunaiomba Serikali, ripoti hii iliyoandaliwa itoke haraka ili tuweze kuijadili inavyostahili lakini hatma yake mwishoni tuwahusishe wakulima na wafugaji wa ngazi za chini ili kupata mawazo yao asilia ambayo yatakuwa ni ufumbuzi mkubwa katika kuleta amani baina ya wakulima na wafugaji katika nchi yetu na kuiendeleza nchi yetu kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kipekee ninaomba nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara na Mashirika yaliyo chini ya Wizara hii kwa kazi nzuri na hatimaye taarifa iliyoletwa mbele ya Bunge lako leo hii ambayo tunajadili kutokana na taarifa hiyo. Ninaomba ufafanuzi kwa machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi zinazofanywa na *National Housing Corporation*, bado kuna malalamiko yanayohusu utunzaji wa nyumba zake na upandishwaji wa kodi ulioutolewa tamko huku Bungeni leo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia nzuri ya kuziboresha nyumba za *NHC*, bado kinachofanyika ni kupaka rangi kwa nje na sio kushughulikia vifaa vya ndani kama milango, masinki, mabomba, sakafu na madirisha hata kupiga rangi ndani ya nyumba hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi kifupi cha miaka mitatu tangu *flat* za *NHC* Dodoma eneo la Mpwapwa *flats* zihamishwe, nyumba hizo zimeshapigwa rangi mara tatu kwa nje, lakini kila wapangaji wakilalamika matengenezo ya ndani hayafanyiki.

Mheshimiwa Spika, ni lini sasa Mkurugenzi Mkuu/Kaimu atasikiliza kilio cha wapangaji wa Mpwapwa *Flats*? Ni lini vyoo, mabomba ya nyumba hizo yatatengenezwa?

Mheshimiwa Spika, kupandishwa kodi mpwapwa *flats* kwa asilimia 33.3 ni kilio cha wapangaji. Mwaka 2007, nyumba hizo za Mpwapwa zilipangishwa kwa bei iliyokuwa kwenye soko nayo ilikuwa Sh. 150,000/= kwa nyumba ya vyumba vitatu vidogo bila makabati jikoni wala kwenye vyumba viwili.

Mheshimiwa Spika, bomba zimeshachakaa kila mahali na sakafu iko hoi. Nyumba hizo sasa zimetolewa taarifa kuwa kodi itapandishwa hadi kufikia Sh. 200,000/=. Hivi kweli kwa kipindi cha mwaka mmoja, *market rates* zimeshabadilika kiasi hicho! Mbona kwa kipindi hicho Serikali haijapandisha mishahara ya wafanyakazi? Hela hizo zitatoka wapi? Ninaomba wakati wa majumuisho nipatiwe majibu ili nisihangaike kuubana mshahara wa Waziri kwa kuwa nitajibiwa vyema.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri iliyosomwa mbele ya Bunge letu Tukufu pamoja na kwamba Waziri hana Naibu na ni Wizara kubwa yenye migogoro mikubwa jitihada zake zinaonekana na ameonyesha kuimudu Wizara hiyo, migogoro inapungua. Katibu Mkuu pamoja na timu yote ya Watendaji hao nawapongeza.

Mheshimiwa Spika, Wizara inaitwa `Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi.' Je, hizi nyumba na makazi ni kwa mijini tu. Mbona sioni harakati au mipango

(sehemu)za kuhamasisha wananchi walioko vijjini kujenga nyumba bora.  Nyumba bora ni kigezo kimojawapo cha kupungua kwa kiwango cha umaskini nchini.

Kama kweli Wizara inapaswa kuwasaidia watu waishio vijijini ili wawe na nyumba bora, inahitaji kuanzisha mikakati/mipango *(schemes)* mbalimbali kwa mfano vikundi vya kujengeana nyumba, kutoa ruzuku/mikopo kwa ajili ya vifaa vya viwandani mabati, saruji na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, mimi sikubaliani na dhana kwamba Tanzania ina ardhi kubwa.  Ardhi kubwa ni hifadhi za Taifa, mapori ya akiba na ardhi nyingine imemilikiwa na watu binafsi.  katika sehemu nyingine za nchi hii hakuna ardhi inayoitwa ya vijiji mkoani Kagera, ni vijiji vichache vyenye ardhi inaitwa ya vijiji.

Naishauri Serikali iwe na mpango wa kuitathmini upya na kujua kwa uhakika kuna ardhi kiasi gani inayoweza kukidhi idadi ya watu kiasi gani na kwa miaka mingapi? Je, ongezeko la watu wa kulinganisha na ardhi iliyopo vinaendana? Hapa nina maana hasa huko vijijini, mtu akiwa na ekari tano akazaa watoto wanne baada ya miaka michache itabidi awagawie nao watoto wake kila mmoja ekari moja.  Je, hao watoto nao wakizaa watoto wao watapata nini?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:**  Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi - Mheshimiwa John Z. Chiligati pamoja na Katibu Mkuu, viongozi na Watumishi Wizarani na kwenye Taasisi zake kwa hotuba nzuri na kazi nzuri kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kupitia *RCC* ya Mkoa wa Tanga, Wilaya ya Mkinga ilifikisha Wizarani mapendekezo kuhusu kufuatia hati ardhi kubwa ambayo imegawiwa kwa Taasisi kama vile JKT na *Mwele Seed Farm* na mashamba mengine makubwa ambayo yana hadhi maeneo makubwa bila kuyatumia kwa muda mrefu. Kutokana na mwito wa kilimo kwanza ama Taasisi hizo na wamiliki wa mashamba hayo makubwa watakiwe kuyaendeleza au ardhi hiyo igawiwe kwa wananchi wanaohitaji ardhi hiyo kwa maendeleo ya kilimo na makazi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ahadi nyingi za Wizara hii, ugawaji viwanja na utoaji wa hati za ardhi bado una mlolongo mrefu na kero kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mipango miji, ni muhimu maeneo yanayotengwa kwa ajili ya viwanda, yawekwe katika maeneo mahususi na ambayo yatakuwa na miundombinu yote muhimu zikiwemo barabara, maji, umeme na simu.

Mheshimiwa Spika, Makao Makuu ya Wilaya mpya ya Mkinga yana ramani nzuri na hatimaye mji wa Kasera utakuwa miongoni mwa miji mizuri hapa nchini endapo ramani hiyo itatekelezwa ipasavyo.  Pamoja na kuhamasisha wananchi na wawekezaji

binafsi kujenga nyumba za kisasa hapo Kasera ningependa kuchukua fursa hii kurudia ombi letu kwa Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC)* kujenga nyumba Kasera.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DK. CHARLES MLINGWA:** Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu, Watendaji wote wa Wizara, Taasisi na Mashirika ndani ya Wizara kwa kazi muhimu zinazofanyika zenye lengo la kuboresha matumizi ya ardhi ikiwemo makazi na mengine mengi.

Shukrani kwa ujenzi wa jengo la biashara, ghorofa tano katika Mtaa wa Balewa – Shinyanga mjini. Ahsante sana. Naomba Shirika la Nyumba la Taifa liendelee kujenga majengo ya kisasa ya makazi na biashara katika viwanja vyake vilivyopo mji wa Shinyanga, bado kuna viwanja vingi pale vinahitaji kuendelezwa.

Mheshimiwa Spika, sote tunafahamu lengo la kuwa na Shirika la Nyumba la Taifa, pamoja na mambo mengine, ni kuwapatia makazi bora Watanzania wengi hususan mijini kwa tozo nafuu. Hili linafanyika hadi leo.

Lakini ni vyema ieleweke kuwa unafuu wa asilimia 40 chini ya tozo za nyumba za watu wengine sio utaratibu endelevu. Shirika haliwezi kupata uwezo wa kusimamia kazi zake ikiwa ni pamoja na uwezo wa kuhudumia nyumba zake.

Mheshimiwa Spika, wapangaji katika nyumba hizo za makazi wanaonekana kuwa ni wateule wachache miongoni mwa wananchi wengi wanalipia pango kwa viwango vya soko. Watu wachache wanaweza kutumia mwanya huo kuwapangisha watu wengine *(sub – letting).*

Shirika litaendelea kulaumiwa kwa matatizo yatokanayo na tozo hizi za chini sana. Hali hii inawafanya wenye pesa wakimbilie nyumba hizi kwa gharama yoyote na kung’ang’ania kwa kurithishana.

Hivyo, nashauri Waziri azidi kulisaidia Shirika kuwa tozo za pango kwa makazi kwani ziko chini sana na vinasababisha matatizo mengi hata yasiyostahili kwa Shirika. Unafuu wa asilimia tano chini ya tozo za soko ungetosha na kuepusha lawama kwa Shirika. Pia Shirika lingeongeza uwezo wa kujenga nyumba kwa huduma ya makazi ya watu wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, nashauri Shirika liwekeze pekee, bila ubia, katika ujenzi wa majengo ya biashara. Hii inawezekana kwa sababu ya Uwepo wa Sheria ya *mortgage*, Shirika kuwa na miliki ya viwanja na Shirika kuongeza tozo katika nyumba za makazi kwa viwango stahili ili kupata fedha nyingi zaidi kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji huo utalifanya Shirika kuwa moja ya mashirika makuu ya kuimarisha uchumi nchini kwani majengo mazuri na makubwa ni rasilimali imara ya uchumi katika kutoa ajira, mapato ya watu na kwa Serikali. Ahsante.

**MHE. OMARI S. KWAANGW':** Mheshimiwa Spika, hoja ya kwanza nitakayozungumzia ni kuhusu utoaji wa haki katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania – kifungu 107 (a) (1) (2) (a) – (e) chini ya Katiba ya Tanzania.

Kifungu 2 (b) kinasema: "Kutocheleweshа haki bila sababu za msingi.'' Mheshimiwa Rais wa awamu ya tatu, alifuta hatimiliki ya shamba la *Babati Sisal Estate 1999* na kuelekeza shamba hilo wapewe wananchi.

Wananchi walitakiwa kulipa Shilingi milioni 48 ambazo hadi sasa zipo mikononi mwa Wizara yako. Mmiliki wa *Babati Sisal Estate* alizikataa na kwenda Mahakamani. Kwa taarifa nilizonazo, wananchi walishinda kesi mwaka jana baada ya Mdhamini wa Serikali kuridhika kuwa hiyo ndiyo fidia halali.

Bado mmiliki amekata rufaa japo sina uhakika. Huu ni mwaka wa 10 tangu shamba hili lifutwe na fedha za wananchi kwa muda mrefu zipo mikononi mwa Serikali. Bila shaka Waziri utakubaliana na mimi kuwa hii sasa na kwa vigezo vyovyote ni haki iliyocheleweshwa na kibaya zaidi, wale waliotoa fidia fedha zao haziwasaidii na wanazidi kuwa maskini na wanasononeka sana. Naomba Wizara ione namna ya kufikisha ujumbe huu kwa wahusika bila kuingilia uhuru wa Mahakama, Jaji Mkuu ajue jinsi watu hao wanavyosononeka.

Halmashauri ya Babati inalipa fidia ya eka moja tupu kwa Sh. 350,000/= hadi Sh. 360,000/= katika ekari moja, Halmashauri inapima viwanja nane na kimoja anaweza kupewa mwenye eneo hilo. Halmashauri inapima na kuuza au kugawa kiwanja kwa bei ya kati ya Shilingi milioni moja mpaka tano kutegemea eneo. Fidia kwa mwenye eneo ni ndogo mno na bado hatujui itakwenda wapi au ataishi vipi kwa Sh. 350,000/=.

Tatizo la fidia bado linahitaji kuangaliwa zaidi na kwa makini. Vinginevyo tunazidi kuongeza umaskini, tunaondoa amani na upendo, tunajenga chuki miongoni mwa jamaii na wananchi na Serikali yao. Naomba kufahamu ni nani anapanga fidia zinazotolewa na Halmashauri mji, ni Wizara au ni Halmashauri Mji yenyewe ndiyo inapanga thamani ya ardhi? Jibu hili ni muhimu sana kwani wapo wanaopewa maelekezo na maamuzi ya Wizara. Naomba ufafanuzi wa kina.

Mheshimiwa Spika, hoja ya tatu ni kwamba, Serikali iliunda timu ya kusikiliza kero za ardhi kwa kila Wilaya: Je, ni malalamiko mangapi yalipokelewa katika Wilaya ya Babati, mangapi yalipata ufumbuzi na waliohusika wamepewa adhabu zipi? Naomba jibu kwa maandishi na pia naomba kupewa ripoti nzima ili wananchi wa Babati wajue ukweli wa kero zao.

Mheshimiwa Spika, hoja ya nne: Je, mwongozo wa kuweka *Master Plan* ukoje? Naomba Wabunge tuupate kwa sababu sasa kumezuka tamaa ya Maafisa Ardhi kutaka kugawa *plots* kila eneo bila kujali Ukanda wa Kijani, maeneo yenye rutuba sana na yanayofaa kwa kilimo cha mijini, mfano siku maghorofa tunayaona Osterbay, Msasani,

karibu na Ikulu, haya maeneo katika *Master Plan* ya Dar es Salaam bila shaka hakukuwa na ujenzi wa maghorofa. Tatizo hili sasa linasambaa Mikoani na Wilayani kwetu.

Mheshimiwa Spika, hoja ya tano ni kwamba mpango wa mikopo kwa watu kujenga nyumba unakwamishwa sana na Mkurabita. Hatuna maelezo mazuri pamoja na ahadi ya nguvu kwenye ilani ya 2005 – 2010.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na ufafanuzi.

**MHE. SIGFRID SELEMANI NG'ITU:** Nashukuru Mheshimiwa Waziri kwa jitihada zako. Lakini kule Rwanga hakuna wapimaji wa kutosha na pia zana za kupimia hawana na usafiri hawana. Je, utanisaidia vipi? Wilaya yetu ni mpya na tunahitaji ikamilike kiupimaji.

Suala la Watumishi pungufu katika Halmashauri ya Rungwa kama ilivyo Halmashauri zote nchini linafanyiwa kazi na Wizara ikishirikiana na Watumishi na TAMISEMI. Wizara haina uwezo wa kununua vitendea kazi pamoja na usafiri. Hili ni jukumu la Halmashauri yenyewe.

**MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri ambaye ni mahiri kabisa, Katibu Mkuu, Wakurugenzi, Wataalam na Watendaji wao wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ina kazi kubwa kabisa ya kuhakikisha Watanzania kuwa na makazi bora na ya kisasa katika nchi hii, kwa kuzingatia hayo Wizara hii ni lazima iwe na mipango madhubuti ya kuboresha makazi yaliyo kwenye ramani zilizoandaliwa na kuondokana na bomoa bomoa zisizo na mipango kwani hiyo hutokana na kutokuwa na mipango thabiti na ufuatiliaji bora katika Miji yetu.

Mheshimiwa Spika, *NHC* ni Shirika la Serikali kati ya Mashirika machache hapa nchini yanayojikongoja katika kufanikisha shughuli zao. Kwa kuzingatia hilo, ni dhahiri shirika hili liendeleze ujenzi wa nyumba za kisasa na kuziuza kwa wananchi hasa wale wenye kipato cha chini ndani ya nchi hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo machache, naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HALIMA OMAR KIMBAU:** Mheshimiwa Spika, kwanza nachukua fursa hii kuwapongeza Wabunge wapya wote wawili. Pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake yenye matumaini kwa Wizara hii. Ninayo machache ya kuchangia juu ya ukusanyaji wa kodi za ardhi. Napongeza Wizara kwa mtindo wao mpya wa kuwakumbusha wateja kujua wanadaiwa nini. Hii ni hatua, lakini: Je, hakuna njia ya kufanya wateja walipe kodi zao kwa njia nyepesi. Mfano mzuri wa

Idara ya Maji sasa hata umeme imebainiwa njia ya kulipia ukiwa popote pale. Inawezekana, jaribuni.

Mheshimiwa Spika, juu ya *National Housing* kwa wapangaji ambao ni waajiriwa, hakuna mfumo wa kutozwa kodi kutokana na mishahara yao? Hata kwa mashirika au kampuni pia hebu jaribuni kutumia njia ya kuwatoza kutokana na mapato yao.

Mwisho, juu ya *National Housing* bado sioni ni jinsi gani wananchi wengi watakavyonufaika na nyumba hizi. Zamani ilikuwa hakuna mikataba, sasa ipo mikataba. Bado haitoshi kwani, iwe na kikomo. Mpangaji kuwa mpangaji wa mikataba ya miaka isiyo na kikomo, hebu kuwe angalau na upangaji wa kikomo kama miaka mitano. Hii itasaidia na wengine kufaidika na nyumba hizi. Hasa vijana wetu wanaoanza maisha ambao wanakodi vyumba mitaani kwa bei kubwa mno. Kama chumba Sh. 20/= mpaka Sh. 50/=. Hiki ni chumba sio nyumba.

Mwisho kabisa, juu ya maeneo ambayo yako wazi naomba sana yawe ya wazi kweli na kwa matumizi yaliyodhamiriwa.

Mheshimiwa Spika, naona kwa leo yatosha. Ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, napenda kusema naunga mkono hoja.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Uongozi wake kwa kazi nzuri wanayoifanya kuboresha utendaji wa Wizara na matunda ya juhudi zao zinaonekana.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Ardhi pamoja na Katibu Mkuu wameondoa kero nyingi sana zilizokuwepo katika Wizara hiyo na hivyo sura ya Serikali mbele ya wananchi kuboresha na hata kuweza kupata tuzo ambayo inatolewa na Umoja wa Mawaziri wa Utumishi Barani Afrika kwa Taasisi zilizofanya ubunifu katika kuongeza ufanisi wa Taasisi na kuwaondolea kero wananchi wanaopelekea huduma toka Taasisi husika.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri na Uongozi wake kufuatilia shamba la mkonge la Kabisera *(Mikindani sisal estate)* lililopo Mtwara, kwani tangu libinafsishwe shamba hilo halijaendelezwa hata kidogo matokeo yake yamekuwa ni mazalia ya nyoka ambao wanaendelea kuhatarisha maisha ya wananchi kutokana na nyoka hao kumaliza panya wote ndani ya shamba hilo na sasa kutoka nje ya shamba hilo kutafuta chakula. Hali ni mbaya sana katika maeneo hayo, kuanzia Januari hadi Juni 30, 2009 jumla ya watu 15 wameuliwa na nyoka. Halmashauri imeshatoa mapendekezo ya kuomba shamba hilo linyang'anywe toka kwa mwekezaji ambaye tangu apewe ameliacha bila kuliendeleza.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nasisitiza pongezi zangu kwa Wizara kwa kupata tuzo ambayo ni heshima kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MTUTURA ABDALLAH MTUTURA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimshauri Mheshimiwa Waziri wa Ardhi juu ya Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 na kanuni zake.

Mheshimiwa Spika, kwa kiwango kikubwa, watendaji wa Wizara na Wathamini wa Serikali hawazifuati kanuni za ardhi hasa kipengele cha *FIDA*. Naomba sana wahusika wazifuate sheria na kwa kufanya hivyo, wataweza kupunguza malalamiko mengi hapa nchini. Ahsante sana.

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kumshukuru Mungu kwa kunijalia nafasi hii nami niweze kuchangia hotuba iliyopo mbele yetu. Nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri, Naibu Waziri pamoja na wataalam wote kwa hotuba yao nzuri.

Mheshimiwa Spika, naomba naianze na suala la *National Hosing.* Nyumba hizi zilijengwa kwa ajili ya watu wasio na kipato hasa wafanyakazi ili waweze nao kuishi katika nyumba nzuri na zenye hadhi, watoto wao waweze kukua na kusoma wakiwa hapo hapo.

Mheshimiwa Spika, inapofikia kwamba yule mtu amestaafu hana kazi na watoto wao wamekwishaondoka na kwenda kutafuta makazi, mengine ikiwa yule amekwishakuwa mzee na hana kazi. Je, atapata wapi uwezo wa kuweza kulipa kodi ya nyumba Sh. 250,000/= kwa mwezi? Hivi mtu huyo atapata wapi Sh. 150,000/= kila mwezi na yeye amestaafu? Naomba Serikali ione uwezekano wa kupunguza kodi ili wazee wale waweze kulipa.

Mheshimiwa Spika, Fremu za Maduka. Ikiwa Fremu ya duka ni Sh. 420,000/= hivi hizi zimejengwa kwa ajili ya Watanzania au ni kwa ajili ya Wachina? Serikali ipunguze kodi hizi ili watu wa kawaida wamudu.

Mheshimiwa Spika, kuna matatizo makubwa ya viwanja. Wafanyakazi wa Manisapaa wamekuwa wakitoa hati kwa watu zaidi ya wawili. Je, inakuwaje wafanyakazi hawa wanatoa *offer* zaidi ya moja? Je, huku sio kuchochea vurugu kwa wananchi?

Mheshimiwa Spika, hivi mnataka kuona watu wakiuana?

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Arusha kumekuwa na malalamiko makubwa sana ya ardhi hasa Njiro. Kiwanja kimoja kina zaidi ya watu watatu, wawili.

- Je, Serikali inasemaje kuhusu tatizo hilo? Watumishi hawa wamefanya Viwanja kuwa miradi yao?

- Je, Serikali haioni kwamba kuendelea kuwalea Watumishi wabovu wanaouza viwanja vya Serikali ni kuwaumiza wananchi?

- Kwa nini Serikali inawafumbia jicho Watumishi hawa wabovu hasa katika Mkoa wa Arusha? Ni vyema Serikali ikaangalia watendaji wabovu na kuwaondoa badala ya kuwapa uhamisho kwa sababu hata huko wanakohamishiwa tatizo ni hilo hilo.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iwaondoe. Ahsante. Naunga mkono hoja.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA**: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu, kutujalia kuwa wazima na salama. Baada ya shukurani hizo, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii kwa namna anavyotekeleza majukumu yake kwa uaminifu kabisa.

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia bajeti hii, mimi napenda kumuarifu Mheshimiwa Waziri kuwa viwanja vya kujenga nyumba za makazi vimekuwa ghali sana kiasi kwamba mtu wa kawaida inakuwa vigumu kununua haswa vile vinavyopimwa na kuuzwa na Serikali haswa vile vinavyouzwa katika Jiji la Dar es Salaam na hapo Dodoma, hivyo ninaiomba Serikali iliangalie upya suala hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upimaji wa ardhi: Je kuna tofauti gani kuhusu upimaji wa MKURABITA na ule unaofanywa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi?

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka huu wa fedha Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kujengea nyumba za kukodisha na za kuuza: Je, kazi hii itafanyika kwa Mikoa yote au kwa baadhi tu ya Mikoa ambayo haimo katika mpango huu na maelezo ni kwanini haikutengewa fedha?

**MHE. MCH. LUCKSON MWANJALE:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba kuunga mkono hoja hii.

Pamoja na kuunga mkono hoja hii, naomba nichangie kidogo katika eneo la upimaji wa viwanja.

Mheshimiwa Spika, gharama za upimaji wa viwanja ni kubwa mno, kiasi cha kumfanya mwananchi wa kawaida, kutoweza kumudu kupimiwa maeneo yale.

Mheshimiwa Spika, hata wananchi ambao wamefanikiwa kupimiwa maeneo yao, lakini bado kunakuwepo na ucheleweshaji wa utoaji wa hati *(lease)*. Je, Serikali haiwezi

kurekebisha hali hiyo ikiwa ni pamoja na kuziangalia upya gharama za upimaji ili ziweze kuwafaidia wananchi wengi?

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu la Mbeya Vijijini, kuna wananchi ambao maeneo yao yamechukuliwa hususan katika eneo la Songwe, mkabala na uwanja wa ndege, tangu 2007 hadi leo hakuna malipo yoyote yaliyofanywa. Je, ni lini Serikali itawalipa fidia zao hawa wananchi? Wananchi wanaoishi katika eneo lile, hawajui lini watapata haki zao ili waondoke kwenda sehemu nyingine na kujiendeleza.

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Waziri, pamoja na Wasaidizi wake, kwa kazi nzuri na mipango mizuri waliyojiwekea kwa ajili ya kuboresha huduma zao.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Spika, sambamba na Hotuba ya Waziri wa Ardhi na Maendeleo Mijini, naomba kupatiwa ufafanuzi juu ya masuala yafuatayo:-

Kwa kuwa baadhi ya Miji Midogo na Center nyingi hapa nchini zinakua kwa kasi sana; na kwa kuwa Mji Mdogo wa Lamadi uliopo Wilaya ya Magu umekua kwa kasi sana; na kwamba bado haujapimwa ili kupangiliwa kwa kuweka mfumo wa miundombinu kwa barabara, soko, stendi ya mabasi na kadhalika.

Serikali ina mpango gani wa kuupima Mji huu wa Lamadi ili kuliepusha Taifa na hasara inayoweza kujitokeza kutokana na Mji kukosa mpangilio na kusababisha hasara ya fidia kubwa?

Mheshimiwa Spika, hali ya mpango mji katika Jiji la Mwanza inatisha kwa vile kuna wananchi wamejenga katika maeneo ambayo hayakupimwa na vilimani; hivyo kupelekea ugumu wa kuwaondosha wananchi hawa pasipo kukiuka haki za msingi za binadamu pamoja na kulipa fedha kubwa. Je, Serikali kupitia bajeti hii imeweka mkakati gani kuhakikisha kuwa suala hili linashughulikiwa kwa Wananchi wa Lamadi na Jijini Mwanza sehemu hizi zinapimwa haraka?

Mheshimiwa Spika, nitaunga mkono haja hii baada ya kupata majibu kwa hoja hizi. Ahsante.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Shirika la Nyumba (NHC), lazima lifanyiwe *Due-deligence*, Muundo wake na Sera ya Taifa upitiwe upya, kunusuru wanyonge wa nchi hii.

Kuwe na viwanja kwa bei ndogo (kupimwa) ili watu wengi wa kipato cha chini waweze kumiliki.

NHC ianze kuuza Nyumba ipate mtaji wa kujenga nyingine bila ubaguzi wala tabaka, hasa maeneo ya mjini.

Nyumba zote za msajili zikabidhiwe Halmashauri za Mji. Huu ni utaratibu unaofanywa na nchi nyingi zikiitwa *Council Houses.*

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mara nyingi nimeomba Wizara hii isaidie na kusimamia maandalizi ya matumizi bora ya ardhi (Land Use Plan) ya Wilaya ya Ludewa, badala ya eneo linalozunguka Mgodi wa Mchuchuma na Liganga tu.

Naomba kwamba, endapo Wizara haiwezi kufanya kazi hii, basi itutafutie fedha nasi tutafanya kazi hiyo wenyewe.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu kazi hii ifanywe ili kuepuka fujo na ugomvi, vinavyoweza kutokea Ludewa kama inavyotokea hivi sasa maeneo ya migodi iliyoko Kaskazini mwa Nchi. Ludewa inatarajiwa katika muda mfupi ujao, itakuwa na uchimbaji mkubwa wa madini na ujenzi mkubwa wa viwanda. Wilaya hii ina watu wapatao 140,000 tu na itavamiwa na watu wengi kutoka nje ya Ludewa.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii, nami kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi.

Mchango wangu hasa nitauelekeza kwenye matatizo, ambayo wananchi wamekuwa wakiyapata pale wanapopisha ujenzi wa barabara.

Mheshimiwa Spika, imekuwa ni kawaida kwa wadhamini wa majengo ya wananchi, wamekuwa wanawadhulumu wananchi pale wanapofanya tathmini ya nyumba za wananchi. Kuna malalamiko kwamba, kuna baadhi ya wananchi, nyumba zao zinathaminiwa kwa bei ndogo mno, ambayo hailingani na thamani ya nyumba yenyewe. Kuna nyumba za matofali ambazo zimeunganishwa maji na umeme, lakini bei zake zinawekwa za chini ukilinganisha na nyumba za tope zilizoezekwa bati, lakini hazina maji wala umeme.

Mheshimiwa Spika, zoezi zima la kutathmini nyumba za wananchi linagubikwa na upendeleo, undugu na harufu ya rushwa. Nitoe mifano hii hasa pale palipofanyika tathmini ya nyumba za wananchi kupisha ujenzi wa Barabara ya Mwandiga – Manyovu. Ninaishauri Serikali kuchukua hatua za dharura, kupitia upya tathmini iliyofanywa na kupitia malalamiko ya wananchi ili haki itendeke na wananchi walipwe haki zao.

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya wananchi kule Kiseke, Ilemela, Mkoani Mwanza na baadhi ya Kata nyingine, mashamba ya wananchi yanapimwa na kukatwa viwanja kwa ajili ya makazi. Jambo la kushangaza ni pale unapoona mwananchi shamba lake linapimwa na kukatwa viwanja labda vitano na mwananchi huyu hupewa kiwanja kimoja tu, hata kama ana watoto ambao wanayo haki ya kuishi pale hawafikiriwi kupewa sehemu ya viwanja hivyo. Aidha, mwananchi huyu hutakiwa kiwanja hicho kukilipia Sh. 400,000, jambo hili ni uonevu mkubwa.

Mimi ninaishauri Serikali, wananchi ambao mashamba yao yanakatwa, basi na warithi au watoto wa mwananchi huyo wapewe fursa ya kupatiwa sehemu ya viwanja hivyo ili nao wajijengee nyumba zao za kudumu.

Mheshimiwa Spika, imekuwa ni kawaida kwa madai ya wananchi ya kulipwa fidia ya majengo yao au viwanja vyao, ambavyo tayari vimetathminiwa, inachukuwa muda mrefu sana kulipwa kinyume na sheria inavyoagiza. Tatizo hili ni kubwa na linasababisha manung'uniko na usumbufu mkubwa kwa wananchi.

Aidha, tathmini za majengo ya wananchi huandikwa kwa Lugha ya Kiingereza, ilhali tunajua wazi kwamba, wananchi wengi huko vijijini hawaielewi lugha hiyo. Kwa kufanya hivyo, ndipo pale Maofisa wanaohusika, hutumia mwanya huo kuwaibia wananchi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Serikali kuhakikisha kwamba, madai ya wananchi yanalipwa kwa wakati na yakiwa sahihi. Kadhalika, maandiko yoyote ya tahmini ya majengo ya wananchi, mashamba na mengineyo, yafanywe kwa Lugha ya Kiswahili, ambacho wananchi wengi wa vijijini wanaielewa.

Pale inapokuwa mwananchi haielewi Lugha ya Kiswahili ipasavyo, basi ni vyema wakaelezwa kwa namna yoyote ile, ilimradi mwananchi aifahamu haki yake.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Napenda kuchangia Wizara hii muhimu.

Nitaanza na majengo yaliyoko mikoa yetu; yote yanatia aibu, yanaonekana machafu. Nitapenda kujua watu wanaoishi kwenye nyumba hizo wanalipa kodi au wanakaa bure? Kama wanalipa kodi kwa nini yasifanyiwe ukarabati au kama hawalipi kodi kwa nini wasifukuzwe wakawapa wanaolipa kodi au waliokaa humo wasiyanunue, yakajengwa majengo ya kisasa? Majengo mengine yatawaangukia watu, hasa Kariakoo, yale maghorofa yameoza tena katikati ya mji, ambao tuna wageni wa kila aina. Leo Jiji lenye hadhi ya kuitwa Jiji na huku chafu, majengo machafu, mitaa michafu na mitalo michafu.

Nakwenda kwenye Wizara hii; wagawaji viwanja mkoani; wanaitia Serikali hasara. Wanagawa viwanja ovyo, baada ya muda yanaanza malalamiko, Serikali wanawatoa eti ni sehemu ya vyanzo vya maji. Pamoja na kuwa viwanja hivyo walipewa na Ofisi ya Ardhi na wamekwishajenga, wengine wamepanda mazao yao, Serikali inaanza kulipa inakuwa migogoro mikubwa kati ya ofisi na yule anayeondolewa. Suala hili lisipodhibitiwa, litaleta shida kwa wananchi kama wakulima na wafugaji. Sasa naomba tusifike mbali, ziba ufa tujenge ukuta. Ofisi inawatangazia wananchi kugawa viwanja, wanatoa pesa wanawazungusha mpaka wanakata tamaa.

Sisi kama Wabunge, tuna malalamiko mengi sana kuhusu suala hilo Bukoba Mjini (Kyambitembe). Muwekezaji amechukua ardhi ya Wananchi wa Kijiji cha Kanshundo, kiwanda pamoja na mashamba ya chai. Ardhi yote imechukuliwa, hawana

hata sehemu ya kiwanja cha watoto kuchezea mpira. Amechukua mpaka njia ya kutokezea kwenda barabara kubwa amewazuia.

Hivi Mikoa na Wilaya hawana Sheria ya Ardhi na iwe inatolewa elimu kwa wananchi wajue Sheria ya Ardhi, wasiwe wananyanyasika na kudhulumiwa na wenye pesa. Wakijua Sheria ya Ardhi ni vyema.

Nitapenda kujua, mtu akiwa amezaliwa sehemu ambayo baba zake na mababu zake wamezaliwa hapo hapo, kwa mfano, kama sisi Wahaya wazazi wetu milele na milele ardhi yetu na makazi yanakuwa ni yale yale. Ndio ardhi yetu tunazaliana hapo hapo, lakini leo hii wanaletwa watu wanawanyang'anya ardhi yao, wanawaibia, wanawaambia waondoke sehemu ni ya mwekezaji. Watu hawa hawapewi ardhi nyingine. Je, Wizara inategemea watu hawa waende wapi?

Kwa masikitiko makubwa, wazee wengine hawana uwezo. Kwa nini wasitafutiwe sehemu mapema kuliko kuleta tatizo juu ya tatizo? Je, tunakwenda wapi? Upimaji wa viwanja uharakishwe ili watu wasiwe wananyang'anywa ardhi, pamoja na mashamba yao, hasa wasio na uwezo; kwa mfano, Wananchi wa Bubale na Kakunyu Misenyi. Ardhi yao ingekuwa imepimwa, migogoro iliyopo isingekuwepo, pamoja na kuoneka huyo mtu ni mvamizi.

Mheshimiwa Spika, naomba suala hili lifanyiwe kazi kupunguza kero.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, ni dhahiri tangu tupate uhuru idadi ya watu imeongezeka sana na miji yetu kupanuka kwa kasi, lakini inasikitisha sana kuona jambo hili halikuzingatiwa na Serikali na kupelekea kuwepo na ujenzi holela katika miji yetu mingi. Napongeza jitihada zinazochukuliwa sasa za kupima viwanja katika miji yetu na hasa miji ambayo kwa sasa inakua, Mpanda ikiwa ni moja ya miji inayokua na ambayo ina makazi holela kidogo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada hizo za kupima viwanja, zoezi ambalo lina gharama kubwa na wataalamu, kuzingatia mahitaji na kutenga maeneo ya huduma kama Shule, Zahanati, Nyumba za Ibada na Makaburi.

Baada ya ramani husika kupitishwa na kuridhiwa na mamlaka zinazohusika na viwanja kuanza kutolewa kwa mujibu wa ramani na Wananchi kulipa ada zinazohitajika na kupewa milki ya viwanja husika; je, Sheria inampa Mamlaka Mkuu wa Wilaya kufuta matumizi ya viwanja vilivyopimwa kuwa makazi na kubadili matumizi kwa maslahi yoyote yale? Waathirika hawa wanapaswa kulipwa fidia na mamlaka gani waliotoa hati (Halmashauri) au aliyefuta (Mkuu wa Wilaya kwa maana Serikali Kuu)? Naomba nipate maelezo ya kina ili kuondoa usumbufu wanaopata wananchi waliopewa viwanja eneo la Kazima Mpanda Mjini.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyotangulia kusema, Mji wa Mpanda unakua kwa kasi pia mahitaji ya makazi yameongezeka; je, Serikali ipo tayari sasa kulishawishi Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kuwekeza kwa kujenga nyumba za kupangisha au kuuza katika Mji wa Mpanda, tunayo maeneo mazuri na yaliyopimwa tayari?

Mheshimiwa Spika, mwisho, nizungumzie mgogoro wa ardhi kati ya wananchi na mmiliki wa ardhi inayofahamika Shamba la Benki katika Kijiji cha Kakese, Tarafa ya Kubungu Mpanda. Mgogoro huo tumeufikisha katika mamlaka kadhaa, lakini haujapatikana ufumbuzi, pamoja na wananchi na Serikali ya Kijiji hicho kuomba hati miliki ya shamba hilo ifutwe ili wananchi wanaotumia ardhi hiyo hivi sasa, waweze kuendeleza kazi zao za kilimo bila hofu na bugudha ya kudaiwa na kufukuzwa. Hadi sasa Serikali inasuasua kutoa maamuzi ya kufuta hati hiyo; tatizo ni nini?

Mheshimiwa Spika, Serikali kuchelewa kutoa maamuzi ya haraka katika mambo mengi tu yanayogusa maisha na ustawi wa wananchi, inapelekea kuwepo manung’uniko kwa Serikali yao, migogoro na hatimaye machafuko, tatizo ni uamuzi; naomba kupata maelezo na hasa kupata uamuzi wa Serikali, inafuta hati hiyo au haifuti ili wananchi wanaotegemea ardhi hiyo wajue hatma ya maisha yao.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

**MHE. DKT. CYRIL A. CHAMI:** Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa kazi nzuri sana anayofanya. Nawapongeza sana Watendaji wote kwa kazi nzuri sana.

Naomba Wizara hii muhimu sana iuangalie mgogoro unaofukuta kati ya Manispaa ya Moshi na Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, juu ya matumizi ya ardhi ya eneo la Moshi Vijijini, kwa upanuzi wa Mji wa Moshi. Tatizo ni kubwa na nitaleta maandishi yanayojaribu kuelezea kiini cha tatizo na mapendekezo ili kwa pamoja tulipatie tatizo ufumbuzi hili.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA:** Kwanza, nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalamu wote wa Wizara, kwa maandalizi ya hotuba nzuri.

Kupima mashamba na kutoa hati milki za kimila – kurasimisha ardhi vijijini. Katika juhudi za kuendeleza kilimo cha umwagiliaji maji mashambani, ni muhimu kuendeleza wakulima wadogo, wakulima wa kati na wakubwa. Lengo ni kubadilisha kilimo kitoke kwenye aina ya kujikimu *(subsistence farming),* kiwe kilimo cha kibiashara.

Nashauri mambo yafuatayo yatiliwe mkazo:-

(i) Kasi ya upimaji wa mashamba na utoaji wa hakimilki za kimila iongezwe.

(ii) Mabenki yashawishiwe (hasa NMB yenye mtandao mkubwa) kukubali kutoa mikopo kwa wakulima wadogo kwa kuzitambua hakimilki za kimila.

(iii) Mimi naamini wananchi wa kawaida hawaelewi dhana ya Mkurabita. Iko haja kutoa elimu na hamasa (kwa vitendo/mifano hai) ya walionufaika na mpango huo kwa kutumia rasilimali kuu waliyonayo (Ardhi).

(iv) Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi iangalie uwezekano wa kushirikiana na Wizara ya Maji na Umwagiliaji ili kutumia vizuri fursa iliyopo *(Take Advantage)* ya mashamba ya umwagiliaji, ambayo kitaalam yanapimwa kwanza *(Topographical Survey).* Suala hili/ushirikiano huu, unaweza kupunguza gharama za upimaji, kwa sababu Wizara zote mbili zinavyo vifaa na wataalamu *(Surveyors)* wa kupima ardhi.

(v) Suala la Benki ya Ardhi *(Land Bank)* lipewe msukumo. Ardhi iliyopo Wilayani ijulikane kwa wanaotaka kuwekeza.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Kwanza ni pongezi nzuri kwake Mheshimiwa Waziri, kwa namna anavyofanya kazi yake vyema. Ofisi yake iko wazi na huduma zinaridhisha sana. Nampongeza pia Katibu Mkuu na Viongozi wote katika Wizara hii.

Mwaka 2006 nilipochangia hoja, nilizungumzia majukumu ya NHC kujenga nyumba katika Wilaya pia na si katika Miji Mikuu tu. Ni kweli wito huo umeitikiwa katika Wilaya kama za Cheto na Tarafa ya Chilinge pia.

Naomba sasa Wilaya ya Mbinga (Mjini) pia ifikiriwe angalau *blocks* mbili za ghorofa tatu ili kupunguza matatizo ya malazi.

MKURABITA ni utaratibu mzuri sana lakini kesi ni ndogo. Sioni kama MKURABITA wamepewa ushirikiano wa kutosha hata katika Halmashauri zetu. Pengine Wizara ya Ardhi na TAMISEMI zishirikiane ili rasilimali fedha za MKURABITA na Halmashauri, ziweze kutumika kwa pamoja. Faida ni kwamba, Wananchi wa Wilaya hizo kama watakopesheka, wataweza kulima na kufanya biashara zaidi, hivyo vyanzo vya mapato katika Halmashauri vitaongezeka.

Dhana ya Satelite Town ni utaratibu mzuri. Ni vyema mikoa ikahamasishwa kuanza pia. Tatizo mipango yetu haifahamiki. Hatuna mbinu za kutangaza, zipo juhudi za kutengeneza kupitia magazeti. Mbinu hii haitoshi, tuanzishe vituo vya maelezo katika Mikoa na Kata na maeneo yenye mikusanyiko ya watu kama Old Post/New Office, Kariakoo na kadhalika ili kuelimisha wananchi kuondoa malalamiko lakini pia kuwapata wazawa.

Pamoja na hotuba hii nzuri na mipango mizuri katika Wilaya mbalimbali, Wilaya ya Mbinga haionekani kufahamika. Naomba, kwa kuwa kwa muda mrefu Wilaya hii imeshauliwa sana, sasa iingizwe pia katika programu hizi kwa kuanzia na NHC. Viwanja vipo na tunatumia matofali ya kuchoma, hivyo ni rahisi.

Nawatakia mafanikio katika mwaka huu.

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kuwapongeza Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, pamoja na Watendaji wake, kwa kazi nzuri.

Baada ya pongezi hizo, napenda kuchangia mambo machache kama ifuatavyo:-

Wananchi katika maeneo mbalimbali ikiwemo Manispaa ya Musoma, wanapata adha mbalimbali ya kubomolewa nyumba zao kwa kujenga kiholela maeneo ambayo hayajapimwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua mikakati ya Wizara kupata fedha za kutosha kupima viwanja vya kutosha ili kuepusha adha hiyo.

Mheshimiwa Spika, gharama za upimaji wa viwanja na mashamba ziko juu sana na hii inakuwa vigumu kwa wananchi wengi kupimiwa viwanja na mashamba, kwa kuwa malipo yale si gharama halisi. Napenda kujua Wizara imejipanga vipi kupunguza gharama hizo ili wananchi wengi zaidi waweze kupimiwa maeneo yao?

Mheshimiwa Spika, Manispaa ya Musoma kwa kuwa Mji unakua na kupanuka, umeomba kuongezewa ardhi na Halmashauri ya Musoma, yapata miaka zaidi ya mitano pasipo mafanikio; napenda kujua Wizara yako itaisaidiaje Manispaa ya Musoma ipate eneo la kutosha kwa uendelezaji wa Mji wake?

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, naomba niwapongeze Mheshimiwa Chiligati (Mb), Waziri wa Wizara hii, Katibu Mkuu, Ndugu Salome Sijaona na Watumishi wa Wizara ya Ardhi, kwa kuleta hotuba safi, ambayo naiunga mkono moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, nina machache ya kuzungumzia bajeti hii:-

Mheshimiwa Spika, kuna suala la muda mrefu linalohusu kodi ya majengo ama *Property Tax,* lengo la kukusanya kodi hii ilikuwa ni kuboresha miundombinu ya makazi kama barabara za mitaa, kujenga mifereji ya maji machafu na kadhalika. Wizara ya Ardhi, ndio kimsingi yenye majukumu hayo mijini. Hivi sasa majukumu haya hayatekelezwi vizuri na TAMISEMI; hivyo fedha nyingi za maendeleo ya miundombinu hii zinatumiwa kulipia makongamano na warsha. Huu sio utekelezaji mzuri,

napendekeza kuwa, TRA ikusanye fedha hizi lakini mipango ya matumizi yawe katika Wizara ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, Mtwara ni Mji unaokua haraka sana, kutokana na utumiaji wa rasilimali za gesi zilizoibuka miaka ya hivi karibuni. Shirika la Nyumba, yaani *Natioanal Housing Corporation,* halijaanza kutumia fursa hizi kwa kujenga makazi na Ofisi ambazo zinahitajika sana. Chuo Kikuu cha St. Augustine, chenye idadi ya wanafunzi 1,000 kwa kuanzia, kitafunguliwa huku hali ya makazi ikiwa nyuma kabisa. Namwomba Waziri, awaamshe NHC waje kuwekeza kwa hali ya juu Mtwara ili kupunguza shida kubwa ya nyumba.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Nashauri Nyumba za NHC zilizopo mijini zisiuzwe kabisa.

Nyumba zote zilizopo *prime areas* zitumike kama *collateral* kwenye mabenki ili fedha zipatikane kujenga nyumba za makazi na biashara, ambazo zinaweza kuuzwa.

*Satelite town* zianzishwe na kujengwa. NHC na watu binafsi, wajenge nyumba za kuishi nyingi kwa pamoja na kwa maeneo maalum, ambazo zitauzwa kwa wananchi. Pia kwenye maeneo hayo ya *Satelite Towns,* yatengwe maeneo ya misitu na *green areas.*

Miji isiwe ya majengo tu, lazima kuwe na miti ikiwezekana na mito. Uangalifu mkubwa uwepo wa kuchagua ni nyumba zipi ziuzwe na zipi zibakie NHC.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. Hata hivyo, nichangie machache kuhusu sekta hii.

Tatizo la uvamizi wa maeneo ya wazi katika miji yetu ni tatizo sugu, tena wakati mwingine uvamizi huo hupata baraka za Watendaji wa Wizara yako. Je, ni mkakati gani Endelevu wa Wizara yako Kisera ambao umeandaliwa au utaandaliwa ili kusaidiana na Halmashauri, Wilaya, Miji, Manispaa na Jiji ili kumaliza tatizo hili?

Mfano; uwanja wa wazi wa Msimbazi Mission uliovamiwa hivi karibuni na tajiri; ni namna gani Wizara yako inasaidia kuondoa aibu hii kwa Taifa?

Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu kwa miaka zaidi ya miwili tumekuwa na tatizo la Afisa Ardhi Mteule pale Kasulu, ambaye angetusaidia kupunguza usumbufu wa kusaini nyaraka mbalimbali za ardhi hasa Hati, kuidhinisha michoro na hata kusimamia upimaji viwanja, mashamba na maeneo ya biashara.

Tafadhali, namwomba Mheshimiwa Waziri, awasiliane na DED Kasulu ili ampe ushauri wa Kitaalamu wa namna na kurekebisha tatizo hili. Hizo taratibu za Halmashauri ya Wilaya kuwasiliana na Kamishna wa Ardhi ili kumpandisha hadhi Afisa mwenye

hadhi ili awe Mteule, basi zielezwe wazi kwa Watendaji wetu kwenye Halmashauri ya Wilaya ili wajue *exactly, what to do and how to do it.* Wakati mwingine *it is frustrating.*

Nilimwandikia memo Mheshimiwa Waziri Chiligati, juu ya tatizo la uhaba wa Afisa Mteule wa Wilaya ya Kasulu kwa miaka miwili sasa.

Ninapenda sana kuipongeza NHC na Wizara, kwa uamuzi wa kujenga Jengo la Kitega Uchumi katika Mji wa Kigoma na hatua zinazochukuliwa kwa sasa. Ninaomba NHC waje Wilaya ya Kasulu, Wilaya inayokua sana na sasa kibiashara ni Wilaya Kiongozi katika Mkoa wa Kigoma. NHC karibuni Kasulu, tutawapa viwanja vya kujenga vitega uchumi.

Kutokana na jiographia ilivyo, pamoja na umbali toka Kigoma hadi Mwanza (km 780), ninaomba Wizara ifikirie kuufanya Mkoa wa Kigoma kuwa Kituo cha Kupokea Hati za Viwanja na Nyumba ili kuondoa usumbufu huu, ambao wananchi wanaupata kwa kusubiri muda mrefu na wakati mwingine, wananchi kuombwa kwa wazi au siri eti kuchangia gharama za usafiri wa Maafisa Ardhi kusafiri kupeleka nyaraka Mwanza. Tafadhali uangaliwe uwezekano huo sasa.

Mheshimiwa Spika, mpango wa upimaji mashamba ya wanavijiji Wilayani Kasulu ili kupata hati zao za kimila utafika lini Wilaya ya Kasulu? Kwa nini maeneo tete yaliyo mpakani mwa nchi yetu yasipewe kipaumbele katika mpango huo? Ninaomba maelezo ya kina toka kwa Mheshimiwa Waziri.

Ninashauri sana Mkoa wa Kigoma upewe kipaumbele katika mpango huu.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 64 wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, umebainisha wazi chini ya Sheria ya Ardhi Na. 4 ya Mwaka 1999 kwamba, viwango vya fidia ni vidogo sana na haviendani na wakati uliopo. Je, Mheshimiwa Waziri alitaarifu Bunge hili hizo taratibu zinazoandaliwa na *Chief Valuer* zitakamilika lini ili Sheria iletwe Bungeni haraka?

Katika maeneo yenye migodi, ujenzi wa barabara na hata mijini, viwango wanavyolipwa watu wetu ili kupisha shughuli fulani iliyokubaliwa Kitaifa vinasikitisha. Ninashauri *strongly*, Serikali ilete Muswada wa Marekebisho ya Sheria hii haraka kwa dharura ili sheria mpya iwe ndiyo zawadi ya wananchi wetu ya mwaka mpya wa 2010.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja hii.

**MHE. DKT. WILLIBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia kama ifuatavyo:-

Ni kweli kuwa Mabaraza ya Ardhi ngazi ya Vijiji na Kata, yamesaidia sana katika kupeleka huduma karibu na Wananchi. Waziri anatoa wito (Ukurasa wa 26) kwa Halmashauri kuimarisha Mabaraza ya Vijiji na Kata.

Je, kwa kauli hii Waziri anatoa tamko gani sasa kuwa gharama zote za uendeshaji wa Mabaraza haya ziwe jukumu la Halmashauri? Tatizo hili la nani hasa anahusika na gharama limeua kabisa *morale* ya Makatibu na Wajumbe wa Mabaraza kwa kuwa wanafanya kazi katika mazingira magumu.

Ni vyema Waziri atoe tamko la Serikali ili kuondoa utata huu, ambao maeneo mengine umezaa matukio ya rushwa ili Wajumbe wa Mabaraza waweze kujikimu.

Je, Waziri anafahamu kuwa gharama za kufungulia *file* katika Mabaraza ni kubwa mara elfu kuliko katika Mahakama za Mwanzo na hasa pale Baraza linapotakiwa kuhamia eneo la mgogoro? Gharama hizi huwanyima haki wananchi wanyonge na hivyo kulifanya kuwa la matajiri na wenye fedha, kinyume kabisa na malengo ya Mabaraza haya. Waziri anatoa kauli na mwongozo gani kuhusu hali hii?

Mheshimiwa Spika, natanguliza shukrani za dhati.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kujitahidi kupima viwanja ili wamiliki wapate hati na kuviendeleza hata kuwawezesha kupata mkopo; kwa mfano, upimaji wa viwanja Kigamboni sehemu za Kimbiji umekamilika lakini miundombinu ni mibovu sana hata wamiliki wakishapata hati watapaendeleza namna gani? Kuna haja ya Serikali kuhakikisha barabara zinatengenezwa, umeme na maji; kupima tu viwanja haitoshi.

Mheshimiwa Spika, huko Mikoani, kwa mfano, Kilimanjaro vitendea kazi kama magari na pikipiki kwa ajili ya upimaji hakuna. Unakuta kutoka Mkoani mpaka Vijijini ni umbali wa kilomita 40; sasa hawa watendaji watafika namna gani katika sehemu zile?

Sio hilo tu pale Moshi wanayo darubini moja tu kwa ajili ya upimaji kwa mkoa mzima. Ningependa kujua je, katika bajeti hii ni kifungu kipi kinachoonyesha vitendea kazi kama darubini kwa mkoa wa Kilimanjaro kipo wapi?

Nashauri pawepo hata pikipiki moja na darubini moja katika Wilaya kwa kuanzia ili kuharakisha upimaji wa viwanja.

Mheshimiwa Spika, kuna wakati unakuta viwanja ni kwa ajili ya makazi, lakini wamiliki wanabadilisha na kuvifanya vya biashara. Kwa mfano, kuna wengine wanajenga hata bar ambazo hupiga muziki mpaka baada ya saa sita usiku na kuleta usumbufu mkubwa sana kwa wakazi, ukizingatia wanakuwa wamelewa, wengine wanatumia lugha chafu na kadhalika. Je, Serikali inatueleza nini kwa wamiliki waliobadilisha matumizi ya awali walipopewa hati? Zaidi ya hapo, la hatari zaidi kuna wateja ambao hujenga hata vituo vya kuuzia mafuta (petrol, diesel) katika makazi ya watu. Je, Wizara inatoa hati kwa wamiliki wa vituo vya mafuta kuweka vituo kwenye makazi ya watu?

Mheshimiwa Spika, kuna nyumba hewa hujengwa na baadae Serikali huja kuzibomoa, mfano, maghorofa yaliyojengwa eneo la Sea Cliff yalibomolewa. Je, Wizara

inakuwa wapi mpaka mtu anafikia kumalizia kujenga *(finishing)* halafu Serikali inakuja kuibomoa na kuleta makubaliano ya kupelekana mahakamani kulipana fidia wakati hili lingeweza kuzuilika katika hatua za awali tangu msingi kuchimbwa?

Shirika la Nyumba (NHC), limekuwa likipokea zaidi ya shilingi bilioni saba kwa kila mwezi. Je, mapato hayo yamepelekwa wapi? Kwa mfano, zipo nyumba za NHC kama *Breweries Estate* (Dar es Salaam), kodi kwa sasa hivi ni 95,000/= kwa mwezi, kwa kisingizio cha ukarabati wa majengo wakati matengenezo yote hufanywa na mpangaji kama ilivyo kwenye Sera ya Shirika, ambao wao hupaka rangi tu baada ya miaka michache. Je, mapato hayo zaidi ya shilingi milioni 800 yaonekane wapi?

Naomba majibu ya kina kwa hili; ni kiasi gani shirika linapata kutokana na kodi wanazozipata kwa mwaka?

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kwa maandishi, Hotuba ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo la muda mrefu limewakumba wananchi katika baadhi ya maeneo ya Majohe, Chanika, Pugu na kadhalika; wamezuiliwa na Serikali wasilime zaidi ya miaka sita sasa, sababu maeneo yao yamo katika mpango wa upimaji viwanja; ni lini basi watafidiwa ili kuondoa kero ya kuwakosesha kulima na kuwasababishia kuwa na maisha magumu?

Mheshimiwa Spika, majumba yanayojengwa Kariakoo pamoja na jitihada kubwa za kudhibiti ujenzi uwe wa kiwango, lakini bado kuna suala zima la ujenzi wa kutoka nyumba moja na kuacha nafasi baina yake na nyumba iliyopo ubavuni mwake; hili ni tatizo ambalo ukitokea moto ni hatari kubwa, baadhi ya maeneo ni vyema Wizara hii ikaliangalia jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, upandaji wa kodi wa nyumba za Serikali; ni kweli inatakiwa ukarabati na ujenzi wa nyumba mpya, kodi ilingane na eneo husika na wale ambao hawapo tayari kulipa, basi hatua za kisheria zichukuliwe na nyumba hizo ziingizwe wapangaji wapya na ni vyema sasa ujenzi wa nyumba mpya uongezwe ili kukidhi tatizo la ukosefu wa nyumba.

Mheshimiwa Spika, uimarishaji wa miundombinu inayofanywa na Wizara hii; ni vyema basi kasi iongezeke ya matengenezo ya barabara ili wananchi wafikie maeneo yao kwa ajili ya ujenzi na lengo la kuifanya Kigamboni kuwa mji wa mfano.

**MHE. HEMED MOHAMED HEMED:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijaalia siku ya leo kuamka hali nikiwa mzima.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu kwako, Naibu wako, pamoja na Wenyeviti wako, kwa umahiri wenu katika kutuongoza.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hayo, sasa naomba uniruhusu niende katika mchango wangu katika Wizara husika. Kwa kuzingatia Hotuba ya Wizara hii, utafahamu nia njema ya Mheshimiwa Waziri Chiligati kuwa, ana nia ya kufanikisha Maisha Bora kwa Kila Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu uliopo katika Wizara hii, utaona iko haja kuongezewa bajeti yake. Kuhusu ardhi ni eneo la kutuletea maendeleo. Hatuwezi kukuza uchumi wetu kama hatukuitumia ardhi. Kinachohitajika ni suala zima la umiliki. Migogoro ya ardhi, mara nyingi inatupelekea kuondoka kwa amani kwa baadhi ya maeneo. Ili Serikali inusuru migogoro ni lazima kugawa maeneo mahususi kwa wakulima, wafugaji na wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kuna migogoro mingi ya ardhi, jambo ambalo hupelekea hasara ama kwa Serikali au kwa mwananchi wa kawaida; kumejitokeza bomoabomoa kila leo katika miji yetu. Uvunjaji wa majumba kila leo ni dosari kubwa. Tatizo linalojitokeza ni pale Serikali inapowaacha wananchi kujenga katika maeneo na hatimaye watu hao huhamia na kuchukua miaka wanaishi katika nyumba zao hizo. Naiomba Serikali inieleze ilikuwa wapi hata watu hao wakajenga?

Serikali haijawatendea haki wale wanaostahili kulipwa fidia; ni vyema Serikali iangalie vyema suala la malipo ya fidia.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi migogoro katika miji yetu, husababishwa na Serikali kutopanga mipango miji. Wananchi wanaanza kisha Serikali inafuata na kusababisha usumbufu mkubwa kwa wananchi. Naiomba Serikali ipange mipango kabla ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Ahsante.

**MHE. KHADIJA SALUM AL-QASSMY:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kuniwezesha kutoa maoni ya hoja iliyoko mbele yetu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Spika, napenda kukupongeza wewe, pamoja na Watendaji wako wote, kwa kazi nzuri mnayoifanya katika Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa sikumtendea haki Waziri, pamoja na Watendaji wake wote, kama sitawapongeza kwa jinsi walivyoandaa hotuba hii. Mwenyezi Mungu, awape uwezo ili wayatekeleze kwa vitendo mambo yote waliyoyapanga.

Mheshimiwa Spika, naanza kuchangia kwa kumwomba Waziri, aliangalie suala la ugawaji wa viwanja. Kwa mfano, viwanja vya Dodoma. Dodoma ni mji mpya na unatakiwa uwe na maendeleo ya haraka, kwa wananchi kupata nyumba bora na za kisasa. Sasa unapopimiwa kiwanja kwa bei ya shilingi 5,000,000; je, Serikali inamlenga nani wakati Wananchi wa Tanzania kipato chao ni duni; hakiwatoshi hata mlo mmoja?

Naiomba Serikali iangalie kwa makini suala hili ili wananchi wa kawaida wafaidike katika suala la kujiletea maisha bora kwa kila Mtanzania ni pamoja na makazi bora.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka Rais wetu alisema, kamwe wananchi wasinyang'anywe viwanja vyao kwa sababu alijua hali za wananchi wake sasa.

Mheshimiwa Spika, wananchi walio wengi ni maskini sana, wamepimiwa viwanja walipe kwa muda wa miezi mitatu. Cha kusikitisha zaidi, Wananchi wa Kigamboni na Buyuni, waliochelewa kulipa wameongezewa mara mbili kulipa; je, Serikali kweli inawatendea haki wananchi hawa?

Mheshimiwa Spika, wananchi wameshindwa kulipa kwa wakati kwa sababu hali zao ni mbaya; je, ukiwaongezea ndio umewasaidia?

Mheshimiwa Spika, jambo kubwa linalosikitisha katika nchi yetu ni kuwaacha wananchi wakijenga, baada ya miaka Serikali inawavunjia ghafla, bila hata ya kuwalipa malipo ya uhakika na kuwasababishia wananchi usumbufu mkubwa na wakati mwingine kuwasababishia hata kufa kwa *pressure*.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ianze kupanga mji kabla wananchi hawajajenga, kwa kuwawekea miundombinu ya uhakika, kabla wananchi hawajajipanga wenyewe halafu wakavunjiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi kirefu sasa kumekuwa na machafuko ya kupigana na watu baina ya wakulima na wafugaji, naiomba Serikali iwe na mipango madhubuti ili kuwanusuru wananchi wasiokuwa na hatia kwa kupanga mipango madhubuti ya ardhi, kwa kuwapa ardhi ya kutosha ili kuepusha migogoro isiyo ya lazima.

Mheshimiwa Spika, Wizara iiongezee uwezo Shirika la Nyumba ili lizidi kujenga nyumba nzuri na za uhakika, wananchi wetu waweze kukodi kwa bei rahisi na vile vile kununua na kulipa kidogokidogo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na napenda kumpongeza Waziri Chiligati, kwa kazi yake nzuri. Ahsante.

**MHE. MWINCHOUM A. MSOMI:** Naomba kuchukua fursa hii kwanza, kumpongeza Mheshimiwa Captain Chiligati, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kwa jinsi anavyoitumikia vyema Wizara hii na kuwa na maamuzi ya haraka ya kazi zake. Aidha, nawapongeza Wasaidizi wake wote. Kubwa kwake ni kufanya kazi kwa uwezo na ufanisi bila ya kuwa na Naibu Waziri.

Katika Jimbo langu, nakabiliwa na matatizo makubwa matatu yafuatayo:-

(a) Mradi wa kupima viwanja 20,000 Dar es Salaam umeikumba pia Kata ya Kibada ndani ya Jimbo la Kigamboni, lakini mpaka sasa kuna malalamiko mbalimbali ya Wananchi, juu ya mradi huu ikiwa ni pamoja na malalamiko ya fidia, kunyang'anywa

viwanja, kutopewa viwanja, ikiwa na Ofisi za Serikali za Mitaa na Chama Tawala (CCM).

(b) Tatizo linginge ni kusuasua kwa Mradi wa Ujenzi wa *Refinery* eneo la Amani Gomvu, Kata ya Somangila zaidi ya miaka miwili sasa imepita. Wanashindwa kuendeleza maeneo yao, baada ya kusitishwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Je, Mradi umefikia hatua gani mpaka sasa?

Kuna maelezo yasiyothibitishwa kwamba, Mradi huu haupo tena; je, habari hizi ni sahihi? Kama ni kweli Wananchi wanapenda kujua Serikali itawafidia vipi kutokana na kuwarejesha nyuma kimaendeleo na kimapato? Aidha, naishauri Wizara iandae Mkutano Maalum katika eneo hilo kuwaeleza Wananchi yanayoendelea.

(c) Wizara hivi sasa imo katika mchakato wa kutambua Wakazi wa Kigamboni; Kigamboni yenyewe, Vijibweni, Mjimwema na Kibada, juu ya mpango wote wa kuupanga na kuujenga upya Mji wa Kigamboni, kudadisi wenye kumiliki majengo na viwanja na mashamba. Ilielezwa na Wizara hii kupitia Waziri katika Mkutano ya Hadhara kwamba, kila hatua kutakuwa na uwakilishi wa wananchi; je, mbona hatua hii ya awali hakuna uwakilishi wowote wa Wananchi au Viongozi Wawakilishi? Je, suala la kuundwa mamlaka ya kusimamia utekelezaji wa mradi limefikia wapi/hatua gani?

Naishauri Wizara kuwasiliana na Wizara ya Nishati na Madini, kupeleka huduma za umeme kwenye viwanja vilivyopimwa chini ya Mradi wa Viwanja 20,000 Dar es Salaam, pamoja na kuzungumza na Wizara ya Maji na Umwagiliaji, kuchimba visima virefu katika maeneo hayo vilevile kufuatia ujenzi wa haraka.

**MHE. IDDI M. AZZAN:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Viongozi na Watendaji wa Wizara hii, kwa kazi nzuri wanazofanya hasa kwenye maendeleo ya makazi.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Shirika la Nyumba (NHC), lijiendeshe kibiashara ili liweze kuendelea kujenga nyumba za gharama nafuu na kuwasaidia wananchi wetu kupata makazi bora. Tunafahamu gharama za kodi ya pango ilivyopanda, hasa mitaani kwetu ambapo chumba kimoja ni Sh. 35,000 kwa mwezi, kwa wenye nyumba binafsi na watu binafsi wenye nyumba za biashara ni Sh. 150,000 hadi 350,000 kwa chumba, tena kwenye maeneo ya Jimbo langu tu; maeneo ya Mjini; Kariakoo, Upanga na kadhalika, gharama ya nyumba ya kuishi ni kati ya Sh. 400,000 hadi 1,500,000 kwa mwezi, huku maeneo hayo hayo kwa chumba cha biashara ni kati ya USD 500 hadi 100 kwa mwezi. Hivyo, naomba sana NHC liwe makini katika pango la nyumba zao, hasa nyumba za biashara waendane na soko.

Nyumba za kuishi sisemi mpandishe kodi kulingana na nyumba za watu binafsi, bali angalieni na wananchi wanaokaa nyumba hizo, wasiokuwa na uwezo walipe kodi nafuu na wenye uwezo walipe kuendana na soko. Sambamba na hilo la kodi ni lazima mhakikishe kuwa, nyumba zenu zinakuwa na ubora unaostahili, muwe mnafanya matengenezo ili nyumba zenu ziwe bora zidi.

Mategemeo makubwa kwa wananchi ni kuona Shirika linajenga nyumba nyingi zaidi ili na wafaidike nazo. Yote haya, yatategemea shirika kukusanya mapato yake vizuri.

Wapo wapangaji wenu wengine wana majumba makubwa na wanayapangisha kwa bei kubwa huku wakiendelea kuishi nyumba za NHC na kulipa kodi ndogo. Naomba watu hao mkiwagundua muwahamishe kwenye nyumba hizo za NHC ili nafasi hizo wapangishwe wananchi wetu wengine wasio na nyumba na wenye kipato kidogo.

Mheshimiwa Spika, Wizara iangalie utendaji wa Shirika hili na kama kuna watendaji wabovu, waondolewe haraka.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza Waziri, Katibu Mkuu na Watumishi wote, kwa kuandaa hotuba hii na kuiwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu. Hata hivyo, napenda kuchangia mambo machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ina Mradi mkubwa wa upimaji wa viwanja 20,000 Jijini Dar es Salaam. Kwanza, napenda niipongeze Wizara kwa hatua hiyo, ambayo italifanya Jiji la Dar es Salaam lipangwe vizuri zaidi na hivyo kuwezesha huduma mbalimbali kama vile maji, barabara, umeme na kadhalika, kuwafikia wananchi kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, ugawaji wa viwanja hivyo una kasoro kubwa sana. Kwanza, Maafisa wengi wa Wizara ya Ardhi, wamehodhi viwanja vingi sana na kama Wizara hii itafanya uchunguzi wa kina, itabaini ukweli huu. Pili, kuna watu ambao wamejipatia viwanja zaidi ya kimoja kwa kutumia majina tofauti tofauti. Je, hili halijulikani na mamlaka za ugawaji viwanja hivyo? Tatu, kuna mazingira makubwa sana ya rushwa katika ugawaji wa viwanja hivyo.

Mheshimiwa Spika, kuna ucheleweshaji wa kuweka miundombinu katika maeneo mbalimbali yaliyopimwa. Hali hiyo huchelewesha uendelezaji wa maeneo hayo.

Ninashauri kuwa, viwanja vinapogawanywa ni vizuri majina ya waombaji wote yabandikwe kwenye mbao za matangazo, pamoja na picha zao. Nasema hivyo, kwa sababu watu/waombaji wengine hutumia majina ya watoto ambao wapo shuleni; picha zikitumika hilo halitafanyika. Pili, mwombaji akabidhiwe *Offer* yeye mwenyewe *(in person)* ili kumfahamu muhusika. Tatu, viwanja visivyoendelezwa kwa miaka mitatu tangu vigawanywe, wanyang’anywe ili watu wengine wenye shida wagawiwe. Nne, maafisa watakaobainika kujihusisha na vitendo vya rushwa na kuhodhi viwanja, wachukuliwe hatua kali za kinidhamu/kisheria.

Mheshimiwa Spika, watu wengi wamepata mwamko na elimu ya kutosha juu ya umuhimu wa kuwa na hati za nyumba na mashamba yao. Hata hivyo, kumekuwa na urasimu mkubwa juu ya kukamilishwa kwa zoezi hilo. Aidha, kumekuwa na malalamiko makubwa kutoka kwa wananchi wengi kwamba, wengi wao hudaiwa rushwa ili waweze kukamilishiwa kazi zao.

Mheshimiwa Spika, hali hii siyo nzuri hasa kwa nchi kama yetu inayoongozwa kwa misingi ya Utawala Bora. Naomba Waziri alieleze Bunge lako Tukufu, mwananchi anatakiwa afanye nini ili maombi yake yasikwamishwe Wizarani au hatua nyingine yoyote? Je, katika zoezi hilo mwananchi anatakiwa alipe kiasi gani cha fedha ili apate hati miliki yake?

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kuja na zoezi la hati miliki za kimila. Hati hizo zimesaidia/zimewezesha watu wengi, hasa wale wa Mbozi, kupata mikopo ya pembejeo za kilimo, matrekta na kadhalika. Hata hivyo, kumekuwa na tatizo moja kubwa, nalo ni hati hizo kuendelea kutotambuliwa na mabenki kama hati halali kwa ajili ya dhamana ili kuwawezesha wananchi kupata mikopo. Naomba kujua, kwani pia kupitia Bunge hili, Serikali kwa nyakati tofauti, imewahi kusema kwamba, hati hizo zingetambuliwa na mabenki kama dhamana na hivyo kuwawezesha wenye hati hizo kupata mikopo kwa maendeleo yao.

Je, suala hilo limefikia wapi kwani Wananchi wa Mbozi ambao ndio walikuwa wa kwanza kufaidika na hati hizo za kimila wana hamu ya kuona hati hizo zinatambuliwa rasmi na taasisi za fedha kama mabenki?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuchukua nafasi hii, kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kazi kubwa anayoifanya, pamoja na Katibu wa Wizara, Mama Sijaona na Timu yao.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu mkuu ni juu ya umuhimu wa kutenga maeneo ya wafugaji, ambalo limekuwa ni tatizo kubwa sana na hivyo kuzidi kuleta malalamiko kati ya wafugaji na wakulima.

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri umeeleza katika taarifa yako kuwa, unatarajia kuuza nyumba, nami niombe kufikiriwa katika nyumba zitakazouzwa katika Mji wa Dodoma au Songea muda ukifika.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa mpango uliowasilishwa wa kuboresha Jiji la Dar es Salaam, ili kuwezesha Jiji hilo kuwa na mandhari ya mji wa kisasa.

Ushauri wangu ni umuhimu wa kuzingatia kuwa, wadau wote watoa huduma, wanahusishwa katika mpango huo, ili nao waweze kutoa gharama zao na hivyo kuingizwa kwenye mradi mfano; umeme na maji taka.

Kasi ya kuendeleza miji ya pembezoni *(satellite towns)*, kama ilivyosemwa kwenye Budget ya 2008/09, iongezwe kwani msongamano wa *city centre* sasa umezidi na wafanyakazi hutumia muda mrefu kusafiri na hivyo kupunguza saa za kazi; na pengine wagonjwa kupoteza maisha wakiwa kwenye foleni kuelekea hospitalini.

Mara ya mwisho nilitembelea kituo chenu kilichopo mwenge ili kujifunza na kuona uwezekano wa kupata machine za kupigia matofali ya *interlocks*, utaalam wa kisasa. Kazi zao ni nzuri, lakini inaonekana hawana mtaji wa kutosha na hivyo kuchelewesha kusambaa kwa teknolojia hiyo.

Ni vyema wawezeshwe kwa kuongezewa mtaji ili waweze kutengeneza mashine hizo kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia katika Wizara hii. Napenda kutoa pongezi kwa Waziri na Wataalam wake wote, walioandaa Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imeanza kuwa na migogoro ya ardhi na hili kama hatua za haraka na kali hazitachukuliwa, litaleta hali ya hatari na hata kusababisha vifo kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, tumeona kwenye vyombo vyetu vya habari, jinsi wananchi hasa maskini wanavyonyang'anywa ardhi zao, wanavyobomolewa nyumba zao na kuwafanya waishi maisha magumu na ya hatari, kwa sababu wanapobomolewa, familia zao hukosa mahali pa kuishi. Matokeo yake, wanakaa kwenye mahema kama wakimbizi. Kibaya zaidi, watoto ndiyo wanaoathirika zaidi wanapokosa huduma hasa matibabu na elimu, pale familia zinapofukuzwa katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, tatizo hili zaidi linasababishwa na rushwa kwa Watendaji wetu, ambao wanatumia kigezo cha uwekezaji kwa kuwaondoa wananchi katika maeneo yao ya asili. Tunaomba sana suala hili lifuatiliwe kwa makini ili wananchi wetu wapate haki zao. Tusiwajali wawekezaji, tukawasahau ndugu zetu Wananchi wa Taifa hili. Kama wawekezaji wakipewa maeneo hayo, basi wananchi wapewe fidia halali na kupewa maeneo mengine kwa ajili ya kuanza maisha mapya.

Mheshimiwa Spika, katika Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, nilizungumzia suala la upimaji wa viwanja Kigamboni. Kwanza, naupongeza Mradi huo na Waziri amesema, wananchi hawataondolewa watakuwa wa kwanza kupewa maeneo. Katika mchango wangu kwa Waziri Mkuu, nilitaka kujua tatizo la Shule ya Sekondari Kibada, ambayo baadhi ya majengo yanatakiwa kubomolewa eti kwa sababu yamejengwa kwenye kiwanja ambacho si cha shule.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe shule hizi za Kata zilijengwa kabla ya Mradi huo kuanza na itakuwa ni jambo la ajabu, shule hiyo majengo yake yakibomolewa. Wananchi hawatatuelewa kabisa. Pia lipo tatizo lingine la kisima cha maji, ambacho kilichimbwa katika Kata hiyo nacho kimepimwa.

Mheshimiwa Spika, tunaomba sana maeneo haya yawe ya jamii ili tuweze kupunguza kero kwa wananchi wetu. Nategemea majibu mazuri toka kwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, bado tuna tatizo kubwa sana kwa wataalam wetu wa mipango miji. Sijajua ni kwa nini hawataki kufanya kazi zao kwa kufuata taratibu zilizopo. Inashangaza kuona yale maeneo ya wazi kupewa watu kujenga na kusababisha watoto wetu kukosa maeneo ya kucheza. Hili pia linafanana na wale Watumishi wa Ardhi, wanaogawa kiwanja kimoja kwa zaidi ya mtu mmoja. Tunaomba sana watumishi hawa, ambao ndiyo chanzo kikubwa cha migogoro ya ardhi, wachukuliwe hatua kali ili iwe fundisho kwa watumishi wengine.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii.

**MHE. NURU A. BAFADHIL:** Mheshimiwa Spika, suala la ardhi limepelekea kusababisha migogoro mingi ndani ya jamii. Tunaiomba Serikali iharakishe kutoa hati miliki za ardhi ili kupunguza migogoro na dhuluma zinazofanywa na wale wenye uwezo wa fedha.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa jitihada zake za kuwezesha uhamasishaji wa nyumba za gharama nafuu, pia kutoa mikopo ya nyumba (ujenzi).

Mheshimiwa Spika, kuna mtindo wa kuwanyang’anya wananchi ardhi zao, kwa kisingizio kuwa kupanua miji au majiji. Mfano Jiji la Tanga, wananchi wananyang’anywa ardhi yao, kwa kulipwa fidia ndogo sana na baadaye viwanja hivyo vinauzwa kwa watu wenye uwezo tena kwa pesa nyingi.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Mipango Miji ya Jiji la Tanga imekithiri kwa rushwa. Naiomba Wizara husika ipitie Ofisi hii; wapimaji ardhi ni wachache na hiki ndio chanzo kikuu cha rushwa; raia anapohitaji kiwanja anapopitia mipango miji atazungushwa, lakini hapati ila wapo watu waliowekwa kwa ajili ya kazi hii. Muhitaji anamwona huyo anapangiwa bei anayotaka kama 2,000,000 au 3,000,000 na kadhalika, lakini atakwenda mipango miji akapewe hati ya muda au *Offer* kwa bei ya Serikali. Je, Serikali haioni huu ni ufisadi? Tunaomba Wizara iunde Tume ya kuchunguza ufisadi huu uliopo katika Jiji la Tanga.

Jiji la Tanga limekithiri kwa ufisadi huu wa ardhi kupitia Idara husika, wameihodhi Idara kama yao na wakati mwingine wanasaidiana na Wenyeviti wa Mitaa/Vitongoji, kuuza mashamba ya watu na wao hujipangia sehemu zao na baadaye wanaziuza kwa bei kubwa. Hiyo haitoshi, Wizara iangalie uwezekano wa kumpa uhamisho Afisa Mipango Miji wa Jiji la Tanga. Ameshanufaika kwa kiasi kikubwa, ingawa hata ukimuuliza ana rasilimali gani atajibu hana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu nyumba za Shirika la Nyumba la Taifa, kuna baadhi ya wananchi wanahangaishwa na Watendaji wa Shirika hili. Wengine wanalazimishwa kutoa sehemu za maeneo yao kuwapa watu wengine, wakati hati inaonesha mipaka yake yote ni eneo moja; iweje eneo hilo ligawiwe mara mbili?

Mheshimiwa Spika, tunaomba Wizara itupe ufafanuzi kuhusu ugawaji wa maeneo ambayo tayari yamekwisha milikishwa mtu ligawiwe mara mbili. Huu nao ni mgogoro mwingine kati ya watendaji na wateja wao.

Mheshimiwa Spika, kumezuka mtindo wa kuyauza maeneo ya wazi *(Open Spaces)*, kuna maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya michezo; cha kushangaza maeneo haya yanauzwa na kujengwa nyumba hatimaye watoto wanakosa maeneo ya michezo. Wizara inasemaje kwa hili?

Mheshimiwa Spika, kuna maeneo ya fukwe yameuzwa kwa wawekezaji. Wahusika wa ardhi hiyo wamelipwa fedha kidogo sana, wakati watendaji ndio waliochota pesa nyingi. Utakuta mmiliki amelipwa shilingi milioni tano wakati eneo hilo limeuzwa kwa mwekezaji kwa shilingi milioni 30.

Je, Wizara haioni huu ni ufisadi na ukiukwaji haki za binadamu. Tuanomba Wizara itembelee Kijiji cha Machui Tanga, ikaone jinsi fukwe zilivyouzwa na wahusika kupata fidia ndogo, lakini baadhi ya Watendaji Kijijini humo kunufaika na uuzaji wa fukwe hizo.

Kwa ujumla suala la ardhi linawadhoofisha baadhi ya wananchi na linawanufaisha baadhi ya watu.

**MHE. DKT. GUIDO SIGONDA:** Wilaya ya Chunya ambayo ina ukubwa wa asilimia 46 ya Mkoa wa Mbeya, wapo Watumishi/Wataalam watatu tu. Idadi hii haitoshelezi hata kidogo kumudu kazi za Kitaalam. Kwa Wilaya kubwa kama Chunya ni vyema Watumishi wakaongezwa kutoa huduma za kitaalam kwenye Wilaya hiyo.

Kwenye Wilaya ya Chunya, Watumishi watatu walioko kwenye Ofisi ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, hawana usafiri wa aina yoyote. Nashauri Wizara itoe usafiri wa gari kwenye Ofisi hiyo.

Kazi ya kutoa Hati Miliki ya Ardhi inakwenda polepole mno, hasa kwenye maeneo ya Vijijini. Nashauri Serikali ishughulikie suala hili kwa uharaka.

Utaratibu wa mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba kwa bei nafuu bado haujaanzishwa Wilayani Chunya. Je, ni lini mpango huo utatekelezwa Wilayani humo?

Wananchi walio wengi vijijini, hawaelewi vizuri Sheria ya Matumizi ya Ardhi; ni vyema Serikali ikawa na mipango ya kuanzisha elimu ya sheria hizo hasa vijijini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ZAKIA HAMDANI MEGHJI:** Kwanza, natoa pongezi kwa Waziri, Katibu Mkuu na Viongozi wote wa Wizara.

Suala la mikopo ya nyumba ni ukombozi mkubwa kwa wananchi. Ni vizuri wakati wananchi wanapewa mikopo hii, elimu itolewe kwao ili waweze kutekeleza yale yanayohitajiwa ili wasipoteze hizo nyumba watakazojenga au kununua. Utaratibu huu ni mzuri pale ambapo mwananchi anacho kipato kingine au atakodisha hiyo nyumba ili aweze kulipa. Kwa maana badala ya kulipa kwa Landlord analipa Bank.

Ni vizuri pia kusiwe na ukiritimba mkubwa kutoka mabenki muda wa uamuzi wa kutoa mkopo uwe mfupi.

Suala la mipango katika matumizi ya ardhi. Ni jambo la kawaida kuona viwanja vingi vinagawiwa katika eneo bila ya kufikiria kutenga maeneo ya wazi ya viwanja vya watoto.

Suala la *satelite towns* ni la muhimu sana, kwani litapunguza hata msongamano katika Jiji la Dar es Salaam.

Land Bank imezungumzwa miaka mingi hivi sasa. Jambo hili lina umuhimu mkubwa katika masuala ya uwekezaji, kuna maeneo mfano ya fukwe, yamechukuliwa na watu ambao hawayaendelezi hata kidogo. Ni vyema kukawa na Land Bank ili hata *serious investors* wakija, basi inakuwa rahisi na kuchukua muda mfupi kuwapatia maeneo.

Hivi sasa kumezuka tabia ya kujenga majengo marefu katika maeneo ambayo kulikuwa na nyumba za chini na ambazo walikuwa wakiishi familia moja au mbili. Hivi sasa eneo hilo hilo, wanaishi familia zaidi ya kumi. Tatizo *infrastructure* ya maji taka mfano makaro, hubaki vilevile, kwa hiyo wakati wa mvua barabara zinajaa maji, mifano ya wazi iko Dar es Salaam. Ni muhimu Wizara ikazibana Halmashauri za Jiji ili jambo hili lisiwepo.

Katika maeneo mengine hasa pale ambapo nyumba za Serikali zimeuzwa, utakuta maeneo yanabadilishwa matumizi ya ardhi kiholela. Jirani haulizwi, kwa huyo utakuta watu wanaishi katikati ya mabaa. Ni vizuri sheria zikafuatwa.

Naunga mkono Serikali kuhusu upandishaji wa kodi za NHC.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RITA L. MLAKI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nichukue nafasi hii, kuwapongeza sana Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara ya Ardhi, kwa kazi nzuri wanayofanya.

Nawapongeza kwa ubunifu mkubwa mnaofanya na jinsi mnavyotatua kero za wananchi. Napenda kuchangia maeneo kadhaa kama ifuatavyo:-

Mpango wa ujenzi wa nyumba wa ubia umebadilisha maeneo mengi na ni mzuri sana. Shirika lilisimamisha kwa muda, kupokea maombi mapya kwa ajili ya wabia kadhaa kuzorotesha ujenzi. Ninashauri Shirika linapoweka Mkataba, wazingatie muda wa ujenzi. Pale mbia anapochelewesha kwa sababu zisizokubalika, basi anyang'anywe na apatikane mbia mwingine. Ubia uendelee kwa kasi kubwa.

Tunaomba Baraza la Ardhi la Kinondoni lipatiwe eneo kubwa la kufanyia kazi. Hii inatokana na wingi wa matatizo ya ardhi ya Wilaya ya Konondoni. Tunashukuru tumepatiwa watenda kazi wazuri na wenye uwezo mkubwa. Msongamano uliopo ni mkubwa sana na hali ya usuluhishi inakuwa ngumu.

Kuhusu uboreshaji wa makazi katika Jiji la Dar es Salaam, tunaomba Serikali ifanye *special project* ya kuboresha maeneo ya Manzese, Msimbazi Bondeni, Kigogo na Jangwani. Watu wanaoishi Manzese wahamishwe na mji mpya ujengwe hapo, kwani ni vigumu kuboresha kwa hali iliyopo sasa. Napendekeza Mradi huo mkubwa, utafutiwe fedha za wafadhili.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja kwa asilimia zote iliyoletwa mbele yetu na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Ninayo matumaini makubwa na utendaji kazi wa Waziri Chiligati, pamoja na Wataalamu wake wote, bila kumsahau Mama Sijaona, Katibu Mkuu wa Wizara. Nina matumaini, wataendelea kutekeleza Sera ya Ardhi na utatuzi wa migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Serikali iendelee na mpango wake wa kuzikopesha Halmashauri, fedha za kupima viwanja kama ilivyofanya kwa Jiji la Mbeya. Mpango usimamiwe kwa karibu sana na Wizara na kufanya *monitoring* ili kusitokee dhuluma hasa wakati wa kutathmini fidia, Serikali ipambane na watendaji wasiokuwa waaminifu kama ilivyojitokeza katika Jiji la Mbeya eneo la Isyesye. Rushwa na uongezaji wa fedha za fidia ukomeshwe na wananchi walipwe fidia ya haki na wakati na kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Serikali iingilie kati mgogoro wa eneo la soko, Kata ya Uyole Jiji la Mbeya. Wananchi walilitenga eneo hili kwa matumizi ya soko, lakini kwa mshangao eneo hili limepimwa viwanja vya makazi na kuleta malumbano kati ya Viongozi wa Halmashauri na Wananchi wa Kata hiyo. Nashauri wananchi wafikiriwe kwanza na viwanja vile vifutwe ili soko lipatikane pale.

Mheshimiwa Spika, naomba ujenzi wa makazi/nyumba za bei nafuu utakapoanza, nafasi ya mwananchi wa chini izingatiwe na kigezo kiwe ni pato la mfanyakazi wa chini na uwezo wake. Bei ya pango au ya kuuziwa iwe na *component* ya *affordability to the lumpen proletariats*, ambao ni wengi sana. Nyumba si anasa bali ni haki ya kimsingi na

ni sehemu ya kutimiza Dira ya Taifa ya 2025 na Ilani ya CCM 2005, inayosisitiza juu ya Makazi Bora.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri, Mheshimiwa Captain Chiligati (Mb), kwa kazi kubwa anayoifanya.

Mheshimiwa Spika, nashauri yafuatayo:-

Mabaraza ya Ardhi hasa ya Vijiji na Kata yaundwe kwa umakini wa hali ya juu sana, yakizingatia sheria iliyopo. Kwa sasa, Mabaraza haya yanaundwa kwa upendeleo mkubwa na kutazamana usoni. Vile vile, Mabaraza hasa ya Kata, yanateuliwa bila kujali uwezo.

Napenda kujua je, Mabaraza ya Kata yakilalamikiwa kwa kutotenda haki; walalamikaji waende wapi?

Yatolewe mafunzo kwa Wajumbe, hasa Mwenyekiti na Katibu wa Baraza. Aidha, wapewe kipindi cha uangalizi ili kuona kama wanamudu vizuri majukumu yao.

Itamkwe wazi Mamlaka ya Baraza kwa mfano, wanapohamishia kikao kwenye eneo watoze shilingi ngapi? Zipo habari kuwa Baraza mojawapo la Kata la Muleba Kaskazini hutoza kati ya shilingi 30,000 – 100,000, wanapokwenda kukagua maeneno na mipaka. Pesa hizi huwa hazina risiti, mashahidi wapo. Hii ni aibu na ukweli ni ulafi wa kujipatia kipato bila jasho.

Suala la kutenga maeneo ya maendeleo katika vijji liwe ni la lazima. Kwa sasa hivi, maeneo yanavamiwa na kuuzwa ovyo ovyo kama vile tumetamani kiama. Panapotakiwa eneo la kujenga au kuanzisha mradi wa kijamii panakuwa hakuna eneo, wakati huo huo maeneo hayo yanamilikiwa kinyemela na watu wasioidhinishwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji.

Wananchi waelimishwe juu ya haki zao kuhusu umiliki wa ardhi na mamlaka yao katika ardhi, kisheria.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Pongezi kwa Mheshimiwa Waziri Chiligati, pamoja na Watendaji wote wa Wizara, kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kusimamia masuala ya ardhi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Wataalam wa Ardhi kwenye Wilaya zetu bado ni wachache sana, hawaendani na mahitaji tuliyonayo. Pamoja na uchache huo wa Watumishi, pia hakuna vifaa vya kupimia ardhi kwenye Wilaya.

Mheshimiwa Spika, ardhi ni rasilimali ya pekee, ambayo maisha ya Watanzania wote wanaitegemea kwa kila kitu. Hili ni jambo la kusikitisha kwamba, katika Halmashauri zetu Sekta/Idara hii ya Ardhi iliyobeba misitu, wanyamapori, samaki na kadhalika, haipewi ruzuku kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha Serikali kuacha Idara hii muhimu kuendeshwa na fedha zitokanazo na makusanyo ya Halmashauri ni kuendelea kuidumaza Sekta hii.

Halmashauri mapato yake ni madogo na hivyo kutotoa umuhimu kutenga fedha za kutosha kwenye Sekta hii. Utendaji katika upande wa ardhi ni dhaifu sana na ndiyo maana migogoro haipungui vijijini.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ardhi 1999, inatamka ardhi ni mali ya Wananchi na Rais amepewa dhamana ya kuisimamia. Mwananchi Mtanzania ndiye mwenye fursa ya kumiliki ardhi na kupanga matumizi ya ardhi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatakiwa kuwa makini sana na wawekezaji wanaokuja kwa kofia ya kuendesha kilimo cha mibono na mazao mengine. Tusije wahamisha wananchi kwenye ardhi yao na tukawamilikisha wawekezaji, hali inayopelekea wananchi kuishi maisha duni na huku wawekezaji wakijineemesha.

Mheshimiwa Spika, mwekezaji wa Mashamba ya Mpunga Mbarali ameshindwa kuendesha kilimo alichotakiwa na sasa amefanya eneo hilo ni kituo cha kukusanyia mpunga, anaonunua kutoka kwa wakulima wadogo wadogo. Eneo la shamba hilo, ambalo vijana wazalendo walilima miaka yote na kuzalisha sana, leo limekaa bure kwa kumpa mwekezaji feki.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu iko nyuma sana kwenye mipango ya matumizi ya ardhi. Hali hii inatia aibu Taifa na kuleta adha kubwa kwa wananchi. Kitendo cha Serikali kusubiri wananchi wajenge nyumba maeneno ambayo hayastahili au ni *mad reserve*, halafu waje wavunje haki na tija kwa Taifa na ni kuonesha udhaifu wa utendaji mipango ya Serikali itangulie mipango ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, tatizo la wafugaji kuhama hama ni tatizo kubwa na ni uharibifu mkubwa kwa mazingira. Serikali ihakikishe wafugaji wanatengewa maeneo ya kutosha kufugia na pia wahamasishwe kufuga kitaalam, kulingana na rasilimali ardhi iliyopo. Tuendako suala hili linaweza kusababisha amani kupotea, kwani wafugaji wanaona wanaonewa, hawathaminiwi na wakulima, pia wanaona wanaharibiwa mashamba yao.

Mheshimiwa Spika, Nyumba za Shirika la Nyumba zinazojengwa na kuuzwa ni ghali sana kwa hali ya Watanzania, labda mafisadi nchini wanaweza kununua nyumba

kwa Tsh. Milioni 60 – 110; ni nyingi sana kumudu. Kama lengo ni kusaidia wananchi wa kawaida kupata nyumba bora, dhamira hiyo ionekane wazi. Basi hata gharama zake zitakuwa zinawapa fursa hiyo ya kumiliki.

Mheshimiwa Spika, wapo wananchi waliopanga Nyumba za NHC kwa muda wa miaka mingi; cha kusikitisha wakati wa nyumba hizi kuuzwa, hawa wananchi hawaangaliwi kwanza/kupewa kipaumbele. Malalamiko ni mengi kwa wananchi hawa kwamba, kwa sababu ya rushwa, watumishi wa NHC wanawaleta ndugu zao, rafiki zao na watu wenye uwezo, wanawapa nyumba hizi kwa muda mfupi Shirika linatangaza kwamba nyumba inauzwa. Kwa hiyo, anayeuziwa ni yule aliyeingia kama mpangaji wa muda mfupi na siyo mpangaji wa miaka mingi, aliyeondolewa kwa vigezo vya kodi.

Shirika hili linatakiwa lisaidie kuboresha maisha ya Watanzia kwa kupata makazi mazuri na kwa gharama nafuu na siyo kujali wenye pesa tu. Hili ni Shirika la Umma.

Mheshimiwa Spika, chonde chonde, ardhi ya Watanzania isiingizwe kwenye Shirikisho la Nchi za Afrika.

**MHE. ELIETTA N. SWITI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Waziri wa Ardhi, Naibu Waziri na Wafanyakazi wa Wizara ya Ardhi, kwa kufanya kazi bila kuchoka, licha ya uchache wa Wafanyakazi katika Wizara hiyo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kazi kubwa ya upimaji ardhi na uharaka wenyewe wa shughuli hiyo, iko haja kwa Serikali kuongeza Bajeti ya Wizara hii ili upimaji ardhi uende kwa kasi na kupunguza migogoro kati ya wakulima/wafugaji au na wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji katika maeneo ya vijiji ni kero kubwa; kwa nini wawekezaji wasipewe maeneno yaliyo mbali na vijiji? Hapa natoa mfano wa Shamba la Molo Manispaa ya Sumbawanga, ambapo Mwekezaji Ephata Ministry, ameomba kuwekeza katika Shamba la Mifugo lililokuwa likimilikwa na Serikali; badala ya kufuga analima. Tena ameamua kufunga njia za kienyeji alizozikuta na mwananchi akipita pale anapigwa vibaya. Haya manyanyaso yataisha lini? Wakulima hawa wa Molo wanazaa na wamejenga shule na dispensary kwa matumizi ya jamii yao. Uwekezaji wa namna hii ni uonevu. Naomba Serikali iangalie upya uwekezaji huu.

Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Fyengelezya, Manispaa ya Sumbawanga, nacho kina mgogoro wa Ardhi ya Kijiji hicho, ambapo mwekezaji anazidi kupanua mipaka yake. Ushauri wangu ni kwamba, Serikali ichukue hatua katika Kijiji hicho cha Fyengelezya ili kuepusha mauaji. Hali ya pale ni mbaya. Wananchi wamewahi kupigwa mabomu ya machozi na police kwa ajili ya mwekezaji huyo binafsi, lakini wanasema hawaruhusu mipaka kuongezwa kiholela eti atakufa mtu. Kwa nini Serikali imekaa kimya? Hili suala ni la muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, migogoro yote ingekwisha kama Watumishi wa Ardhi wangefuata sheria na miongozo ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, msongamano wa nyumba mijini ni kero na siyo salama kwa miji yetu hususan Dar es Salaam na miji mikubwa nchini. Nyumba chakavu ni nyingi mno, ndiyo maana likitokea janga kama la mabomu Mbagala, Serikali inajikuta eti inadiwa kulipa nyumba chakavu! Kwa nini Serikali isihimize zaidi ujenzi wa nyumba bora hasa mijini (Planning)?

Mheshimiwa Spika, viwanja pia vinapangwa vibaya na mara nyingi barabara ziko karibu mno na nyumba.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, natoa shukrani kwa Wizara, kwa kushugulikia suala la nyumba ya Bint Mzee wa Manzese, yenye kugawanya namba A na B. Pamoja na kwamba, halijaisha ninaamini watalimaliza na haki itatendeka.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na desturi ya kuchukua ardhi zenye hati za kimila kwa kusudi la kuendeleza jambo fulani la Serikali, hili ni jambo zuri na wananchi kwa hiari yao hutoa maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, migogoro huanza pale tu baada ya kufanya tathmini kwa kusudi la kuwalipa wenye maeneo hayo na wasiwalipe. Fidia huchukua miaka na hata fidia hiyo vilevile huwa haifanani na ardhi hiyo na hata vilivyomo ndani ya ardhi hiyo.

Mheshimiwa Spika, malalamiko haya yako kila Mkoa, Wilaya na hata Vijiji.

Mheshimiwa Spika, ninao mfano hai wa Wananchi wa Wilaya ya Kilwa, katika Kijiji cha Mnazimmoja, ambako wananchi wana miaka kadhaa, wakiwa wametoa ardhi hii kwa Serikali na hadi leo hawajalipwa.

Cha kusikitisha ni kwamba, hata maeneo hayo hawawezi kuyatumia na hayajaendelezwa kwa lolote. Sana sana, hugawa viwanja vya kujengea nyumba kinyemela (kisirisiri). Naiomba Wizara, iiangalie Wilaya ya Kilwa kuhusu ardhi isije ikaleta migogoro ambayo haijawahi kutokea.

Mheshimiwa Spika, ombi maalum kwa Wizara; angalieni sana Halmashauri zetu za Wilaya katika Kitengo cha Ardhi. Kuwepo na Mkakati Maalum wa kuzikagua idara hizi ili kuona nini kinatendeka na kama utaratibu unafuatwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. SAMSON F. MPANDA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja. Ila yafuatayo napendekeza yangeongezwa ili kuboresha Wizara:-

Nyumba zilizopo Kigamboni (licha ya viwanja elfu ishirini), hadi leo hazijapata hati ya umiliki wa nyumba zao, licha ya kwamba, Mheshimiwa Rais alitegua kitendawili cha kuwa Kigamboni imeuzwa. Sasa Serikali ina mpango gani wa haraka ili kuwapatia hati wale wenye nyumba pale Kigamboni?

Kwa kuwa NHC wameshavunja nyumba walizozihitaji katika Mtaa wa Vijibweni Upanga lakini Block 293 halijavunjwa. Kwa bahati nzuri na mimi kama mlemavu, nimefanya ukarabati wa hali ya juu. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kuwahamasisha NHC ili niweze kununua *apartment* ile? Akumbuke kwa sasa mimi ni mpangaji wa nyumba ile.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Spika, Shirika la Nyumba la Taifa, kuanzishwa kwake kulikuwa na lengo la kuwasaidia wenye vipato vya chini wawe na makazi bora; lakini Shirika hili limepoteza mwelekeo, wanaopanga katika nyumba hizi ni wenye vipato vikubwa na wanaonunua nyumba hizi ni wenye vipato vikubwa.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu nyumba zilizopo mathalani maeneo ya mijini kama Dar es Salaam, maeneo ya Upanga na katikati ya Jiji, idadi ya wenye vipato vikubwa wanaokaa katika nyumba hizo ni kubwa zaidi ya wale wenye vipato vidogo wanaokaa katika nyumba hizo. Inawezekana hali hiyo imetokana na makosa yaliyofanywa huko nyuma na Wafanyakazi wasio waaminifu wa Shirika la Nyumba la Taifa.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa nyumba zilizoko katika baadhi ya maeneo, NHC wameamua kuingia ubia. Ubia huu hauwezi kumridhisha mtu maskini na wala hauko kwa manufaa ya wenye vipato vya chini. Sasa kwa nini Serikali kupitia NHC haijengi nyumba nzuri za gharama nafuu katika maeneo mazuri ili kuziuza kwa bei ya chini kwa wananchi wenye vipato vidogo?

NHC iwe na utaratibu wa kujenga nyumba za gharama nafuu ili kuendeleza dhana nzima ya uanzishaji wa shirika hilo.

Mheshimiwa Spika, nyumba zilizoko Arusha ambazo zimejengwa hivi karibuni zitauzwa? Naomba nyumba hizo ziuzwe kulingana na mshahara wa mwananchi wa kawaida.

NHC iwe na utaratibu wa kuangalia na kufanya tathmini ya kina kuona kama inawalenga watu wa kipato cha chini; je, hata wakiamua kukopa wataweza kununua nyumba hizo?

Mfano, kama mtu mwenye mshahara wa Sh. 300,000 ana uwezo wa kukopa Sh. 20,000,000; ni kwa vipi mtu wa kiwango hicho ataweza kununua nyumba hizo ambazo nyingi bei yake ni Shilingi milioni 50 ambayo mtu wa kipato cha chini hawezi kumudu?

Mheshimiwa Spika, Serikali iliangalie suala hilo kitaalam.

**MHE. GAUDENTIA MUGOSI KABAKA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja 100%.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Chiligati kwa kumudu vema kazi za uongozi wa Wizara hii nyeti. Nampongeza pia mama Salome Sijaona, kwa uzoefu na umakini wake mkubwa kwenye Wizara hii. Lakini nawapongeza Wakurugenzi na Watendaji wote wa Wizara kwa uaminifu wao kazini. Salaam za pekee ni kwa mama Bura, Mkurugenzi wa Mipango Miji, kwa utayari wa kusikiliza wateja na kuwahudumia kila wanapomwendea. Namwomba sana aendelee na juhudi za kutusaidia suala la Sirari kabla hali haijawa ngumu sana kwani watu wanaendelea kujenga holela holela, naamini atajitahidi kadri awezavyo.

Mheshimiwa Spika, katika kufikia Mkoa wa Mara kwenye mpango mzima wa kupima mipaka ya vijiji, nashauri na naomba sana Wizara ianzie Wilaya ya Tarime ambako ardhi ni *`issue'*. Pamoja na mambo mengine ndiyo inayochangia mapigano ya koo, wakigombea ardhi ambayo ina rutuba nzuri lakini ni ndogo kwa idadi ya watu walioko. Wananchi hawa wakipimiwa (si vijiji tu) ardhi na kupewa Hati Miliki wanavyostahili, naamini hakutakuwa na ugomvi tena kuhusu ardhi. Hivyo nawasihi sana hili lifanyike mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, mtakumbuka vijiji vya Remagwe na Ngerengere, Wilayani Tarime, vimekuwa ni chanzo kikubwa cha mgogoro kati ya koo za Wakira na Wanchari/Warenchoka kwa muda mrefu huko nyuma. Aliyekuwa Waziri Mkuu huko nyuma, aliamua eneo hili Serikali ilichukue na kupewa JKT/Magereza etc. Hata hivyo, nashauri kuwa kwa kuwa hili agizo halijatekelezwa, ni vema likapimwa na kumilikishwa wananchi wa vijiji hivyo. Hii ni kutokana na ukweli kwamba ardhi haitoshi na kuichukua maana yake wananchi watakosa au kupungukiwa eneo muhimu la kilimo hasa kwa muda huu ambao Serikali imetangaza kauli mbiu ya `Kilimo Kwanza'. Nina hakika vijiji vikipimwa na ardhi hii ikipimwa na kumilikishwa kimila au vinginevyo kwa wananchi, itamaliza mgogoro wote uliokuwapo. Ukweli ni kwamba wananchi wanahitaji sana ardhi hiyo, ahsante sana.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mungu kwa ulinzi wake. Nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu, Makamishna na Watendaji wote, kwa kuandaa bajeti baadaye kusomwa Bungeni.

Mchango wangu uko maeneo machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu utoaji wa Vyeti vya Vijiji. Naishukuru Serikali kupima takribani vijiji 108 Wilayani Bukombe. Naomba Serikali inipe ufafanuzi, ni lini vijiji hivi vitapewa cheti ili wananchi wapate Hati Miliki za Kimila? Hivi Serikali inaona vizuri kuwacheleweshea kupata Hati Miliki? Kuondoa umaskini ni vigumu sana.

Mheshimiwa Spika, matumizi mazuri ya ardhi, naomba Serikali mfuatilie ili wafugaji wa Bukombe wajue maeneo yao ya kufugia ni yapi. Mheshimiwa Waziri, naomba aniambie ni maeneo yapi yametengwa kwa ajili ya wafugaji wa Bukombe?

Mheshimiwa Spika, malalamiko ya wananchi, naomba Serikali itusaidie kujua msimamo wa Serikali na haki ya wananchi wa maeneo yafuatayo yaliyotaifishwa, Butambala, Kalente na Maganzo. Maeneo haya wananchi wanahangaika sana kutafuta haki yao. Wananchi hawa wameteseka sana, ni vizuri tujue hatima yao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante.

**MHE. JOYCE N. MACHIMU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata fursa hii ili nami niweze kusema machache kuhusu Wizara hii nyeti ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hapo nyuma kuna watu au wananchi ambao walipatiwa viwanja kwa ajili ya makazi, biashara na kadhalika lakini kutokana na hali halisi ya uchumi duni uliopo, wamechelewa kuviendeleza kwa kukosa fedha kutokana na riba kubwa za mabenki yetu na kwa kuwa hakukuwa na sheria zinazoweka mazingira mazuri ya kupata mikopo ya ujenzi, je, Serikali au Wizara hii, haioni sasa ni vyema kusitisha zoezi lililokuwepo la kubatilisha umiliki na utwaaji wa viwanja vya watu ambao watakuwa hawakutendewa haki kwani hawakuwa na namna ya kupata fedha za kujengea vyumba na badala yake zoezi hilo lianzie sasa baada ya Sheria mbili zilizopitishwa na Bunge lako Tukufu zinazoweka mazingira mazuri ya fedha kwa maana ya kwamba badala ya miaka mitatu ya nyumba, sasa zoezi hilo lianze mwaka 2009/2010, 2010/2011, 2011/2012 na kuendelea? Wakati huo huo Serikali iharakishe kuleta chombo kitakachotoa mitaji ya ujenzi wa nyumba kupitia mabenki itakayoyateua kusaidia wananchi wetu ili waweze kukopa na kuviendeleza viwanja vyao. Naomba jambo hili litolewe kauli na ufafanuzi wakati Waziri atakapokuwa anahitimisha hoja ya Wizara hii ili wananchi waweze kuchangamkia fursa hiyo na pia kupata faraja kutoka kwa Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu ardhi ya wafugaji, naomba Wizara hii iseme bayana kwa kushirikiana na Wizara ya Mifugo, Maji, TAMISEMI, Kilimo na kadhalika kwamba itaongeza na kutenga maeneo kwa ajili ya wafugaji ili kuwaweka katika mazingira mazuri na kujisikia kama nao ni Watanzania kwani wamesumbuka muda mrefu sasa na hata kusababisha maafa kati yao na wakulima kitu ambacho si chema sana katika jamii yetu. Naomba Serikali kupitia Wizara hii iseme kitu kuhusu suala hili ili litatulike mapema.

Mheshimiwa Spika, mwisho, Serikali ijipange vizuri kuwa na utaratibu wa kuweka mipango miji mapema kwa miji inayochipuka ili kuepusha zoezi la ubomoaji wa makazi baada ya miji kujengwa ovyo ovyo. Serikali ifanye hivyo mapema kwani hata fidia zinazotolewa hazikidhi gharama kulingana na wakati.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, niwasilishe na naomba kuunga mkono hoja, ahsante.

**MHE. BAKARI SHAMIS FAKI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nachukua nafasi hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuwa mzima na kunipa wasaa wa kuweza kuandika maoni yangu japo machache juu ya hotuba ya bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Spika, kama inavyojulikana kwamba katika maisha yake, binadamu yeyote anategemea ardhi katika ustawi wake kwa ujumla sio tu kwamba anaitumia ardhi kwa makazi au kuishi juu yake, bali mwanadamu hupata karibu mahitaji yake yote kutoka ardhini, kutegemea maendeleo yake ya sayansi na teknolojia. Ardhi ni kitu muhimu sana hapa duniani, kwa hiyo, ni lazima pawepo na mipango na mikakati muhimu na mahususi ya matumizi ya ardhi nchini na hasa tukizingatia kwamba sisi tanaotumia ardhi (Watanzania) tunaongezeka kila siku lakini ardhi ni ile ile, haiongezeki.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi hapa nchini inasadikika kwamba wapo baadhi ya wananchi (hasa vijijni) wanauza ardhi kwa wageni kwa kasi kubwa sana kwa kupatiwa pesa ambazo ni chache hazilingani na ardhi wanayoitoa. Ni vizuri Mheshimiwa Waziri alitolee maelezo suala hili wakati wa majumuisho ili wanaofanya ukatili huu dhidi ya Watanzania wenzao wasikie na waache mara moja. Pia Mheshimiwa Waziri alitolea tamko suala hili ili kama wako watu wenye nia ya kuuza ardhi basi wasite mara moja.

Mheshimiwa Spika, namuomba Mheshimiwa Waziri atueleze bayana wakati wa majumuisho hivi Leseni ya Makazi kwa mtu aliyenunua nyumba mbovu, akaivunja na akajenga nyingine mpya kiwanja kile kile itakayotumika ni ile ya nyumba ilivyovunjwa au ni leseni mpya baada ya kujenga nyumba mpya?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nchi yetu mara nyingi huwa inakumbwa na migogoro ya mipaka ama ya ardhi ya kijiji kimoja na kingine au mwana kijiji mmoja na mwingine hali ambayo viongozi wa vijiji kwa kiasi fulani wanachangia kuwepo kwa migogoro hiyo, je, sasa hali kwa ujumla hapa nchini ikoje?

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 19, ameelezea juu ya utwaaji na ubatilishaji milki za ardhi, ameendelea kueleza kwamba mwananchi aliyemilikishwa ardhi na akashindwa kutekeleza masharti ambayo mojawapo ni kulipa kodi ya pango ya ardhi, milki yake hubatilishwa. Sasa kwa sababu wananchi wengi ni maskini sana na baadhi ya misimu wanashindwa kupata mavuno ambayo anaweza kuuza na kupata pesa za kulipia pango kwa ardhi aliyomilikishwa, je, Serikali haioni kwamba huku ni kumdumaza mwananchi kimaendeleo pindi pale anaposhindwa kulipa kodi ya pango na hivyo ardhi ile kumtoka? Je, sasa ni muda gani Serikali italeta hapa Bungeni Sheria hii ili ifanyiwe marekebisho ili kumpa unafuu mwananchi ambaye uwezo wake ni duni?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kuna ushauri wa muda mrefu kwamba sasa umefika wakati Serikali itumie ardhi tuliyo nayo kwa njia ya uchumi zaidi kwa kujenga nyumba za ghorofa kuliko nyumba moja moja kama vile Kisasa. Kwanza nyumba au ujenzi ule haupendezi licha ya kutumia eneo kubwa la ardhi yaani zina mwelekeo wa kuwa kama

Kambi. Je, Serikali inasemaje sasa kuhusu ushauri huu wa aina ya ujenzi wa maghorofa badala ya nyumba moja moja? Ahsante sana.

**MHE. MARIA IBESHI HEWA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja itokanayo na hotuba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Spika, naipongeza hotuba hii ya Serikali iliyotolewa na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa John Zefania Chiligati, ambayo imeonyesha wapi tumeanza kutatua matatizo, tuko wapi na mpango mkakati wa mbele wa kuyatatua matatizo haya.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi Sheria za Ardhi huvunjwa na wananchi kutokana na ukosefu/uduni wa kuijua Sheria ya Ardhi sehemu zote sheria hii inapohitajika. Naishauri Serikali kupitia wataalam na mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali kuweza kutoa elimu hii ya Sheria ya Ardhi na hasa vijijini ambako watu wengi wako na ardhi kubwa iko.

Mheshimiwa Spika, mkakati wa upimaji viwanja, naipongeza Wizara kwa taratibu walizoweka za kuzikopesha Halmashauri kwa upimaji wa viwanja. Tatizo ni Wizara kutokuwa na ufuatiliaji wa urejeshaji wa mikopo hiyo mapema. Nashauri kuwepo na muda wa ukopeshwaji na urejeshaji wa mkopo.

Mheshimiwa Spika, viwanja kupandanishwa *(double allocation)*, pale panapojitokeza tatizo hilo, naishauri Serikali kuwafukuza mara moja wataalam watakaobainika kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, fidia, kama ilivyo kawaida, upimaji wa ardhi huanza ikiwa eneo hilo lina mazao, nyumba na mambo mengine mengi ambayo hudai fidia. Tatizo la Wizara na wataalamu wake ni:-

(a) Kutofidia mali walizozikuta kwa kudai havina thamani;
(b) Kutoa bei ya chini sana bila kujali gharama iliyopo kwa wakati ule;
(c) Kuchambua vya kufidia na vyakutofidia; na
(d) Kuchelewesha fidia nje ya Sheria (Miezi Sita).

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Spika, kabla ya yote, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote, kwa ushirikiano wao wanaouonyesha katika maandalizi ya hotuba hii na pia utekelezaji wake wa 2008/2009, nawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, sababu nilizozitaja hapo juu, zinanifanya niunge mkono 100/100 bali nitatoa ushauri tu baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Spika, suala la mipango miji, ni suala muhimu, hivyo juhudi za upimaji wa viwanja ni jambo muhimu, itasaidia kutokuwa na ujenzi holela ambao ni matumizi mabaya ya ardhi. Serikali iendelee na mpango wake wa *(PDRF) Plot Development Revolving Fund*, pesa nyingi zielekezwe huko ili Wilaya nyingi hapa nchini wanufaike na

mfuko huo. Mimi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Misungwi, naishukuru Serikali kwa kukubali maombi yetu ya mkopo wa *(PDRF)* Tshs.50,000,000/= si haba, niahidi kuwa pesa hizo zitatumika kwa makusudio tuliyoyasema wakati wa maombi.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie Shirika la nyumba la Taifa *(NHC).* Shirika hili, ni muhimu sana kwa Taifa na watu wake. Kama kuna uwezekano wakopeshwe mtaji au wapewe ruksa ya kumogeji (kuweka rehani) nyumba zao ili wapate pesa za kujenga nyumba wao wenyewe badala ya kuingia ubia wakati nyumba tunazo. Mimi sifurahishwi na mpango wa ubia, uwe wa mwisho kwa mikataba iliyoishafanyika na baadaye tujenge wenyewe *(NHC).*

Mheshimiwa Spika, kuhusu ongezeko la kodi ili angalau ziwe karibu na bei ya soko, nawaunga mkono kama kutakuwa na huruma kwa Serikali basi utolewe/watoe ruzuku ambayo haitaliathiri Shirika kiuendeshaji.

Mheshimiwa Spika, utoaji wa vyeti na Hati Miliki Kimila ni jambo ambalo bado halijakaa vizuri. Mfano Misungwi, tuna vijiji 78 lakini ni vijiji 38 tu vimepewa vyeti, je, vingine vitapewa lini? Naomba majibu.

Mheshimiwa Spika, suala la *bulding permit*, ni tatizo hasa kwa wakazi wa Dodoma ambapo pia Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla bado wanaliona ni tatizo kwao. Je, *CDA* wana tatizo gani? Naomba majibu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ni kurudia kupongeza na kutoa wito kwa *NHC* waje Misungwi, wanunue viwanja kwa vile tayari tumepima, tulikuwa tunasubiri mkopo ambao nao tayari tumepewa hivyo bajeti ijayo Misungwi iwe ni moja ya maeneo yatakayojengwa na *NHC*. Kwa vile sehemu zingine wamewekeza na Misungwi waje kwani itasaidia kibiashara kwa vile ni karibu sana na Mwanza na ni mji unaokuwa kwa haraka.

Niungane na Waheshimiwa wenzangu kuwaombea Wizara yetu ipitishiwe bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Waziri, Katibu Mkuu, Makamishna, Wakurugenzi na Watendaji wote wa Wizara, kwa kazi nzuri wanazofanya. Hongereni sana na naomba muendelee na kasi na moyo huo huo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo mazuri yanayofanyika, bado kuna mambo ambayo yanawaumiza sana wananchi wetu. Sheria mpya ya Ardhi bado inatumiwa vibaya na Mahakama zetu hasa Mahakama za Mwanzo na Wilaya. Sheria imeelekeza wazi kwamba matatizo yote yanayohusu migogoro yaende kwenye Mabaraza ya Ardhi Iramba Mashariki. Wananchi wa Mwanga, Hominiki, Kidarafa, Mwangeza na maeneo mengine, wamenyanyaswa sana na Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo Nduguti akishirikiana na Hakimu wa Mahakama ya Wilaya. Naomba sana Serikali iingilie tatizo hili la sivyo wananchi wetu watakosa haki kwenye nchi yao wenyewe.

Mheshimiwa Spika, Mabaraza ya Ardhi huko kwenye Kata, bado wanaochaguliwa hawajui majukumu yao nao bado wanawanyanyasa sana wananchi. Naomba sana ichukuliwe kama jambo la dharura hawa viongozi wa Mabaraza ya Ardhi wapewe elimu ya kutosha waelewe wanatakiwa wafanye nini.

Mheshimiwa Spika, naomba sana nia njema ya kutaka wananchi wapate Hati Miliki za Ardhi za Kimila, iharakishwe na kuenea kote hapa nchini. Nakuomba sana usaidie wananchi wa Iramba Mashariki wapewe ili kuepukana na manyanyaso toka kwa watu wachache wenye fedha.

Mheshimiwa Spika, vijiji vyote Iramba Mashariki vimepimwa cha kusikitisha mpaka leo ramani za vijiji hazijatoka, tunaomba zitolewe haraka kuepusha migogoro.

Mheshimiwa Spika, tunaomba matumizi bora ya ardhi yafuatwe kwa kupima maeneo ya wakulima na wafugaji pia maeneo ya misitu ya asili yapimwe na watu wasiruhusiwe kuingilia na kuharibu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa John Zephania Chiligati, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kwa kazi nzuri katika Wizara hii bila kumsahau Katibu Mkuu, bibi Salome Sijaona na Watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii, kulipongeza Shirika la Nyumba la Taifa, kwa juhudi wanazozifanya kwa kujenga nyumba za kisasa katika nchi yetu. Kwa sasa, Shirika hili limeingia ubia na watu binafsi kujenga nyumba nchini siyo jambo baya. Tatizo langu, ni kwa nini Shirika hili lisiingie ubia na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kujenga nyumba zake? Mifuko hii ni mali ya Serikali, ni mali ya umma na mifuko hiyo hutoa mikopo ya maendeleo kwa taasisi mbalimbali kiasi kwamba *NHC* ingeweza kupata mikopo kutoka katika mifuko hiyo bila shida yoyote. Kwa nini *NHC* iingie ubia na watu binafsi je, wanaweza kueleza faida ya ubia hiyo na hasara ya kutokopa katika vyombo vya umma?

Mheshimiwa Spika, kwa sasa wageni wanaotaka kuwekeza nchini, humilikishwa ardhi kwa ajili ya kuwekeza kwa muda maalum kwa mfano miaka 33, 66, 99 na kadhalika kama ndivyo ilivyo sehemu kubwa ya ardhi ya Tanzania itamilikiwa na wageni kwa kisingizio cha uwekezaji. Wageni wengine wameomba uraia baada ya kupata ardhi kwa kisingizio cha uwekezaji. Nashauri mwekekezaji asimilikishwe ardhi pasipo na ubia na Mtanzanaia na Mtanzania mwenye ubia na Mgeni/Mwekezaji asiruhusiwe kuuza hisa zake kwa mgeni mwekezaji. Tujifunze kutoka kwa nchi za wenzetu.

Mheshimiwa Spika, nasikitishwa na miji yetu kutokuwa na Mipango Miji *(Master Plan)*. Wananchi wanapoanza kujenga holela, Serikali inaona na inanyamaza kimya pasipo kuzuia. Hivi kuwakataza wananchi kujenga kwenye maeneo yasiyopimwa

kunahitaji pesa?  Wananchi wakishajenga katika maeneo yasiyopimwa miji ikipangwa nyumba za wananchi huvunjwa, huo ni uonevu! Maafisa Mipango Miji wawajibike ili kuondoa usumbufu kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa wazo la kushirikiana na Wizara ya Fedha na Uchumi na Benki Kuu ya Tanzania, kuwezesha kuanzishwa kwa chombo kitakachotoa mtaji kwa mabenki ili yaweze kutoa mikopo ya muda mrefu.  Hofu yangu, ni mabenki hayo kutumiwa na watu wenye fedha/uwezo kupata mikopo.  Wizara ieleze utaratibu utakaotumika katika kupata mikopo hiyo kwa mabenki hayo ili mwananchi wa kipato cha chini wanufaike.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia na kupata fursa hii kuchangia hoja ya Wizara hii kwa maandishi.

Awali ya yote, nimpe pongezi za dhati Mheshimiwa John Zephania Chiligati (Mb), Waziri mwenye dhamana na Wizara hii ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.  Nichukue nafsi hii pia kumpongeza Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mama Salome Sijaona.  Niwapongeze pia Watendaji wote wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika maendeleo ya makazi.

Mheshimiwa Spika, nianze na kiasi cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya Wizara hii, ni kidogo sana ukilinganisha na mahitaji ya Wizara hii pamoja na taasisi zake.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ufinyu wa bajeti, naomba yafuatayo yatiliwe mkazo ili kuboresha sekta ya ardhi kupitia Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ukubwa wa eneo la nchi yetu na eneo kubwa la ardhi lililopo, hivi ni kwa nini hali ya migogoro ya kugombania ardhi inaongezeka siku hadi siku? Mamlaka zinazosimamia sekta hii ambayo ni mtambuka ni kwa kiwango kipi zinajishughulisha katika kuondoa migogoro hii? Wizara kama Wizara inayo mikakati ipi ya muda mfupi, kati na muda mrefu katika kusimamia kwa ukamilifu Sera ya Ardhi?

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kabisa katika kitu ambacho Mungu ametupa na ni haki ya kila mtu, ardhi ndicho chombo pekee kinachoweza kumuondolea mtu umasikini. Utaondoa umaskini kwa njia zifuatazo; kutumia ardhi kama sehemu ya kibiashara kwa namna tofauti kilimo, ufugaji, madini na namna zingine nyingi zinazoleta mapato kupitia Sekta hii. Kadhalika, unaweza kuitumia ardhi kwa kuthaminisha kupitia hati na kujipatia mikopo kupitia taasisi za kifedha na kumfanya yule mwenye ardhi anufaike na mkopo kwa kufanya biashara nk.

Mheshimiwa Spika, faida hizi haziwezi kuja tu bila kuwa na elimu ya kutosha, mwenye wajibu juu ya hili ni Serikali na mamlaka za chini yake zinazoshughulikia tatizo au masuala haya ya ardhi. Ni vema kama Wizara itachukua hatua mahususi kujenga

mtandao na Wizara/Taasisi zozote zile zinazoshirikiana kwa masuala mazima ya ardhi. Kufanya hivyo, kutalinda na kutoa miongozo kwa wadau wote wa ardhi na kuondoa migongano iliyopo hivi sasa kuhusu ardhi. Kutatoa elimu kwa watumiaji ili kufahamu njia bora ya matumizi ya ardhi katika kujiletea mapato.

Mheshimiwa Spika, nashauri nguvu kubwa ielekezwe vijijini ambako ndiko maeneo makubwa yapo na wananchi wengi wanahitaji kupata uelewa juu ya matumizi ya ardhi ili kuondoa umasikini. Aidha, uvamizi au migogoro ya wakulima na wafugaji mikakati ya kukomesha iwekwe bayana.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimwa Waziri wakati akihitimisha, atolee ufafanuzi wa kina juu ya mamlaka na nguvu unazopewa kupitia Sheria ya Ardhi ya Vijiji, Na.5 ya mwaka 1999. Ni dhahiri Sheria hii bado haieleweki vizuri kwa Halmashauri za Vijiji hasa kuingiliwa kimaamuzi na baadhi ya mamlaka zilizo juu yake. Hivyo kujikuta kukosa maamuzi kabisa juu ya udhibiti wa matumizi ya ardhi vijijini jambo ambalo mara nyingi sasa linazua migogoro mingi.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri atoe maelezo ni kwa nini zoezi la upimaji ardhi na utayarishaji wa ramani, ni tatizo kubwa? Kwa nini kuwe na maelezo kwamba maandalizi ya upimaji yanaandaliwa kila mwaka? Tatizo hili ni sugu na sasa linaonekana kupewa vikwazo na baadhi ya Watendaji, ndani ya Wizara hadi Wilayani. Naomba Waziri awe makini na Watendaji wa aina hii aidha urasimu usio na maana sasa ukomeshwe ili watu wapimiwe ardhi na baadaye wamilikishwe ardhi tayari kwa hatua za kujiondolea umaskini.

Mheshimiwa Spika, kupitia nafasi hii, naomba Wizara iongezee Watendaji katika Halmashauri ya Wilaya ya Iramba, Idara ya Ardhi tayari kwa upimaji wa maeneo ya kiomboi, Shelui, Misigiri, Kinampanda, Ndago na kadhalika. Pia vifaa vya upimaji zikiwemo pikipiki na kadhalika vitolewe.

Mheshimiwa Spika, nirejee suala la mwaka 2007/2008, nililowahi kulisemea katika Bunge kuhusu uanzishwaji wa Baraza la Ardhi na Nyumba, Wilaya ya Iramba na Waziri kwa wakati huo alitoa majibu kwamba Serikali ingelitia mkazo. Hatua hii haijatekelezeka hadi sasa.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa utoaji Hati za kumiliki ardhi kimila, haujafahamika kwa wananchi. Wizara itoe machapisho ili kuelimisha zaidi wananchi. Naomba utoaji wa hati hizi pia Wilaya ya Iramba iingizwe katika mpango wa mwaka huu wa fedha. Naomba pia Wizara ipime mashamba ya wakulima wa jimbo la Iramba Magharibi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mheshimiwa Spika, mimi naomba nianze kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam wote wa Wizara ya Ardhi. Nianze pia kwa kusema ninaunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, naanza na hoja ya migogoro ya ardhi itokanayo na kugombea ardhi kati ya wakulima na wafugaji. Tatizo linatokana na mambo mawili yafuatayo:-

(a) Wizara imechelewa kuwapimia watu mipaka ya vijiji vyao;
(b) Vijiji kukosa kuwa na mpango wa matumizi ya ardhi zao. Kama mpango wa kutenga matumizi ya ardhi yao ya kijiji ungekuwepo, ugomvi huu wa wafugaji na wakulima usingetokea.

Mheshimiwa Spika, ni bahati mbaya kwamba miji yetu mingi haikupimwa na hivyo haina mipango miji. Serikali imechangia sana katika migogoro ya ardhi. Kwa kuchelewa kupima ardhi na kutoa Hati za Kimila kama ardhi yetu hasa katika maeneo ya vijiji, zikipimwa basi ugomvi wa ardhi ungekwisha ama kupungua sana.

Mheshimiwa Spika, katika Morogoro Kusini, kuna tatizo la Shamba la Ushirika la Duthumi ambalo wameliacha miaka mingi. Wananchi wakitaka kulima wanaambiwa wanavamia ardhi. Wafugaji wameingia hapa kwa ruhusa ya kijiji cha Mbwade. Wafugaji hawa nao wanafukuzwa wakiambiwa wanavamia. Hata hivyo ardhi ipo pale haina mwenyewe. Wizara isaidie suala hili.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara, kwa kazi nzuri sana wanayoifanya. Pamoja na pongezi hizo, mie leo ninalo jambo moja tu nalo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tatizo la Mpima Ardhi Wilayani Karagwe. Wilaya ya Karagwe kwa miaka mingi sasa haina Mpima Ardhi. Mambo mengine yamekwama sasa, tunaomba Afisa Mpima Ardhi Wilayani Karagwe, ili apime ardhi za Serikali, viwanja na mashamba ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, tatizo la magari/usafiri, Mahakama ya Ardhi ya Wilaya/Mkoa. Tafadhali sana, tunaomba Serikali iipatie usafiri Mahakama ya Ardhi na Baraza la Nyumba Wilaya ya Karagwe na hata pale Mkoani Kagera. Mkoa wa Kagera na Wilaya zake, ni kubwa sana hivyo zinahitaji usafiri wa uhakika.

Mheshimiwa Spika, mwisho naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Waziri, Katibu Mkuu, Mwenyekiti, Wakurugenzi Wakuu wa Idara na Wafanyakazi wake wote wa Wizara hii. Mheshimiwa Waziri na timu yake wameonyesha uzalendo, umahiri na utendaji wa hali ya juu katika kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, napenda kutamka kuwa naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa ushauri katika maeneo yafuatayo katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, lengo ni kuboresha.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 44, kifungu cha 61, mipango ya matumizi ya ardhi ya Wilaya na Vijiji. Nashauri pamoja na kazi nzuri iliyofanywa na Tume ya Taifa, nashauri kuwa, Tume katika mwaka 2009/2010, inapotayarisha mipango ya matumizi Mkoani Mara, Wilaya mpya ya Rorya ipewe kipaumbele kwa kuwa Wilaya hiyo inayo upungufu mkubwa wa wataalamu. Naomba mafunzo ya dharura kwa watendaji wa Wilaya, Kata na Vijiji pia yapewe kipaumbele, naomba ukubali.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 50-52, *NHDRA*, Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi. Nashauri mafunzo kwa vitendo na ushauri kwa wateja kuhusu uzalishaji wa vifaa vya ujenzi utolewe. Wakala ishirikiane na Tume ya Taifa ya Mpango wa Matumizi, aidha katika kutoa semina/mafunzo ili kupunguza matumizi. Naomba Wakala wafanye utafiti Wilaya mpya Rorya.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, narudia kutamka kuwa naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. IDRIS ALI MTULIA:** Mheshimiwa Spika, natoa pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara nzima kwa kutuletea hotuba hii nzuri.

Mheshimiwa Spika, ukurasa 44, kifungu cha 60, mipango ya matumizi bora ya ardhi, Wizara iharakishe kuigawa nchi yetu. Kwanza, ardhi yenye rutuba na maji mengi kama ardhi ya Bonde la Mto Rufiji *(Rufiji Flood Plains)* ibakie kuwa ya ardhi ya kilimo cha nafaka na mazao mengine mengine. Ndio maana Wakoloni waliacha Maasailand *(grassland au the Maasai Steppes), the Sukumaland and central province* kutumiwa na mifugo. Pili, tuweke sehemu ya ardhi kama nilivyotaja hapo juu – Masai, Sukuma na *Central* Tanzania, ziwe kwa ajili ya ufugaji tu.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa mpango wa kuigeuza nchi nzima kuwa malisho ya mifugo, ni mpango mbovu sana na wala hauna tija kwa taifa letu. Wafugaji wanaachia mifugo yao na kulisha katika mashamba ya wakulima, mazao yote yanaliwa.

Mheshimiwa Spika, kule Rufiji ng’ombe wameingizwa katika *Flood plains* ya bonde la mto Rufiji. Mapigano kati ya wafugaji na wakulima, watu zaidi ya watano wameuawa na kuumizwa, ardhi yenye rutuba ya Bonde la Mto Rufiji inaharibika kabisa. Naomba ng’ombe waondolewe toka *food plains* za mto Rufiji inabeba kilimo cha nafaka na mazao ya biashara. Ng’ombe hao wapelekwe sehemu ya juu (kame) ya Rufiji na huko wajengewe malambo na majosho.

Mheshimiwa Spika, migogoro ya mipaka Wilaya ya Rufiji. Tunapongeza kazi nzuri ya upimaji wa vijiji vyetu lakini kuna kero ya mipaka kijiji cha Ikwiriri na Nyamwage, Kijiji cha Ikwiriri (Mgomba) na kijiji cha Mburiju (Mbambe darajani) na Kijiji cha Mbunju (Mbambe) na kijiji cha Ruwe. Tunaomba marekebisho ya mipaka hiyo.

Mheshimiwa Spika, Maafisa Ardhi Wilaya wateuliwe moja kwa moja toka Wizarani. Aidha, wasikae sana katika Wilaya moja, isizidi miaka mitatu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, tunaomba utekelezaji wa bajeti hii ili fedha hizi tupate *"Value for money"*.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana.

**MHE. WILSON M. MASILINGI:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuunga mkono hoja na kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Katibu Mkuu na Kamishna wa Ardhi na Wasaidizi wao kwa uadilifu wao na kazi nzuri sana. Pongezi hizi nazitoa pia kwa niaba ya wananchi wa Muleba Kusini, hususani Kata ya Nshamba, Kijiji cha Bunyagongo. Mwongozo wa Mheshimiwa Waziri wa Ardhi ulisaidia sana kuepusha uvunjifu wa amani kijijini kwa sababu ulizingatia sheria na haki, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali iangalie upya utaratibu wa kutumia Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji na Kata kufanya kazi ya Mahakama. Nia ilikuwa njema lakini matatizo ya fedha, elimu ya kutosha na maadili pungufu kwa wengi wa wajumbe, yamegeuza Mabaraza kuwa kero kubwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Mahakama za Mwanzo sasa zitaongezewa Mahakimu wenye Shahada ya Sheria, ni wakati muafaka kufuta Mabaraza haya na Ardhi. Ni aibu haki za wananchi kuvurugwa wakati wanasheria wako mitaani wanatafuta kazi! Tubadili Sheria ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nashauri Serikali ipitie upya mgawanyo wa ardhi. Watu wachache kupewa maelfu ya ekari za ardhi, ni kuiweka nchi yetu kwenye hatari. Watanzania wanaogezeka lakini ardhi haiongezeki.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARGRETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri John Chiligati, Katibu Mkuu, Wakurugenzi wa Idara na Taasisi zilizomo ndani ya Wizara hii kwa kutuletea hotuba nzuri inayoeleweka. Mchango wangu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tatizo la hati pandikizi kwa viwanja hapa nchini bado linaendelea, kwa sababu ya hatua na mlolongo wa jinsi ya kuwashughulikia watendaji wanaoendeleza tatizo kama hili ni mrefu mno hata pale ambapo ushahidi wa kesi uko wazi. Kwa mtindo huu, wananchi wanaendelea kunyanyasika hasa wale wenye kipato cha chini kwa sababu ndiyo hatimaye wanaosalimu amri katika migorogoro ya *"double allocation"*.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa kuongeza kasi wa upimaji ardhi ya vijiji. Nimefurahishwa na jitihada za Wizara katika hili lakini kasi iliyoahidiwa utafikiwaje

ikizingatiwa kwamba wataalam bado ni wachache, vifaa pungufu na hata rasilimali fedha bado ni tatizo kwa sababu fedha zinazoidhinishwa si kiasi chote kinapatikana kwa matumizi yaliyopangwa! Hata kama madaraka haya yakikasimiwa na Halmashauri zetu lakini ifahamike kuwa si mamlaka nyingi zina uwezo wa kifedha. Hivyo katika hili, Wizara/Serikali Kuu itatoa ruzuku? Naomba ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana kwa kuingilia kati upandaji wa pango la nyumba za Shirika la Nyumba la Taifa. Hapa Wizara imeonyesha kasi ya dhati katika kutatua kero za wapangaji/wananchi. Nashauri ni vema kabla ya kubadili pango pawe na vikao vya majadiliano kati ya wapangaji na Shirika kwa niaba ya Serikali ili kuepusha migogoro isiyo ya lazima.

Mheshimiwa Spika, ingawa katika bajeti ya mwaka 2008/2009, tulielezwa kuwa upatikanaji wa Hati Miliki sasa utaboreshwa lakini mpaka sasa si rahisi kupata Hati hizo kwa muda ule ulioahidiwa. Bado nenda rudi, nenda rudi zinaendelea hivyo kuwafanya wananchi walio wengi kushindwa kuhimili hizo njoo kesho, njoo kesho.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kuwa na mpango kabambe wa kuboresha miji nchini. Hii itasaidia miji yetu angalau ifananefanane na miji ya nchi zingine kwa kupangwa vizuri, kuwa na mazingira safi na kupendezesha macho ya wananchi. Hata hivyo, elimu iongezwe ili wananchi katika miji/maeneo husika nao waeleweshwe wajibu wao katika mpango huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huu, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge. Kwenye Wizara hii, mjadala ni siku moja na kuhitimisha, kwa hiyo, inakuwa vigumu kuwafikia wote. Kwa hiyo, hapo ndiyo mwisho wa mchango kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge na kwa utaratibu wetu, sasa kwa ajili ya mtoa hoja tunazo dakika thelathini ukiondoa ule muda wa kuwataja Wabunge, kwa hiyo, ni kiasi kama dakika arobaini hivi. Muda wote wa kuwataja Wabunge tunauondoa ili awe na dakika thelathini kamili za mchango. Kwa maelezo hayo, sasa namwita mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuhitimisha hoja niliyoitoa leo asubuhi.

Napenda kutoa shukrani kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia na hata ambao hawakuchangia kwa sababu wote lengo letu ni moja kuwahudumia Watanzania. Nawashukuru zaidi wale waliochangia ama kwa maandishi ama kwa kusema ndani ya Bunge, wametoa mawazo mazuri, ushauri mzuri na napenda kuwahakikishia kwamba ushauri tumeuzingatia, wala msiwe na wasiwasi. Shemeji Beatrice Shellukindo, alikuwa na wasiwasi kwamba waliotukosoa labda tutanuna hapana, hata kidogo! Wote waliotukosoa ama kwa sauti ya chini ama kwa sauti ya juu tunapokea zile kosoa zao kwa

sababu ni katika kukosoana ndipo tunaweza kujisahihisha na tukasonga mbele kuwahudumia wananchi wetu. Kwa hiyo, nawashukuru sana kwa kosoa mlizotukosoa, zinatujenga.

Mheshimiwa Spika, sasa baada ya shukrani hizo, kama ilivyo ada, naomba niwatambue wale wote waliochangia hoja hii ya leo kwa kuzungumza ndani ya Bunge wako 12 na wa kwanza ni Mheshimiwa Lucas Lumambo Selelii, kwa niaba ya Kamati ya Ardhi Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa John Mamose Cheyo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Ponsiano Damiano Nyami, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Ephraim Madeje, Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Castor Raphael Ligallama, Mheshimiwa Beatrice Matumbo Shellukindo, Mheshimiwa Felix Christopher Mrema, Mheshimiwa Halima James Mdee, Mheshimiwa Herbert James Mtangi na Mheshimiwa Clemence Beatus Lyamba

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna Waheshimiwa Wabunge 62 wamechangia kwa maandishi, nao ni Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale, Mheshimiwa Dr Rapahel Masunga Chegeni, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Sevelina Mwijage, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Cyril August Chami, Mheshimiwa Shoka, Mheshimiwa Eng. Christopher Kajoro Chiza, Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi, Mheshimiwa Raynald Alfons Mrope, Mheshimiwa Kimaro na Mheshimiwa Daniel Nicodem Nsanzugwanko. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Ania Chaurembo, Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed, Mheshimiwa Khadija Salum Al-Qassmy, Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mheshimiwa Idd Azzan, Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Nuru Bafadhili, Mheshimiwa Dr. Guido Gorogolio Sigonda, Mheshimiwa Zakia Hamdani Meghji, Mheshimiwa Rita Louise Mlaki, Mheshimiwa Benson Mwailugula Mpesya, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, Mheshimiwa Emannuel Jumanne Luhahula, Mheshimiwa Joyce Nhamanilo Machimu, Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Elietta Namdumpe Switi, Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi, Mheshimiwa Castor Ligallama, Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mheshimiwa Mbaruk Kassim Mwandoro, Mheshimiwa Dr. Charles Ogesa Mlingwa na Mheshimiwa Maria Hewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mshemiwa Felister Bura, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda, Mheshimiwa Omari Kwaangw', Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Prof. Philemon Sarungi, Mheshimiwa Prof. Idris Mtulia, Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mheshimiwa Magreth Mkanga, Mheshimiwa Sigfrid Seleman N'gitu, Mheshimiwa Halima Kimbau, Mheshimiwa Hamza Abdallah Mwenegoha, Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mheshimiwa Dorah Mushi, Mheshimiwa Hawa Ghasia na Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nimewasahau wengine bado nafasi ipo mtanikumbusha ili niweze kuwatambua wale wote ambao mmechangia. Labda nianze kwa kujibu hoja zile za jumla kwa sababu hoja za binafsi zipo nyingi sana, ma- *book* yote haya sidhani kwa nusu saa kama nitaweza kutenda haki kuwajibu wote, walau yale ya jumla niweze kuyasema.

Mheshimiwa Spika, kwanza la migogoro ya ardhi. Wabunge wengi wamezungumza habari ya migogoro ya ardhi hapa nchini na mimi nakiri kwamba migogoro ya ardhi ipo na kwamba zipo sababu nyingi ambazo zinasababisha tuwe na migogoro mingi ya ardhi katika sehemu nyingi. Sababu ya msingi, ni kwamba karibu 90% ya ardhi ya Tanzania haijapimwa wala haijamilikishwa, inazagaazagaa tu, kwa hivyo, kunakuwa na migongano mingi ya wanaotaka kuitumia, iko vurumai kubwa kwa sababu haijapimwa na haijamilikishwa.

Mheshimiwa Spika, ziko athari nyingine licha ya kukaribisha migogoro, kwamba kama ardhi haijapimwa na kumilikishwa yule mwenye nayo hawezi kuitumia kwa shughuli za kiuchumi, atalima tu mchicha na maharage atakula lakini aitumie kama dhamana Benki, apate mtaji, afanye mambo makubwa; hawezi mpaka hapo itakapopimwa na kumilikishwa, hii ni dosari kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile Serikali nayo inakosa mapato kwa sababu Serikali haiwezi ikakusanya kodi ya ardhi katika ardhi ambayo haijapimwa wala haijamilikishwa. Kwa hiyo, katika hili ndio chanzo kikubwa cha migogoro mingi na pengine chanzo cha umaskini wa Watanzania. Watanzania wana ardhi lakini bado wanaonekana kama ni maskini; duniani kote mtu ukishakuwa na ardhi, ni *Landlord* wewe ni tajiri. Tanzania tuna ma- *Landloard* maskini na hili nimesema katika hotuba yangu kwamba changamoto kubwa tulionayo ni kuwekeza, kuweka fedha nyingi katika kupima ardhi na kumilikisha ardhi.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi shughuli ambazo zinatakiwa zifanyike na ambazo tunazifanya lakini kwa kasi ndogo, ni hizi za kupima ardhi kwenye Miji na Vijijini. Zoezi hili lina gharama, anayetakiwa kupima ardhi kwenye Miji na kwenye Vijiji, ni Halmashauri za Miji, Wizara yangu kazi yake ni kuweka taratibu au Sheria na Sera, Wizara yangu haiwezi kwenda kupima ardhi kila mahali au kila kijiji, haiwezekani! Ndiyo maana, Sheria imeweka madaraka ya kupima na kumilikisha ardhi chini ya Halmashauri. Kwa hiyo, wito wangu ni kwamba, Halmashauri kila mwaka ziweke fedha na Serikali Kuu vilevile ina wajibu wa kuzisaidia Halmashauri za Wilaya, kuongeza fedha katika kupima na kumilikisha ardhi.

Mheshimiwa Spika, taratibu za kumilikisha, kuna baadhi ya wachangia hoja wanasema taratibu za kumilikisha ni ndefu na zina mlolongo mrefu. Napenda kusema mlolongo wa kumilikisha ardhi umefupishwa sana baada ya kuunda ofisi za Kanda. Sasa hivi Hati inaandaliwa na Halmashauri husika, inatiwa saini kwenye ofisi ya Kanda huko huko Mikoani, hakuna haja ya mtu sasa kutoka Kagera kuja Dar es Salaam, kuja kutafuta Hati Miliki. Kwa hiyo, sisi tumerahisisha taratibu za kutoa Hati, ila kasi ya kupima na

kupitisha ndilo jambo ambalo tunakwenda nalo. Naomba Halmashauri kwa kusaidiana na Serikali Kuu, tuweke hela nyingi zaidi katika hili zoezi la kupima na kumilikisha ardhi.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ambalo tutalishughulikia, ni hili la wataalamu wa kupima ardhi. Kupima ardhi inahitaji utalaam, kama nilivyosema, anayepima ardhi ni Halmashauri, kwa hiyo anayetakiwa kuajiri Wapima Ardhi, ni Halmashauri. Wengine walikuwa wanasema Wizara yangu ina upungufu mkubwa wa watalaam, hapana! Upungufu upo kwenye Halmashauri, ndiko wanakotakiwa waajiriwe wale wapimaji na watalaamu wapo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Faki, alisema tuchukue hata waliostaafu kama wataalamu waliopo ni wachache. Kila mwaka wengi tu wanamaliza kozi pale Chuo Kikuu cha Ardhi, wenye Diploma wanamaliza katika Chuo cha Ardhi Tabora na Chuo cha Ardhi Morogoro lakini hawaajiriwi, anayeajiri ni Halmashauri chini ya TAMISEMI, mimi siwaajiri wale watu, mimi siwafukuzi kazi, lawama zingine mnanilaumu bure tu, Wizara hii haiajiri ni wenzetu wa Halmashauri chini ya TAMISEMI. Ndiyo maana sisi tumetoa ushauri tu kwamba, hebu TAMISEMI, Halmashauri na Ofisi ya Rais Utumishi, wafanye kama walivyofanya kwa Walimu na Madaktari kwamba, hawa wataalamu wa Fani ya Ardhi, wakimaliza masomo kwenye vyuo wapangiwe kazi moja kwa moja, waende kwenye Halmashauri, kwa sababu inafahamika Halmashauri gani ina upungufu wa watu gani na wangapi? Hizo *data* zipo! Naamini kama ushauri wetu ukikubalika, Halmashauri zitajaza ule upungufu haraka ili kazi ya upimaji ipate wataalamu.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo linasababisha mgogoro ni la mpango wa matumizi bora ya ardhi, kwa sababu ardhi ikishapimwa ni lazima sasa ipangwe kuanzia ngazi ya Kijiji, Wilaya mpaka Taifa, kwamba ardhi hii ni kwa ajili ya makazi, hii ni kwa ajili ya mifugo, kilimo, huduma mbalimbali, makaburi, hifadhi tu kwa ajili ya kizazi kijacho, lazima ipangwe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala hili, tunayo Tume ya Mpango wa Matumizi ya Ardhi, ambayo kazi yake ni kuratibu. Tume haiwezi kwenda kupima kila Kijiji, kwani Tanzania ni kubwa sana. Kazi ya Tume, ni kuwezesha tu Halmashauri ili Wilaya zipate utaalamu wa kufanya kazi hiyo. Kwa hiyo, ikienda katika Wilaya fulani inakaa na wataalamu wa Wilaya ile, inafundisha jinsi ya kufanya kazi hiyo, wanafanya kwa majaribio katika vijiji vitatu, vinne, baada ya hapo wanaambiwa sasa endeleeni na wanaunda kitu kinaitwa *District Land Use Planning Team*, hawa wanafundishwa na Tume na ikishamaliza kuwafundisha inaondoka inakwenda katika Wilaya nyingine ili hawa waendelee na kazi.

Mheshimiwa Spika, uzoefu unaonyesha kwamba, hawa hawaendelei na kazi, Tume ikishaondoka na ile kazi inaishia hapo hapo ambapo si sawasawa. Kwa hiyo, naomba kutoa wito kwa Halmashauri zile ambazo tayari zimeshafundishwa jinsi ya kupanga matumizi bora ya ardhi, zianze kupanga, zile ambazo hazijafikiwa, nataka kutoa ahadi kwamba, Tume itafika ili na ninyi mpate mafunzo hayo ili Halmashauri ziendelee kupima zenyewe.

Mheshimiwa Spika, Mabaraza ya Ardhi. Nakubaliana na hoja ya Wabunge kwamba, tuimarishe Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji, Kata hadi Wilaya, ila niseme kwamba, tumegawana madaraka haya. Mabaraza ya Vijiji na Kata, anayeyaunda na kuyahudumia, ni Halmashauri na Wizara yao ni TAMISEMI, ndiye anayewafundisha, kuyaunda na kuyasimamia. Kesi ikitoka kwenye Kata unapokata rufaa inakwenda kwenye Baraza la Wilaya, kwenye Baraza la Wilaya ndipo Wizara yangu inapoanza kuhusika. Kwa hiyo, katika hoja hii TAMISEMI wamesikia na mimi nimesikia, wao watatekeleza wajibu wao kuimarisha na kuelimisha Mabaraza yao ya Vijiji na Kata na mimi haya ya Wilaya vile vile nitajitahidi.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu wa fedha, tumepata magari ambayo nafikiri yatatosha katika Mabaraza yaliyo Makao Makuu ya Mkoa, yote yatapata magari, ili Hakimu awe anatembea kwenda kwenye Wilaya zingine kusikiliza kule kule badala ya wao kumfuata pale Makao Makuu ya Mkoa. Kwa kufanya hivi, nadhani itarahisisha na watu wengi ambao pengine wanashindwa kupata nauli kwenda Mkoani kupeleka kesi, kwa sababu sasa Hakimu atawafuata kwenye Wilaya kule waliko na atafungua *registry* kule. Nina hakika sasa usikilizaji wa kesi utakwenda haraka zaidi.

Mheshimiwa Spika, lakini tunalo deni la kufungua haya Mabaraza katika Wilaya zote. Tumefika Wilaya 39, lengo ni kufikia Wilaya zote, lakini fedha za kufika katika Wilaya zote ndiyo hatuna, ndiyo maana tunakwenda kidogo kidogo na kuimarisha haya yaliyopo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kutoa elimu ya Sheria za Ardhi na Sheria ya Mabaraza, kama nilivyosema awali, Wizara yangu haiwezi kwenda kila kijiji kutoa elimu, kwenda kila Wilaya kutoa elimu, sisi tunawezesha tu Halmashauri ziweze kutoa elimu, tunawezesha kwa kuwapatia nakala za zile Sheria na tumezitafsiri kwa Kiswahili. Mwaka huu wa fedha kama nilivyosema kwenye hotuba yangu, tutatoa nakala elfu kumi (10,000) na kuzisambaza katika Halmashauri mbalimbali ili zitumike kufundisha Mabaraza, Serikali za Vijiji na wananchi kwa ujumla, ili wajue haki zao.

Mheshimiwa Spika, malipo ya fidia. Nimepokea hoja nyingi kuhusu malipo ya fidia kwamba, kuna wengine wanapunjwa na sehemu zingine wanalipa chini ya bei ya soko na kwingine hawalipi kabisa. Nataka kusema kwamba, fidia ina Sheria yake na Wizara tunasimamia hiyo Sheria, lakini walipaji wa hiyo fidia ni yule mtu ambaye amechukua ardhi ama Wizara, ama Shirika la Umma, ama mtu binafsi, amechukua ardhi mahali kwa ajili ya shughuli ya umma, waliokuwa wanamiliki ile ardhi ni lazima walipwe fidia, anayelipa fidia ni yule aliyechukua ile ardhi. Maana wengine walikuwa wanazungumza kana kwamba, sisi Wizara ndio tunaolipa fidia kila mahali, wakisikia *airport* inajengwa kule Songwe Wizara ikalipe, sijui pale Kipawa Wizara ikalipe, hapana! Yule mwenye mradi ndiye anayetakiwa kulipa, sisi Wizara ni kama *referee* kwamba, watendeane haki watu hawa, mlipaji na anayelipwa kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, hivi viwango ni lazima kila wakati viwe vinafuata bei ya soko, ndiyo maana katika hotuba yangu nimesema Mthamini Mkuu wa Serikali, tumempa jukumu la kuhuisha, kwa sababu bei ya soko inabadilika sana baada ya miezi

sita ama mwaka mmoja, kwa hiyo na sisi ni lazima tukimbizane na bei ya soko. Kama bei mwaka jana ilikuwa bei fulani na mwaka huu bati imepanda, unapothamini mabati ya mtu ni lazima uthamini kwa bei ya leo si bei ya mwaka juzi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *National Housing*. Wabunge wengi sana wamezungumzia habari za *National Housing* na wametoa ushauri mwingi. Wengine wamesema tuchunguze kwamba, kuna ubadhirifu, kuna mwenendo wa utendaji ambao hauridhishi, Tume iundwe kuchunguza na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, sina nia ya kutetea utendaji usioridhisha ndani ya shirika hili hata kidogo, lakini ni muhimu tutazame pande zote mbili za shilingi, yaani upande wa udhaifu wa *National Housing* na upande wa kazi au mafanikio ya shirika hili ili tuweke mizania sawasawa.

Mheshimiwa Spika, *National Housing* ilipozaliwa pale mwanzoni tulipopata uhuru, yalizaliwa mashirika mengi, haikuwa *National Housing* peke yake, hayo mashirika pacha ya *National Housing* sote tunajua leo hii yapo wapi, lakini shirika hili bado liko hai na sasa tunapozungumza linajiendesha lenyewe, halipati ruzuku hata kidogo kutoka Serikalini na bado linafanya kazi ambazo zinaonekana. Kuna majengo mapya nimeyasoma kwenye hotuba yangu, nyumba zinakarabatiwa, kwa hiyo, huu ni ukweli ambao hautuwezi kuufumbia macho, Waswahili wanasema, ‘mnyonge mnyongeni lakini haki yake apewe’.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tuhuma za ubadhirifu. Wizara yangu imezipokea na tutazifuatilia kufuatia ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali yaani *Controller and Auditor General* katika ripoti yake ya mwaka wa fedha 2008/2009. Tutafuatilia kulingana na mlivyoshauri Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, sasa niseme mambo ya jumla kuhusu mwelekeo wa *National Housing*. Kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya bajeti, baada ya kutungwa Sheria ya Mikopo ya Nyumba, mwelekeo wa Shirika hili utabadilika kutoka kuwa mpangishaji yaani mtu anapangisha, unakusanya tu kodi kila mwezi, hiyo sasa itakuwa siyo kazi yenyewe itabadilika sasa *National Housing* iwe ni mfanyabiashara wa kujenga nyumba na kuuza nyumba, ndiyo kazi mpya ambayo tunampa. Atakopa benki, atajenga nyumba, atauza na zitakuwa nyumba za aina zote, za ngazi ya chini, nyumba za kati na hali ya juu kulingana na soko. Lakini hasa itazingatia ngazi ya chini, wenye kipato cha chini na wenye kipato cha kati, ndiyo jukumu hasa, tunarudi kwenye jukumu la msingi la *National Housing*.

Mheshimiwa Spika, pili, ili kutimiza azma hii au kupata mwelekeo mpya, sasa hivi Serikali tunatafuta Mkurugenzi Mkuu wa *National Housing* mwenye ujuzi, uzoefu na ari ya kutekeleza jukumu hili jipya ili Watanzania wengi zaidi wanufaike na Shirika hili la *National Housing.* Vilevile tunatazama upya tuwe na Menejimenti na Bodi ambayo ina ujuzi na uzoefu wa biashara ya aina hiyo. Hivyo wananchi watarajie mabadiliko makubwa ambayo yatakuja hivi karibuni katika Shirika hili la *National Housing*.

Mheshimiwa Spika, tatu, kuhusu *National Housing* kujenga nyumba kwa ubia na sekta binafsi. Utaratibu huu sasa umefutwa, *National Housing* watakopa fedha wenyewe katika mabenki na watajenga wenyewe bila kuingia katika ubia, isipokuwa katika ile miradi mikubwa yenye gharama kubwa, hapo tutawapa kibali cha kuingia ubia na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, jambo la nne, kuhusu *National Housing* kujenga nyumba kwa bei kubwa hivyo watu wa kipato cha chini kushindwa kununua. Suala hili ni sahihi, hali hii ilisababishwa na uamuzi wa awali kwamba, ijiendeshe kibiashara, ni kweli ikawa inajenga nyumba kibiashara ni aghali, lakini katika hii *National Housing* mpya tunayoiunda yenye majukumu mapya, jambo hili sasa litazingatiwa na kutakuwa na kitengo mahsusi cha kujenga nyumba za bei nafuu na ili watimize lengo hili Serikali ni lazima tuisaidie *National Housing* kwa namna moja au nyingine, ili kweli nyumba hizo ziweze kuwa za bei nafuu ili na watu wa kipato cha chini waweze kuzinunua.

Mheshimiwa Spika, migogoro ya ardhi kwa wananchi wa Manispaa ya Dodoma na *CDA*. Mbunge wa Jimbo la Dodoma ameeleza kwa uchungu sana malalamiko ya wananchi wa Dodoma, kuhusu kutokulipwa fidia na bomoabomoa ya kila mara na ameshauri Wizara yangu iunde Tume kuchunguza malalamiko haya. Kwanza, nampongeza Mheshimiwa Mbunge Madeje, kwa kueleza kwa ufasaha kilio cha wananchi wa Manispaa ya Dodoma, hata hivyo, kimuundo *CDA* ipo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Waziri Mkuu ndiye Waziri mwenye dhamana ya *CDA*. Kwa hiyo, mimi kuunda Tume kumchunguza Waziri Mkuu si sahihi, isipokuwa kama Waziri Mkuu itampendeza kuunda Tume kuchunguza haya malalamiko yako, bila shaka ataagiza na mimi nilete wataalam wangu kwenye hiyo Tume ambayo Waziri Mkuu ataiunda na amefanya hivyo mara nyingi tu.

Mheshimiwa Spika, katika hoja mahsusi, nianze na Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Cheyo, ambaye aliuliza kwamba, hivi viwanja kwa nini mnauza na fedha zinazopatikana kutokana na kuuza viwanja hivyo ziko wapi mbona kwenye bajeti yenu hazionekani? Ni kwamba, hivi viwanja vikishapimwa, kuna gharama na gharama kubwa kabisa ni ya fidia. Wale watu waliokuwa wanalima pale au walikuwa wanafanya shughuli zao, ni lazima wafidiwe. Kwa hiyo, vikishapimwa, wewe unayepata kile kiwanja unarudisha zile gharama na bei ambayo unauziwa ni kama tu unafidia zile gharama za upimaji. Asilimia tisini ya pesa utakazolipia kile kiwanja chako, ni kumfidia yule aliyekuwa anamiliki kiwanja kile, asilimia kumi ndizo gharama ndogo ndogo za utawala za kupima kile kiwanja. Lakini asilimia tisini, unafidia zile hela alizolipwa fidia yule aliyekuwa anamiliki kile kiwanja na pesa hizi zinaingia kwenye mfuko unaoitwa Mfuko wa Kupima Viwanja wa Mzunguko, yaani *Plot Development Revolving Fund.* Huu ndiyo mfuko tunaotumia kukopesha Halmashauri mbalimbali kupima viwanja na mfuko huu uko Hazina ndiyo maana katika bajeti yangu hii, usingeweza kuziona.

Mheshimiwa Spika, samahani Mheshimiwa Steven Galinoma, alichangia kwa maandishi lakini sikumtaja, hivyo *Hansard* itamchukua.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Ligallama kwa maelezo yako, kuhusu mgogoro. Ni kweli mwaka jana ulisema na mimi niliahidi kwamba, tutaushughulikia na ni kweli Tume mbalimbali wamekwenda, TAMISEMI wamekwenda, Wizara ya Ulinzi wamekwenda, *CDF* - Mkuu wa Majeshi mwenyewe amekwenda na wakatoa ripoti kwa Mheshimiwa Rais na Rais akatoa maelekezo. Baada ya maelekezo yale ya Rais na katika barua yangu uliyoitaja, nimenukuu Rais alielekeza nini kifanyike.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli baada ya maelekezo ya Rais, tuliona kama ule mgogoro umekwisha, kwa sababu Rais alisema kwamba, kwa kuwa wananchi wameongezeka na mahitaji ya watu yameongezeka, hii Tume ya *CDF* ilikiri mbele ya Rais, wao wakawa tayari kutoa sehemu ya ardhi yao kuwapa wananchi na Rais, akasema tekelezeni. Akawaandikia TAMISEMI na Jeshi la Wananchi na mimi Wizara yangu ilipata nakala. Kwa hiyo kama wale Wanajeshi wenyewe wako tayari kutoa ardhi kwa wanavijiji, mimi nikawa nangoja tu wakubaliane ili ile mipaka watakayokubaliana sisi tukaweke mipaka mipya, ndiyo nililokuwa nangoja tu, hata katika barua yangu niliyokupa kopi nilikuwa namuuliza Waziri wa Ulinzi, je, mmeshakubaliana ili sisi tuje, kwa sababu kazi ya kuweka mipaka ni ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Spika, mgogoro huu kama Jeshi wangekuwa hawataki kutoa ardhi hata kidogo hapo kungekuwa kuna mgogoro lakini Jeshi wako tayari kutoa na Mkoa ulitujulisha kwamba, wanataka wafanye mpango wa matumizi ya ardhi ili wajue wale wananchi ni wangapi, wanahitaji ardhi kiasi gani kwa matumizi gani. Wanataka ardhi ya kujenga, wanataka ardhi ya kulima, watataka ardhi ya kufuga, ardhi ya makaburi na kadhalika, ni kiasi gani ili eneo lile limegwe. Tunasubiri tu hayo makubaliano yafanyike ili Wizara yangu tukaweke mipaka mipya. Kwa hiyo wakishakubaliana kwamba, Jeshi watatoa hekari kadhaa kuwapa wananchi kwa ajili ya matumizi mbalimbali, mimi Wizara yangu, watalaamu watakuja kuchora ramani mpya inayozingatia makubaliano yenu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naomba Mheshimiwa Mbunge tushirikiane tu, mgogoro ni mdogo kwa sababu wananchi wanataka ardhi na Jeshi limekubali kutoa ardhi. Sasa hivi kinachofanywa ni kubaini kiasi gani, ndiyo maana inafanyiwa huu mpango wa matumizi ya ardhi ili ujulikane ni kiasi gani, wakishakubaliana ni ardhi kiasi gani, hicho watakachokubaliana hiyo mipaka mipya, ndipo Wizara yangu itakuja kutekeleza hayo mtakayokuwa mmekubaliana kuja kuweka mpaka mpya na ramani mpya. Hapo ndipo tulipofika Mheshimiwa Ligallama na ninadhani ni mahali pazuri tu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Shellukindo, ni kweli mgogoro wa Kilindi na Kiteto umekwisha, tunasubiri tu TAMISEMI au Ofisi ya Waziri Mkuu, kwani ndiyo huwa wanaandaa *GN* baada ya watalaamu kusema mpaka utapita hapa. Maneno hayo ni lazima yaandikwe kwenye *GN* na wananchi watajulishwa, lakini kwa ujumla ule mpaka wa mazoea umekubalika sasa hivi unawekewa *GN* ili tatizo liishe.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Shelukindo, ajira ya Maafisa Ardhi nimeshakujibu; kwamba, siajiri mimi, wanaajiriwa kule kule Kilindi na ninyi mnawasimamia, mnawafukuza kazi huko huko. Kama mna upungufu muajiri na mimi

nawasihi sana muajiri kwa sababu napokea maswali mengi sana, ardhi haipimwi na ninyi kwenye Halmashauri hamuajiri.

Mheshimiwa Spika, Hati Miliki kwa vijiji vitano tu tukaondoka, Mheshimiwa Shellukindo, Wizara yangu haiwezi ikapima vijiji vyote, ndiyo maana sisi tunakuja tu kuonesha mfano, ku-*train* ama kufundisha watalaamu wenu kule kwenye Halmashauri kwa vitendo tunapima kwa pamoja vijiji vitano, tukishaondoka tunasema sasa endeleeni. Tatizo ni kwamba, hawaendelei lakini kwa kweli tunajitahidi sana kutoa mafundisho haya kwa vitendo. Kwa hiyo, natoa wito kwa kwa Halmashauri zote ambazo tumeshazifundisha waendelee, lakini zile ambazo hatujazifundisha tutakuja.

Mheshimiwa Spika, mlolongo wa kutoa Hati Miliki, nimeshaueleza kwamba tumeurahisisha sana.

Mheshimiwa Spika, nyumba za kupangisha, kodi zipo juu ya nyumba za mitaani, ni kweli kodi ipo juu kwa sababu ya upungufu mkubwa sana wa nyumba. Amezunguza hapa Mheshimiwa Felix Mrema kwamba, hapa nchini tuna upungufu wa nyumba milioni mbili (2,000,000), mahali penye upungufu mkubwa kama huo ni lazima hizo nyumba chache zilizopo zitakuwa bei juu na masharti yatakuwa magumu. Ndiyo hayo sasa ya kwamba, ulipe kodi ya mwaka mzima, wakati wewe unapokea mshahara kwa kila mwezi. Ndiyo maana Serikali tumeleta zile Sheria mbili, ya mikopo ya nyumba na Sheria ile ya *Unit Titles,* ili kuhamasisha wajengaji wa nyumba wajenge nyumba nyingi zaidi, wapangishe ama wauze. Nyumba zikishakuwa nyingi, haya masharti makubwa yatapungua, matatizo haya yapo kwa sababu ya upungufu mkubwa sana wa nyumba kwani wanaotafuta nyumba ni wengi sana na nyumba ni chache sana matokeo yake ndiyo haya, lakini kwa kutumia sheria hizi mbili naamini kabisa *Estate Developers* watajenga nyumba nyingi na *supply* ya nyumba ikiwa nyingi tutaanza kuona bei ya kodi itapungua na masharti vilevile yatapungua.

Mheshimiwa Spika, *National Housing,* nimeishajibu kwamba, sasa hivi tunaisuka upya na inarudi kwenye misingi yake ya awali ya kujenga nyumba kwa watu wa kipato cha chini na kipato cha kati.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuuza nyumba kwamba mtajuaje mmuze ipi na ipi msiuze; sasa hivi *National Housing* wameweka Mtalaamu Mwelekezi anayefanya *study* ya kiuchumi ili ajue ni nyumba zipi katika maeneo yapi ziuzwe jinsi zilivyo, zipi zibomolewe zijengwe zingine ambapo zitakuwa kubwa zaidi na zitahudumia Watanzania wengi zaidi na zitatoa mapato mengi zaidi; na zipi zisiuzwe ili *National Housing* wazitumie kama dhamana wanapokwenda kukopa fedha ili wajenge nyumba zingine.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mrema tunakubaliana kabisa na uchambuzi wako kwamba, tuna upungufu mkubwa sana wa nyumba, tunatakiwa kila mwaka tujenge nyumba laki mbili (200,000) ili tuendane na ongezeko la watu lakini tunajenga nyumba elfu kumi na tano (15,000) tu nchi nzima kwa mwaka. Ni kweli, umenitaka nikose usingizi na niko tayari kukosa usingizi, lakini tukose usingizi Watanzania wote na tuone

kuwa hili ni tatizo letu wote na kwa pamoja inawezekana na hasa baada ya fursa mpya za mikopo ya nyumba, ni fursa nzuri tuzitumie katika kuboresha sekta ya nyumba.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upimaji wa nyumba, tuwe wabunifu. Ni kweli nimekuwa nikiwaambia Halmashauri tunapokutana nao kwamba, wasinga'ng'anie Halmashauri kupima wao wenyewe, sasa hivi wapeni sekta binafsi wapime mtu anakuja kama ni mwekezaji anataka kujenga nyumba mia moja ama mia mbili mpeni tu *block* ili mradi nyumba anazojenga mnakubaliana ziwe za namna gani na mahali gani na kwa matumizi gani, kulingana na mipango miji yenu, tusing'ang'anie sisi wenyewe kupima kila kitu, kila kiwanja, tuwape sekta binafsi, nchi zingine ndivyo wanavyofanya na wamefanikiwa sana. Huo ndiyo ubunifu ambao alikuwa anausema.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mtangi kuhusu yale mashamba ya Muheza na tumekubaliana baada ya Bunge hili kuisha, tutakuja kuona hali ilivyo. Lakini kwa ujumla, Wizara imetoa maelekezo kwa Halmashauri zote, yale mashamba ambayo yametelekezwa, yaani wenyewe hawalimi, kodi hawalipi na yamekuwa ni mapori, tumesema mambo mawili; kwanza watuletee *profile* hili shamba ni la nani, alipata Hati lini na amelitelekeza tangu lini? Tupate hadithi yote ya shamba hilo.

Mheshimiwa Spika, pili tumesema waanze sasa kutoa *notice* za kufutwa haya mashamba, Halmashauri zina uwezo wa kutoa *notice* kufuta haya mashamba na hii tumetoa kwa wote. Nashukuru Wilaya ya Muheza wameanza na kuna mashamba matano wameshatoa *notice* ya kuyafuta na sisi kama Wizara wametupa nakala, Halmashauri zingine zote za Korogwe, Mkinga na kadhalika fanyeni hivyo, wapeni *notice,* uwezo mnao ili tuyafute na pale ambapo wananchi wanashida ya ardhi watakuwa wa kwanza kupewa ardhi, ile inayobakia tutaitoa kwa wawekezaji wa mashamba makumbwa ili tuzalishe chakula kingi zaidi na mazao mengi zaidi, tuinue uchumi wetu kwa kutumia ardhi yetu.

Mheshimiwa Spika, suala la Chavda. Niseme tu kwamba, kama Chavda alikuwa ametoroka na sasa anakuja kwa jina jingine kununua shamba, nafikiri vyombo vya dola vimesikia kwamba mtu wao wanayemtafuta kumbe yupo na anataka kununua shamba Tanzania; basi watafanya kazi yao kama vyombo vya dola.

Mheshimiwa Spika, hili la mkataba, nafikiri ni mkataba wa kati ya anayeuza ambaye ni *CRDB* na *CRDB* ni benki binafsi wala sio chombo cha Serikali lakini kama kuna faulo, basi vyombo vya dola vitafuatilia hizo faulo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mheshimiwa Halima Mdee, kwanza niseme kwamba, ni kweli niliunda Tume lakini kwa maneno yako unasema kwamba ile Tume ilimpotosha Waziri. Labda niseme, hiyo ni tafsiri yako au maoni yako, lakini kwangu mimi ile Tume ilipokwenda kuchunguza vile viwanja na ikaniletea ripoti ambayo inaonyesha kwamba, mchakato wa vile viwanja vya shule kumgawia mwekezaji, Serikali ya Mtaa ilihusishwa na mihutsari ikaja. Manispaa ya Kinondoni, ile Kamati ya Madiwani, ile *Town Plan Committee* ambao ndiyo yenye *authority* tena kuliko hata mimi Waziri, maana ndiyo wenye ardhi, mimi Waziri sina ardhi, nasimamia taratibu tu wenye ardhi ni wenyewe,

walikaa wakaidhinisha na muhtasari ukaja wakapendekeza kwamba, hiyo ardhi igawiwe na huyu mtu apewe. Kwa sababu unapobadilisha sura ya kiwanja, ni lazima Waziri atoe ridhaa, Waziri wa wakati huo, mimi nilikuwa sijafika bado akatoa ridhaa. Sasa yote hayo Mheshimiwa Mdee, hata kama wewe ungekuwa ni Waziri, yaani uwe unapinga Muhtasari wa Kijiji, unapinga Muhtasari wa Kamati ya Madiwani, unampinga Waziri, hata kidogo, kwa hiyo mimi niliridhika.

Mheshimiwa Spika, ile ripoti Mheshimiwa Mdee nikafanya uungwana tu na wewe nikakupa nakala, sasa kama na wewe ungekuwa muungwana kama mimi ungekuja ofisini, ukaniambia nimepata ripoti yako lakini, kwanza ulinilenitea meseji ukisema nashukuru nimepata ripoti, lakini kuna mambo fulani fulani katika ripoti hii naona kama wamekudanganya. Baada ya meseji nikadhani kwamba, ama utakuja ama utanipa *details* lakini ukanyamaza sasa leo nadhani hata kwenye mshahara wangu utasimama, sasa shida ni mshahara wa Waziri au ni nini? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ile ripoti mimi niliridhika nayo na kama kuna mahali una habari mpya, unakaribishwa ofisini kwangu bado unaweza kuja ukaniletea hizo habari mpya ambazo kwenye ripoti hazipo na ambazo zinajenga hoja mpya, lakini kwa ile ripoti niliyoipata, mimi niliridhika.

Mheshimiwa Spika, muda umekwisha, niende kwa Mheshimiwa Clemence Lyamba, kuhusu hoja ya watu waliokuwa milimani na kuambiwa wahame sasa wanatangatanga. Kwa kweli ni suala la Halmashauri, watazame katika Wilaya yao ni eneo gani ambalo wanaweza wakapelekwa watu wale, wakitaka msaada wa kitalaamu labda kulipima hilo eneo ama kuweka matumizi bora ya ardhi katika eneo wanalokwenda, sisi Wizara tutaoa utalaamu kwa Halmashauri. Kwa hiyo, ni lenu kupitia Halmashauri, lakini Wizara inaweza ikawezesha kwa maana ya kutoa maelekezo ya kitaalamu.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli hata nijitahidi namna gani kujibu haya yote, siwezi kumaliza ila tu tutajitahidi kuyajibu kwa maandishi ili kila mtu aliyetoa hoja yake aridhike kwamba tumempa jibu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**FUNGU 48 – WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**

Kif.1001 – *Administration and General* ……… Tshs. 4,058,434,700/=

**MHE. FELIX C. MREMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *subvote* 1001 mshahara wa Waziri. Katika mchango wangu, niligusia suala la *VAT* na nilikuwa nategemea Waziri

kwa sababu ya umuhimu wa ongezeko hilo la kodi na *impact* yake katika sekta nzima ya ujenzi wa nyumba za kukodisha, Waziri alitolee kauli kama je, ni kweli *VAT* kwa nyumba hizi kwa pango ndivyo tulivyopitisha wakati tulipopitisha bajeti ya Waziri wa Fedha au kama siyo hivyo je, atafanya nini ili kuhakikisha kwamba *VAT* hiyo inasitishwa ili isiathiri sekta nzima ya ujenzi wa nyumba za kukodisha?

Mheshimiwa Spika, kuoanisha na hiyo, nilikuwa nategemea suala zima la kuuza nyumba *National Housing Cooperation* kwamba atahakikisha zile nyumba…

**MWENYEKITI:** Swali ni moja tu lile la kwanza la *VAT*. Hii ni *VAT* kuhusu pango, ni *VAT* kuhusu kuuzwa nyumba au ni *VAT* anatozwa *Landlord* anapopangisha?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza lazima nikiri kwamba hili suala la *VAT* ndiyo nimelipata sasa hivi kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge, kwa hiyo, naomba anipe muda tulitazame kwanza kupitia kwa wenzetu wa Wizara ya Fedha, Hazina na vile vile kwa *National Housing*.

**MWENYEKITI:** Tutapata jibu nadhani *in due course*, ulitaka ufafanuzi zaidi Mheshimiwa Mbunge, maana Waziri hana jibu hivi sasa!

**MHE. FELIX C. MREMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nategemea basi isitishwe mpaka hapo ufafanuzi utakapopatikana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Lakini huyu hana mamlaka hayo, mwenye mamlaka hayo ni Waziri wa Fedha na bahati mbaya leo hayupo. Lakini nadhani Serikali imesikia tutaona namna tutakavyolichukua kwa sababu bado tupo hadi tarehe 31 Julai, 2009.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina sababu ya kupingana na ushauri wa Rais kuhusu mgogoro ule. Lakini ninachosema, Rais alitoa maelekezo yale *based on* taarifa aliyotolewa ambayo ilimpotosha. Ndiyo maana nasema, hapa hatuwezi kuongea sana, Waziri hajafanya *revocation* ya kijiji lakini baadaye imekuja kuchorwa ramani kinyemela. Jeshi, wamepewa labda kama tunaruhusiwa kutoa mifano hapa Bungeni, *row* anayokaa Waziri Mkuu ndiyo walivyopewa Jeshi, wameruka wamekwanda *row* ya kushoto na ya kulia, halafu baadaye utawaambiaje wawagawie wananchi wakati walikokwenda wamekwenda kinguvu? Wao kwao walikopewa ni *row* hii ya Waziri Mkuu, katikati ya mito miwili, Mto Lendi na Mto Mkaja, sasa wamevuka wamekuja huku mpaka labda kwa Mzee Malecela na kule kote wamekwenda. Halafu unakwenda sasa unawaambia wawagawie ardhi wananchi wakati kule walikokwenda ni ardhi ya wananchi na wana Hati! Ndicho ninachosema. Namwomba Mheshimiwa Waziri anitafutie mtu hata kesho, Kamishna twende kule kwenye *site* kwa sababu hizi hoja zote zimejibiwa hapa bila kufika kwenye *site*, wanitafutie mtu twende naye. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, utata bado upo.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, utata wala haupo wananchi wale wanataka ardhi kwa shughuli mbalimbali. Rais ameelekeza kwamba eneo la Jeshi ambalo sasa hivi ni la Jeshi, limegwe wananchi wapewe. Sasa hivi unafanyika mchakato kujua kiasi gani wapewe kulingana na mahitaji. Ndiyo maana sasa inafanyika mchakato wa kujua ni kiasi gani kinahitajika kwa ajili ya makazi, kiasi gani kwa ajili ya mashamba, kiasi gani kwa matumizi mbalimbali kujenga shule na kadhalika. Kwa hiyo, nasema huu mchakato unavyokwenda wala mimi sioni kama kuna utata ila tu tuharakishe kutekeleza maagizo ya Rais kwamba wananchi wapewe ardhi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nadhani, tatizo ni neno 'wapewe'. Kwa mujibu wa Mbunge, nadhani anasema 'warejeshewe' ni yale yale wapewe ardhi iliyokuwa yao kwa Kiswahili warejeshewe. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu ni hicho hicho, sina shida na mshahara wa Waziri. Lakini nilitambua kwamba Mabaraza ya Ardhi yana umuhimu mkubwa sana na kwa kweli yameondoa kero kubwa sana kwa watu wetu.

Katika mchango wangu wa maandishi, nilieleza kwamba nia hii njema inadhoofishwa kwa sababu watendaji hasa wale Makatibu, hawajui sasa wanalipwa *exactly* na nani, mfumo wao ukoje, lakini kwa upande wa pili ni gharama zinazotozwa kwa wananchi wenyewe wanaopeleka kesi, ni kubwa kuliko hata gharama za Mahakama ya Mwanzo, jambo ambalo linakwenda tofauti na ilivyokisiwa kwamba Mabaraza yako karibu na wananchi yatasaidia.

Sasa nilitaka Waziri atoe labda tamko la Serikali, ameeleza ni suala la TAMISEMI lakini Serikali ni moja, ningependa tu Serikali kwa kuwa ipo, tupate tamko kueleza kwamba hawa kuhudumiwa na Halmashauri maana yake nini, Halmashauri walipie kile kitu na zile gharama ambazo wanatozwa kufanya gharama ziwe kubwa nazo zilipwe na Halmashauri au mwongozo huu utolewe kwa utaratibu gani?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza kwenye maelezo yangu ya kwenye hoja kwamba Mabaraza ya Vijiji na Kata, yanaundwa na Halmashauri. Katibu anaajiriwa na Halmashauri, analipwa na Halmashauri, anafukuzwa na Halmashauri. Viwango, walipane kiasi gani, ile ada ya pale vile vile inapangwa na Halmashauri wenyewe. Hii imewekwa ili kurahisisha mfumo wenyewe huu wa kuendesha haya Mabaraza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tamko langu mimi ni kwamba kama Waziri mwenye dhamana ya jumla ya kusimamia Sera ya Mabaraza haya, ni kwamba Halmashauri zione umuhimu wa kuyahudumia Mabaraza hayo kwa kuwapa mafunzo wale wazee, vitendea kazi, wakati mwingine nasikia hata karatasi za kuandikia hukumu wanakosa, tuweke umuhimu pale. Halafu katika kuweka ada basi waweke ada ambazo ni nafuu kwa wananchi. Mimi sijui Karatu wanatoza kiasi gani lakini madhumuni ya Baraza haya ni kwamba haki ipatikane kwa urahisi na kwa bei nafuu. Hilo ndiyo agizo nalitoa kama Waziri wa Kisekta wanapoweka hizi ada.

*(Hapa Mhe. Dr. Willibrod P. Slaa alisimama)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, huwezi kuuliza swali la pili, ndiyo tulivyobadili tena Kanuni.

**MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, huwezi kuuliza swali la pili.

**MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA:** Hakuna swali la pili?

**MWENYEKITI:** Ndiyo!

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nataka kumtoa wasiwasi Mheshimiwa Waziri, sitachukua senti yake hata moja kwa vile amejibu maswali yake vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana ambayo imeletwa ya kuweka viwanja kwa tenda, ni mpya, ni kwamba sasa tunaleta dhana ya biashara ya ardhi. Kama Serikali ndio inaamua kwenda huko, basi tuelezwe wote tufanye hivyo, wale walio na mashamba makubwa wana ruhusu ya kuyagawa mashamba yao na kuyaweka kwenye tenda. Mashamba ambayo yako Muheza kule wenyewe wayagawe mashamba yao, yawekwe kwenye tenda. Hii ni dhana mpya. Kama ndiyo hivyo, basi wote tuelezwe ndiyo hilo ambalo nataka *clarification*. Sisi wote tumezoea kwamba Serikali inapima inaweka gharama, kama ni gharama ya kufidia inakuwemo halafu watu wanatangaziwa kama vile walivyofanya Dodoma kuna viwanja kadhaa na gharama yake ni kadhaa. Lakini sasa kusema njooni mshindane, ni dhana ambayo itakaribisha watu kutoka nje kuchukua mashamba yetu, kuchukua ardhi yetu na wale ambao hawana fedha hawatakuwa na ardhi hata kidogo. Huu ni mwelekeo ambao mimi nafikiri unahitaji maelezo zaidi.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mheshimiwa John Cheyo kwa kuuliza swali hili ili Watanzania wajue vizuri. Hii dhana ya uuzaji kwa tenda, ni katika mazingira ya viwanja vya kibiashara, wenye miradi ya kibiashara. Hivi viwanja vya kawaida katika maeneo ya kawaida, iwe ni *commercial*, iwe ni *residential* katika maeneo ya kawaida, utaratibu ni ule ule kwamba utakwenda kulipia kama nilivyoeleza pale kwa kweli unacholipia ni fidia tu ya ile gharama za kile kiwanja.

Mheshimiwa Spika, kwenye *speech* yangu, nimesema eneo la Luguruni *Satellite Town* ambapo tunaweka huduma mbalimbali za kibiashara pale, wawekezaji watajenga mabenki, maduka makubwa na huduma mbalimbali. Vile viwanja vya namna ile ndivyo tunavyouza kwa tenda. Pale Kurasini, tunapanua lile eneo la Kurasini kwa ajili ya bandari. Kuna wawekezaji mbalimbali wanataka kuweka huduma mbalimbali za kibandari za kibiashara, pale vile vile tunauza kwa tenda. Ni katika mazingira hayo tu lakini viwanja vya kawaida tunatumia utaratibu wa kawaida.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, *vote* hiyo hiyo, mshahara wa Waziri, nataka ufafanuzi tu kwa mfano nikitaka kununua kiwanja Dar es Salaam, kwa Halima Mdee na ananipa *document* zote, nakwenda Wizarani, wanafanya *search* kiwanja kile kinajulikana kabisa ni cha Halima Mdee, lakini wakati unakuja ku-*process Title Deed* pale Wizarani, wanakuambia kiwanja kile siyo cha Halima Mdee, ni cha mtu mwingine wakati *information* wame-*print*, kwa mfano wanakuonyesha ni Halima Mdee. Mimi nilitaka kujua utata huu unakuwaje wakati *information* unaipata pale pale Wizarani lakini wakati wa ku-*process Title Deed* unaambiwa kiwanja kile siyo cha Halima Mdee, ni cha mtu mwingine, naomba ufafanuzi, utata huu unatokea wapi?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nifafanue hoja ya Lucy Owenya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili linaweza likatokea, sikatai na mara nyingi linatokea katika viwanja vya zamani, hivi viwanja vinavyopimwa sasa hivi ambavyo vinaingizwa mpaka kwenye kompyuta na picha yako, si rahisi kufanya miliki pandikiza *(double allocation).* Lakini kwa viwanja vya zamani ambapo kwanza kumbukumbu zilikuwa zinawekwa tu kwenye majalada mara linapotea, wanafungua faili jipya, wakati huo Jiji linatoa viwanja, Manispaa inatoa viwanja ilikuwa vurugu kubwa kweli. Sasa hivi hiyo vurugu tumeshaachana nayo na ndiyo maana tunafanya uhakiki upya katika baadhi ya maeneo pale Dar es Salaam kule *Mbezi Beach*, *Jangwani Beach*, Tegeta, ambako ndiko kuna vurumai kubwa kweli kweli. Tunafanya uhakiki ili watu wale wote wenye hati pandikizi tujue sasa tunampa nani, tunaingiza kwenye *database*, kwenye kompyuta, picha zipo kwa hiyo, hili analolisema Lucy Owenya tunataka liwe historia kwa sababu teknolojia sasa imetufikisha mahali pazuri. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mshahara wa Waziri, *subvote* 1001. Katika mchango wangu, nilizungumzia suala zima la mgogoro wa ardhi baina ya mwekezaji aliyekuwa Kiwanda cha Saruji na sasa hivi *Twiga Cement* na wananchi wa Kijiji cha Boko, eneo la Chasimba kwenye Jimbo la Mheshimiwa Rita Mlaki. Sasa nahitaji maelezo, kwa sababu katika mchango, nilimtaka Waziri aniambie kama kile kijiji ambacho kilisajiliwa kama Kijiji cha Ujamaa mwaka 1976, Hati ilishabatilishwa kwa sababu kwa taarifa zilizopo zinaonyesha kwamba yule mwekezaji katika miaka ya 1990 alipokuwa na dhamira ya kupanua kiwanda alipewa maeneo yenye viwanja 1, 4 na 7 ambapo kijiji husika kipo. Sasa nataka tu Mheshimiwa Waziri anisaidie kama eneo hili lilibatilishwa kuwa kijiji, lilifanya lini na kwa makubaliano gani na wanakijiji husika?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili lilikwenda Mahakamani na baada ya kwenda Mahakamani, mwekezaji alishinda kesi hiyo. Mpaka sasa hivi, sisi upande wa Serikali, tunajipanga tuone ni jinsi gani aidha kuwaondoa wale ambao wamekaa pale au vinginevyo. Kwa hiyo, kesi ilikuwa Mahakamani, mwekezaji ameshinda na tunatafuta njia ya kuweza kuangalia wale watu tutawapeleka sehemu gani. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Naona hilo limekwisha.

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi, nilikuwa nataka kufahamu mamlaka ya Mkuu wa Wilaya kufuta viwanja kama anayo kisheria na wale wanaoathirika na maamuzi ya Mkuu wa Wilaya kwa kufuta viwanja vyao, ni nani anawalipa fidia kwa sababu Halmashauri hazijatenga fedha kwa ajili ya kulipa fidia ya viwanja ambavyo Halmashauri yenyewe imetoa na mamlaka nyingine, inanyang'anywa. Nataka ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, kuhusu viwanja vya pale Kazima katika Halmashauri ya Mji wa Mpanda.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa maelezo yafuatayo kujibu hoja ya Mheshimiwa Arfi. Hili suala la Kazima ndiyo leo nalipata kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge. Sijui ni katika mazingira yepi *DC* akafuta hivyo viwanja. Kwa hiyo, unipe tu muda tufanye uchunguzi tuone nini kilichotokea, ni katika mazingira gani hayo yalitokea ili tuweze kuelekeza sawa sawa katika suala hili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Vema, litashughulikiwa hivyo.

**MHE. OMARI S. KWAANGW':** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Niliomba kuchangia lakini sikufikiwa kwa hiyo, nilitoa mchango wangu kwa maandishi na katika mambo ambayo nimejaribu kuomba, moja ni kwamba Serikali iliunda Tume za kuchunguza kero za ardhi katika kila Wilaya nchi nzima. Sasa taarifa ya Tume hizo binafsi sina, sina hakika kama Wabunge wenzangu wanazo lakini mimi sina. Tulitaka tujue kwa sababu watu bado wanaendelea kuja kwa Mbunge na kuuliza yale yale ambayo walitakiwa kuyapeleka pale kwenye hiyo Tume na Tume zile kila Wilaya iliteuliwa na ikafanya kazi, hatujajua kero ngapi walizipokea, ngapi wamezitatua. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri anipe ufafanuzi na kama inawezekana basi tungependa kuziona ripoti za Tume hizo ili tuone hatua zilizochukuliwa kwa wale ambao kwa kweli waliharibu kabisa au walisababisha matatizo mengi sana na kuleta kero za ardhi kwenye Wilaya zetu au katika maeneo yetu, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, taarifa za Tume.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume iliyoundwa na Mheshimiwa Rais, ilikuwa ni Tume ya Rais kufuatilia migogoro ya ardhi na sidhani kama taarifa za ile Tume ni siri. Kwa hiyo, Mheshimiwa Kwaangw' sisi tutaitafuta hiyo taarifa inayohusu Wilaya yako ya Babati ili muweze kuipata. Hata baadhi ya Wabunge ambao wangependa, watujulishe ili tuzitafute hizo taarifa tuwape, sidhani kama hayo ni mambo ya siri hayo ni mambo ya wananchi. (*Makofi*)

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina shida kabisa na Mheshimiwa Waziri, naomba nimpe taarifa na ufafanuzi zaidi.

Katika mchango wangu wa maandishi, nilieleza jinsi migogoro ya ardhi ilivyo kero na jinsi migogoro hii inavyokula muda wa Serikali katika kusuluhisha. Hivi karibuni

Serikali imejiingiza katika mgogoro na *Mbeya Club* kule Mbeya kwa Serikali kunyang'anya majengo ya *Mbeya Club* kwamba ni mali ya Serikali. Lakini sisi tuliozaliwa Mbeya, tulikuwa tunashuhudia waanzilishi wa *Mbeya Club* akina Jacob Disuza, akina Beldon, akina Mgiriki Ferdinandizi wakijenga yale majengo. Sasa ninahofia ni kwa nini Serikali inaamua kujiingiza kwenye migogoro na makundi haya ya watu hasa katika kipindi hiki ambacho tunaelekea kwenye uchaguzi? Ninataka tu nimwambie Waziri, Waziri unayo taarifa hii na kama huna mimi sina haraka na jibu naomba uwe karibu na mgogoro huu. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumjibu Mheshimiwa Mpesya kama ifuatavyo:-

Kwanza tu kwa haraka haraka, kwa kweli huu mgogoro siujui, ndiyo nausikia leo kwamba Serikali imechukua majengo ya *Mbeya Club*, kwanza ni nani, Serikali ya Kijiji, ya Mtaa, ni Halmashauri, ni nani au Wizara yangu? Kwanza nakushukuru kwamba umenihurumia kwamba nichunguze nione huyu Serikali ni nani kwa sababu huyu *Mbeya Club* bila shaka atakuwa labda na Hati Miliki ya hayo majengo. Huyu Serikali sijui ni nani ambaye anakwenda kuchukua jengo ambalo lina Hati Miliki, tutachunguza. *(Makofi)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Mimi nataka kujua zaidi kuhusu Hati Miliki hasa za kimila na hili Mheshimiwa Waziri amelizungumza kwenye hotuba yake ukurasa wa 62, *item* 85 na mimi pia kwenye mchango wangu niliandika hili.

Kwanza nimshukuru sana Waziri wa Ardhi, Maendeleo ya Makazi kwamba Wilaya ya Mbozi ndiyo ilikuwa Wilaya ya kwanza ambako majaribio ya Hati Miliki za Kimila yalifanyika na kwa kweli zoezi hili limekuwa la mafanikio makubwa sana na wananchi wametumia Hati hizi kwa ajili ya kupata mikopo kutoka Mfuko wa Pembejeo wa Taifa. Lakini tuna tatizo moja na Hati za Kimila kwamba vyombo vya fedha bado havijakubali kuzitambua Hati hizi kama nyaraka ambayo inaweza ikatumika kupata mikopo kwenye mabenki. Lakini pia hili jambo tulilizungumza mwaka jana, tukaomba Serikali izungumze na mabenki ili hizi Hati ziweze kutumika kwenye mabenki, bado Serikali haijatoa majibu. Mimi wananchi wa Mbozi, nadhani na wananchi wa sehemu nyingine ambako Hati hizi zinatumika, wana hamu ya kutaka kujua majibu ya Serikali kuhusu matumizi ya Hati za Kimila, ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi kwa suala la Mheshimiwa Zambi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli katika Wilaya za mfano za utoaji wa Hati Miliki za Kimila, Mbozi inaongoza, wamefanya vizuri sana. Ni kweli nimefika Mbozi nimekutana na wanavijiji na baadhi walikiri mbele yangu kwamba wameshatumia zile Hati za Kimila kupata mikopo ya matrekta kule Mbozi. Sasa yako matatizo mawili kwa nini hizi Hati hazijachangamkiwi sana na mabenki. Jambo la kwanza, hili ni jambo jipya,

mabenki wamezoea hizi Hati za kawaida za viwanja vya mjini, hawana matatizo nazo hizi Hati za Kimila, ni jambo jipya kidogo, kwa hiyo, bado wana mashaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilishakutana na watu wa mabenki mara mbili kuwaelimisha kwamba hii Hati ya Kimila, ina nguvu ya kisheria, inawakilisha mali fulani, ni shamba *physically* lipo, kwa hiyo msiziogope maana wakisikia za kimila wanafikiri ni karatasi tu kama ya *primary school*. Hizi ni Hati ambazo zinawakilisha mali fulani. Kwa hiyo, baadhi ya mabenki wameanza kuonyesha mwelekeo mzuri kuzikubali na kuzikopesha na tutaendelea kuwaeleza ili wawe na imani na Hati Miliki hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tatizo la pili bado ni mashaka tu na uaminifu; nilipokwenda kijiji fulani kule Mbozi, nilikwenda na Meneja wa *NMB* wa Tawi la Mbozi, tulikwenda naye tukafanya mkutano wa hadhara na katika Mkutano ule wakalalamika kwamba Hati tunazo, tunapokwenda benki hawatupi mikopo na kwa kuwa Meneja wa Benki tulikuwa naye kwenye mkutano wa hadhara, tukamwambia hebu jibu hilo. Akasimama yule Meneja wa wa *NMB*, Tawi la Mbozi, akasema ninyi hizi Hati Miliki tunajua mnazo na mashamba yenu ya Kahawa na migomba tumeyaona lakini ninyi hamlipi mikopo. Kijiji hiki hiki alikuwa amekopesha watu sijui wanne sijui watano, wote walikuwa hawajalipa. Akasema sasa ninyi watu ambao hamlipi hata hizi ndogo ndogo hizo kubwa mtalipa, badilikeni tabia na sisi benki tutabadilika. Kwa hiyo, tunafanya yote mawili, tunaelimisha benki wazikubali Hati hizi lakini vile vile hawa wanaokopeshwa nao wajenge tabia mpya ya kulipa mikopo ya benki. *(Makofi)*

**MHE. MTUTURA ABDALLAH MTUTURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imeshuhudia migogoro mingi ya ardhi na mimi naamini asilimia zaidi ya 50 inatokana na utaratibu wa fidia. Bahati nzuri nchi yetu imeandaa Sheria nzuri na Kanuni zake ni nzuri sana, lakini tatizo kubwa ni namna watendaji wanavyokiuka zile Sheria na Kanuni za ardhi upande wa fidia. Kwa mfano, migogoro ya Kurasini, nimeshuhudia watu wengi sana wakilalamika kwamba fidia walizopewa na kiwango cha ushirikishwaji wa wananchi wakati wa tathmini ni mdogo sana ingawa sheria imeeleza vizuri kabisa namna gani wananchi wanatakiwa washirikishwe wakati wa kutathmini. Vile vile migogoro ya Shirika la *TANESCO* dhidi ya wananchi ambao wamechukuliwa mali zao na maeneo yao kule Mbagala, naomba ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, Wizara imejipanga vipi kutoa elimu ya kutosha kwa wale wanaothamini ili wahakikishe kwamba Sheria ya Fidia inafuatwa kama ilivyoandikikwa kwenye vitabu?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la fidia nimelizungumza sana kwenye hotuba yangu kwamba Sheria inasema fidia lazima izingatie bei ya soko ya wakati huo. Kwa hiyo, bei ya soko inabadilika mara kwa mara na kwenye hotuba yangu na katika maelezo yangu niliyotoa hivi punde nimesema kwamba Mthamini Mkuu wa Serikali yaani *Chief Government Valuer,* tumeshamwelekeza sasa ahuishe hivi viwango ili vifanane kwa sababu viwango hivi vinavyotumika ni bei za mwaka jana, sasa mwaka jana bei zimebadilika tu. Kwenye kazi ambayo tumemwambia aifanye, nadhani ataifanya haraka iwezekanavyo ili bei za fidia zifanane na bei ya sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ushirikishwaji, sasa sijui kama kuna mahali mahususi ambapo watu kweli hawakushirikishwa kwa sababu inatakiwa hawa wathamini wanapokwenda katika eneo Fulani, yule mwenye mali awepo ama mwakilishi wake aliyemteua mwenyewe, viongozi wa eneo lile wa Serikali ya Mtaa au ya Kijiji lazima wawepo, majirani zake wanaojua mali zake lazima wawepo. Kwa hiyo, inakuwa timu, sio kazi ya mtu mmoja kama anakadiria nyumba ya Chiligati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli kuna mahali ambapo amekiuka haya, tuambie lakini Sheria iko wazi ushirikishwaji wa yule mwenye mali, Serikali ya Mtaa au ya Kijiji pale anapoishi, majirani na hao wathamini. Lakini vilevile kama yule aliyethaminiwa anahisi hakutendewa haki, Sheria vilevile inampa haki ya kukata rufaa kwamba mimi siridhiki rudieni kufanya uthamini, mara nyingi tunarudia.

**MHE. DR. LUKA J. SIYAME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni katika kukazia suala alilouliza Mheshimiwa Mpesya kuhusu *Mbeya Club*. Inaeleweka kwamba katika miji mbalimbali hapa nchini yametengwa maeneo maalum kwa ajili ya ujenzi wa nyumba na viwanja vya michezo kwa mfano tuna *Gymkhana Club, Ruhana Club, Tabora Club na Mbeya Club* ambavyo humilikiwa na wanachama wenye kulipia ada zao kila mwezi. Sasa basi kwa kuwa miezi kama mitatu iliyopita Mbeya ilifungwa na kuchukuliwa na Serikali ya Mkoa wa Mbeya, je, Mheshimiwa Waziri anaweza kutuambia kwamba sasa Serikali ameanza kutaifisha hizo *Club* za Jumuiya hizo kwa kuanzia na *Mbeya Club?*

**MWENYEKITI:** Kumbe ilichukuliwa na Mkoa?

**WAZIRI WA ARDHI NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyomjibu Mheshimiwa Mpesya ni kwamba jambo hili ndiyo leo limefika hapa Wizarani kwangu. Naomba tu Dr. Siyame kama nilivyomwomba Bishop Mpesya, watuachie tutazame ni nini hii? Serikali inachukua hii kwa misingi gani ili tuone kama kuna taratibu zimekiukwa au vipi? Naomba muda kwa kweli tulichunguze vizuri kuliko kutoa majibu ya haraka haraka.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, zimesalia kama dakika kumi kufikia kipindi cha kuahirisha Bunge kwa jioni lakini kwa mamlaka mliyonipa chini ya Kanuni ya 104 (1), naongeza muda usiozidi dakika 30 ili tuweze kuhitimisha *vote* hii. Hoja hii huamuliwa na Spika, tunaendelea Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitoa mchango wangu kwa maandishi kuhusu utoaji wa Vyeti na Hati Miliki za Kimila ambapo vipo ukurasa wa 74 na 75. Ukiangalia jedwali lile na orodha ya ile Mikoa, ni Mikoa 14 ambayo imepimwa ili kutoa Vyeti na Hati ya Kimila. Katika Mikoa ile, utaona Mikoa 10 ni Mikoa iliyopo kwenye mipaka ya nchi yetu, kuna Tanga, Ruvuma, Rukwa, Pwani, Mwanza, Mbeya, Mara, Manyara, Lindi, Kagera, Iringa na Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashawishika kuamini kwamba Sera iliyotumika ni kuanza kupima Mikoa iliyoko kwenye mipaka ya nchi yetu na kwa sababu ambazo ni za dhahiri kabisa. Kuna wakimbizi wengi na mikanganyiko mingi ya ardhi katika maeneo

yale. Sasa katika Mikoa ile, Mkoa pekee wa mpakani ambao haumo kwenye orodha ile, ni Mkoa wa Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba kwa sababu Mheshimiwa Waziri ana ubia na watu wa Kigoma, nipate uhakika kwake, mwaka huu ni zamu ya Kigoma? Maana kwenye bajeti yake ya *development* naona kuna shilingi bilioni nane kwa ajili ya upimaji na mimi mwenyewe nilifanya jitihada ya ziada nikam-*consult* Kamishna wa Ardhi pale nje lakini hata hivyo nilitaka Mheshimiwa Waziri atazame ile orodha yake kwamba ni Mkoa wa Kigoma pekee ambao ni Mkoa wa pembezoni ambao hauko katika orodha ile. Nimwombe sasa afikirie ili Mkoa huo sasa uwe ni zamu yake kuingizwa katika orodha hii ya kupimwa kwa ajili ya Hati za kimila, naomba ufafanuzi.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye hotuba yangu ya bajeti kwamba kabla ya kijiji hakijapewa Hati ya Ardhi ya Kijiji, ni lazima kipimwe mipaka yake ijulikane. Katika mipaka hii sasa tunakupa Hati au Cheti cha Ardhi ya Kijiji na ukishapata kile Cheti, sasa ndiyo unaingia kwenye zoezi la kupima mashamba ya mtu mmoja mmoja na kumpa Hati Miliki ya Kimila. Mwaka huu wa fedha wa 2009/2010, kuna vijiji 1500 ambavyo haijapimwa mipaka yake, kwa hiyo, bado havina sifa ya kuanza hilo zoezi la kutoa Hati Miliki za Kimila. Vijiji vyote 1500 ambavyo vingine viko Mkoa wa Kigoma, vyote mwaka huu vitapimwa nchi nzima ili vyote vipate sifa ya kupata Hati Miliki au Cheti cha Kijiji. Sasa Cheti kikipatikana, ndiyo litafuata zoezi sasa la kupima mashamba ya mkulima mmoja mmoja ndani ya kijiji hicho na kuwapa Hati Miliki ya Kimila. Kwa hiyo, kwa kifupi na Kigoma mwaka huu wa fedha tutafika Mheshimiwa Nsanzugwanko.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Kuhusu utaratibu!

**MWENYEKITI:** Kuhusu utaratibu, Mheshimiwa Mdee, Kanuni!

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Kanuni ya 64(1)(a). Bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nimeshika kifungu cha Mheshimiwa Waziri, nilizungumzia suala zima la kutaka kujua kutoka kwa Waziri ni lini kijiji cha Boko kilichokuwa cha Simba kimebatilishwa hivyo mwekezaji ambaye alikuja baadaye akapewa maeneo ya kijiji pasipo ridhaa ya wananchi. Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, katika kurukia swali ambalo *actually* halikuwa la kwake, akaeleza kwamba suala husika lilikuwa Mahakamani.

**MWENYEKITI:** Sio kurukia Mheshimiwa, Serikali ni moja, wewe nenda kwenye *point*.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Alieleza kwamba suala lilikuwa Mahakamani na limeshakwisha. Sasa ili kuondoa upotoshaji na vilevile kuweka *record* za *Hansard* sawa, suala husika bado lipo Mahakamani na halijakwisha hivyo tunamtaka Waziri wa TAMISEMI afute kauli yake.

**MWENYEKITI:** Alichosema ni kwamba kwa sasa iko hukumu. Sasa kwa sababu Mahakama ina ngazi mbalimbali inawezekana halijaisha kwa maana labda kuna rufaa lakini nina hakika Waziri hawezi kusema, maana wanayo hukumu, sasa ni ya ngazi gani na linaweza kuwa linaendelea kwa maana ya kwamba limekatiwa rufaa.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, naona umemsaidia kuweka maneno sawa lakini yeye hakuweka hivyo. Sasa asipotoshe na hii inaonesha jinsi ambavyo hajui mambo yanayoendelea katika Wizara yake.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko Yoyote)*

Kif.1002 *Finance and Accounts* ………………..Shs.2,790,004,000/=
Kif.1003 *Policy and Planning* …………………… Shs.673,683,100/=
Kif.1004 *Management Info System* ……………… Shs.379,902,100/=
Kif.1005 *Internal Audit Unit* ………………………..Shs.174,828,600/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif.1006 *Procurement Management Unit*………Shs.254,891,500/=

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka ufafanuzi kidogo tu kwenye *item 210100, basic salaries*. Nimeona mwaka jana mshahara ulikuwa shilingi 2,964,840/- mwaka huu umekwenda mpaka shilingi 44,891,500/-, umeongezeka karibu mara 18 zaidi. Sasa nimepata wasiwasi, nataka Waziri atueleze maana ongezeko hilo ni kubwa sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri umekiona? Pale kwenye *sub-vote 1006, item* ya kwanza 210100, *approved estimates* mwaka jana shilingi milioni 2.9 mwaka huu shilingi milioni 44.8.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la vitabu vyetu vya mwaka huu nadhani watakubaliana hata wakati mnavipitia kwenye Wizara mbalimbali kuna vifungu vimebadilishwa sana inawezekana katika *mix up* hiyo ikatokea hilo badiliko nadhani ni la kiufundi.

**MWENYEKITI:** Lakini ni vizuri kutafuta ili tuelewane vizuri baadaye.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif.2001 *Land Administration Division* …………. Shs.1,980,496,100/-

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif.2002 *Surveys and Mapping Division* …………Shs.3,073,960,200/-

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *item* 410500 *acquisition of household and institutional equipment*. Katika mchango wangu wa maandishi, nilikuwa nimeulizia kuhusu vitendea kazi ambavyo ni vichache sana, kama darubini kwa mfano Kilimanjaro iko moja tu. Lakini vitendea kazi vile ni bei ghali sana moja kama shilingi milioni 40/- hapa naona wametenga shilingi milioni 7.8. Tungependa kupata ufafanuzi je, fedha hizi zitatosha kwa vitendea kazi hivyo ambavyo ni ghali sana?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitoe ufafanuzi kwenye kile kifungu cha utumishi. Maelezo niliyopata ni kwamba watumishi waliokuwa kwenye Kitengo cha Manunuzi, awali walikuwa wanalipwa kwenye *vote* ya utawala kwa *DAP*, sasa mwaka huu wa fedha wamehamishiwa kwenye Idara hii ya *Procurement* ndiyo maana imeongeza mshahara kiasi kile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikija kwenye suala la Mheshimiwa Lucy Owenya, kifungu hiki hakihusiani kabisa na hizo *equipment* anazozisema. Upungufu wa vifaa huko kwenye Halmashauri, anayenunua vifaa vya kupima ni Halmashauri zenyewe si kwamba Wizara yangu inanunua vifaa halafu inagawa, wananunua wenyewe. Hivi ni vifaa vidogo vidogo vya ofisini pale Wizarani na sio darubini ama *GPS* kama Mheshimiwa Mbunge alivyokuwa anadhani.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif.2003 *Registration of Title Unit* ……………….. Shs.523,653,000/-
Kif.2004 *Valuation Unit* …………………………..Shs.444,282,100/-
Kif.3001 *Physical Planning Division* …………….Shs. 2,738,009,300/-
Kif.3002 *Housing Division* ………………………..Shs.1,927,760,700/-
Kif.3003 *District Land and Housing Tribunal Unit* ...Shs.2,445,850,600/-

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 48 – Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.**

Kif.1001 Administration and General ……………Shs.858,000,000/-

| | | |
|---|---|---|
| Kif.1002 | *Finance and Accounts* …………………..Shs.0/- | |
| Kif.1003 | *Policy and Planning* ………………………..*S*hs.844,400,000/- | |
| Kif.2001 | *Land Administration Division* …………….Shs.8,564,608,000/- | |
| Kif.2002 | *Surveys and Mapping Division* ……….. Shs.1,602,535,000/- | |
| Kif.2003 | *Registration of Title Unit* ……………… Shs.144,000,000/- | |
| Kif.3001 | *Physical Planning Division* ………………Shs.0/- | |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, mtoa hoja, naomba utupe taarifa ya kazi iliyofanyika kwenye Kamati ya Matumizi.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba, Bunge baada ya kukaa kama Kamati ya Matumizi, imepitia Makadirio ya Mapato ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2009/2010, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Hivyo basi naliomba Bunge lako Tukufu kuyakubali makadirio hayo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ya ilitolewa iamuliwe)*

*(Makadirio ya Mapato ya Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka 2009/2010 yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Nafurahi kuwatangazia kwamba Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka 2009/2010, yamepitishwa rasmi na Bunge la Jamhuri ya Muungano na sasa kilichabaki Wizara kutekeleza majukumu yake kama ilivyoahidi na pale ambapo kuna masuala yaliyohitaji ufafanuzi basi waendelee kutupatia ili twende vizuri. Hongera sana Mheshimiwa Waziri na wataalam wako. *(Makofi)*

Mimi nafarijika kutamka kitu kimoja tu, Katibu Mkuu wa Wizara hii, Mama Salome Sijaona, ni mmoja katika Makatibu Wakuu bora katika nchi yetu. Ndiyo maana mambo yanakwenda, kwa hiyo, wanawake wanaweza jamani. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, jana mligawiwa ratiba ya shughuli zetu. Lipo badiliko kwamba kesho si Wizara ya Elimu, ni Wizara ya Maji, nafasi ya Elimu ni tarehe 23 Julai. Kwa hiyo, ni vizuri mlione hilo mnavyojipanga katika kuchangia.

Baada ya maelezo hayo, bahati mbaya, simuoni Mheshimiwa Zungu lakini Mheshimiwa Azzan unaweza kwenda kumpa salamu, jana kule Dar es Salaam timu ya Ilala ilifungwa na timu ya Tabora inayoitwa Walugaluga. Kwa hiyo, nampa pole nadhani ndiyo maana hayupo hapa. Hayo ndiyo mambo yanavyokwenda, kwa hiyo, mfikishie pole za Spika, ndiyo mchezo unakwenda namna hiyo. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo, sasa naliahirisha Bunge hadi hapo saa tatu asubuhi tarehe 14/7/2009.

*(Saa 1:52 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne Tarehe 14 Julai, 2009 Saa Tatu Asubuhi)*